

# **Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

## **MAJADILIANO YA BUNGE**

### **MKUTANO WA KUMI NA SITA**

**Kikao cha Thelathini na Nane – Tarehe 25 Julai, 2009)**

*(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)*

#### **DUA**

*Spika (Mhe. John S. Sitta) Alisoma Dua*

### **HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Taarifa ya Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge juu ya Zabuni ya Kuzalisha Umeme wa Dharura Ulipoa Ushindi *Richmond Development Company LCC* ya Houston Texas mwaka 2006.

Taarifa ya Wizara ya Nishati na Madini kuhusu Mgodi wa Kiwira.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO – (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA NISHATI NA MADINI):** Taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka 2008/2009 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

**MHE. SEVELINA S. MWIJAGE – (K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA NISHATI NA MADINI):** Taarifa ya Msemadi Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Randama za Makadirio ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

### **HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010**  
- **Wizara ya Nishati na Madini**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, nimerejea juzi kutoka Nigeria na nawajibika kuwashukuru sana, Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uongozi wake wakati wote, Waheshimiwa Wenyeviti, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid na Mheshimiwa Jenista Mhagama, wamefanya kazi nzuri sana na tumeendelea kuwa na utulivu ndani ya Bunge. Nawashukuru sana kwa kazi hiyo.

Wakati niliposafiri, niliongozana na ujumbe ufuatao:-

Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mheshimiwa Anna Abdallah, Mheshimiwa Fatma Maghimb, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Zaynab Vullu, Mheshimiwa Zitto Kabwe na Katibu wetu, Ndugu Thomas Kashililah. (*Makofi*)

Nawataja hawa, kwa sababu wamejenga heshima kubwa huko Port Harcourt, Nigeria. Watanzania walichomoza katika masuala mawili makubwa, kuwa na umoja mzuri, mshikamano na isitoshe walikuwa wanatuambia hata wale wenzetu kutoka Mabunge mengine ya Afrika kwamba ninyi Watanzania mko tofauti ndani na nje ya ukumbi.

Tukio moja ambalo lilikuwa zuri kwa jinsi tunavyokuwa na mshikamano, mwenzetu Mheshimiwa Fatma Maghimb, alipatwa na homa kidogo ambapo ilibidi apelekwe hospitali. Waliomhudumia, ni Mheshimiwa Anna Abdallah na Mheshimiwa Zaynab Vullu, kwa upendo mkubwa kabisa. Kwa siku hiyo, wala hawakuhudhuria tena Kikao na baadaye wote tuliweza kwenda kumwangalia mwenzetu. Nawahakikishia kwamba sote tumerudi salama. Ahsante sana. (*Makofi*)

Namwita sasa mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba kutohana na Taarifa iliyowasilishwa leo mbele ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini, Bunge lako sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka 2008/2009. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka 2009/10.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, makadirio ya matumizi ya fedha kwa ajili ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka 2009/2010.

Awali ya yote, nawashukuru, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, kwa uongozi wao imara, jinsi wanavyoliongoza Taifa kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005. Aidha, nampongeza Waziri Mkuu na Mawaziri wote walionitangulia kwa kuwasilisha na kupitishwa bajeti zao.

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru wewe binafsi, Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kuliongoza Bunge hili kwa ufanisi mkubwa. Aidha, nawashukuru wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, chini ya Mwenyekiti Mheshimiwa William Hezekia Shellukindo na Makamu Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Dkt. Harrison George Mwakyembe, kwa mchango wao mahsus wakati wa uchambuzi wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka 2009/10. Pia, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushauri wanaonipa pamoja na watendaji wa Wizara na taasisi zake, katika kusimamia na kuongoza sekta za nishati na madini. Natumaini kuwa ushirikiano huo utaendelea ili tuweze kuleta maendeleo endelevu ya sekta za nishati na madini na kuongeza mchango wa sekta hizi katika Pato la Taifa, maendeleo ya kijamii na hatimaye kupunguza umaskini nchini.

Aidha, namshukuru sana Mheshimiwa Adam Kigoma Ali Malima, Mbunge wa Mkuranga na Naibu Waziri wa Nishati na Madini kwa ushirikiano wake thabiti anaonipa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara yetu.

Mheshimiwa Spika, vilevile, nawapongeza Mheshimiwa Charles Nyanguru Mwera, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Tarime, Mheshimiwa Mchungaji Luckson Ndaga Mwanjale kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini, Mheshimiwa Lolesia Jeremia Bukwimba, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Busanda na Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Biharamulo Magharibi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kati ya mwezi Julai, 2008 na Aprili, 2009, Bunge lako liliwapoteza Waheshimiwa Chacha Zakayo Wangwe (Tarime), Richard Said Nyaulawa (Mbeya Vijijini), Faustine Kabuzi Rwilomba (Busanda) na aliyekuwa Mbunge Phares Kasheemeza Kabuye (Biharamulo Magharibi). Natoa pole kwa Bunge lako, familia zao na wote walioguswa na misiba hiyo. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Spika, tarehe 29 Machi, 2009 yalitokea maafa katika machimbo ya Mgusu Wilayani Geita ambapo wachimbaji wadogo saba wa madini walipoteza maisha. Maafa hayo yalisababishwa na kuporomoka kwa kifusi ndani ya mgodi. Serikali kwa kushirikiana na vyombo mbalimbali inaendelea kuchukua hatua zinazopasa ili kuhakikisha kuwa maafa ya namna hii hayatokei tena. Tunamuomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Sengerema na viongozi wa Wilaya hiyo kwa ujumla, kwa ushirikiano wao wanaonipa katika kutekeleza na kuendeleza kazi mbalimbali ambazo zinachangia katika maendeleo ya Jimbo na Wilaya ya Sengerema kwa ujumla. Nina imani kuwa ushirikiano huo utaendelea kuimarika kwa manufaa ya Jimbo letu na Taifa kwa ujumla. Aidha, naendelea kumshukuru kipekee, mke wangu Blandina, familia yangu na wazazi wangu, kwa jinsi wanavyoendelea kunitia moyo katika utekelezaji wa majukumu yangu. Mke wangu Blandina ndiye chachu ya utendaji wangu wa kazi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana kwa namna anavyowalea watoto wetu Brian na Brigitte na familia yetu kwa ujumla. Nawaombea baraka tele kwa Mwenyezi Mungu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kutumia fursa hii kwa niaba ya wananchi wa Sengerema, kuishuru sana Taasisi ya *Christian Life World Mission Frontiers* inayoongozwa na Mchungaji Dr. Kim kwa kukubali kufadhili ujenzi wa Chuo Kikuu katika kijiji cha Isole, Kata ya Buyagu, Jimboni Sengerema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2008/09, ulizingatia: Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2005; Malengo ya Maendeleo ya Milenia 2015; MKUKUTA; Mwongozo wa Kutayarisha Mpango na Bajeti 2008/09 – 2010/11; maagizo ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Mpango na Bajeti ya maendeleo ya mwaka 2008/09, maeneo yafuatayo yalipewa kipaumbele: kupeleka umeme katika Makao Makuu ya Wilaya tisa ambazo ni Kilolo, Kilindi, Ludewa, Mbinga, Rufiji, Bahi, Uyui, Mkinga na Simanjiro; kusimamia na kutekeleza miradi katika sekta za nishati na madini; kuboresha na kukarabati njia za umeme na vituo vya kupozea umeme katika gridi ya Taifa; kusimamia na kuhamasisha uwekezaji, utafutaji, uchimbaji na uongezaji thamani katika madini; kutekeleza Mkakati wa Kuwaendeleza Wachimbaji Wadogo wa Madini; kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa ofisi za madini za kanda; pamoja na kuendeleza ujenzi wa miundombinu ya Chuo cha Madini Dodoma na Wakala wa Jiolojia Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2008/09, Wizara ilipata mafanikio mbalimbali katika sekta za nishati na madini. Kwa upande wa nishati mafanikio ni pamoja na kukamilika kwa upelekaji umeme katika Makao Makuu ya Wilaya za Ludewa, Mbinga, Simanjiro na Mkinga; Shule ya Sekondari ya Chifu Oswald Mang'ombe-Musoma na Mto wa Mbu; kukamilika kwa mradi wa kupeleka umeme mji wa Namanga; kukamilika kwa ujenzi wa mtambo wa Ubungo MW 100 uliofunguliwa rasmi mwezi Novemba, 2008 na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; kuongezeka kwa idadi ya wateja wapya wa umeme kutoka wateja 36,000 mwaka 2007 hadi kufikia wateja 58,000 mwaka 2008; kurahisisha ununuvi wa umeme kwa kutumia simu za viganjani na benki (*CRDB* na *NMB*); kuendeleza mpango wa kueneza ufungaji wa mita za LUKU nchi nzima, mijini na vijijini na pia kuongezeka kwa makusanyo ya mapato ya umeme kufikia asilimia 95 ya mauzo kwa mwezi. *TANESCO* kutenga asilimia 15 ya mapato yake ya kila mwezi kwa ajili ya kukarabati miundombinu ya kusafirisha umeme nchini kote kwa lengo la kuboresha huduma pamoja na kupunguza upotevu wa umeme, mwaka hadi mwaka; kusainiwa kwa Mkataba wa makubaliano kati ya *African Development Bank [ADB]* na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa kugharimia mradi wa upelekaji umeme Bukombe na Longido; Kuanza utekelezaji wa miradi inayofadhiliwa chini ya *ADB*, *JICA*, *MCC* na *Sida*; kuanza kwa mchakato wa kumpata Mtaalamu Mwelekezi kwa ajili ya mradi wa kudhibiti matumizi ya umeme (*demand – side management*) unaofadhiliwa na Benki ya Dunia wenye thamani ya Dola za Marekani 200,000; kutekelezwa kwa miradi ya umeme wa jua katika Mikoa ya Rukwa, Kigoma, Ruvuma, Shinyanga na Tabora chini ya mradi wa *Tanzania Energy Development and Access Expansion Program - TEDAP*; kukamilika kwa utafiti wa kuangalia mienendo ya upopo katika maeneo ya Karatu (Arusha), Mkumbara (Tanga), Kititimo (Singida), Mgagao (Kilimanjaro) na Makambako (Iringa) ambapo uwezo wa kuzalisha ulionekana; *REA* imelipa fidia ya shilingi milioni 491 kwa watu wa maeneo ya Serengeti, Bunda, Ukerewe na Urambo ambao mali zao zitaathirika na upitishaji wa umeme; na kukamilika kwa Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta ya Umeme (*Power System Master Plan - PSMP*).

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine ni kuanza kwa utekelezaji wa mkataba wa ununuvi wa jenereta tano kwa ajili ya manispaa ya Kigoma Ujiji; kukamilika kwa mkataba wa kupunguza *capacity charge* ya Songas kwa kiasi cha Dola za Marekani milioni moja kwa mwezi; kuongezeka kwa uwezo wa kusafisha gesi kutoka futi za ujazo milioni 70 hadi 90 kwa siku; Kukamilika kwa asilimia 90 ya ujenzi wa mtambo wa Serikali wa kuzalisha umeme wenye uwezo wa MW 45 unaotumia gesi asili katika eneo la Tegeta; kudhibitiwa kwa upandaji holela wa bei ya mafuta kwa kutoa taarifa za kila baada ya wiki mbili za bei elekezi ya bidhaa za mafuta ya petroli, ambazo zimesaidia kupunguza bei za bidhaa hizo na hivyo kuleta nafuu kwa wananchi; na kuimariswa udhibiti wa uchakachuaji wa bidhaa za petroli.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni: kudhibitiwa kwa bei ya ugavi wa gesi asili kwa watumiaji wa viwandani; kuongezeka kwa viwanda vinavyotumia gesi asili kutoka 20

hadi 26; kukamilika kwa mtambo wa kushindilia gesi asili na kituo cha kwanza cha kujaza gesi kwenye magari yanayotumia petroli; kuanza kazi kwa karakana mbili za kwanza za kubadili magari ili kutumia gesi asili; kukamilika maandalizi na kuwasilishwa maombi rasmi kwa wakati ya kuongeza eneo la nchi nje ya ukanda wa kiuchumi baharini (*beyond Exclusive Economic Zone – EEZ*) na kukamilika kwa Mwongozo wa Kuendeleza Biofueli nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sekta ya madini mafanikio yanajumuisha kukamilika kwa Sera ya Madini ya Mwaka 2009; kuimarika kwa ukaguzi na udhibiti wa shughuli za uzalishaji na usafirishaji wa dhahabu katika migodi mikubwa; kampuni ya Anglogold/Ashanti kuanza kulipa kodi ya mapato; kuendelea kubainisha na kutenga maeneo ya wachimbaji wadogo, kwa mfano, Barrick imetenga maeneo Kimambo, Tarime; kutolewa kwa mafunzo ya wachimbaji wadogo wa maeneo ya Songwe, Merelani na Nyarugusu kuhusu mbinu za utafutaji, uchimbaji na uchenjuaji wa madini, utafutaji wa masoko, uongezaji thamani madini, afya na usalama kazini, kulinda na kutunza mazingira, elimu ya ujasiriamali na masuala mengine yaliyomo kwenye sheria na kanuni za madini (Sheria ya Madini ya Mwaka 1998 na kanuni za madini za mwaka 1999); kukabidhiwa rasmi kwa kituo cha majoribio ya teknolojia cha wachimbaji wadogo cha Matundasi kwa mwendeshaji mpya aitwaye - *Matundasi ASM Development Company Limited* mwezi Januari; kupatikana kwa mkopo wa masharti nafuu wa Dola za Marekani milioni 50 kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya Mradi wa Uendelezaji na Usimamizi wa Sekta ya Madini (*SMMRP*); kuboreshwa kwa Mfumo wa utoaji leseni za madini (*Mining Cadastral Information Management System–MCIMS*) ambao umesaidia kupunguza muda wa kushughulikia utoaji wa leseni za madini kutoka leseni 36 kwa wiki mwaka 2007, hadi zaidi ya leseni 100 zinazotolewa sasa.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni kufanyika kwa ukaguzi wa ubora na kiasi cha dhahabu kilichozalishwa na kuuzwa nje na kampuni kubwa za dhahabu zinazoendesha migodi ya Geita, Bulyanhulu, Tulawaka, Resolute, North Mara na Buzwagi kwa lengo la kujua mapato yaliyopatikana na kiasi kinachostahili kulipwa kama mrabaha kwa Serikali. Ukaguzi huu umewezesha Serikali kuanza kulipwa *Corporate Tax* kutoka kwa Kampuni ya Geita Gold Mining Limited; kukamilika kwa ramani maalumu tatu za jiolojia zinazoonesha uwepo wa madini Mkoani Tanga na maeneo ya Nachingwea na Liganga; kuondolewa kwa Shirika la Madini la Taifa (*STAMICO*) kutoka kwenye orodha ya mashirika ya umma ya kubinafsishwa; kukamilika kwa taratibu za kujiunga na Mpango wa Uwazi katika Tasnia ya Uziduaji (*Extractive Industries Transparency Initiative - EITI*) na Tanzania kupewa hadhi ya uanachama wa awali (*candidate country*).

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2008/09, changamoto zifuatazo zililitokeza katika utekelezaji: kupanda kwa bei za mafuta ya petroli katika soko la dunia katika robo ya kwanza ya mwaka 2008/09 kulikoathiri mwenendo wa kasi ya upandaji bei na ukuaji wa uchumi; kuchelewa kwa mpango wa kubadili mtambo wa *IPTL* kutoka kutumia dizeli na kutumia gesi asili kutokana na mgogoro wa kisheria ulioko mahakamani; kukatika mara kwa mara kwa umeme kutokana na uchakavu wa njia za usafirishaji na usambazaji umeme; uhujumu wa miundombinu ya usambazaji umeme na wizi wa mafuta kwenye transfoma; kutokamilika kwa miradi mingi ya maendeleo kutokana na kuchelewa kupata fedha na wakati mwagine kupata fedha pungufu; na kutokea kwa mtikisiko wa kiuchumi duniani katika kipindi cha nusu ya pili ya mwaka 2008, ambao umeathiri maendeleo ya miradi mipyä na inayoendelea katika sekta za nishati na madini.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ni kutofuatwa kwa taratibu za kisheria kwa wachimbaji wadogo na hivyo kuwepo kwa uvamizi wa maeneo, migogoro na ajali za migodini; kuwepo kwa mifumuko ya madini ambayo inaharibu mazingira; upungufu wa

maeneo ya wachimbaji wadogo; migogoro inayojitokeza kati ya wachimbaji wakubwa na wadogo, na wachimbaji wakubwa na jamii zinazozunguka maeneo ya migodi; ukosefu wa teknolojia rahisi na sahihi na mitaji kwa wachimbaji wadogo; na kutokuwa na wataalamu wa kutosha kukidhi kasi ya ukuaji wa sekta za nishati na madini.

Mheshimiwa Spika, sekta ya nishati. Ukuaji wa sekta na mchango katika pato la Taifa. Katika mwaka 2008 sekta ya umeme na gesi asili ilikua kwa asilimia 5.4 ikilinganishwa na asilimia 10.9 mwaka 2007. Kupungua kwa kasi ya ukuaji kulitokana na kushuka kwa uzalishaji wa umeme kwa kutumia gesi asili baada ya kuvunjwa kwa mkataba wa *Dowans* mwezi Agosti, 2008, na kuisha mkataba wa *Aggreko*, kuchelewa kukamilika kwa miradi mipy ya usuaji umeme na kusimama kwa uzalishaji katika kituo cha *IPTL*. Aidha, sekta ya umeme na gesi asili ilichangia asilimia 2.0 katika Pato la Taifa mwaka 2008 ikilinganishwa na asilimia 2.1 mwaka 2007, kwa bei za mwaka 2001.

Mheshimiwa Spika, hali ya umeme kwenye gridi ya Taifa. Umeme uliozalishwa kwa kutumia maji katika gridi ya Taifa ulikuwa *Gigawatt-hour (GWh)* 2,918.6 mwaka 2008 ikilinganishwa na *GWh* 2,512.8 mwaka 2007, sawa na ongezeko la asilimia 16.2. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa umeme unaotokana na nguvu za maji hasa katika bwawa la Kihansi lililopata mvua za kutosha. Vyando vingine vilivyochangia kuzalisha umeme katika gridi ya Taifa ni gesi asili, mafuta mazito, makaa ya mawe, na tungamotaka (*biomass*). Umeme uliozalishwa mwaka 2008 kutokana na vyando hivyo ulikuwa *GWh* 1,440.1 ikilinganishwa na *GWh* 1,719.2 mwaka 2007, sawa na upungufu wa asilimia 11.1. Upungufu huo ulichangiwa na kuvunjwa kwa mkataba wa kituo cha kukodisha cha *Dowans*, kufika mwisho wa mkataba wa kituo cha kukodisha cha *Aggreko* na kutumika kwa kituo cha *IPTL* kutokana na mgogoro na *TANESCO* uliopo katika vyombo vya sheria. Aidha, mahitaji ya juu ya umeme (*maximum demand*) nchini yalikuwa Megawati 693.8 mwaka 2008 ikilinganishwa na Megawati 653.3 mwaka 2007, sawa na ongezeko la asilimia 6.2.

Mheshimiwa Spika, usambazaji umeme Vijijini. Katika mwaka 2008/09, Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa miradi ya usambazaji umeme vijijini, kama ilivyoainishwa katika Ibara ya 43(c) ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005. Fedha zilizotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi husika ziliwu shilingi bilioni 12.378 (sawa na asilimia 56.15) ikilinganishwa na shilingi bilioni 22.043 zilizopangwa. Upungufu na ucheleweshaji wa upatikanaji wa fedha ulisababisha miradi iliylengwa kutokamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Nishati Vijijini, uliendelea kutoa ruzuku kwa watekelezaji wa miradi mbalimbali ya nishati vijijini, kuendesha mafunzo ya kujenga uwezo wa waendelezaji wa miradi ya nishati pamoja na wafanyakazi wa Wakala. Katika kutekeleza Ibara ya 43a (iv) – (vi) ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005, Wakala ulitoa mafunzo ya uendelezaji wa miradi ya umeme kutokana na maporomoko ya maji, upepo na umeme wa juu. Aidha, mafunzo mengine yalikuwa katika matumizi ya bayogesi na utengenezaji wa vitofali vya mkaa (*charcoal briquettes*) kama mbadala wa kuni na mkaa.

Mheshimiwa Spika, kupeleka umeme Makao Makuu ya Wilaya. Katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005, Ibara ya 43(b), Serikali ilikamilisha uperekaji umeme katika Makao Makuu ya Wilaya ya Mkinga na Sekondari ya Chifu Oswald Mang'ombe iliyopo Musoma. Aidha, *TANESCO* iliendelea kutekeleza miradi ya kupeleka umeme katika Makao Makuu ya Wilaya nne (4) za Kilolo, Kilindi, Bahi na Uyui. Miradi mingine ni pamoja na Mto wa Mbu, Wilayani Monduli; kijiji cha Ngage “B” Wilayani

Simanjiro na Matema Beach Wilayani Kyela. Miradi yote hii inakadiriwa kugharimu jumla ya shilingi bilioni tisa na inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2009. Miradi hii itakapokamilika inatarajiwa kuwaunganishia umeme wateja wa awali wapatao 1,200.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Bodi ya Wakala wa Nishati Vijijini, iliidhinisha ruzuku ya shilingi bilioni 17.895 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya nishati vijijini. Maeneo yaliyopewa kipaumbele ni: usambazaji umeme Makao Makuu ya Wilaya; miradi ya nishati ambayo utekelezaji wake ulisimama kutokana na ukosefu wa fedha; kukamilisha miradi inayoendelea; miradi iliyokamilika lakini inahitaji upanuzi; miradi mipy ya umeme vijijini; na miradi mingine ya nishati bora kama vile umeme wa juu, upepo na uendelezaji wa nishati mbadala wa kuni na mkaa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini ilitoa jumla ya shilingi milioni 491 kugharimia malipo ya fidia kwa watu ambaa mali zao ziliathirika kutokana na shughuli ya upelekaji umeme Serengeti, Bunda, Ukerewe na Urambo. Wakala unaendelea na mikakati ya kuhakikisha kuwa Makao Makuu ya Wilaya zote yanapatiwa umeme kama inavyoelekezwa katika Ibara ya 43(b) ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, juhudi zilifanyika kutafuta ufadhili wa kutekeleza mradi wa kupanua gridi ya Taifa ikiwa ni pamoja na kushauriana na Washirika wa Maendeleo kama *Sida*, *JICA*, Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*). Katika kipindi cha mpito, zabuni ya kununua mitambo itakayotumia mafuta ya dizeli kwa ajili ya miji ya Kigoma/Ujiji, Kasulu, Kibondo, Sumbawanga na Loliondo, ilikamilika. Katika Bajeti ya 2008/2009, Serikali ilitoa fedha kwa ajili ya ununuzi wa jenereta tano za kuzalisha umeme katika Manispaa ya Kigoma/Ujiji. Aidha, fedha zinatafutwa ili kununua jenereta 12 kwa ajili ya Makao Makuu ya Wilaya za Ngorongoro, Kibondo, Sumbawanga na Kasulu. Mpango wa usambazaji umeme katika Makao Makuu ya Wilaya utaendelea kutekelezwa kwa kuzingatia Ibara ya 43(b) ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005 kadri fedha zitakavyopatikana.

Mheshimiwa Spika, miradi ya umeme Inayoendelea – usafirishaji na usambazaji. Mradi wa *electricity V*. Benki ya Maendeleo ya Afrika iliidhinisha Dola za Marekani milioni 50 kwa ajili ya kuimarisha na kuendeleza usambazaji wa umeme katika sekta za maendeleo ya kiuchumi katika vijiji, miji midogo na Makao Makuu ya Wilaya katika Mikoa ya Arusha, Shinyanga, Mwanza na Dar es Salaam. Benki hiyo pia iliidhinisha kuajiriwa kwa mshauri atakayefanya kazi na TANESCO ya kutoa huduma ya ushauri na usimamizi wa ujenzi wa mradi.

Mheshimiwa Spika, miradi inayofadhiliwa na *MCC*, Serikali kupitia *Millenium Challenge Corporation* (*MCC*) itaimarisha na kupanua mifumo ya kusafirisha na kusambaza umeme kwa Mikoa ya Tanga, Dodoma, Morogoro, Iringa, Mbeya na Mwanza; itajenga kituo cha kuzalisha umeme cha MW 8 kwenye mto Malagarasi pamoja na kufikisha na kusambaza umeme Manispaa ya Kigoma/Ujiji, Uvinza na Kasulu; na kujenga *sub-marine cable* kutoka Ras Kilomoni – hadi Ras Fumba, Unguja. Gharama ya miradi hii inafikia jumla ya Dola za Marekani milioni 206.47.

Mchakato wa kujua gharama ya huduma (*cost of service*) na bei ya mauzo (*tariff study*) kwa mradi wa *sub-marine cable* kutoka Ras Kilomoni, Dar es Salaam hadi Ras Fumba Zanzibar umekamilika kwa upande wa Zanzibar na mchakato huo unaendelea kwa upande wa Tanzania Bara. Michakato ya pande zote itakapokamilika, itawezesha makubaliano ya

kuuziana umeme baina ya pande hizo mbili za mradi. Makandarasi wataanza kazi kati ya mwezi Februari – Mei, 2010 baada ya kumaliza zoezi la kulipa fidia ya mali na mpango wa makazi mbadala kwa wale watakaoathiriwa na mradi.

Mheshimiwa Spika, mradi wa kuboresha miundombinu ya usambazaji umeme Dar es Salaam unaofadhiliwa na *JICA*. Serikali ya Japan kupitia Shirika lake la Maendeleo ya Kimataifa la *JICA* imetoa Shilingi bilioni 30 kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa kuboresha miundombinu ya usambazaji umeme katika maeneo ya Masaki, Mikocheni na Oysterbay. Kituo cha kupoza umeme cha kV 132/33 kitajengwa eneo la Makumbusho. Uzinduzi wa mradi kwa kuweka jiwe la msingi ulifanyika mwezi Juni, 2009. Mradi umepangwa kukamilika mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, mradi wa Makambako – Songea kV 132 *Transmission Line*. Mradi unahusu ujenzi wa laini ya umeme ya kV 132 ya urefu wa km 250 kutoka Makambako hadi Songea; vituo vya kupoza umeme vya kV 132/33 Madaba na Songea; na kupanua na kusambaza umeme, takriban, km 900 katika miji/Wilaya za Songea, Namtumbo, Mbinga, Makambako, Njombe na Ludewa. Mradi utagharimu Dola za Marekani milioni 70.4 kwa msaada wa Serikali ya Uswisi kupitia Shirika lake la Maendeleo ya Kimataifa la Sida. Mkataba wa kupata fedha za msaada kati ya Serikali ya Uswidi na Serikali ya Tanzania ulisainiwa mwezi Desemba, 2008. Mchakato wa kuajiri Mshauri Mtaalamu wa kuandaa zabuni za kuwapata Wakandarasi na kusimamia mradi umeanza na unatarajiwa kukamilishwa mwezi Agosti, 2009. Mradi unatarajiwa kukamilika ifikapo Desemba, 2013.

Mheshimiwa Spika, Gridi ya Kaskazini – Magharibi. Uimarishaji na upanuzi wa gridi ya Kaskazini – Magharibi, ni muhimu kwa ajili ya maendeleo ya maeneo yanayohudumiwa na gridi hii. Katika kipindi cha mwaka 2008/2009, gridi ya Kaskazini - Magharibi iliendelea kupanuliwa ambapo mgodi wa Buzwagi uliunganishwa mwezi Aprili, 2009. Aidha, kufuatia makubaliano kati ya *TANESCO* na kampuni ya Barrick, uunganishaji wa mgodi wa North Mara kwenye gridi unaendelea vizuri na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Agosti, 2009.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliendelea na mkakati wa kuunganisha gridi ya Taifa na gridi za nchi jirani. Mashauriano katika ngazi za wataalamu na Mawaziri wanaoshughulikia masuala ya nishati yalifanyika kupitia Jumuuya ya Afrika ya Mashariki (*EAC*), Jumuuya ya Uchumi Kusini mwa Africa (*SADC*), Uendeshaji wa Programu Tanzu ya Nchi za Maziwa Makuu (*NELSAP*) na Washirika wa Maendeleo, hususan, kwa mradi wa Zambia-Tanzania-Kenya *Power Interconnector*. Juhudi za kutafuta fedha za ujenzi wa mradi zinaendelea. Hadidu za rejea kwa ajili ya kudurusu upembuzi yakinifu wa kuunganisha gridi za Tanzania na Kenya zimekamilika. Pia, fedha za kudurusu upembuzi yakinifu wa awali zimepatikana. Aidha, chini ya *NBI – NELSAP*, tafiti zinakamilishwa kwa ajili ya kujenga mradi wa umeme wa Rusumo ambao utazalisha MW 60 na utahusisha kuziunganisha gridi za umeme za Rwanda, Burundi na Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuimarisha uzalishaji umeme. Mahitaji ya juu (*maximum demand*) ya umeme nchini yameendelea kukua kwa wastani wa asilimia 12 kwa mwaka. Kuisha kwa mikataba ya mitambo ya kukodisha ya Aggreko (MW 40) na Alston (MW 40) pamoja na kuvunjwa kwa mikataba wa *Dowans* (MW 100) na kutokutumika kwa kituo cha *IPTL* (MW 100), kulisababisha pengo la MW 280. Mwaka 2008, Serikali kupitia *TANESCO* ilijenga kituo cha MW 100 Ubungo cha kufua umeme kwa kutumia gesi asili (Ubungo I) na hivyo kufanya pengo hilo kuwa MW 180. Ili kuondokana na upungufu huo na uwezekano wa mfumo wa gridi

kushindwa kuhimili mahitaji, Serikali kwa kushirikiana na *TANESCO* imeandaa mkakati wa muda mfupi (2009-2012), unaolenga kukabiliana na tatizo hilo. Mkakati huo unahusisha utekelezaji wa miradi mipyä ya kudumu yenye kipaumbele kama ifuatavyo: Mradi wa Tegeta utakaotumia gesi asili *MW 45*; Mtambo wa Ubungo II utakaotumia gesi asili *MW 100*; Mtambo utakaotumia mafuta mazito wa MW 60 utakaojengwa Mwanza; na Mradi wa makaa ya mawe Kiwira wa *MW 200*.

Mheshimiwa Spika, Kukamilisha Mradi wa Tegeta MW 45. Mradi huu ni sehemu ya mpango wa Serikali wa kuongeza ufuaji umeme kwa kutumia gesi asili ya Songo Songo. Mradi utaimarisha upatikanaji wa umeme kwenye gridi ya Taifa na unatarajiwaa kukamilika mwezi Desemba, 2009.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha *IPTL MW 100*. Hatua za awali za kurekebisha mitambo ya kituo cha *IPTL* ili iweze kutumia gesi asili badala ya mafuta mazito zilikamilika. Mtengenezaji wa mitambo hiyo, kampuni ya Wartsila ya Finland alikamilisha kazi za usanifu wa kihandisi na kufanikiwa kufanya majoribio (*bench prototype testing*). Serikali inaendelea kushirikiana na wadau wanaohusika kuondoa mgogoro wa kisheria ili kituo cha *IPTL* kianze tena kuzalisha umeme mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, mradi wa Ubungo II MW 100. *TANESCO* ilitangaza zabuni mwezi Aprili, 2009 kwa ajili ya kupata mkandarasi atakayejenga mtambo wa *MW 100* utakaotumia gesi asili kufua umeme. Mradi huu utajengwa sehemu ya *TANESCO* Ubungo kwa fedha za Serikali. Mchakato wa zabuni utakamilika Oktoba, 2009.

Mheshimiwa Spika, mradi wa Mwanza *MW 60*. Mchakato wa zabuni ya kumpata mkandarasi wa ujenzi wa mradi utakamilika mwezi Oktoba, 2009. Mradi utagharimiwa na Serikali na ni sehemu ya mkakati wa kuongeza na kuimarisha upatikanaji wa umeme kwenye Mikoa iliyopo kanda ya Ziwa na kuimarisha sehemu ya gridi ya Taifa ya Kaskazini – Magharibi.

Mheshimiwa Spika, mradi wa Kinyerezi *MW 240*. Matayarisho ya awali yanaendelea ikiwa ni pamoja na kusafisha eneo ambalo mitambo itafungwa, kuweka huduma za umeme, maji na barabara. Mchakato unaendelea wa kuajiri Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kubainisha njia bora ya kuendeleza mradi, kutayarisha michoro ya awali, kutayarisha zabuni pamoja na kumpata mkandarasi wa ujenzi wa mradi.

Mheshimiwa Spika, mradi wa Kiwira *MW 200*. Mradi wa umeme wa Kiwira wa *MW 200*, ni mradi uliorithiwa na Serikali mwaka 2006 na ambaa unatekelezwa kuititia sekta binafsi. Uendelezaji wa mradi ulikwama kutokana na kutokamilika kwa makubaliano ya mkopo wa fedha za utekelezaji. Mradi huu ni muhimu katika mkakati mzima wa kukidhi ukuaji wa mahitaji ya umeme katika kipindi kifupi na kuimarisha mpango wa kuendeleza vyanzo vingine vya nishati visiviyotokana na maji. Serikali itachukua hatua za makusudi kukwamua mradi huu na kuhakikisha unakamilika katika kipindi cha muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, miradi midogo ya uzalishaji umeme. Wizara iliendelea na utekelezaji wa mkakati wa kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi katika uzalishaji na usambazaji wa umeme, kama ilivyobainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005 Ibara ya 43(g). Taratibu zimekamilika za kuendeleza miradi midogo isiyozidi *MW 10* kuititia sekta binafsi, kwa ajili ya kuuza umeme kwenye gridi ya Taifa au kuusambaza kwa wateja waliopo nje ya gridi kwa kutumia mikataba mahsusii ya kuuzia umeme (*Standardised Power Purchase Agreements – SPPA*), ambapo kila mwaka mwongozo

wa bei za umeme (*Standardised Power Purchase Tariffs – SPPT*) unatolewa. Lengo la utaratibu huu ni kupunguza urasimu na muda wakati wa majadiliano ya mikataba, kama njia ya kuvutia sekta binafsi kushiriki katika kuendeleza miradi midogo nchini. Miradi ya awali yenye uwezo wa kuzalisha jumla ya MW 40, ni pamoja na: TPCL na Kikuletwa - Moshi, TANWAT - Mufindi, Mafia, Sao Hill Saw Mill - Mufindi, maporomoko ya maji ya Mwega - Mufindi, Kilocha - Njombe, Tosamaganga na Kitonga - Iringa, na Mbalizi - Mbeya .

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kuimarisha Miundombinu na Kuongeza Wigo wa Upatikanaji wa Nishati ya Kisasa (*TEDAP*). Lengo la mradi huu ni kuboresha mifumo ya gridi katika Mikoa ya Dar es Salaam, Kilimanjaro na Arusha; kuimarisha upatikanaji wa huduma za umeme; na kuhamasisha matumizi ya nishati jadidifu kama vyanzo mbadala katika uzalishaji umeme nje ya gridi. Mradi huu wa miaka minne unatekelezwa kwa mkopo wa masharti nafuu wa Benki ya Dunia (Dola za Marekani milioni 105) na msaada wa *Global Environment Facility* (Dola za Marekani milioni 6.5). Jumla ya fedha zote ni Dola za Marekani milioni 111.5. Aidha, mchakato wa kuwapata Wakandarasi kwa ajili ya kutekeleza kipengele cha uboreshaji wa mfumo wa gridi katika Mikoa ya Dar es Salaam, Kilimanjaro na Arusha, umekamilika. Vilevile, chini ya mradi huu, miradi midogo 22 ya kuzalisha umeme katika mifumo nje ya gridi, yenye uwezo wa zaidi ya MW 70 imekwishaibuliwa. Serikali inawasiliana na Benki ya Dunia ili kuanzisha utaratibu wa kuwapatia mikopo waendelezaji wa miradi pamoja na kujenga uwezo kwa mabenki kutoa mikopo.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Umeme kwa ajili ya miji ya Kigoma, Kasulu, Kibondo, Sumbawanga na Ngorongoro. Ili kuipatia umeme wa haraka Manispaa ya Kigoma/Ujiji, ununuzi na ufungaji wa mashine aina ya Perkins utakamilika Septemba, 2009. Aidha, taratibu za ununuzi wa mitambo mingine mitano yenye uwezo wa MW 1.25 kila mmoja kwa ajili ya kupatia umeme mji wa Kigoma/Ujiji, zimekamilika. Mradi unategemewa kukamilika katika kipindi cha miezi 15 kuanzia Juni, 2009. Ufumbuzi wa kudumu ni kuunganishwa kwenye gridi ya Taifa na mradi wa umeme wa mto Malagarasi. Aidha, jenereta 12 kwa ajili ya Sumbawanga, Kasulu, Kibondo na Ngorongoro zitanunuliwa mwaka 2009/10.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Umeme wa Somanga Fungu wa MW 6. Mradi huu ulihusisha: ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme cha Somanga Fungu MW 6 ambaa umekamilika kwa asilimia 90; ujenzi wa njia ya umeme ya km 240 ya msongo wa kilovoti 33 ambaa umekamilika kwa asilimia 80; ujenzi wa vituo viwili vya kupoza umeme katika mji wa Singino na Ikwiriri na usambazaji umeme Kisiwani Songo Songo umekamilika. Aidha, vijiji vitano kaskazini ya Mkuranga vimeunganishwa na gridi ya Taifa. Mradi pia utahusisha kuvipatia umeme vijiji vilivyopo kandokando ya bomba la gesi asili itokayo Songo Songo katika Wilaya za Kilwa, Rufiji, Mkuranga na Temeke. Mradi huu ambaa unatekelezwa chini ya mradi mkubwa wa uendelezaji wa gesi asili ya Songo Songo, umechelewa kukamilika kwa takriban miaka miwili kutokana na mabadiliko ya upeo wa mradi, ujenzi wa barabara ambaa umelazimu kubadilisha njia ya umeme na matatizo ya kiutendaji ya mkandarasi. Matarajio ni kuwa mradi utakamilika mwaka 2009/10.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Gesi Asili. Serikali iliahidi kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Gesi Asili mwezi Novembra, 2008. Hata hivyo, Muswada huo haukuwasilishwa kwa lengo la kupata maoni na ushauri wa kina kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na wadau wengine. Wizara inachambua maoni hayo ili muswada huo uweze kukamilishwa. Aidha, Wizara inatarajia kukamilisha mchakato wa maandalizi ya Muswada wa sheria hiyo ili uwasilishwe Bungeni mwezi Novembra, 2009.

Mheshimiwa Spika, Matumizi ya Gesi Asili. Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2005, Ibara 43(d), imeelekeza kuwa na mkakati wa uzalishaji wa umeme wa kutosha na kwa gharama nafuu zaidi kwa lengo la kuongeza ufanisi viwandani. Hadi kufikia Mei, 2009 jumla ya viwanda 26 pamoja na Kambi ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania ya Mgulani vimeunganishwa na bomba la gesi asili katika jiji la Dar es Salaam. Aidha, katika kipindi cha mwaka 2004 hadi Mei, 2009, matumizi ya gesi asili ya Songo Songo na Mnazi Bay yameiwezesha Serikali kuokoa zaidi ya Dola za Marekani bilioni 1.38 na Dola za Marekani milioni 8.07, sawia, ambazo zingetumika kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya mitambo ya umeme na ya viwandani. Mwezi Februari, 2009, EWURA ilianza kudhibiti bei ya ugavi wa gesi asili. Bei mpya ya ugavi wa gesi asili ilipungua kutoka Dola za Marekani 1.42 hadi 0.52 kwa kipimo kimoja cha nishati cha “giga joule”. Udhibiti huu umesababisha watumiaji wa gesi asili viwandani kupata unafuu wa takriban senti za Dola za Marekani 94 kwa kila futi za ujazo 1000. Aidha, marekebisho ya valvu za mitambo ya kusafishia gesi asili (John Thomson valves) yaliwezesha Songas kuongeza uzalishaji wa gesi asili kutoka futi za ujazo milioni 70 kwa siku hadi futi za ujazo milioni 90 kwa siku. Marekebisho haya yataleta unafuu wa muda kwa kupitisha gesi nyingi zaidi wakati upanuzi wa mitambo ya kusafisha gesi asili ukiendelea.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Gesi Asili ya Mnazi Bay. Serikali imeingia mikataba na kampuni ya Artumas kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kuzalisha, kusafirisha na kusambaza umeme katika maeneo mengine ya Mikoa ya Lindi na Mtwara ambayo hayajapata umeme. Aidha, Serikali imetoa kiasi cha Shilingi bilioni 8.7 mwaka 2008/09 kutoka kwenye mfuko wa kufidia bei za umeme (*National Tariff Equalization Facility - NTEF*) kwa ajili ya ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 33 kuunganisha miji ya Nyangao, Masasi na Lindi. Mkandarasi amechaguliwa, ununuzi wa vifaa unaendelea na ujenzi utachukua miezi minne, yaani, kuanzia Agosti hadi Novemba, 2009.

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Taifa ya Mafuta. Katika mwaka 2008/2009, Serikali iliendelea na mchakato wa kuiwezesha TPDC kusimamia uanzishwaji wa Hifadhi ya Taifa ya Mafuta (*National Oil Strategic Reserve*). Mpango huu umeanza kutekelezwa kwa kuifanya TIPPER kuwa hifadhi ya mafuta ya jumla (*bonded warehouse*) ambapo baadhi ya matanki ya kuhifadhia mafuta yameanza kukarabatiwa.

Mheshimiwa Spika, uagizaji mafuta kwa pamoja (*bulk procurement*). Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilikamilisha mchakato wa kumpata mtaalamu mshauri (*Petroleum Development Consultants Ltd*) mwezi Januari, 2009. Mtaalamu huyo anaendelea na kazi ya kuandaa namna bora ya kutekeleza utaratibu wa kuagiza mafuta kwa pamoja, ikiwa ni pamoja na kuandaa rasimu za mikataba kati ya wadau mbalimbali na kanuni za uendeshaji wa mfumo huo.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Kiwanda cha Kusafisha Mafuta Ghafi na Bomba la Mafuta la Dar es Salaam – Mwanza. Itakumbukwa kuwa tarehe 20 Aprili, 2007 Serikali ilisaini makubaliano ya utekelezaji (*Implementation agreements*) na *Kampuni ya Noor Oil Industrial Technology (NOIT)* kuhusu miradi ya kujenga kiwanda cha kusafishia mafuta ghafi na bomba la kusafirisha mafuta kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza. Utekelezaji wa mradi huo umeshaanza, kwa sasa waendelezaji wa mradi wanaendelea na taratibu za kupata ardhi katika Wilaya ya Mkuranga kwa ajili ya kujenga kiwanda cha kusafisha mafuta.

Mheshimiwa Spika, utafutaji wa mafuta nchini. Katika mwaka 2008/2009, shughuli za utafutaji wa mafuta katika maeneo mbalimbali nchini ziliendelea kwa kuzingatia utekelezaji wa Ibara ya 43 (h) ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005. Jumla ya

visima vinne (4) vilichorongwa katika maeneo ya Mkuranga (2) na Mafia (1) Mkoani Pwani; na Mandawa Mkoani Lindi (1). Aidha, kisima cha Mafia Deep-1 kimeonesha dalili za kuwepo gesi asili na kinaendelea kufanyiwa utafiti.

Mheshimiwa Spika, kazi za kurekodi takwimu zaidi za mtetemo (*seismic data*) na kudurusu taarifa za jiojolia na jiofizikia, ili kubaini maeneo muafaka ya kuchoronga visima vya utafutaji iliendelea kufanyika. Jumla ya takwimu mpya za mtetemo (*2D seismic*) zenye urefu wa kilometa za mstari 16,133 zilirekodiwa katika maeneo ya Kisangire, Kimbiji, Kilwa Mashariki, Ukanda wa bahari -Tanga na kwenye maji ya kina kirefu cha Bahari ya Hindi. Aidha, takwimu za mtetemo (*3D seismic*) za mraba wa kilometa 3,560 zilikusanya katika kina kirefu cha maji. Majadiliano yaliendelea na kampuni 4 za utafutaji mafuta zilizoshinda zabuni katika maeneo yaliyo wazi. Kampuni hizi ni: Beach Petroleum ya Australia (eneo la kusini mwa Ziwa Tanganyika); Motherland Industries ya India (eneo la Malagarasi); na Tower Resources ya Uingereza (eneo la Wembere mpaka Maziwa ya Eyasi, Manyara na Natron).

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Ansco ya Tanzania, ilishindwa masharti ya zabuni kwenye eneo la Ruhuhu. Maeneo ya kusini mwa Selous, Kilosa-Kilombero na Ruhuhu yatatangazwa kwa wawekezaji wengine. Aidha, majadiliano na Kampuni ya Tullow Oil (eneo la kaskazini mwa Ziwa Tanganyika) yalikumbwa na m dororo wa kifedha, na majadiliano na Petrobras (eneo la Kitalu Na. 8 katika kina kirefu cha Bahari ya Hindi) yalikumbwa na masuala yenye utata katika utafutaji wa mafuta na gesi asili baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa bei za mafuta ya petroli. Kwa ujumla, upatikanaji wa mafuta nchini mwaka 2008/2009, ulikuwa wa kuridhisha. Kutokana na kukua kwa uchumi na kuongezeka kwa shughuli za kijamii, matumizi ya mafuta ya petroli nchini yanaongezeka kwa wastani wa asilimia tano (5) kwa mwaka. Matumizi ya mafuta ya petroli nchini yanakadiriwa kufikia tani milioni 1.4 kwa mwaka. Bei za mafuta ghafi katika soko la dunia zilipanda na kufikia kiwango cha juu kabisa cha Dola za Marekani 147 kwa pipa mwezi Julai, 2008. Kupanda kwa bei za mafuta ghafi katika soko la dunia kulisababisha pia kupanda kwa bei za bidhaa za mafuta katika soko la ndani ambapo wastani wa bei ya mafuta ya petroli ilikuwa Shilingi 1,720 kwa lita, dizeli shilingi 1,923 kwa lita na mafuta ya taa shilingi 1,368 kwa lita. Mwezi Januari, 2009 bei za mafuta ghafi zilishuka hadi kufikia Dola za Marekani 38 kwa pipa.

Mheshimiwa Spika, kushuka kwa bei katika soko la dunia kulileta unafuu kidogo wa bei kwa soko la ndani ambapo mwezi Januari, 2009, bei ya bidhaa za mafuta zilishuka hadi kufikia wastani wa Shilingi 1,359 kwa lita ya petroli, Shilingi 1,397 kwa lita ya dizeli na Shilingi 859 kwa lita ya mafuta ya taa. Aidha, kuanzia mwezi Januari, 2009, EWURA ilianza kudhibiti bei ya mafuta, kwa kuweka bei elekezi kutokana na mwenendo wa bei ya mafuta nchini kutokuwa wa kiushindani. Vilevile, EWURA ilihakikisha kuwa taarifa za kila baada ya wiki mbili za bei elekezi za bidhaa za mafuta ya petroli zinatolewa. Taarifa hizo zimesaidia kupunguza bei za bidhaa za mafuta ya petroli, hivyo kuleta unafuu kwa mwananchi.

Mheshimiwa Spika, uendelezaji wa nishati Jadidifu na Mbadala. Katika mwaka 2008/2009, Wizara iliendelea kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 Ibara ya 43a (iv) – (vi) kwa kuhamasisha matumizi ya nishati jadidifu na mbadala. Majadiliano na kampuni zenye nia ya kuendeleza nishati ya upepo, yaliendelea. Takwimu za uendelezaji wa jotoardhi eneo la Songwe zilichambuliwa na kujadiliwa na wadau, na hatua zaidi za uendelezaji zilipendekezwa. Zoezi la ubainishaji vyanzo vya maporomoko madogo ya maji

liliendelea katika Mikoa ya Iringa na Mbeya ambapo jumla ya vituo 11 vilitembelewa na kukusanya takwimu. Katika Mkoa wa Iringa, vituo hivyo viko katika mito ya Mhanga (Kilolo), Ndembela (Mufindi), Hagafiro (Njombe), Uwemba (Njombe), Itidza (Njombe) na Balali (Njombe).

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Sayansi na Teknolojia iliendelea na zoezi la uhakiki wa gesi zinazozalishwa wakati wa kupika kwa kutumia vitofali vitokanavyo na makaa ya mawe (*coal briquettes*). Uchambuzi wa awali bado umeonesha haja ya kufanya maboresho katika utengenezaji vitofali ili kupunguza gesi zenye sumu. Aidha, Wizara ilikubaliana na Kampuni ya Kiwira kuhusu umuhimu wa kuhakiki zaidi ubora wa vitofali vinavyotengenezwa Mgodini kwa kutumia utaratibu kati ya Mgodi na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kulingana na viwango vya Wakala wa Usalama na Afya katika Maeneo ya Kazi (OSHA) na Shirika la Afya Duniani (*WHO*).

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Umemenuru unaotekelozwa kwa ufadhili wa Sida (*Sida/MEM Solar PV*) uliendelea kutekelezwa kwa kuzingatia Ibara ya 43 (vi) ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005. Lengo ni kuondoa vikwazo katika soko la umemenuru kwa njia ya uhamasishaji, kujenga uwezo wa kuandaa mipango ya kibashara, mafunzo kwa mafundi, uanzishwaji wa *SACCOS* na kuongeza mtandao wa wauzaji wa vifaa vya umemenuru. Mikoa iliyonufaika na mkakati huo katika mwaka 2008/09 ni Ruvuma, Dodoma na Lindi. Hivyo, jumla ya Mikoa 11 imenafaika na mradi kuanzia Julai, 2005. Aidha, mradi ulianza kuijengea uwezo Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) na Shirika la Viwango Tanzania (*TBS*) katika kutambua ubora wa vifaa vya umemenuru na pia *VETA* kuweza kuingiza teknolojia ya umemenuru katika mitaala.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi wa matumizi ya umemenuru unaofadhiliwa na *GEF* kwa kushirikiana na *UNDP* uliendelea kutekelezwa katika Mikoa ya Mwanza, Kagera, Mara na Shinyanga. Madhumuni ya mradi huu ni kujenga na kuwezesha ukuaji wa soko la umemenuru. Tangu mradi uanze mwaka 2004, jumla ya mifumo 66 ya vifaa vya umemenuru imejegwa katika Mikoa minne. Kati ya mifumo hiyo, mifumo 11 imejengwa katika shule za sekondari, 22 katika zahanati na 33 katika vituo vya afya. Aidha, mafundi mchundo 200 kutoka Mikoa hiyo wamefundishwa utaalamu wa ufungaji na matengenezo ya mifumo ya umemenuru ikiwa ni mpango wa muda mfupi katika kukabiliana na tatizo la upatikanaji wa mafundi mchundo. Kutokana na uzoefu wa *VETA* Mwanza katika kutekeleza mtaala wa mafunzo ya umemenuru mradi umeanzisha mafunzo kama haya katika Mikoa ya Mara, Kagera na Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, uendelezaji wa Biofueli nchini. Maandalizi ya uendelezaji endelevu wa biofueli yaliendelea kuratibiwa na Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Mwongozo wa Uendelezaji Biofueli nchini ulikamilishwa. Aidha, Mkataba Maalumu wa kuandaa sera na sheria ya kuendeleza mradi wa biofueli nchini ulisainiwa kati ya Serikali za Tanzania na Uswidi tarehe 22 Desemba, 2008. Katika mkataba huo, Serikali za Uswidi na Norwe zitatoa Dola za Marekani milioni 3.1 na Serikali ya Tanzania itachangia kiasi cha Dola za Marekani 372,500.

Mheshimiwa Spika, matumizi bora ya nishati. Katika juhudzi za kuendeleza ufahamu kwa umma kuhusu matumizi bora ya nishati kuitia mradi wa *SADC-ProBEC*, uhamasishaji wa teknolojia bora kwa ajili ya kupikia majumbani na kwenye taasisi uliendelea kutolewa katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Iringa, Mbeya, Ruvuma na Dodoma. Katika kipindi cha mwaka 2008/09, jumla ya makaushio bora 13 ya tumbaku yalijengwa kwa ajili ya kukaushia tumbaku Mkoani Tabora.

Mheshimiwa Spika, mgawanyo wa gharama na mapato ya mafuta katika pande mbili za Muungano: Mwezi Oktoba, 2008, Mshauri (Kampuni ya AUPEC ya Uingereza) aliwasilisha rasimu ya mwisho ya taarifa kuhusu suala la utafutaji mafuta na mgawanyo wa mapato na gharama zitokanazo na mafuta na gesi asili katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Taarifa hiyo ilijadiliwa na wadau wa pande zote mbili za Muungano katika warsha iliyofanyika Zanzibar mwezi Aprili 2009. Mshauri aliwasilisha taarifa ya mwisho kwa Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar tarehe 23 Juni, 2009. Kimsingi Mshauri Mwelekezi amependekeza yafuatayo: mgawanyo wa gharama na mapato yatokanayo na uchimbaji na uzalishaji wa mafuta na gesi uzingatie mahala inapochimbwa rasilimali husika; matakwa ya Kikatiba; kuundwa kwa chombo cha pamoja cha kusimamia shughuli za utafutaji na uzalishaji wa mafuta (*Joint Petroleum Board*); na kurekebisha muundo wa TPDC kwa kurekebisha Sheria iliyoianzisha. Kwa sasa Wizara ya Nishati na Madini inaendelea kuipitia taarifa hiyo kabla ya kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Spika, sekta ya madini, ukuaji na mchango wa sekta ya madini kwenye Pato la Taifa. Sekta ya madini ilikua kwa asilimia 2.5 mwaka 2008 ikilinganishwa na asilimia 10.7 mwaka 2007, kwa bei za mwaka 2001. Kushuka kwa kiwango cha ukuaji kulitokana hasa na: kushuka kwa uzalishaji wa almasi katika mgodi wa Williamson Diamonds Ltd kulikosababishwa na ukosefu wa mtaji; kuporomoka kwa machimbo ya Nyankanga na hivyo kusimamisha uchimbaji katika chanzo kikuu cha uzalishaji katika mgodi wa dhahabu wa Geita; na kupungua kwa shughuli za kampuni za utafutaji wa madini kulikosababishwa na m dororo wa uchumi duniani.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kushuka kwa ukuaji wa sekta ya madini, mchango wake katika Pato la Taifa ulipungua kutoka asilimia 2.7 mwaka 2007 hadi asilimia 2.6 mwaka 2008, kwa bei za mwaka 2001. Hata hivyo, thamani ya mauzo ya madini nje iliongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 982.711 mwaka 2007 hadi kufikia Dola milioni 1,075.943 mwaka 2008. Ongezeko hilo la asilimia 9.5 lilitokana na kuongezeka kwa bei ya dhahabu katika soko la dunia.

Mheshimiwa Spika, Sera na Sheria ya Madini, katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005 Ibara ya 39(g), Serikali ilikamilisha mchakato wa maandalizi na kuitisha Sera ya Madini ya Mwaka 2009. Sera hiyo imezingatia maoni ya wadau na kamati mbalimbali zilizoundwa na Serikali. Malengo makuu ya Sera hiyo ni kuongeza fungamanisho la sekta ya madini na sekta nyingine za uchumi ili kuongeza mchango wake katika Pato la Taifa na mapato ya Serikali; na kuleta maendeleo endelevu ya sekta. Malengo mengine muhimu ni kuboresha mazingira ya kiuchumi; kuimarisha mfumo wa sheria; kurekebisha mfumo wa kodi; kuimarisha usimamizi wa sekta ya madini; kuimarisha ushiriki wa Serikali na Watanzania katika shughuli za madini; kuboresha uchimbaji mlogo; kuboresha taratibu za malipo ya fidia ya ardhi kwa wanaopisha ujenzi wa migodi; kuhamasisha na kuendeleza uongezaji thamani ya madini; na kuimarisha usimamizi wa mazingira, afya na usalama katika shughuli za madini.

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea na mchakato wa marekebisheso ya Sheria ya Madini ya Mwaka 1998, kwa kukusanya maoni ya awali ya wadau. Matarajio ni kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Madini Bungeni mwezi Oktoba, 2009. Marekebisheso hayo ya sheria yatasaidia kusimamia sekta ili kuleta maendeleo endelevu na kuongeza mchango katika Pato la Taifa, hivyo, kuchangia kikamilifu katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini kama ilivyobainishwa katika MKUKUTA.

Mheshimiwa Spika, majadiliano na Kampuni ya Willcroft. Katika kipindi cha mwaka 2008/2009, Serikali iliendeleza majadiliano na Kampuni ya Willcroft inayomiliki asilimia 75 ya hisa za Kampuni ya *Williamson Diamonds Limited (WDL)* kuhusu kuboresha uzalishaji wa almasi katika Mgodi wa Mwadui. Hata hivyo, majadiliano hayo yalisitishwa baada ya umiliki wa Kampuni ya Willcroft iliyokuwa ikimilikiwa na Cheviot Holding, kampuni tanzu ya De Beers, kuhamia Kampuni ya Petra Diamonds Limited na Serikali kuridhia uhamisho huo mwezi Februari, 2009. Serikali inaendelea kubaki na hisa asilimia 25 katika Kampuni ya WDL kwa kuzingatia Ibara ya 39g (i) na (ii) ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko hayo ya umiliki wa Willcroft yamesababisha kutofuatwa kwa utaratibu wa kupeleka almasi za WDL London kwa ajili ya kuchambuliwa na TANSORT. Mazingira haya yametokana na kutokuwepo kwa mkataba mpya ambaou ungeonesha kazi za TANSORT bila kuihusisha kampuni ya *Diamond Trading Company (DTC)*, kampuni tanzu ya De Beers, katika biashara ya almasi zinazozalishwa na WDL. Serikali inaendelea na majadiliano na Willcroft ili kupata mkataba mpya wa ubia utakaozingatia maslahi ya pande zote mbili. Mkataba huo, vilevile, utahusisha majukumu mapya ya TANSORT ikizingatiwa kuwa shughuli za TANSORT zitahamia nchini.

Mheshimiwa Spika, uendelezaji wa Wachimbaji Wadogo. Katika kipindi cha mwaka 2008/09, Serikali ilikamilisha upimaji wa viwanja katika eneo la hekta 4,000 lililopo Winza-Mtakanini Wilayani Mpwapwa na kuvigawa kwa wachimbaji wadogo. Leseni za wachimbaji waliogawiwa viwanja zinaendelea kutolewa ili waweze kumilikishwa maeneo hayo kisheria.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, imeendelea kuchukua hatua za makusudi za kuwaendeleza wachimbaji wadogo juu ya uchimbaji salama na wenye tija, kwa kutoa mafunzo kuhusu matumizi bora ya zebaki, matumizi salama ya baruti na taratibu za kisheria za upatikanaji wa leseni za utafutaji na uchimbaji madini. Mafunzo hayo yalihusisha pia kutoa uelewa wa mifuko iliyopo ya kuwawezesha kupata mikopo na fursa za kiuchumi katika biashara ya madini. Wadau walioshirikiana na Wizara katika kutoa mafunzo hayo ni Shirika la Mzinga, Asasi ya *Agenda for Environmental and Responsible Development* na SEAMIC. Jumla ya wachimbaji wadogo 150 walinufaika na mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada za kutaka kuwasaidia wachimbaji wadogo kupata mikopo na maarifa mapya katika fani ya uchimbaji madini, fedha zilizotarajiwa kwa ajili ya shughuli hiyo hazikupatikana kutokana na ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, kuimarisha usalama na utunzaji wa mazingira Migodini. Katika kuimarisha usalama migodini, Wizara iliendelea kutoa maelekezo kwa wachimbaji wadogo juu ya uchimbaji salama unaohakikisha usalama na afya ya wachimbaji na jamii inayowazunguka wakati wa kaguzi za mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, licha ya maelekezo ya uchimbaji salama yaliyotolewa, katika kipindi cha mwaka 2008/2009, yalitokea maafa katika machimbo ya Mgusu yaliyoko Wilayani Geita na kusababisha vifo vya watu saba. Katika kudhibiti uchimbaji hatarishi uliokuwa ukiendelea katika eneo hilo, Serikali imelifunga eneo hilo ili kuweka utaratibu wa kulirasimisha kwa wachimbaji wadogo sambamba na kuendelea kwa shughuli za utafutaji za mwekezaji mkubwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya tukio la ajali mbaya kwenye migodi ya Mirerani mwezi Machi, 2008, Serikali imeendelea kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa suala la uchimbaji hatarishi wa madini ya tanzanite katika vitalu B na D. Chanzo kikuu cha maafa yaliyotokea, ambacho ni mafuriko ya maji ya mvua kupitia shimo la D'Souza, kimedhibitiwa. Nusu ya shimo hilo limefukiwa na mtaro wa kuelekeza maji ya mvua nje ya eneo la hatari umechimbwa. Aidha, uchimbaji holela bila kuzingatia kanuni za mipaka ya viwanja chini ya ardhi ni moja ya sababu zinazosababisha ajali za mara kwa mara kutohana na tatizo la mitobozano. Ili kuепukana na tatizo hilo, Serikali inahamasisha na kuratibu uanzishwaji wa kampuni/ushirika, uunganishaji wa leseni ndogo na utolewaji wa leseni chache zenye maeneo makubwa kwa kila kitalu, yatakayochimbwa kitaalamu.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi wa migodi mikubwa ya Buzwagi, Bulyanhulu, *North Mara*, *Golden Pride* na *Tanzanite One* ulifanyika ili kudhibiti matumizi ya kemikali na baruti na kuhakikisha kuwepo kwa usalama na afya ya wafanyakazi migodini. Aidha, upitiaji wa mipango ya ufungaji wa migodi (*mine closure plans*) ulifanyika kwa migodi ya Tulawaka, *Golden Pride* na Mwadui ili kuhakikisha usalama na utunzaji wa mazingira unazingatiwa katika mchakato wa ufungaji wa migodi hiyo.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi na udhibiti wa shughuli za uzalishaji na biashara ya madini. Kitengo cha Ukaguzi wa Dhahabu (*Gold Audit Program – GAP*), kimefanikiwa kuendeleza kikamilifu kazi zote zilizokuwa zinafanywa na kampuni ya kigeni ya *Alex Stewart (Assayers) Government Business Corporation* kwa kutumia wataalamu 35 ambao wote ni Watanzania. Kitengo hiki kilitekeleza kazi zifuatazo katika mwaka 2008/09:- kuhakiki ubora na wingi wa madini ya dhahabu yanayozalishwa na kusafirishwa nje na migodi mikubwa ili kujua thamani yake halisi na kiwango cha mrabaha unaostahili kulipwa Serikalini; kuhakiki gharama za uwekezaji na uendeshaji wa migodi mikubwa ya dhahabu kwa lengo la kutathmini kodi ya mapato inayostahili kulipwa Serikalini na migodi hiyo; na kufanya ukaguzi wa shughuli za utunzaji na ukarabati wa mazingira kwenye migodi mikubwa ya dhahabu ili kuhakiki gharama za utunzaji wa mazingira wa migodi hiyo. Aidha, Kitengo kilitoa elimu kwa umma kuhusu shughuli zake kupitia ushiriki katika maonesho mbalimbali ya Kitaifa, kuendesha warsha na semina katika maeneo yaliyo jirani na migodi mikubwa ya dhahabu, na kurusha vipindi maalumu katika televisheni mbalimbali za hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2008 hadi Machi, 2009, jumla ya wakia 668,946.61 za dhahabu, wakia 244,650.89 za fedha na ratili 4,032,697.94 za shaba zenye thamani ya Dola za Marekani 587,407,519.73 zilizalishwa na kusafirishwa nje ya nchi na migodi ya *Golden Pride*, Geita, Bulyanhulu, *North Mara* na Tulawaka kama zilivyoahakikiwa na Kitengo. Mrabaha wa awali uliokokotolewa ni Dola za Marekani 15,860,003.03 ikilinganishwa na Dola za Marekani 15,488,098.01 zilizokokotolewa na kulipwa Serikalini na wamiliki wa migodi hiyo. Hii ni pungufu ya Dola za Marekani 371,905.02 zilizotakiwa kulipwa Serikalini. Wamiliki wa migodi hiyo walielekezwa kulipa tofauti hiyo na wamekuwa wakilipa madeni hayo mara kwa mara kila walipoelekezwa kufanya hivyo na Wizara.

Mheshimiwa Spika, kazi ya kuhakiki mahesabu ya fedha ya migodi ya Geita, Bulyanhulu, Tulawaka na *North Mara* kwa kipindi cha 2004 hadi 2007 ilikamilika. Uhakiki huo umebaini kasoro kadhaa ambazo zinaendelea kufanyiwa kazi na Kitengo kwa kushirikiana na *TRA*, pamoja na vyombo vingine vya maamuzi vya Serikali. Baadhi ya kasoro hizo ni pamoja na kuwepo kwa kiwango kikubwa cha gharama za uwekezaji na uendeshaji wa migodi ambazo hazikuwa na vielelezo kuthibitisha uhalali wake; kubainika kwa makosa katika uandaaji na utunzaji wa kumbukumbu za mahesabu ya fedha ya migodi hiyo; kubainika kwa mikopo iliyochukuliwa na baadhi ya migodi bila idhini ya Benki Kuu ya Tanzania; na

kubainika kwa malipo pungufu ya mrabaha wa madini yaliyozalishwa na kuuzwa nje na migodi.

Mheshimiwa Spika, uimarishaji wa mfumo wa utoaji na usimamizi wa Leseni za Madini. Mwaka 2008/2009, Wizara imeendelea kuimarisha Mfumo wa Utoaji na Usimamizi wa Leseni za Madini (*Mining Cadastral Information Management System*), ikiwa ni pamoja na kuongeza ukubwa wa *server*. Hii imeongeza kasi ya utayarishaji leseni kutoka wastani wa leseni 15 hadi 41 kwa leseni kubwa na kutoka wastani wa leseni 41 hadi 148 kwa leseni ndogo, kwa wiki. Aidha, mfumo huo umesaidia kupunguza tatizo la kutoa leseni zaidi ya moja kwenye kiwanja kimoja na pia umerahisisha ufuatiliaji wa maduhuli ya Serikali yatokanayo na ada za leseni za madini.

Mheshimiwa Spika, uimarishaji uwezo wa Serikali kusimamia sekta ya madini. Katika kuimarisha usimamizi wa sekta ya madini, muundo mpya wa Wizara ya Nishati na Madini ulipitishwa kwa kuteua Kamishna Wasaidizi sita kuongoza Sehemu sita zilizopo Makao Makuu na kuwateua wengine wanane kuongoza ofisi za Kanda.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Mafunzo ya Wachimbaji Wadogo cha Matundasi. Kituo cha mafunzo kwa vitendo ya uchimbaji na uchenjuaji wa dhahabu, Matundasi–Chunya kwa ajili ya wachimbaji wadogo kilikabidhiwa rasmi kwa mwendeshaji M/S Matundasi ASM *Development Company Limited* mwezi Januari, 2009. Mwendeshaji huyo atazalisha dhahabu, kutoa mafunzo na huduma mbalimbali kuhusiana na uchimbaji na uchenjuaji wa madini.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali ya Madini (SMMRP). Maandalizi ya mradi ikiwa ni pamoja na kutayarisha miongozo ya Usimamizi wa Mazingira na Jamii (*Environmental and Social Management Framework*) pamoja na *Resettlement Policy Framework* yalikamilika na kuridhiwa na Benki ya Dunia. Aidha, makubaliano ya mkopo kati ya Serikali na Benki ya Dunia, yalikamilika. Mradi una malengo makuu matatu: kuboresha manufaa yatokanayo na rasilimali ya madini; kuboresha uwezo wa usimamizi wa sekta na utawala bora; na kuvutia uwekezaji katika sekta ya madini. Aidha, Serikali kuitia Mradi huu, imeandaa programu ya kuwawezesha wachimbaji wadogo kwa kuwafundisha mbinu za ujasiriamali na mikakati ya kupata fedha kutoka mifuko ya maendeleo. Vilevile, wachimbaji wadogo watashindanishwa katika utayarishaji na uendeshaji wa miradi ya uchimbaji mdogo ambayo itafadhiliwa chini ya Mradi huu.

Mheshimiwa Spika, utafutaji na uchimbaji wa Urani Nchini. Shughuli za utafutaji wa madini ya urani nchini zimeendelea kuimarika ambapo kati ya kampuni 20 zenye leseni za utafutaji, kampuni mbili za Mantra Tanzania Limited na Uranex Tanzania Limited zipo katika hatua za juu za utafutaji. Kampuni ya Mantra Tanzania Limited ya Australia inafanya utafutaji wa madini ya urani katika eneo la mto Mkusu, Wilaya ya Namtumbo. Taarifa za utafiti wa kijiolojia hadi mwezi Januari, 2009 zinaonesha kuwepo kwa mashapo ya urani ya tani milioni 39.9 yenye takriban ratili milioni 35.9 za urani. Kampuni ya Mantra Tanzania Limited inatarajia kuanza kuchimba madini ya urani ifikapo mwaka 2012. Aidha, Kampuni ya Uranex Tanzania Limited ya Australia inafanya utafutaji wa urani Wilayani Manyoni ambapo taarifa za utafiti zinaonesha kuwepo kwa mashapo ya tani milioni 14 yenye ratili milioni 6.7 za urani. Kampuni hii iko kwenye hatua ya upembuzi yakinifu wa awali ambao utakamilika mwishoni mwa mwaka 2009. Kampuni hii inatarajia kuanza kuzalisha madini hayo mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, kutokana na matumaini makubwa ya uanzishwaji wa migodi ya urani nchini, Wizara imeanza mchakato wa kutunga kanuni kwa ajili ya kusimamia shughuli za utafutaji na uchimbaji wa madini ya mionzi. Sambamba na mchakato huu, Wizara ya Nishati

na Madini, inawasiliana kwa karibu na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Tume ya Taifa ya Nguvu za Atomiki na Kampuni zinazojihusisha na utafutaji wa urani nchini ili kuwianisha kanuni za kusimamia utafutaji, uchimbaji, utunzaji, usafirishaji, biashara na uhifadhi wa madini ya mionzi. Taarifa muhimu zimekusanywa kutoka katika nchi zinazochimba madini ya urani na taasisi za ndani na nje ya nchi zinazosimamia masuala ya mionzi.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Ofisi za madini. Wizara iliendelea na mpango wa ujenzi wa ofisi za kanda za Mwanza, Mbeya na Singida ambapo viwanja vitatu na hati zake zimepatikana. Aidha, mchoro kwa ajili ya ofisi ya Singida umekamilika. Lengo ni kujenga ofisi zinazoweza kukidhi utoaji wa huduma bora kwa wateja na wadau.

Mheshimiwa Spika, migogoro ya fidia katika Sekta ya Madini. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana kutokana na kukua kwa sekta ya madini tangu mwaka 1998 kumekuwepo na migogoro kati ya wawekezaji na wananchi wanaoishi katika maeneo ya migodi. Sababu kubwa ya migogoro hiyo inatokana na fidia isiyordhisha kwa wananchi wanaofidiwa kupisha shughuli za uwekezaji mkubwa katika sekta ya madini inayotolewa kulingana na Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999. Hali hii imepelekea wananchi wengi kudai fidia zaidi kuitia vyombo vya sheria vikiwemo Mahakama na Tume ya Haki za Binadamu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutafuta suluhisho la migogoro ya fidia katika sekta ya madini kwa kutafuta ufumbuzi wa muda na wa kudumu. Ufumbuzi wa muda ni kuyashauri makampuni ya uchimbaji madini kutoa fidia na kuwa ufumbuzi wa kudumu utakaoondo tatizo hili ni marekebisho ya Sera ya Madini ya mwaka 1997 na Sheria ya Madini ya mwaka 1998 ambayo yanafanya hivi sasa na maboresho ya Sheria ya Ardhi yatakayofanywa ambayo yatawapasa wawekezaji kuwafidia na kuwapa makazi (*compensation and relocation*) bora wananchi, ikiwa ni pamoja na kuwashirikisha katika uwekezaji huo.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niliarifu Bunge lako Tukufu baadhi ya migogoro ya fidia katika sekta ya madini kama ifuatavyo: Mgogoro wa mgodi wa dhahabu wa Geita *Gold Mines Limited (GGM)* na wananchi wa vijiji vya Nyakabale, Nyamatagata na eneo la *Mine Mpya*; Mgogoro wa fidia wa mgodi wa dhahabu wa *North Mara Gold Mine (NMGM)* na wananchi wa maeneo ya Nyabigena na Nyamongo; na mgogoro wa mgodi wa dhahabu wa Buzwagi (*Pangea Minerals Limited – PML*) na wananchi wa vijiji vya Mwendakulima, Chapulwa na Mwime.

Mheshimiwa Spika, *Geita Gold Mines (GGM)*. Kwenye eneo la Mgodi wa dhahabu wa Geita, wananchi wa eneo la *Mine Mpya* kwenye Kijiji cha Mtakuja hawakufidiwa kwa sababu eneo hilo halikuwa eneo la makazi bali makambi madogo madogo ya kusafishia dhahabu kutoka mabaki ya mgodi wa zamani na walitakiwa kuacha shughuli hizo na kuondoka. Wananchi katika kaya zipatazo tano waliokuwa wanatumia eneo hilo kuchenjua dhahabu walikataa kuondoka sehemu hiyo na kupeleka shauri mahakamani. Uamuzi ultolewa na Mahakama Kuu kuwa wananchi hao hawakuwa na haki kisheria na waliondolewa kwenye eneo hilo kwa amri ya mahakama na kuwekwa kwenye jengo la mahakama mjini Geita ili wapate makazi mapya kwenye eneo lililokuwa limetengwa na Uongozi wa Wilaya ya Geita. Wananchi hao walikataa kuhamia eneo walilotengewa na kuendelea kukaa katika jengo la mahakama. Ili kutatua mgogoro huo, mwaka 2008, Halmashauri ya Wilaya ya Geita ilitenga tena eneo la makazi katika kijiji cha Mpomvu, kata ya Mtakuja na kupima viwanja 56 kwa ajili ya wananchi hao na wananchi hao wameshauriwa kuhamia eneo hilo la makazi.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la Nyamatagata walikuwepo wananchi 111 waliokuwa wanadai fidia. Hata hivyo wananchi 39 walitathminiwa na kulipwa na kubakia wananchi 72. Kwa mpango wa uchimbaji wa dhahabu katika mgodi wa Geita eneo hilo halihitajiki kwa sasa. Serikali inawasiliana na uongozi wa mgodi ili wananchi hawa wafidiwe na kuhamishwa sasa badala ya kusubiri hapo baadae kwa vile wananchi hawa wanashindwa kuendeleza ujenzi wa makazi ya kudumu kwa sababu hawafahamu hatima yao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mgogoro kati ya wananchi 23 wa kijiji cha Katoma na Mgodi wa dhahabu wa Geita, tarehe 23 Machi, 2007 Serikali iliwashauri wananchi hao waliokuwa wamefungua kesi mahakamani kuifuta na mazungumzo ya fidia yakafanyika ambapo wananchi 13 wameshafanyiwa tathmini na wananchi 10 bado wanaendelea na mazungumzo na uongozi wa mgodi ili tathmini ifanyike walipwe haki yao.

Mheshimiwa Spika, *North Mara Gold Mine*. Mgogoro wa fidia kati ya wananchi wa maeneo ya Nyamongo na Nyabigena na mgodi wa *North Mara* katika Wilaya ya Tarime umesababisha hali ya kutolewana kati ya wananchi na mgodi huo. Sehemu kubwa ya mgogoro huo inatokana na historia ya makubaliano kati ya kampuni ya awali ya Afrika Mashariki *Gold Mine* na Serikali za Vijiji na wananchi mbalimbali tangu mwaka 1999. Kampuni ya *Placer Dome* iliyoingia mwaka 2005 na kuondoka mwaka 2006 na kampuni ya *Barrick Gold Corporation* iliyoanza mwaka 2006 hadi leo zimerithi hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, kampuni ya Barrick, mmiliki wa sasa wa mgodi wa North Mara iliendolea kutathmini maeneo ya wananchi na kuwafidia ikiwa ni pamoja na kuwajengea nyumba. Baadhi ya wananchi wamekubali kufidiwa na kuhamia lakini baadhi wamekataa tathmini au malipo ya tathimini na kuendelea kuishi kwenye maeneo yaliyokaribu sana na shughuli za uchimbaji.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa, kuna jumla ya maeneo 157 yanayomilikiwa na wananchi mbalimbali ndani ya eneo linalohitajika kwa shughuli za uchimbaji kufanyika kwa usalama. Kati ya maeneo hayo, maeneo 99 yamefanyiwa tathmini na wenyewe maeneo wamelipwa fidia. Maeneo 58 yamefanyiwa tathmini lakini wenyewe maeneo walikataa kulipwa fidia, na kati yao 43 walifunga kesi kwenye Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Licha ya kwamba uamuzi wa kesi hiyo ulikwishatolewa na kuthibitisha kwamba tathmini iliyofanyika ni sahihi na wananchi hao kutakiwa kuchukua fidia, bado wananchi hao hawajakubali kupokea fidia hadi hivi sasa hali ambayo inajenga mazingira ya uhasama.

Mheshimiwa Spika, katika kutafuta suluhisho la uhusiano mbaya kati ya wananchi na mgodi, Kamati ya Uhusiano mwema ilianzishwa mwaka 2007. Kamati hiyo ina majukumu ya kushughulikia fidia na mahusiano kati ya wanaoathirika na shughuli za mgodi, kutafuta njia za kuimarisha mahusiano na kuingiza mipango ya maendeleo ya jamii katika mipango ya baadae ya kampuni. Kamati hiyo ina wajumbe kutoka vijiji 13 vilivyoko ndani ya eneo la mgodi, viongozi wa kata 5 na vijiji vinavyozunguka mgodi, na uongozi wa mgodi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo kwa Kamati hiyo kuendelea kuwepo kwa matukio ya uvamizi wa mgodi wa mara kwa mara yamedhoofisha utendaji wa kamati. Serikali pia imepeleka askari Kikosi cha Kutuliza Ghasia (FFU) kushiriki katika kuimarisha ulinzi katika eneo hilo. Pamoja na ulinzi huo kumekuwepo na matukio mengi ya uvamizi na mara nyingine kusababisha vifo. Hali hii, imezidisha malalamiko kutoka pande zote zinazohusika yaani wananchi na uongozi wa mgodi. Serikali inaendelea kuchukua hatua zinazostahili kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, tarehe 4 Mei, 2009, kuliripotiwa uchafuzi wa mazingira katika mgodi wa North Mara, ambapo maji yenyе tindikali yalivuja kutoka kwenye miamba yenyе madini ya salfa na kutiririka hadi mto Tigithe. Serikali ilichukua hatua za kisheria kuiagiza kampuni hiyo kuzuia na kusafisha mazingira hayo. Aidha, Serikali imechukua hatua za kuwapima wananchi, maji na wanyama katika eneo hilo ili kujiridhisha kama madhara hayo yanatokana na athari za uchafuzi wa mazingira na kuchukua hatua stahili dhidi ya mgodi huo. Serikali itatoa tamko rasmi bungeni kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Spika, Buzwagi Gold Mine. Ulipaji fidia ya ardhi, nyumba, mazao na mali nyinginezo ulianza mwezi Aprili 2007 chini ya usimamizi wa Kamati Shirikishi ya Makazi Mbadala ambayo iliundwa mwezi Novemba, 2005 ikiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kahama. Jumla ya watu 550 walistahili kulipwa fidia kwa mchanganuo wa: Kijiji cha Mwime watu 168; Kijiji cha Mwendakulima 220; na Kijiji cha Chapulwa watu 162. Aidha, kaya 207 kati ya hizo ni za wananchi waliomiliki nyumba na 333 ni za wananchi waliomiliki ardhi na mali nyinginezo ndani ya eneo la mradi. Katika zoezi hili nyumba 207 zilijengwa na kukabidhiwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kazi ya uthamini ilifanya kwa mara ya kwanza na jumla ya shilingi 2,464,868,367.06 zililipwa kutokana na tathmini hiyo. Hata hivyo, kulijitokeza malalamiko mbalimbali kutoka kwa wananchi kuhusiana na jinsi uthamini huo ulivyofanyika. Ili kutatua tatizo hilo Kampuni ya Pangea Minerals ilifanya tathmini ya awamu ya pili. Katika tathmini hiyo jumla ya shilingi 804,684,577.00 za ziada zililipwa kwa wananchi waliokuwa wamepunjwa. Malalamiko yaliendelea na hatimaye tathmini ya awamu ya tatu ilifanyika na fidia ya nyongeza ya shilingi 980,792,588.55 ililipwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na tathmini hizo kufanyika ili kusahihisha makosa yaliyotokana na tathmini ya kwanza, ya pili na ya tatu bado malalamiko ya wananchi yaliendelea kuwepo kuhusu malipo hayo ya fidia. Kutokana na hali hii, Serikali ilichukua hatua ya kufufua kamati ya Makazi Mbadala ili ipitie tena madodoso ya tathmini kubaini upungufu uliopo. Kamati hiyo, ilifanya kazi yake kuanzia mwezi Juni, 2008 na kukamilisha kazi hiyo mwezi Januari, 2009. Katika matokeo ya kazi hiyo, jumla ya shilingi 285,782,511.99 zililipwa kwa wananchi 45. Pamoja na kazi hiyo kukamilika, wananchi watano walikataa kulipwa fidia hii kwa vile hawajaridhika. Serikali inaendelea kushughulikia suala hili ili kumaliza kabisa mgogoro huu.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Jiolojia Tanzania – GST. Katika mwaka 2008/2009, Wakala wa Jiolojia Tanzania ilifanya kazi zifuatazo: shughuli za ugani katika QDS 137, 138 na 139 kwenye eneo la Sikunge- Tabora; kuweka kwenye mfumo wa kompyuta ramani 17 za aina hiyo katika ukanda wa Mtwara; kuchapisha ramani za kijiolojia na kijokemia za QDS 123 eneo la Kwamtoro, QDSs 155, 156 na 157 eneo la Sikunge; kukamilisha ramani maalumu tatu (ramani za jiolojia na uwepo wa madini Mkoani Tanga, na maeneo ya Nachingwea na Liganga); kuchapisha kitabu chenye maelezo ya upatikanaji wa mawe ya nakshi (dimension stones) ubora wake kwenye Mikoa ya Singida na Dodoma; kutoa mafunzo kwa wachimbaji wadogo wa Nzuguni, Londoni, Sambaru kuhusu namna bora ya uchenjuaji dhahabu; kufanya utafiti wa kubaini uwepo wa chuma (Liganga) na mashapo ya makaa ya mawe (Mbuyura). Aidha, katika kujenga uwezo wake wa kitaalamu, jumla ya watumishi 18 walipelekwa mafunzo, kati ya hao watumishi 10 walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na 8 ya muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Madini. Jumla ya wanafunzi 209 walihudhuria mafunzo katika Chuo cha Madini, ambapo wanafunzi 82 walikuwa ni wa mwaka wa kwanza,

63 wa mwaka wa Pili na 64 wa mwaka wa tatu. Katika mwaka 2008/09, Chuo kiliendelea kutoa mafunzo ya ufundi sanifu sekta ya madini kwa ngazi za vyeti na stashahada, ambapo mwezi Mei, 2009 wanafunzi 64 walifanya mitihani ya kuhitimu katika ngazi ya stashahada. Aidha, Chuo kinaendelea na mpango wa uandaaji wa mitaala ya mafundi sanifu wa fani za Jiomolojia na Jiolojia ya mafuta (*Petroleum geology*) ili kukidhi mahitaji ya mafundi sanifu sekta ya fani hizo, na kupanua wigo wa mafunzo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Chuo kiliendelea na ujenzi wa miundombinu ya maktaba, maabara, zahanati, nyumba za watumishi, karakana na viwanja vya michezo. Miundombinu hii ipo sekta ya hatua za mwisho kukamilika. Mpango wa Kujiunga na Asasi ya Uwazi sekta ya Tasnia ya Uziduaji (*Extractive Industries Transparency Initiatives – EITI*).

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba tarehe 16 Februari, 2009, Tanzania ilijiunga rasmi na Asasi ya Uwazi sekta ya Tasnia ya Uziduaji (EITI) na kupata uanachama wa awali (*candidate status*). Lengo kuu la Asasi hii ni kuhamasisha na kusimamia uwazi na uwajibikaji sekta ya mapato na matumizi ya rasilimali za madini, mafuta na gesi asili ambazo huvunwa kutoka chini ya ardhi ili kuleta maendeleo endelevu kwa nchi zenyne rasilimali hizo. Manufaa muhimu ya utekelezaji wa EITI ni pamoja na kuonesha msimamo wa Taifa kwenye Mkakati wa uwazi; ufanisi sekta ukusanyaji wa mapato; ushirikiano sekta kuongeza uwajibikaji kwa umma baina ya Serikali, kampuni na vyama visivyokuwa vya kiserikali; na kupunguza athari kwa uwekezaji. Hadi sasa Asasi hii ina nchi wanachama 30, kampuni 41 na taasisi za uwekezaji 80.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Madini la Taifa – STAMICO. Mwezi Julai, 2008, Serikali iliondoa STAMICO kutoka kwenye orodha ya mashirika ya umma ya kubinafsishwa, ili itumike kuwekeza sekta ya madini kwa niaba ya Taifa na sekta kuwasaidia wachimbaji wadogo. Uamuza huo ultangazwa sekta Gazeti la Serikali mwezi Aprili, 2009. Mchakato wa kuainisha majukumu mapya umeanza ili sheria iliyoanzisha Shirika irekebishwe.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/09, kazi ya uchorongaji miamba ndiyo ilikuwa chanzo kikuu cha mapato ya Shirika. Kazi hii ilifanyika kwa ushindani na kampuni binafsi za kigeni. STAMICO ilikodiwa kufanya kazi ya uchorongaji sekta maeneo matatu ya: Saza Wilayani Chunya (mita 1,500); Machole, Lindi (mita 550); na Kimbiji Wilayani Temeke (mita 1,550).

Mheshimiwa Spika, *Southern And Eastern African Mineral Centre – SEAMIC*. Kituo cha utafiti na uendelezaji wa sekta ya madini (SEAMIC) kilichopo Kunduchi, Dar es Salaam, kinachomilikiwa na nchi saba (7) wanachama ambazo ni Tanzania, Uganda, Kenya, Ethiopia, Comoro, Angola na Msambiji, kimeendelea kutoa huduma za kitaalamu na mafunzo sekta binafsi kwenye shughuli za madini sekta ya nchi wanachama. Kituo kinatoa mafunzo na huduma za kitaalamu sekta ya madini sekta ya nchi wanachama na sekta binafsi inayowekeza sekta ya madini.

Mheshimiwa Spika, ajira na maendeleo ya Watumishi. Katika kujenga uwezo wa utendaji wa Wizara, mwaka 2008/09 watumishi wapya 40 wa kada mbalimbali walijiriwa. Jumla ya watumishi 118 walipandishwa vyeo, kati yao, watumishi 101 walipandishwa mwaka 2007/2008 na 17 mwaka 2008/09. Aidha, uwezo wa utendaji kazi wa watumishi uliendelea kuimarishwa, ambapo watumishi 101 walipelekwa mafunzioni. Kati yao, watumishi 74 walishiriki mafunzo ya muda mfupi na 27 mafunzo ya muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha mfumo wa utoaji huduma kwa wateja na wadau, Wizara ilikamilisha maandalizi na itazindua rasmi Mkataba wa Huduma kwa Mteja (*Client Service Charter*) tarehe 08 Agosti, 2009. Aidha, Mfumo wa Mapitio na Upimaji wa Utendaji Kazi wa Wazi (OPRAS) kwa watumishi uliendelea kutekelezwa ambapo watumishi 118 walipatiwa mafunzo.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeandaa Mkakati wa Mawasiliano wa miaka mitatu (2009/2010 - 2011/2012). Lengo kuu ni kuhakikisha wadau na umma wa Watanzania unapata taarifa na takwimu sahihi na kwa wakati zinazohusu sekta za nishati na madini ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa za utekelezaji wa miradi mbalimbali ya sekta hizo ambayo inalenga kuwaletaa maisha bora Watanzania.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara imeendelea kutoa huduma ya mlo kamili, malipo ya dawa zilizo nje ya orodha ya Bima ya Afya kwa watumishi wanaoishi na virusi vya UKIMWI, ikiwa ni utekelezaji wa Waraka wa Watumishi wa Umma Namba 2 wa Mwaka 2006 na Mwongozo wa Kudhibiti UKIMWI Katika Utumishi wa Umma wa Mwaka 2007; kutoa mafunzo kwa viongozi wa juu wa Wizara kuhusu wajibu wao katika kusimamia Utekelezaji wa Programu ya UKIMWI Mahala pa Kazi; na Usambazaji wa kondomu za kiume na za kike kwa ajili ya kinga dhidi ya maambukizi mapya.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2009/2010, utazingatia: Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; MKUKUTA; Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005; Malengo ya Maendeleo ya Milenia; Ahadi za Serikali Bungeni za Mwaka 2008/09; Mwongozo wa Kutayarisha Mpango na Bajeti 2009/10 – 2011/12; Maagizo ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Nishati. Ili kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, MKUKUTA, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005 pamoja na malengo mingine ya kitaifa, kazi zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka 2009/10 ni: kukamilisha miradi ya upelekaji umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya ambazo hazijapata umeme; kuimarishe Wakala na Mfuko wa Nishati Vijijini; kuimarishe mifumo ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme; kuboresha na kukanabati njia za umeme na vituo vya kupozea umeme katika gridi ya Taifa; kupanua mitambo ya kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asili ya Songo Songo; kuunganisha gridi ya Taifa na za nchi jirani; kuvutia uwekezaji katika utafutaji wa mafuta; kushiriki katika mikataba ya uzalishaji (*Production Sharing Agreements*) kwa miradi ya Songo Songo na Mnazi Bay; kushiriki katika miradi ya uwekezaji na usambazaji wa gesi asili; na kuanzisha hifadhi ya bidhaa za mafuta ya petroli.

Mheshimiwa Spika, kupeleka umeme Makao Makuu ya Wilaya. Serikali kuitia Wakala wa Nishati Vijijini na TANESCO itaendelea kutekeleza miradi ya kupeleka umeme Makao Makuu ya Wilaya zilizobaki, ikiwa ni utekelezaji wa Ibara ya 43(b) ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005 kuhakikisha kuwa Makao Makuu ya Wilaya zote zisizo na umeme yanapatiwa umeme. Katika Mpango wa 2009/10, Wilaya zitakazohusika ni pamoja na Kasulu, Kibondo, Ngorongoro na Nkasi.

Mheshimiwa Spika, usambazaji umeme Vijijini. TANESCO itaendelea kukamilisha miradi mingine ya umeme vijijini iliyofadhiliwa na Serikali na kwa kuitia Mfuko wa Nishati Vijijini. Aidha, katika Mwaka 2009/2010, Wakala wa Nishati Vijijini kuitia mradi wa Utafiti wa Nishati na tabianchi (*Energy and Climate Research*), utahamasisha matumizi sahihi ya

nishati bora vijijini. Mradi unalenga kuboresha vyanzo vya nishati endelevu kwa shughuli za kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, Wakala utaendelea na mpango wa kujenga uwezo wake na wadau kwa msaada wa Sida. Aidha, Serikali ya Norwe itagharimia upembuzi yakinifu wa vyanzo vya umeme katika maporomoko ya mito ya Mtambo na Nzovwe (Rukwa), Pinyinyi (Arusha) na Kvitanda (Ruvuma).

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Serikali itaendelea kutekeleza miradi mitatu kwa msaada wa *MCC* ambayo ni: kufua umeme wa nguvu za maji wa mto Malagarasi MW 8 na kusambaza katika miji ya Uvinza, Kigoma na Kasulu; kuimarisha na kupanua usambazaji umeme katika Mikoa ya Mwanza, Tanga, Dodoma, Morogoro, Iringa na Mbeya; na kujenga *submarine cable* kutoka Dar es Salaam hadi Unguja. Kazi zitakazofanyika mwaka 2009/2010 kwa miradi yote mitatu ni kutayarisha zabuni za ujenzi, kuajiri makandarasi na kuanza ujenzi wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, upanuzi wa njia za kusafirisha umeme gridi ya Kaskazini - Magharibi itaendelea kupanuliwa. Mgodi wa North Mara unatarajiwa kuunganishwa kwenye gridi ya Taifa mwaka 2010, sanjari na maandalizi ya utekelezaji wa mradi wa kuimarisha njia kuu ya kusafirisha umeme ya Iringa kuititia Dodoma, Singida hadi Shinyanga katika msongo wa kilovoti 650. Ujenzi wa mradi utagharimu takriban Euro milioni 520. Mradi huu unalenga katika kuongeza uwezo wa usafirishaji wa umeme katika gridi ya Taifa na kuongeza uhakika na ubora wa umeme huo.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa mradi wa *TEDAP* katika Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha na Kilimanjaro. Mradi unahusu ukarabati na uimarishaji wa mifumo ya umeme ili kutimiza azma yake ya kuwapatia wananchi nishati ya uhakika pamoja na kuongeza kasi ya kuwapatia umeme waishio maeneo ya mijini na vijijini, kulingana na malengo ya MKUKUTA. Aidha, utawezesha utekelezaji wa miradi midogo ya kuzalisha umeme iliyoibuliwa; kuchangia ufungaji wa mitambo ya umeme wa jua katika Mkoaa wa Rukwa chini ya *Sustainable Solar Market Packages (SSMP)* awamu ya kwanza na kupatia umemenuru Mikoa ya Mtwara, Ruvuma, Mbeya na Shinyanga kwa utaratibu wa *Commercialized Solar Cluster Approach (CSCA)*.

Mheshimiwa Spika, miradi ya kufua umeme Dar es Salaam MW 100, Mwanza MW 60 Serikali, itajenga mtambo wa MW 100 Ubungo II Jijini Dar es Salaam, utakaotumia gesi asili na mtambo wa MW 60 jijini Mwanza utakaotumia mafuta mazito (*Heavy Fuel Oil*). Miradi hii itafidia nakisi ya uzalishaji wa umeme uliopo katika gridi ya Taifa. Pia, kukamilika kwa mradi wa MW 60 Mwanza kutaboresha mfumo wa umeme katika gridi ya Kaskazini Magharibi, ambayo imeelemewa kutohana na migodi mingi iliyopo katika kanda hiyo inayotumia umeme mwingu. Miradi hii inatarajiwa kukamilika 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, mradi wa kufua umeme Kiwira MW 200. Mradi wa umeme wa Kiwira uliorithiwa na Serikali mwaka 2006, ulikuwa utekelezwe kuititia sekta binafsi. Uendelezaji wa mradi huu umekwama kutohana na kutokamilika kwa makubaliano ya mkopo wa fedha za utekelezaji (kutofikiwa kwa *financial closure*). Serikali imejiandaa kuukwamua mradi huu ili uanzse kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, mradi wa kufua umeme Kinyerezi MW 240. Serikali inakamilisha matayarisho ya zabuni na mradi huu utatekelezwa kwa utaratibu wa kushirikisha

sekte binafsi (*Public Private Partnership - PPP*). Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, mradi wa kufua umeme wa *IPT*. Ni matarajio yetu kwamba, mgogoro wa kisheria kati ya *TANESCO* na *IPTL*, utamalizika ndani ya mwaka huu wa fedha, hivyo kuanza kuitumia tena mitambo ya *IPTL* kuzalisha umeme wa MW 100 na kuunganishwa kwenye gridi. Aidha, mitambo hiyo inatarajiwa kuanza kutumia gesi asili.

Mheshimiwa Spika, miradi midogo ya MW 40. Miradi mingine midogo ya *TPCL*, *TANWAT*, *Mafia*, *Sao HILL Saw Mill*, Maporomoko ya maji ya Mwega - Mufindi, Kilocha – Njombe, Tosamaganga na Kitonga– Iringa, Mbalizi – Mbeya na Kikuletwa – Moshi yenye jumla ya MW 40 itaendelea kuzalisha umeme kuchangia kwenye gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa *electricity V*. Mradi huu unahusu ujenzi wa njia mbalimbali za umeme za msongo wa kilovoti 33 na 11, ikiwa ni pamoja na ufungwaji wa transfoma mpya kwenye maeneo mbalimbali katika Mikoa ya Mwanza na Shinyanga. Aidha, ukarabati utafanyika kwenye njia za usambazaji umeme za msongo wa kilovoti 33 na 11 pamoja na vituo vikubwa vya umeme kwenye Mikoa ya Dar es Salaam na Arusha.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Makambako – Songea. Katika mwaka wa 2009/2010, Serikali itaendelea na utekelezaji wa mradi wa kupoletka umeme wa gridi ya Taifa katika miji ya Makambako, Njombe, Songea, Namtumbo, Ludewa na Mbinga. Mradi huu umelenga kufikisha umeme wa uhakika katika Mikoa ya Iringa na Ruvuma, kuongeza ufanisi kwenye shughuli za maendeleo na kupunguza gharama za uendeshaji wa jenereta za dizeli, ambazo zinatumia fedha nyingi za kigeni kununulia mafuta na vipuri katika miji ya Songea, Mbinga na Ludewa. Kazi zitakazofanyika mwaka 2009/10 ni: kuandaa zabuni za kujenga njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 132 ya urefu wa kilometa 250 toka Makambako hadi Songea; vituo vya kupozea umeme vya kilovoti 132/33 vya Madaba na Songea; ujenzi wa njia za usafirishaji na usambazaji za msongo wa kilovoti 33 zenyen urefu wa kilometa 900 kwenye miji na vijiji vya Wilaya za Mikoa ya Iringa na Ruvuma; kuwateua wazabuni watakaojenga njia za kilovoti 132, kilovoti 33 na kuunganisha wateja zaidi ya 6,800; kufanya tathmini ya mazingira na jamii; na kuanza ujenzi wa mradi. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa umeme - Somanga Fungu. Katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Serikali itakamilisha sehemu ya mradi iliyobaki ikiwa ni pamoja na ufungaji wa mitambo, mashine ya kupunguza mgandamizo wa hewa (*pressure reduction valve*), mabomba ya kuitishia gesi, ujenzi wa njia ya umeme wa kilovoti 33 na 11 kwa maeneo yaliyobaki yenye jumla ya kilometra 40 ikiwemo Ikwiriri-Kibiti, Nyamwage-Muhoro na Muhoro-Somanga. Aidha, cable ya umeme itapitishwa kwenye Daraja la Mkapa la Mto Rufiji na kufanya majaribio ili hatimaye kuanza kuzalisha umeme. Umeme huu utasambazwa maeneo ya Kilwa Masoko, Kilwa Kivinje, Nangurukuru, Tingi, Njianne, Somanga Ndumbo, Mohoro, Nyamwage, Kindwitwi, Utete, Ikwiriri, Kibiti, Kibiti Sekondari, Hospitali ya Misheni ya Mchukwi na Bungu.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Ruhudji MW 358. Upembuzi yakinifu wa mradi wa maporomoko ya maji ya Ruhudji, ulikamilika mwaka 1998. Wizara iko katika hatua za kuajiri mtaalamu mshauri (*transaction advisor*) atakayeshauri Kamati ya Majadiliano ya Serikali (*Government Negotiation Team*) katika majadiliano na mwekezaji binafsi wa mradi (*Nordic Group*) ili kufikia hatua ya makubaliano ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, *Stiegler's Gorge*. Mradi huu ni kati ya miradi mikubwa iliyoinishwa katika mpango kabambe wa kuendeleza sekta ya umeme, wenyewe uwezo wa kuzalisha hadi MW 2100. Serikali itatumia ushauri uliotolewa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuielekeza RUBADA njia muafaka ya kuendeleza mradi huo bila kuchelewa.

Mheshimiwa Spika, kuunganisha Gridi ya Taifa na nchi jirani. Wizara inaendelea na mchakato wa kuunganisha gridi ya Taifa na za Zambia na Kenya kwa lengo la kuuza na kununua umeme katika nchi hizo. Mradi huu ni muhimu kama ulivyoainishwa katika Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta ya Umeme Nchini (PSMP 2009).

Mheshimiwa Spika, Nishati Jadidifu na Mbadala. Miradi ya nishati mbadala katika kipindi cha mwaka 2009/2010, itatekelezwa kwa kuendeleza teknolojia za matumizi bora ya viwaa (*fuels*) muafaka kwa ajili ya kupikia, kutoa mwanga, kuendeleza na kukuza teknolojia za matumizi bora ya nishati na kulinda mazingira. Matumizi bora ya nishati ni moja ya njia za kupunguza gharama ya upatikanaji wa huduma za nishati na pia kuongeza uhakika wa upatikanaji endelevu wa nishati.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya nishati mbadala kama gesi asili na biofueli yanasaidia kupunguza uchafuzi wa mazingira. Wizara itaendelea kuandaa sera, sheria, kanuni na muundo wa kitaasisi kuhusu uendelezaji endelevu wa biofueli. Aidha, Wizara inalenga kuendeleza vyanzo jadidifu vya nishati ya upepo, jotoardhi (*geothermal*) na maporomoko madogo ya maji. Pia, teknolojia ya vitofali (*briquettes*) vitokanavyo na makaa ya mawe na tungamotaka (*biomass*) itaendelezwa kama nishati mbadala wa kuni na mkaa.

Mheshimiwa Spika, matumizi bora ya Nishati (*Demand Side Management*). Mkakati wa kupunguza matumizi ya umeme (*demand side management strategy*) majumbani na viwandani kwa lengo la kupunguza mahitaji ya juu ya umeme kwa zaidi ya asilimia 20 sawa na MW 120 unaendelea kutekelezwa kwa Wizara kushirikiana na TANESCO. Hatua itaruhusu umeme wa ziada kupatikana kwa matumizi mengine pasipo ulazima wa kujenga mitambo mipya. Uzoefu uliopo unaonesha kwamba uwekezaji katika kuzalisha umeme wa MW1 (kutokana na gesi au maji) ni zaidi ya Dola za Marekani milioni 1.8. Uzoefu uliopo unaonesha kwamba ni rahisi kuokoa MW 1 kuliko kuzalisha kiasi hicho.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuchangia katika kulinda mazingira, matumizi bora ya umeme yatapunguza kiwango cha ankara, ambacho mteja angelazimika kulipa kwa huduma hiyo hiyo. Jitihada za kuhimiza matumizi ya vifaa vinavyotumia umeme kwa ufanisi (*energy efficient appliances*) zimeanza, zikiwemo taa za *compact fluorescent lights* badala ya *inacandescent bulbs*; mota na majokofu yenye ubora stahiki. Taratibu za kumpata mshauri wa kutayarisha programu ya kuokoa nishati na kupunguza matumizi ya umeme katika sekta mbalimbali zimeshaanza, na inategemewa kwamba ataanza kazi mwezi Oktoba, 2009.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Kiwanda cha Kusafisha Mafuta Ghafi na Bomba la Mafuta la Dar es Salaam – Mwanza. Katika mwaka 2009/2010, Kampuni ya *Noor Oil Industrial Technology* (NOIT), inatarajia kukamilisha yafuatayo: upatikanaji wa eneo la kujenga kiwanda; upembuzi yakinifu ukihuisha masuala ya mazingira; mahusiano na wanahisa wenza; na kuthibitisha uwezo wa kifedha na mpango wa utekelezaji wa miradi kwa kuainisha kazi zitakazofanyika mwaka 2009/10 hadi kukamilika kwa miradi. Kutokana na umuhimu wa miradi hii kwa Taifa, Wizara itaendelea kusimamia utekelezaji wa makubaliano yaliyoko kwenye mikataba kati ya Serikali na NOIT.

Mheshimiwa Spika, utafutaji mafuta na gesi asili. Katika mwaka 2009/2010, Wizara inatarajia kukamilisha majadiliano ya mikataba sita ya Utafutaji na Uzalishaji wa Mafuta (PSAs) na kampuni za: Tullow Oil ya Ireland katika eneo la Ziwa Tanganyika Kaskazini; Beach Petroleum ya Australia katika eneo la Ziwa Tanganyika Kusini; Petrobras ya Brazil katika Kitalu Na. 8 kwenye maji ya kina kirefu cha Bahari ya Hindi; Motherland Industries ya India katika eneo la Malagarasi; na Tower Resources ya Uingereza katika bonde la Wembere-Ziwa Eyasi, Manyara hadi Natron. Aidha, Wizara itakamilisha Rasimu ya Muswada wa Sheria ya Gesi Asili kwa kuzingatia maoni ya pande mbili za Muungano.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kusimamia kampuni za utafutaji mafuta ili zitekeleze mipango ya kazi ya utafutaji ikiwemo kukusanya takwimu za kijiolojia na kijiofizikia na kufanya tathmini ya takwimu hizo ili kubaini maeneo ya kuchoronga visima kwa ajili ya utafutaji mafuta. Aidha, kwa kushirikiana na Wizara inayohusika na masuala ya nishati ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, itapitia na kuchambua taarifa ya Mshauri Mwelekezi kuhusu utafutaji na mgawanyo wa gharama na mapato yatokanayo na mafuta na gesi asili na kupendekeza hatua muafaka.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji katika miradi ya Songo Songo na Mnazi Bay. Serikali itaendeleza jitihada za kutafuta wawekezaji ili kujenga mitambo mingine miwili ya kusafisha gesi asili ya SongoSongo na kujenga bomba lingine sambamba na bomba la gesi lililopo. Upanuzi wa mitambo ya kusafisha gesi asili ya SongoSongo utawezesha kuwepo gesi ya kutosha na hivyo kukidhi mahitaji ya mitambo ya kuzalisha umeme na matumizi mengine. Aidha, *EWURA* ilipitisha ombi la kampuni ya Songas juu ya kupanua miundombinu ya kusafisha gesi asili kisiwani SongoSongo, kutoka kiwango cha futi za ujazo milioni 70 kwa siku na kufikia futi za ujazo milioni 140 kwa siku. Songas wapo kwenye maandalizi ya utekelezaji. Mradi huu utakapoanza utachukua miezi 18 kukamilika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Serikali imepanga kuiwezesha *TPDC* kushiriki katika miradi ya SongoSongo na Mnazi Bay. Lengo ni kuiwezesha *TPDC* kuchangia gharama za uendelezaji miradi ya gesi ya SongoSongo na Mnazi Bay, ukiwemo uchorongaji visima, ujenzi wa mabomba ya ukusanyaji gesi asili na upanuzi wa mitambo ya usafishaji gesi asili. Matarajio ni kuongeza mgawo wa mapato kwa Serikali. Aidha, *TPDC* itapata mrejesho wa gharama za uendelezaji kulingana na kiasi kitakachowekezwa.

Mheshimiwa Spika, *TPDC* kwa kushirikiana na *Pan African Energy* inatekeleza awamu ya kwanza ya mradi wa usambazaji gesi asili iliyoshindiliwa (*Compressed Natural Gas - CNG*), uliozinduliwa tarehe 14 Julai, 2009 eneo la Ubungo-Maziwa, Dar es Salaam. Awamu hii itagharimu Dola za Marekani milioni tatu na itahusisha ujenzi wa vituo viwili vya kujazia gesi asili kwenye magari 200 katika Jiji la Dar es Salaam. Gesi asili pia itapelekwa katika magereza ya Keko na Ukonga, hoteli kubwa za Southern Sun, Holiday Inn, Kempiski na Movenpick, JKT Mgulani, Hospitali ya Taifa Muhimbili na nyumba 70 eneo la Mikocheni.

Mheshimiwa Spika, awamu ya pili ya mradi itagharimu Dola za Marekani milioni 32, na itahusisha kutandika mabomba ya kusafirisha gesi asili Dar es Salaam kwa kuweka bomba kuu la urefu wa kilometra 45 na mtandao wa kupeleka gesi asili katika nyumba 30,000 wenyе urefu wa kilometra 20. Aidha, magari 8,000 yatabadilishwa ili yatumie gesi asili. Faida zinazotokana na matumizi ya gesi asili ni pamoja na kuokolewa kwa takriban shilingi bilioni 150 kwa mwaka, ambazo zingetumika kununulia kuni, mkaa na petroli kwenye magari, kupunguza kasi ya uharibifu wa misitu na uchafuzi wa mazingira. Manufaa mengine ni pamoja na kupunguza kwa kiasi kikubwa uharibifu wa misitu na mazingira unaotokana na kukata miti kwa ajili ya kuni na mkaa (kwa mfano, jiji la Dar es Salaam pekee kwa sasa linakadirwa

kutumia kiasi cha magunia 30,000 ya mkaa kwa siku). Mradi huu utapunguza kiasi hicho cha matumizi ya mkaa kwa siku hadi chini ya magunia 15,000.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendeleza mazungumzo na kampuni kutoka China kwa lengo la kuingia ubia katika kuendeleza miradi ya gesi asili ili iweze kutumika majumbani, kwenye taasisi na kwenye magari kama mbadala wa mafuta. Mkakati huu utapunguza matumizi ya kuni na mkaa na hivyo kuchangia katika kupunguza kasi ya ukataji miti kama ilivyolekezwa katika Ibara ya 43(i) ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, *TPDC* kwa kushirikiana na wawekezaji kutoka nje ya nchi itaanza kufanya utafiti ili kubaini uwezekano wa kuanzisha mradi wa usambazaji gesi asili ya mabomba (*Piped natural gas – PNG*) na iliyoshindiliwa (*compressed natural gas-CNG*) kutoka Mnazi Bay kwa matumizi katika magari, taasisi na majumbani kwa Mikoa ya Mtwara na Lindi.

Mheshimiwa Spika, sekta ya madini. Mipango ya sekta ya madini kwa mwaka 2009/2010, ni pamoja na: kukamilisha marekebisho ya Sheria ya Madini ya mwaka 1998; kuendeleza majadiliano na kampuni kubwa za madini zenyenikata baati na Serikali; kuimarishe ukaguzi wa gharama za uwekezaji na uendeshaji wa migodi mikubwa; kuimarishe ukaguzi wa usalama, afya na utunzaji wa mazingira migodini; kuanza utekelezaji wa Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali ya Madini; kukamilisha kanuni za usimamizi wa utafutaji, uchimbaji na biashara ya urani (*uranium*) nchini; kuendelea kutenga maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo; kuanzisha mfuko maalumu wa mikopo kwa ajili ya wachimbaji wadogo; na kuendelea kuimarishe miundombinu katika ofisi za madini.

Mheshimiwa Spika, Sera na Sheria ya Madini. Utekelezaji wa Sera ya Madini ya Mwaka 2009, utalazimu kufanyika marekebisho katika baadhi ya sheria, kanuni na taratibu mbalimbali ikiwa ni pamoja na Sheria ya Madini ya Mwaka 1998, Sheria ya Fedha za Kigeni ya Mwaka 1992, Sheria ya Kodi ya Mapato ya Mwaka 2004, Sheria ya Ardhi ya Mwaka 1999 na sheria nyingine za nchi kama itakavyobainika. Marekebisho ya sera na sheria ya madini yatasaidia kuleta maendeleo endelevu ya sekta na kuongeza mchango katika Pato la Taifa na maendeleo ya kijamii.

Mheshimiwa Spika, majadiliano na Kampuni za uchimbaji wa Madini. Serikali itakamilisha majadiliano na Kampuni ya Willcroft ili kupata mkataba mpya wa ubia utakaozingatia maslahi ya pande zote mbili; ikiwemo taratibu za uuzaji wa almasi zinazozalishwa katika Mgodi wa Mwadui na majukumu mapya ya *TANSORT*. Aidha, Serikali itaendelea na majadiliano na kampuni za madini kuhusu kuondoa misamaha ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, uchimbaji mdogo wa Madini. Katika kuwaendeleza wachimbaji wadogo nchini, Serikali itaipatia *STAMICO* majukumu ya kutoa huduma za kiufundi kwa wachimbaji wadogo. Wizara itaendelea kutenga maeneo ya kugawa kwa wachimbaji wadogo yatakayobainika kufaa kwa uchimbaji mdogo. Aidha, mafunzo yataendelea kutolewa kuhusu uchimbaji, uchenjuaji na utumiaji wa baruti na zebaki ulio salama na wenyewe tija. Serikali itaanzisha mfuko maalumu kwa ajili ya wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, usalama, afya na utunzaji wa mazingira migodini. Kazi ya kusimamia usalama, afya na utunzaji wa mazingira katika migodi midogo na mikubwa ni ya kipaumbele cha kudumu. Katika mwaka 2009/10, Wizara itaendeleza shughuli za: urasimishaji wa machimbo ya Mgusu; upimaji na uandaaji wa ramani za chini ya ardhi za machimbo ya vitalu B na D vya Mirerani; na baadhi ya leseni za uchimbaji wa tanzanite katika eneo la

Mirerani ambazo hazikutimiza masharti; na ubadilishaji wa mfumo hatarishi wa uchimbaji tanzanite unaotumiwa na baadhi ya wachimbaji wadogo wa Mirerani kama njia ya kuhakikisha usalama, afya na utunzaji wa mazingira vinalindwa katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, sambamba na shughuli zinazolenga kulinda usalama, afya na mazingira katika maeneo ya wachimbaji wadogo, migodi mikubwa ya Mwadui, Resolute (Nzega), Geita, Bulyanhulu (Kahama), North Mara (Tarime), Tulawaka (Biharamulo), TanzaniteOne (Mirerani) na Buzwagi (Kahama), itaendelea kufanyiwa ukaguzi wa mara kwa mara ili kuhakikisha shughuli za uchimbaji haziathiri usalama na afya kwa wafanyakazi na wananchi wanaoishi kuzunguka migodi hiyo na zinatunza na kurudishia mazingira kwa kiwango kilichokubaliwa kupitia Tathmini ya Athari za kimazingira (*Environmental Impact Assessment - EIA*) na Mipango ya Usimamizi wa Mazingira (*Environmental Management Plans - EMP*) za migodi hiyo. Wizara ya Nishati na Madini itashirikiana na taasisi nyingine husika za Serikali kufanikisha ukaguzi huo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Serikali itakamilisha uchambuzi na kupidisha mipango ya kufunga migodi (*Mine Closure Plans*) za migodi ya Tulawaka na Resolute. Aidha, Serikali itaendelea kujadili mipango ya ufungaji wa migodi ya Mwadui, Buzwagi, Bulyanhulu, Geita, North Mara na TanzaniteOne. Mipango hiyo ya ufungaji migodi itasaidia Serikali kupanga viwango na aina ya dhamana ya ukarabati wa mazingira (*rehabilitation bond*) itakayowekwa na wawekezaji wa migodi hiyo ili ikitokea ulazima wa kufunga mgodi wowote kwa njia ya dharura, rehabilitation bond yake itumiwe na Serikali kugharimia kufunga na kurudisha mazingira ya mgodi husika katika hali ya awali.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi wa gharama za uwekezaji na uendeshaji wa migodi mikubwa. Wizara itaendelea kuimarisha ukaguzi wa madini kwa lengo la kuimarisha ukaguzi wa madini yote katika kutimiza azma ya Serikali ya kuhakikisha kuwa migodi inachangia ipasavyo kwenye ukuaji wa uchumi. Aidha, Wizara itaendelea na mchakato wa kuunda chombo mahsus Cha ukaguzi wa shughuli za uzalishaji na biashara ya madini nchini. Chombo hicho kinatarajiwa kuundwa katika mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, usimamizi endelevu wa rasilimali za madini. Ili Taifa linufaika ipasavyo na rasilimali ya madini nchini, Ilani ya Chama cha mapinduzi ya mwaka 2005, Ibara ya 39(d) imeelekeza hatua za kuchukua ili kusaidia wachimbaji wadogo kupata mikopo na maarifa mapya katika fani ya uchimbaji madini. Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia itaanza utekelezaji wa Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali ya Madini, utakaotekelizwa kwa miaka mitano kuanzia Mwaka 2009/2010. Mradi huu pamoja na mambo mengine utasaidia kukuza shughuli za uongezaji thamani madini na kutoa elimu kwa wachimbaji wadogo na umma kuhusu shughuli za madini. Aidha, Wizara itaongeza kasi ya kuhamasisha uwekezaji katika Sekta ya Madini kwa kubuni mkakati wa kujitangaza na kutumia takwimu mpya za kijiolojia zitakazokusanywa wakati wa utekelezaji wa mradi huu. Chini ya mradi huu, jengo la Arusha *Gemstones Carving Centre* litakarabatiwa, na mashine mahsus zitanunuliwa na kufungwa kwa shughuli za usanifu vito na usonara (*lapidary and jewellery*).

Mheshimiwa Spika, utafutaji na uchimbaji wa Urani. Serikali imeunda Kamati ya Kiseka ambayo inaandaa rasimu za kanuni zitakazosimamia utafutaji, uchimbaji, uchenjuaji, hifadhi, usafirishaji na uuzaaji wa madini ya urani nchini.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Ofisi za Madini. Katika mwaka 2009/2010, Serikali itaendelea na ujenzi wa ofisi za madini kwa kukamilisha michoro ya ofisi za Mbeya na Mwanza na kuanza taratibu za ujenzi wa ofisi za Mbeya, Mwanza na Singida.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Jiolojia Tanzania – GST. Ili kutekeleza azma ya Serikali ya kutangaza hazina ya madini na kuvutia wawekezaji nchini, Wakala utaendelea na shughuli zifuatazo: kuchora ramani za jiolojia na jioskemia katika QDS nne (58, 75, 74 na 74W) katika Wilaya za Kasulu na Kibondo; kuchapisha vitabu vinavyoonesha madini yapatikanayo katika kila Wilaya na namna bora ya kuyatumia; kujenga ghala la kutunzia sampuli za choronge za mawe (*core shed*); kukamilisha ukarabati wa jengo la kutunzia sampuli za miamba na madini (museum); na kubadilisha mfumo wa sasa wa kutunza kumbukumbu za maktaba na takwimu kuwa kwenye mfumo wa kompyuta (*Computer-Based Meta-Data Management System*) ili kurahisisha upatikanaji wa takwimu hizo kwa wadau.

Mheshimiwa Spika, Chuo Cha Madini. Katika mwaka 2009/2010, Chuo cha Madini kitaendelea na mchakato wa kuunganishwa na Chuo Kikuu cha Dodoma. Mchakato huo utakapokamilika, mafunzo yanayotolewa Chuo cha Madini yatatolewa chini ya Chuo Kishiriki cha Sayansi ya Ardhi cha Chuo Kikuu cha Dodoma. Chuo hicho kitakuwa na sehemu mbili: *School of Mines and Petroleum*; na *School of Environmental Science and Technology*. Lengo la Serikali ni kuendeleza na kuboresha mafunzo ya taaluma mbalimbali za fani za madini na nishati kwa kutoa vyeti, Stashahada na Shahada bila kuathiri mafunzo yanayotolewa kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Kujiunga na Asasi ya Uwazi katika Tasnia ya Uziduaji (*Extractive Industries Transparency Initiative – EITI*). Baada ya Tanzania kujiunga na Asasi ya Uwazi katika Tasnia ya Uziduaji (EITI) na kupewa uanachama wa awali, Serikali itaendelea kutekeleza programu ya kazi ya EITI ili kuwa mwanachama kamili. Utekelezaji wa taratibu za EITI utaleta uwazi, uwajibikaji na utawala bora katika uvunaji na matumizi ya rasilimali za madini, mafuta na gesi asili nchini.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Madini la Taifa – *STAMICO*. Katika mwaka 2009/2010, Sheria ya *STAMICO* itarekebishwa. Aidha, uainishaji wa majukumu ya Shirika utakamilishwa. Lengo ni kuwa na chombo imara kitakachonufaisha Taifa na wananchi katika sekta ya madini. Miongoni mwa majukumu ya Shirika hili ni utafutaji na uchimbaji wa madini; ushiriki kwa niaba ya Serikali katika migodi; na utoaji wa huduma kwa migodi ya ukubwa wa kati na midogo ya mfano.

Mheshimiwa Spika, Southern And Eastern African Mineral Centre – *SEAMIC*. Mkutano wa kila mwaka wa Baraza la *SEAMIC* la Mawaziri wa Madini wa nchi wanachama uliofanyika mjini Luanda, nchini Angola mwishoni mwa Mwezi Mei, 2009, chini ya uenyekiti wa Tanzania, ulielekeza *SEAMIC* ijitangaze ili kupata wanachama zaidi kutoka bara zima la Afrika. Lengo ni kukuza ushirikiano wa nchi za Afrika katika masuala ya uvunaji na matumizi ya rasilimali ya madini na mafuta katika nchi za Afrika. Tanzania ikiwa mwanachama na mwenyekiti wa *SEAMIC* kwa mwaka 2009/10, itaendelea kusimamia maendeleo ya Kituo hicho ikiwa ni pamoja na kuongeza mawasiliano na *SADC* na AU ili *SEAMIC* kiwe kituo cha Afrika.

Mheshimiwa Spika, ajira na maendeleo ya Watumishi. Wizara inatarajia kuajiri watumishi wapya 183 mwaka 2009/2010. Lengo ni kuwa na jumla ya watumishi 1,150 ifikapo mwaka 2011/2012 kutoka watumishi 525 mwaka 2008/2009. Aidha, Wizara inatarajia kuwapeleka mafunzoni baadhi ya watumishi ili kuwajengea uwezo katika utaalamu mahsus kuwafanya waweze kutekeleza majukumu yao kwa umahiri na ufanisi zaidi. Aidha, Mfumo wa Mapitio na Upimaji wa Utendaji Kazi wa Wazi (*OPRAS*) kwa watumishi utaendelea kutekelezwa kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara itakamilisha maandalizi na kuanza utekelezaji wa Mkakati wa Habari, Elimu na Mawasiliano. Mkakati huu utasaidia kuimarisha mawasiliano kati ya Wizara na wadau, hususan, kutoa taarifa sahihi na kwa wakati kuhusu shughuli za sekta za nishati na madini.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kuwahamasisha watumishi wapime afya zao; kutoa elimu kwa watumishi wa Wizara kuhusu masuala ya UKIMWI; na kuendelea kuwashudumia watumishi walijitokeza wanaoishi na virusi vya UKIMWI kulingana na Waraka wa Utumishi wa Umma Namba 2 wa mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, ushirikiano wa Kimataifa. Katika mwaka 2008/2009, Wizara ya Nishati na Madini ilinufaika kwa misaada na ushirikiano kutoka kwa washirika mbalimbali wa maendeleo. Kwa niaba ya Serikali, napenda kutoa shukurani za dhati kwa Serikali za nchi za China, Japani, Kanada, Korea ya Kusini, Marekani, Swideni na Ujerumani. Vilevile, natoa shukurani kwa Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Rasilimali ya Ulaya, Umoja wa Nchi za Ulaya, pamoja na mashirika ya *ADF*, *Commonwealth Secretariat*, *GEF*, *IAEA*, *IDA*, *JICA*, *MCC*, *NDF*, *NORAD*, *Sida*, *SAEDF*, *UNDP* na *UNIDO*. Kwa mwaka 2009/2010, Serikali itaendelea kushirikiana na washirika hao na wengine katika kuendeleza sekta za nishati na madini.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Adam Kighoma Ali Malima, Mbunge wa Mkuranga na Naibu Waziri wa Nishati na Madini, kwa ushirikiano wake thabiti anaonipa katika kusimamia utekelezaji wa shughuli za Wizara.

Aidha, nawashukuru Katibu Mkuu, Bwana Arthur Gwanaloli Mwakapugi, Wakuu wote wa Idara na Vitengo, viongozi wa taasisi zilizopo chini ya Wizara wakiwemo Wenyeviti, wajumbe wa Bodi na watendaji wakuu, kamati zinazosimamiwa na Wizara na wafanyakazi wote wa Wizara ya Nishati na Madini na taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali na kuidhinisha mapendekezo ya Bajeti ya shilingi 226,926,047,000 kwa ajili ya matumizi ya Wizara na taasisi zake kwa mwaka 2009/10. Mchanganuo wa Bajeti hiyo ni kama ifuatavyo:-

- (i) Bajeti ya Maendeleo ni shilingi 171,646,469,000, kati ya fedha hizo shilingi 96,598,691,000 ni fedha za hapa na shilingi 75,047,778,000 ni fedha za nje; na
- (ii) Bajeti ya Matumizi ya Kawaida ni shilingi 55,279,578,000, ambapo shilingi 6,257,173,000 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 49,022,405,000 ni matumizi mengineyo (*OC*).

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofī*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki!

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**SPIKA:** Ahsante sana Waziri wa Nishati na Madini kwa kuweza kuiwasilisha kwa muhtasari mzuri tu uliotuwezesha kuelewa nini kinaendelea. Lakini ninawaomba Waheshimiwa Wabunge, waisome hotuba kikamilifu kwa sababu ina mambo mengi zaidi, ila Kanuni yetu ilivyombana ilibidi awasilishe kwa nusu saa.

Kabla sijamwita Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, naomba tuwatambue wageni waliopo katika ukumbi huu.

Wageni wa Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa William Ngeleja, ni Mama Blandina Ngeleja, yule chachu yake ya maendeleo, yule! Tunakushukuru sana mama kwa kumlea Waziri, anaendelea vizuri na anafanya kazi safi kabisa hapa Bungeni. Nakuomba uendelee na moyo huo huo. (*Makofī*)

Pamoja naye, wapo wanafamilia, lakini sasa hawa hawakutajwa, kwa hiyo ninaomba wanafamilia wasimame. Kuna mtoto wa Mheshimiwa Waziri, anaitwa Brian, nadhani ndiye yule mbele pale! Aisee, huyu Brian huyu anaonekana naye, ahsante Brian. Naona na yeze anaaandaliwa kuja kuchukua Kiti cha Sengerema, sijui itakuwa bado inaitwa Sengerema au Jimbo litakuwa limegawanywa, baba upande mmoja na mwanaye upande wa pili. Karibuni sana! (*Makofī/Kicheko*)

Wapo Watendaji Wakuu wa Wizara ya Nishati na Madini, wakiongozwa na Katibu Mkuu, ndugu Arthur Mwakapugi. Naomba asimame, yule pale. Karibu sana Katibu Mkuu. Naomba wasimame wote, maana hawakutajwa majina. Viongozi wa Nishati na Madini pamoja na mashirika yanayohusika na Nishati na Madini. Naomba wote msimame, tafadhalini. Asantee sana, karibuni sana. (*Makofī*)

Wale wakerekereketwa wa mambo ya jinsia, wataona kwamba pale bado iko kazi kuweza kupata watalaam wanawake katika Nishati na Madini, wachache.

**WABUNGE FULANI:** Wengi!

**SPIKA:** Wengi eeeh!

Wapo wageni kutoka Jimbo la Sengerema. Naomba wageni wa kutoka Jimbo la Mheshimiwa Waziri, tafadhalii wasimame. Wako upande huu. Karibuni sana ndugu zetu. (*Makofī*)

Wageni wengine wa Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Ngeleja ni Wakurugenzi wa Kampuni ya Singida Wind Power wakiongozwa na Chris Chao kutoka Korea Kusini. *We warmly welcome you partners in progress from South Korea. We hope wind power will be a reality and therefore assist in the power sector in Tanzania.* Bwana Isaac Mwamanga ambaye amesindikiza wageni hao ndiye yule pale na ndugu Emmanuel Kasyanju, Mtanzania mwingine ambaye yuko nao. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wapo wageni wa Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka na Mheshimiwa Dorah Mushi ambao ni viongozi wa Chama cha Wachimbaji wadogo wadogo wa Madini ya Tanzanite, Mererani. Wale wa kutoka Mererani, naomba wasimame tafadhali. Hawa ndio viongozi wa wachimbaji wadogo wadogo wa pale Mererani wakiongozwa na ndugu Zephaniah Mungaya, Mwenyekiti na ndugu Abuu Mollel, Naibu Katibu ni ndugu Stella Shayo. Hawa wametumia busara sana, Mweka Hazina ni mwanamke, Rachael Njau. Maana ukiweka midume kwenye shughuli hizi, watakulalia tu, maana wanaume kwa makeke, ndiyo tabu yao hiyo. (*Makofi/Kicheko*)

Wageni wa Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, wa Jimbo la Mkanyageni Pemba ambao ni Waheshimiwa Madiwani wawili kutoka Chama cha CUF, Mzee Ame Mkui, naomba Mzee Ame Mkui asimame. Msubiri wageni wetu, tunataka kuwatambua, maana ni nadra kupata Waheshimiwa wa Mkanyageni kuja hapa. Tafadhali ketini kwanza niwatambue kwa majina. Waheshimiwa Madiwani ni Mzee Ame Mkui, Mheshimiwa Fatuma Chuma Othman, wale pale. Wapo pia, Mwenyekiti na Katibu wa Jimbo la Mkanyageni wa Chama cha CUF ambao ni Ame Juma Fumu na ndugu Abdi Bakar Maulid. Wale pale! Wapo Makatibu wa Matawi 13 ya CUF katika Jimbo hilo. Makatibu msimame. Halafu wapo wawakilishi wa vitengo mbalimbali vya akina mama Chama cha CUF. Inaonyesha huko Pemba huko, hasa Mkanyageni CUF ina nguvu sana. Vyama vingine waitazame vizuri hali hii, nadhani inahitaji marekebisho. (*Makofi/Kicheko*)

Wapo wageni 61 wa Mheshimiwa Magale John Shibuda ambao ni wanakwaya na viongozi wa KKKT na viongozi wa CCM Kata ya Maswa. Ahsanteni sana wanakwaya na viongozi wa CCM kutoka Maswa. Karibuni sana. Kiongozi wa kwaya, ni Mchungaji Mathayo Gwau. Naomba asimame. Kundi la pili linaongozwa na Bi. Ziada Khamis Athuman. (*Makofi*)

Wapo wageni wa sekta ya uwekezaji wa madini na ujenzi ambao ni Bw. Eliamini Mollel, Bw. Fabian Lyamuya na Bw. Alex Changu. Wawekezaji katika sekta ya madini, karibuni. (*Makofi*)

Pia wapo wageni kutoka Hospitali ya Mkoa wa Dodoma, wakiongozwa na Mganga Mkuu, Dkt. Godfrey Mtei. Sijui wapo hapa kweli? Aaah wapo upande huu. Karibu sana Dkt Mtei. Tunashukuru sana kwa huduma zenu. Wapo pia madaktari wengi, Dkt. Zainab Chaula, Prof. Gisepe Hypolito, naona huyu Mwitaliano huyu, Dkt. Viro Francesco na Sister Cecilia Sanya. Karibuni sana. Tnashukuru sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, mnaelewa huduma tunayoipata mara kwa mara tukiwa hapa Bungeni kutoka Hospitali ya Dodoma. Wametusaidia sana sana na tunashukuru sana kwa kazi yenu na salaam ziwfikie pia waauguzi na wasaidizi wenu wote ambao wanatuhudumia vizuri sana. *Thanks very much Doctors from Italy. We are happy that you are here to take care of the people of Dodoma and also MPs when they are in Session.* Ahsante sana! (*Makofi*)

Wapo wageni kutoka UMATI, wakiongozwa na Bi. Josephine Mwankunge, Mkurugenzi Mtendaji wa UMATI. Wale pale upande wa kulia, asante sana. (*Makofi*)

Wapo wageni wa Bunge Sports Club, Waheshimiwa 50 wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar. Ni kweli wamekuja?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo!

**SPIKA:** Wako wapi? Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, naomba msimame tafadhali ili tuweze kuwatambua. Karibuni sana. Naomba Sergeant-at-arms aweze kufanya utaratibu ili Waheshimiwa Wawakilishi wote waweze kupata nafasi ndani ya ukumbi. Inaweza kulazimika labda baadhi ya wageni waweze kupisha. Naona upande huu hapa wanakwaya, kwa nidhamu kabisa wanawapisha Wawakilishi ili tuweze kupata nafasi pale. Karibuni sana, tunashukuru sana kuwapoeka ndugu zetu wa Baraza la Wawakilishi. Tunatumaini kwamba, mbali ya michezo, tutaendelea kuzungumza mambo mengine ya kuimarisha Muungano wetu. (*Makofi*)

Wapo wachezaji na viongozi 25 wa Timu ya Alibino United kutoka Dar es Salaam. Wale pale. Karibuni sana! (*Makofi*)

Wapo wageni wa Mheshimiwa Riziki Lulida, amsema ni Mzee wake, sijui ina maana ya Baba ama Mume, haieleweki. Basi, Mzee wake, ndugu Ali Said Makinda. Karibu sana. Pia nduguye Bw. Hamis Ali Mkeng'endo wa kutoka Dar es Salaam. (*Makofi*)

Hawa wanafunzi nadhani wako kule kwenye *Basement*, wanafunzi 50 na Walimu kutoka shule ya msingi Mbwanga. Sidhani kama wako humu, lakini karibu sana popote walipo katika eneo la Ukumbi wa Bunge. Ni pamoja na wanafunzi 500 kutoka sekondari ya Kikuyu. Wanafunzi 40 na Walimu kutoka shule ya msingi Nkuhungu na wanafunzi 28 na Walimu wao kutoka shule ya sekondari ya Hazina Dodoma. Sidhani kama wapo hapa. (*Makofi*)

Kwa taarifa tu ya Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Wabunge watakaoshiriki katika Mbio Maalum hapa kwetu Dodoma hapo kesho wanaongozwa na Mheshimiwa Hamza Hassan Juma, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Kiongozi. Karibu sana Mheshimiwa Waziri. Yupo pia Mheshimiwa Haji Omar Heri, Mnadhimu Chama Tawala na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Yule pale. Karibu sana Shekh Heri. Karibu sana, tunafurahi kukuona. (*Makofi*)

Sasa huyu Mheshimiwa Ali Haroon Suleiman atachezea timu gani hapa, ye ye atachezea Timu ya Bunge. Karibu sana Mheshimiwa Haroun. Kesho ndiyo tutapima uzalendo wako. (*Makofi*)

Wapo pia Mheshimiwa Machano Othman Said, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mawasiliiano na Uchukuzi. Sina hakika kama Mheshimiwa Dkt. Mwinyi Haji Makame amekuaja.

**MBUNGE FULANI:** Yupo!

**SPIKA:** Yupo! Loh, tena huyu anaonyesha sijui ndiye Captain kabisa, amekwishavalia tayari. Kama mnavyofahamu Mheshimiwa Mwinyi Haji Makame, ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Masuala ya Fedha na Uchumi. (*Makofi*)

Yupo Mheshimiwa Asha Abdallah Juma, yeye ni Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto. Yupo Mheshimiwa Tafana Kassim Mzee, Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi. (*Makofi*)

Yupo kijana wangu huyu, Mheshimiwa Mahmoud Thabiti Kombo, machachari kweli huyu, huwa ni furaha sana kusafiri naye kule nje, ana msimamo safi kabisa. Yeye ni Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo. (*Makofi*)

Yupo pia Mheshimiwa Mzee Ali Ussi, Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi. Yupo Mheshimiwa Khatib Suleiman Bakari, Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira. Yupo Mheshimiwa Khamis Jabir Makame, Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amari. (*Makofi*)

Halafu yupo Mheshimiwa Dadi Faki Dadi, Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba. Huyu ndiye anadhibiti eneo la Micheweni na Kadhalika huko. Karibu sana. (*Kicheko*)

Waheshimiwa basi tunashukuru sana tukiweza kuwa na wenzetu hawa...

Ooh, nimearifiwa kwamba pia Katibu wa Baraza la Wawakilishi, yupo katika msafara huu, Mheshimiwa Ibrahim Mzee Ibrahim. Karibu sana Katibu. Hongera sana kwa kazi kubwa uliyofanya kuweza kuwaleta Waheshimiwa Mawaziri wa SMZ na pia Wawakilishi, ndugu zetu kutoka huko Zanzibar. Kwa kweli jumla ya wageni wetu hapa ni 50, kwa hiyo ni ujumbe mzito. Ninahakika Katibu wa Bunge, mmejiandaa vizuri, tunataka wakae vizuri, wale chakula wanachokipenda, wapate taarab na pia kwenye Michezo nadhani itawezekana wakaondoka na masikitiko kwa sababu timu yetu ya hapa ni kali, kwa hiyo natumaini wenzetu wa Zanzibar mmekuja mmejiandaa vizuri ili mchezo uwe safi. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini aweze kutoa maoni ya Kamati kuhusu hoja ya Mheshimiwa Waziri. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Daniel Nsanzungwako!

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI):** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) ya Kanuni za Bunge Toleo la 2007, naomba kuchukua fursa hii, kwa niaba ya Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Nishati na Madini, kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2008/2009 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kutoa salamu za pole kwa familia ya Mheshimiwa Dkt. Harrison G. Mwakyembe (Mb), kufuatia ajali ya gari aliyoipata tarehe 21 Mei, 2009 Mkoani Iringa. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa upendo alionao kwake kwa kumuwekea mikono na kumrejesha katika hali yake ya afya aliyouwa nayo.

Mheshimiwa Spika, pia naomba nichukue fursa hii kutoa salamu za pongezi kwa Chama cha Mapinduzi (CCM) kufuatia ushindi ilioupata katika chaguzi ndogo za Ubunge zilizofanyika katika Majimbo ya Busanda na Biharamulo Magharibi, ambapo wagombea wake Mheshimiwa Lolesia J.M Bukwimba (Mb) na Mheshimiwa Oscar Rwegesira Mukasa (Mb) waliibuka washindi sawia. Tunapenda kuwapongeza kwa ushindi huo walioupata na tunawatakia kila kheri katika kutekeleza majukumu yao ya Ubunge.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilikutana tarehe 03 Juni 2009, katika Kikao ambacho Mheshimiwa William M. Ngeleja (Mb), Waziri wa Nishati na Madini aliwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka 2008/2009. Aidha, tarehe 04 Juni, 2009, Mheshimiwa Waziri pia aliwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi na Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini (Fungu 58) kwa mwaka wa Fedha 2009/2010. Katika Vikao hivyo, Kamati yangu ilipata fursa ya kufahamishwa mambo mbalimbali kuhusu Wizara kama ifuatavyo:-

- (i) Dira na madhumuni ya Wizara;
- (ii) Uongozi na Muundo wa Wizara;
- (iii) Majukumu ya Idara na Vitengo vya Wizara;
- (iv) Maelezo kuhusu Taasisi zilizo chini ya Wizara; na
- (v) Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2008/2010

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati ilijulishwa mafanikio na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa shughuli za Wizara katika kipindi cha mwaka 2008/2009 kama zinavyoelezwa hapa chini.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2008/2009, Kamati yangu ilitoa maoni na ushauri juu ya utekelezaji wa shughuli katika maeneo mbalimbali. Wakati ikipitia Taarifa ya Wizara, Kamati iliridhika kwa kiasi kikubwa na utekelezaji wa baadhi ya ushauri uliotolewa na baadhi ya ushauri unaendelea kutekelezwa. Aidha, kwa maeneo ambayo utekelezaji wake haukufanyika kabisa, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuwa utekelezaji katika maeneo hayo ufanywe kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Mpango na Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka 2008/2009, maeneo yafuatayo yalipangwa kupewa kipaumbele:-

- (i) Kupeleka umeme katika Makao Makuu ya Wilaya Tisa(9) ambazo ni Kilolo, Kilindi, Ludewa, Mbinga, Rufiji, Bahi, Uyui, Mkinga na Simanjiro;
- (ii) Kusimamia na kutekeleza miradi katika sekta za nishati na madini;
- (iii) Kuboresha na kukarabati njia za umeme na vituo vyakupozea umeme katika Gridi ya Taifa;
- (iv) Kusimamia na kuhamasisha uwekezaji, utafutaji, uchimbaji na uongezaji thamani katika madini ili kuongeza mchango wa sekta hiyo katika Pato la Taifa;
- (v) Kutekeleza Mkakati wa Kuwasaidia Wachimbaji Wadogo wa Madini;
- (vi) Kuendeleza maandalizi ya ujenzi wa miundombinu muhimu ya Wizara, hususan, Ofisi za Madini za Mbeya, Singida, Mwanza, Ludewa; pamoja na
- (vii) Kuendeleza ujenzi wa Chuo cha Madini na wakala wa Jiologia Tanzania (Geological Survey of Tanzania-(GST)).

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2008/2009, Wizara ya Nishati na Madini ilipata mafanikio yafuatayo:-

- (i) Ujenzi wa mtambo wa kuzalisha umeme wenye uwezo wa MW 45 unaotumia gesi asili katika eneo la Tegeta, ambao unamilikiwa na Serikali. Utekelezaji wake umefikia asilimia tisini (90%);
- (ii) Upelekaji umeme katika Makao Makuu ya Wilaya za Ludewa, Mbinga, Simanjiro na Mkinga umekamilika. Sambamba na miradi hiyo, pia mradi wa kupeleka umeme

Shule ya Sekondari ya Chifu Oswald Mang'ombe iliyopo Wilaya ya Musoma Vijijini umekamilika;

(iii) Kuondolewa kwa Shirika la Madini la Taifa (*STAMICO*) katika orodha (*Specified*) ya Mashirika yaliyokuwa yabinafishwe kuitia Tangazo la Serikali Namba 88 la tarehe 3 Aprili 2009;

(iv) Kufanyika kwa ukaguzi wa ubora na kiasi cha dhahabu kilichozalishwa na kuuzwa nje na kampuni kubwa za dhahabu za Geita, Bulyahulu, Tulawaka, Resolute na North Mara kwa lengo la kujua mapato yaliyopatikana na kiasi kinachostahili kulipwa kama Mrabaha kwa Serikali. Ukaguzi huu umewezesha Serikali kuanza kulipwa kodi (*Corporate Tax*) kutoka Kampuni ya *Geita Gold Mining Limited*. Kutohana na ukaguzi uliofanywa na Mradi wa Ukaguzi wa Dhahabu (*Gold Audit Project -GAP*) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*);

(v) Mradi wa kuupatia umeme Mji wa Namanga kutoka Kenya umekamilika mwezi Mei, 2009 ambapo wateja wapatao 56 waliunganishiwa umeme;

(vi) Mkataba wa makubaliano wa kugharamia mradi wa upelekaji umeme Wilaya za Bukombe na Longido ulisainiwa kati ya Benki ya Maendeleo Afrika (*Africa Development Bank-ADB*) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Maandalizi ya mwanzo ya utekelezaji wa mradi huo yamekamilika;

(vii) Mikataba miwili ya makubaliano ya kugharamia ujenzi wa Gridi ya Taifa kutoka Makambako hadi Songea na wa kujenga uwezo wa Wakala wa Nishati Vijijini wenye thamani ya dola za Marekani milioni 70.4 imesainiwa;

(viii) Ujenzi wa vituo vidogo (*substations*) vya kusambaza umeme vya Singino na Ikwiriri umekamilika kwa asilimia themanini (80%);

(ix) Utafiti wa kuangalia mienendo ya upepo ulifanyika maeneo ya Karatu – Arusha, Mkumbara – Tanga, Kititimo – Singida, Mgagao – Kilimanjaro na Makambako – Iringa. Tafiti zilionesha kuwa, Kititimo na Makambako kuna uwezekano mkubwa wa kutumia upepo kuzalisha umeme wa kati ya Megawati 50-100 (MW 50 – 100) kwenye maeneo ya hayo;

(x) Rasimu ya mwongozo wa kuendeleza Bayofyueli “(*Biofuel*)” nchini uliandaliwa na Mkataba Maalum wa Kuandaa Sera na Sheria ya Kuendeleza Mradi wa *Biofuel* nchini ulisainiwa kati ya Serikali ya Tanzania, *Swedish International Development and Cooperation (SIDA)* na *Norwegian Agency for Development Cooperation (NORAD)*;

(xi) Miradi ya umeme wa Jua ilianzishwa katika Mikoa ya Rukwa, Ruvuma, Shinyanga na Tabora chini ya Mradi wa “*Tanzania Energy Development and Access Expansion Program- (TEDAP)*” na mradi huo pia utaanazishwa Mkoa wa Kigoma. “*Solar PV Systems*” zilifungwa kwa majaribio kwenye shule tisa (9) za Sekondari katika Mikoa mbalimbali na Vituo vya Afya hamsini na moja (51) katika Mikoa mbalimbali;

(xii) Uainishaji wa maeneo ya maporomoko madogo ya maji kwa ajili ya kufua umeme kwenye maeneo ya Vijijini ulikamilika katika Mikoa ya Iringa, Rukwa, Ruvuma, Mbeya, Kagera, Kigoma, Tanga na Morogoro. Kutohana na maporomoko hayo, upo uwezekano wa kufua umeme wa Megawati mia tatu tisini (MW 390) kwa kutumia njia hii katika sehemu zilizotajwa;

(xiii) Tozo ya asilimia tatu (3%) kutokana na uzalishaji umeme lilanza kutekelezwa kwa ajili ya kuchangia Mfuko wa Nishati Vijijini (*Rural Energy Fund-REF*). Tozo hilo inatekelezwa kwa awamu na lengo ni kufikia asilimia tano (5%), kama ilivyoainishwa kwenye Vifungu Namba 19 (c) na (d) vya Sheria ya Nishati Vijijini ya Mwaka 2005. Tozo hilo la asilimia tatu (3%) ilitangazwa kwenye Gazeti la Serikali Namba 118 la tarehe 1 Agosti, 2008;

(xiv) Kuanza kwa mradi wa ujenzi wa mtambo wa gesi asili iliyosindiliwa (*compressed natural gas*) na kituo cha kujaza gesi asili kwenye magari kilichopo maeneo ya Ubungo Maziwa. Kituo hicho kilizinduliwa tarehe 14 Julai, 2009 na Waziri wa Nishati na Madini Mhe. William M Ngeleja (Mb);

(xv) Kuunganishwa viwanda sita (6) zaidi kwenye mtandao wa gesi asili Jijini Dar es Salaam na kufanya jumla ya Viwanda vinavyotumia gesi badala ya mafuta kufikia 27;

(xvi) Kutolewa kwa taarifa za kila mwezi za bei elekezi ya bidhaa za mafuta ya petroli zinazotolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (*EWURA*) zimesaidia kupunguza bei za bidhaa hizo na hivyo kuleta nafuu kwa Wananchi;

(xvii) Ujenzi wa mtambo wa nishati ya gesi wa Megawati mia moja (MW100) uliopo maeneo ya Ubungo umekamilika na kuzinduliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete;

(xviii) Kukusanywa kwa takwimu za kijofizikia kwenye kilomita zipatazo 2,641 na kuunganishwa na takwimu za awali. Takwimu hizi zitatumika kama kielelezo (*supporting scientific document*) kwenye maombi ya kuongeza Mpaka wa Bahari (Continental Shelf) wa Tanzania kwa zaidi ya maili za Baharini 200 za sasa;

(xix) Mchakato wa kumpata Mtaalam Mwelekezi kwa ajili ya Mradi wa Kudhibiti Matumizi ya Umeme (*Demand-Side Management*) unaofadhiliwa na Benki ya Dunia wenye thamani ya Dola za Marekani 200,000 umeanza;

(xx) Kufanyika kwa marekebisho ya Sera ya Madini ya mwaka 1997 kwa kushirikisha Wadau mbalimbali kama wawekezaji kwenye migodi, Taasisi za serikali, wawakilishi wa wachimbaji wadogo, Kikundi cha Akina mama Wachimbaji (*Tanzania Women Mining Association-TAWOMA*) na Waheshimiwa Wabunge;

(xi) Kukamilika kwa michoro ya ramani tatu (3) za Jiolojia zinazoonyesha kuwepo kwa madini katika Mkoa Tanga, Nachingwea, Mkoa wa Mtwara na Liganga, Mkoa wa Iringa zimekamilika;

(xxii) Mfumo wa Utoaji Leseni za Madini (*Mining Cadastral Information Management System - MCIMS*), umeboreshwa na umesaidia kupunguza muda wa kushughulikia utoaji wa leseni za madini kutoka Leseni thelathini na sita(36) kwa wiki katika mwaka 2007, hadi zaidi ya wastani wa Leseni mia moja (100) zinazotolewa sasa;

(xxiii) Nchi yetu ya Tanzania kupewa hadhi ya Uwanachama baada ya kukamilisha utaratibu wa kuijunga na Mpango wa Uwazi wa Tasnia ya Uzinduaji (*Extractive Industry Transparency Initiatives-EITI*) mnamo tarehe 16 Februari, 2009;

(xxiv) Mafunzo kwa wachimbaji wadogo wa maeneo ya Songwe, Mererani na Nyarugusu yaliyohusu mbinu za utafutaji, uchimbaji na uchenjuaji wa madini, utafutaji wa masoko, uongezaji thamani madini, afya na usalama kazini, kulinda na kutunza mazingira, elimu ya ujasiriamali na masuala mengine yaliyomo kwenye Sheria na Kanuni za Madini (Sheria ya Madini ya Mwaka 1998 na Kanuni za Madini za 1999) yalitolewa;

(xxv) Kukabidhiwa rasmi kwa Kituo cha Majaribio ya Teknolojia cha Wachimbaji Wadogo cha Matundasi kwa Mwendeshaji mpya aitwae Ms MATUNDAS ASM *DEVELOPMENT COMPANY LTD*, ambapo mkataba ulisainiwa Tarehe 23 Septemba, 2008 na kukabidhiwa tarehe 28 Januari, 2009;

(xxvi) Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta ya Umeme, (*Power System Master Plan-PSPM*) umekamilika na ulipitiwa na Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye semina iliyofanyika wakati wa Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge tarehe 12 julai, 2009; na

(xxvii) Kudhibitiwa kwa bei ya ugavi wa gesi asili ambapo sasa watumiaji wa viwandani wanapata unafuu wa senti 94 za Dola za Marekani kwa kila futi elfu moja za ujazo, kutoka Dola za Marekani 1.42 hadi kufikia bei ya senti hamsini(50) za Dola za Marekani.

Mheshimiwa Spika, licha ya mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha mwaka 2008/2009 kama yalivyoiezwa hapo juu, changamoto zifuatazo zilijitokeza:-

Mheshimiwa Spika, kuchelewa kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo kulikotokana na kuchelewa kupata fedha hasa za bajeti ya maendeleo katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka.

Mheshimiwa Spika, kutokea kwa mtikisiko wa kiuchumi duniani katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka na hivyo kuathiri maendeleo ya miradi mipy na inayoendelea katika sekta za Nishati na Madini. Hali hiyo imechangia katika kupungua kwa maendeleo ya sekta hizo ikiwemo makusanyo ya maduhuli.

Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa bei za mafuta ya petroli katika soko la dunia mwanzoni mwa mwaka wa fedha 2008/2009, ambako kulileta athari za moja kwa moja katika bei za mafuta hapa nchini pamoja na kupanda kwa gharama za uzalishaji umeme kwenye vituo vinavyotumia mafuta.

Mheshimiwa Spika, kukatika mara kwa mara kwa umeme kunakosababishwa na kutofanyika kwa matengenezo katika njia za usafirishaji na usambazaji umeme. Wizi wa mafuta kwenye transfoma ambao husababisha uzalishaji katika viwanda kutokuwa wa uhakika na usumbufu kwa watumiaji wa umeme maofisi na majumbani.

Mheshimiwa Spika, kukua kwa kasi kwa sekta za nishati na madini ambako hakuendi sambamba na ongezeko la wataalamu kwenye maeneo maalum ya uongozi na usimamizi wa sekta hizo.

Mheshimiwa Spika, kusitishwa kwa utaratibu wa kubadili mtambo wa “*Independent Power Tanzania Limited*”-(*IPTL*) kutoka kutumia mafuta mazito (dizeli) na kutumia gesi asili kutokana na masuala ya kisheria.

Mheshimiwa Spika, uelewa mdogo wa baadhi ya wananchi kuhusu sekta za nishati na madini.

Mheshimiwa Spika, kutokamilika kwa miradi iliyopangwa ya kupeleka umeme Makao Makuu ya wilaya za Rufiji, Kilindi, Kilolo, Bahi na Uyui.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2009/2010. Katika Mpango na Bajeti ya mwaka 2009/2010, sekta ya Nishati na Madini imeainishwa kuwa mionganii mwa vipaumbele sita (6) vilivyowekewa mkazo katika bajeti hiyo. Hata hivyo, sekta ya Nishati na Madini imekuwa ya mwisho katika vipaumbele kwa kutengewa shilingi bilioni 285.5 ikilinganishwa na shilingi bilioni 378.8 zilizotengwa mwaka 2008/2009, ambayo ni sawa na upungufu wa asilimia 24.6. Hali hii imeelezwa kuwa imesababishwa na kumalizika kwa mikataba ya kuzalisha umeme kwa kampuni za *DOWANS, ALSTON POWER RENTAL* na *Aggreko*. Kamati haijaridhishwa na sababu zilizotajwa, hivyo inaishauri Serikali kutambua umuhimu wa sekta hii katika kukuza uchumi wa Taifa na hivyo ihakikishe kuwa katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Sekta ya Nishati na Madini inatengewa fedha za kutosha ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inatambua na kuthamini mchango mkubwa unaotolewa na Wizara ya Nishati na Madini katika kusimamia rasilimali za Nishati na Madini nchini. Kwa kutambua umuhimu wa rasilimali hizo katika kukuza pato la Taifa, bado mapato yatokanayo na rasilimali za Nishati na Madini si ya kuridhisha. Hata hivyo, Serikali nayo imeonekana kutoweza mkazo zaidi katika kuiwezesha Wizara hii pamoja na Taasisi na Mashirika yaliyo chini yake ili kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Kwa msingi huo, katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Kamati inatoa maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Shirika la Madini la Taifa (*STAMICO*), lilianzishwa kwa Sheria ya Bunge mwaka 1972, (*The State Mining Corporation Establishment Order*) 1972 chini ya Sheria ya Mashirika ya Umma (*The Public Corporation Act*) mwaka 1969. Shirika hili ni chombo muhimu katika kusimamia rasilimali za nchi hususan madini. Shirika lilianzishwa kwa madhumuni ya kujihusisha na shughuli zote zinazohusu madini ambazo ni pamoja na utafutaji, uchunguzi, uchimbaji, uchenjuaji, utunzaji, usafirishaji wa madini, biashara na uongezaji thamani. Shirika limeweza kutekeleza majukumu hayo pamoja na mengine kwa kuingia ubia na kampuni mbalimbali au kununua hisa na kupata ufadhili kutoka mashirika mbalimbali ya kifedha kama vile “*Southern African Enterprises Development Fund*” (SAEDF) ya *South Africa*. Shirika hili linaendelea kufanya kazi zake kwa kujitegemea na kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Shirika hili lilikuwa mionganii mwa Mashirika arobaini na nane(48) yaliyowekwa katika orodha ya Mashirika ambayo Serikali ilikuwa na lengo la kuyafunga au kuyabinafsisha. Kwa kutambua umuhimu wa Shirika hili kwa Taifa, Kamati yangu iliishauri Serikali kulitoa Shirika hili katika orodha ya Mashirika yaliyotajwa kubinafsishwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kuipongeza Serikali kwa kuzingatia ushauri huo na kuliondoa Shirika hili katika orodha ya Mashirika ambayo yangebinafsishwa kupitia Tangazo rasmi lililochapishwa kwenye gazeti la Serikali tarehe 3 Aprili, 2009 kupitia Tangazo la Serikali Namba 88 (*Government Notice No. 88*).

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kuipongeza uongozi wa *STAMICO* kwa juhudii zake za kulifufua Shirika hili kwa kutumia mbinu mbalimbali zikiwemo kufanya kazi kwa ubia na Kampuni mbalimbali za ndani na nje ya nchi. Shirika hili kwa kutumia wataalamu wake limeweza kufufua mitambo miwili ya uchorongaji miamba pamoja na kutengeneza

mashine muhimu (*air compressor*) moja ambayo ilikuwa haifanyi kazi kwa muda mrefu. Vilevile imeweza kupata mitambo miwili ya uchorongaji miamba aina ya “Atlas Copco” CS 14 chini ya utaratibu wa kukodi vifaa vya kazi (*Asset leasing*) kutoka Kampuni ya “Enterprise Fedha Finance Company Limited”- (EFFCO) Kampuni tanzu ya *Southern African Enterprise Development Fund* (SAEDF). Shirika hili limejizatiti kupata mitambo mingine kadri shughuli za uchorongaji zitakavyoongezeka.

Mheshimiwa Spika, juhudzi za *STAMICO* zilizotajwa hapo juu zimewezesha Shirika kukusanya kiasi cha TSh.1,062,924,413/= mwaka 2008 ikilinganisha na mapato ya TSh. 499,679,242/= kwa mwaka 2007. Mapato hayo ni ongezeko la karibu asilimia mia moja kumi na tatu (113%).

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kuupongeza uongozi wa Shirika kwa juhudzi hizo. Pia Kamati inashauri Mashirika mengine ya uzalishaji kutekeleza majukumu yao kwa kufuata mfano wa Shirika hili.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hiyo nzuri iliyofikiwa na shirika hili, Kamati inaishauri Serikali itekeleze yafuatayo ili kuliwezesha Shirika hili kuendelea kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mchakato wa marekebisho ya Sheria inayounda Shirika hili umekwishaanza na Shirika limekwishaainisha na kupendekeza majukumu yake, Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kuhakikisha kuwa inaleta marekebisho ya Sheria hii katika Mkutano wa Bunge wa Kumi na Saba ili Shirika liendelee kutekeleza majukumu yake bila vikwazo.

Mheshimiwa Spika, Mfumo wa fedha (*Capital Structure*) wa Shirika ni kwamba Hisa zilizoidhinishwa (*Authorized Share Capital*) ni TShs.200 milioni lakini zilizolipiwa ni ni Sh. 65 milioni tu. Mfumo huu ni wa zamani tangu mwaka 1972, hivyo, Kamati inashauri kuwa ubadilishwe haraka kwa kuwa haukidhi mahitaji ya kuliendesha Shirika kibiashara katika mazingira ya sasa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kuwa mfumo wa hisa katika nchi mbalimbali duniani ambao huyawezesha Mashirika na Kampuni za Serikali kukopa katika vyombo vya fedha. Aidha, hapa nchini kwetu hisa huwekwa HAZINA hadi wakati wa gawio kufika.

Mheshimiwa Spika, Kamati imetafakari utaratibu huu na kuona kuwa hauna manufaa yoyote kwa maendeleo ya nchi. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuweka utaratibu utakaowezesha hisa (*share*) zote za Kampuni za madini kununuliwa au kuhamishiwa *STAMICO* ili Shirika hili liweze kuzitumia kama dhamana ya kukopa kutoka vyombo vya fedha na hivyo kuwezesha kuongeza mtaji na kuzisimamia vizuri hisa hizo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kurejesha majengo yote kumi na nane 18 yaliyokuwa yanamilikiwa na Shirika la Madini (*STAMICO*) ambayo kwa sasa yanamilikiwa na Wakala wa Majengo (*Tanzania Building Agency-TBA*). Majengo hayo yarejeshwe *STAMICO* haraka ili kuimarisha mizania ya Shirika (*strengthern its asset portfolio*) hili. Tunajua kuwa Baraza la Mawaziri mnamo mwezi Julai 2008, lilitoa uamuza kuhusu kurejeshwa majengo hayo, hivyo hapa Kamati inasisitiza utekelezaji wa haraka.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inatambua umuhimu wa rasilimali iliyopo katika Mgodi wa Dhahabu wa Buhemba, hivyo inaishauri Serikali kuukabidhi Mgodi huo kwa *STAMICO* ili uweze kusimamiwa kitaalamu kadiri watakavyoona inafaa.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Umeme Tanzania *TANESCO* lilianzishwa mwaka 1964 likiwa Shirika binafsi chini ya Sheria ya Umeme ya mwaka 1931. Shughuli kubwa za Shirika hili ni kuzalisha/kufua, kusafirisha, kusambaza na kuuza umeme Tanzania Bara pamoja na Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefarijika kwa hatua iliyofikiwa na *TANESCO* katika kushughulikia mchakato wa ukamilishaji wa Mpango Kabambe wa Umeme (*Power System Master Plan -PSMP*) na Mpango wa *TANESCO* wa kujikwamua Kifedha (*Financial Recovery Plan*). Kamati inaona kuwa hii ni hatua nzuri na hivyo nguvu zaidi zielekezwe katika kukamilisha miradi mikubwa ambayo itasaidia kuondoa kabisa tatizo la umeme kwa mfano Stigglers Gorge, Ruhiji n.k.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa sekta ya umeme imekua kutoka asilimia 10 – 15 (10-15%) na *TANESCO* imefikia uzalishaji kitaifa wa MW 700 hivyo kuna changamoto kubwa katika kuwekeza zaidi katika uzalishaji. Kwa kutambua umuhimu wa mpango huo na manufaa yake katika kuboresha huduma ya upatikanaji wa nishati nchini, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa inatenga fedha za kutosha na kusimamia kwa karibu utekelezaji wa miradi ya umeme ya uhakika ya muda mrefu kama ilivyoelezwa katika kifungu kilichotangulia.

Mheshimiwa Spika, Kamati imetafakari kwa undani mahitaji ya umeme nchi yetu hususan katika kipindi hiki cha 2009/2010. Mwaka 2008/2009, Bunge liliidhinisha fedha za ununuzi wa Jenereta 17, lakini fedha zilizopatikana mpaka sasa ni ya ununuzi wa Jenereta 5 tu. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa kiasi cha Sh.44.23 Bilioni kinapatikana katika kipindi cha mwaka 2009/2010 kwa ajili ya ununuzi wa Jenereta 12 zilizobakia kwa ajili ya Wilaya za Kasulu, Loliondo, Kibondo na Sumbawanga. Aidha, kiasi cha Sh. 161 Bilioni kipatikane kwa ajili ya ujenzi wa Mtambo wa kuzalisha umeme wa MW 100 eneo la Ubungo na Sh. 107 bilioni kwa ajili ya ununuzi wa mtambo wa MW 60 wa Mwanza. Mtambo huo utasaidia kupatikana kwa umeme kwa maeneo ya Kanda ya Ziwa wakati tukisubiri kukamilika kwa mpango wa ujenzi wa Njia Mpya kutoka Iringa hadi Shinyanga (*Transmission line*).

Mheshimiwa Spika, ili kuzuia upotevu wa umeme katika miundombinu ya kusafirishia umeme, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa miundombinu iliyopo inakarabatiwa mara kwa mara ili kuzuia upotevu wa umeme na kupunguza hasara katika ukusanyaji wa mapato ya Shirika pamoja na usumbufu kwa wateja.

Mheshimiwa Spika, Kamati ina shauku kubwa ya kuona kwamba Mradi wa *Stiglers Gorge* wenye uwezo wa kuzalisha MW 1200 unatekelezwa. Kwa kuwa kiasi cha umeme kitakachozalishwa “*Stiglers Gorge*” kinatosha kuhimili mahitaji kwa nchi nzima bila kutegemea miradi au utumiaji wa mitambo mingine midogo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa inafanya maamuzi haraka ili kutekeleza mradi huu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuzindua mradi wa kuzalisha umeme wa MW 100 uliopo *TANESCO* Ubungo. Kamati imeona kuwa hatua hii itaongeza upatikanaji wa umeme nchini na inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa Mradi huo unatunzwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kuishauri Serikali kuandaa haraka mwongozo kwa wawekezaji (*Guide for Investors*) ambao utaelekeza hatua na taratibu mbalimbali za uwekezaji katika sekta hii nchini, kwa kuzingatia mpango kabambe wa umeme nchini ambao umetajwa katika vifungu vilivyotangulia.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Madini Dodoma, kilianzishwa rasmi mwaka 1982. Chuo hiki kinatoa mafunzo ya ufundi sadifu katika Sekta ya Madini ikiwa ni pamoja na fani ya Uhandisi wa Migodi/Jiolojia na Utafutaji wa Madini, Uhandisi wa Uchenjuaji Madini na kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wadau wa madini kama wachimbaji wadogo wa madini na mafundi sadifu walio kazini. Pia hufanya utafiti wa madini na kutoa ushauri katika sekta ya madini kwa wadau mbalimbali wa madini.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inatambua umuhimu wa Chuo hiki katika kuendeleza taaluma mbalimbali hususan katika masuala ya madini. Hivyo tunapenda kuipongeza Serikali kwa uamuzi wake wa kukiunganisha Chuo hiki na Chuo Kikuu cha Dodoma ifikapo mwaka 2010. Hatua hii inalenga katika kuanzisha Chuo cha Sayansi za Ardhi (*College of Earth Sciences*) ambacho kitakuwa na Shule mbili za Madini na Mafuta ya Petroli (*School of Mines"and Petroleum*) na Shule ya Sayanzi ya Mazingira na Teknolojia (*School of Environmental Sciences and Technology*). Uamuzi huu utakifanya Chuo hiki kutoa wanataaluma bora zaidi ambao watatambulika ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kufuatia uamuzi huo Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha kwamba inatenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuboresha miundombinu na vitendea kazi katika Chuo hiki.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (*TPDC*) lilianzishwa mwaka 1969, chini ya Sheria ya Mashirika ya Umma Na.17 ya mwaka 1969. Kazi za msingi za shirika hili ni pamoja na kufanya utafiti wa mafuta na gesi na usimamizi wa shughuli hizo kwa maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefarijika sana kuona kuwa Waraka umeandaliwa ili TPDC ipewa asilimia 50 (50%) ya mauzo ya gesi asili (*Retention*). Hata hivyo, Kamati imeshangazwa kuona kwamba utekelezaji wa hatua hii unacheleweshwa na HAZINA. Kwa kuwa kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya Shirika kutekeleza miradi yake kwa mwaka 2008/2009 ni kidogo, hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuitia HAZINA kuhakikisha kuwa katika Mwaka wa Fedha 2009/2010 uamuzi huu wa Serikali unatekelezwa kama ilivyokusudiwa ili miradi iliyopangwa iweze kutekelezwa ipasavyo. Na hasa kuongeza uzalishaji wa Gesi asili huko Songsongo kwani mahitaji yanaongezeka kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza *TPDC* kwa jitihada zake za kuhakikisha kuwa matumizi ya gesi nchini kwa madhumuni mbalimbali yanapewa kipaumbele. Kamati imefarijika na mradi huo kwa kuwa utapunguza ucharibifu wa mazingira na kupunguza gharama kwa watumiaji wa petroli katika magari.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati imesikitishwa na kitendo cha Wakala wa Barabara (*TANROADS*) kushindwa kutoa ushirikiano kwa Shirika hili katika mradi wa usambazaji mabomba ya gesi Jijini Dar es Salaam. Kamati inaishauri Serikali kuitia Wizara ya Miundombinu kuhakikisha kuwa *TANROADS* Inatoa ushirikiano kwa Shirika la Maendeleo ya Petroli (*TPDC*) ili mradi huo utekelezekere.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi wa ubadilishaji wa magari ya petroli ili yatumie gesi unakabiliwa na changamoto kutokana na gharama ya vifaa vitumikavyo kwa kazi hiyo kutopewa msamaha wa kodi mara viingizwapo nchini. Kamati inaiomba Serikali kusamehe kwa muda ushuru wa forodha kwa Kampuni zilizosajiliwa kwa ajili ya mradi huu. Hatua hii itakuwa kama ambavyo Serikali inavyosamehe kodi ya ushuru wa forodha kwenye mitambo, vifaa na malighafi vinavyoagizwa na makampuni ya utafiti, utafutaji na uendelezaji wa uchimbaji wa mafuta ya petroli na gesi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuwa *TPDC* liwe Shirika la Muungano. Hii ni kwa sababu shughuli za utafutaji mafuta zinajumuisha maeneo yote ya Tanzania yaani Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Kulifanya Shirika hili kuwa la Muungano ni sawa kama ilivyo sasa kwa Taasisi ya Mamlaka ya Mawasiliano ya Anga (TCAA). Kamati inaishauri Serikali kufanya kazi suala hili ili Sheria iliyoanzisha *TPDC* ihuishwe na kuliwezesha kukabili changamoto zinazojitokeza kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Jiolojia Tanzania (*The Geologocal Survey of Tanzania*), ulianzishwa chini ya Sheria ya Wakala wa Serikali Namba 30 ya 1997 (CAP. 245) kupitia Tangazo la Serikali Namba 418 la mwezi Desemba 2005. Majukumu makuu ya Wakala ni:-

- (i) Kukusanya, kuchambua, kutafsiri, kutunza takwimu na taarifa mbalimbali za Kijiosayansi (Jiolojia, Jiomkemia na Jiofizikia);
- (ii) Kutengeneza na kusambaza ramani, takwimu na taarifa mbalimbali zinazoainisha kuwepo kwa aina ya miamba;
- (iii) Uchunguzi wa kimaabara kwa sampuli mbalimbali za miamba, madini, maji, mimea na udongo kwa ajili ya tafiti mbalimali hapa nchini;
- (iv) Kuratibu utokeaji wa majanga kama vile matetemeko ya ardhi, milipuko ya volkeno, maporomoko ya ardhi, mionzi asili na kadhalika; na
- (v) Kusaidia Wachimbaji Wadogo wa Madini katika kubaini maumbile na aina ya mashapo yao, kutambua aina na ubora wa madini pamoja na namna bora ya kuchenjua Madini hayo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Wakala kupokea fedha kutoka Serikalini, hujipatia mapato mengine kutokana na huduma itoazo. Kwa mfano, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2008/2009, Wakala umeweza kukusanya jumla ya Sh.184 milioni. Hata hivyo, baada ya makusanyo hayo fedha zote hupelekwa HAZINA, hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuuwezesha Wakala kuwa na kubakiza (*retention*) asilimia 30 (30%) katika Kodi ya Madini (*Mineral rent*) na asilimia 5 (5%) katika Mrahaba (*Royalty*) kama inavyoelekezwa katika Muongozo wa kazi za Wakala (*Framework Document*). Hatua hii itaisaidia Wakala kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo ya kitaalamu kwa watumishi wake.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina rasilimali mali nyingi za madini kubwa sana, hivyo kazi kubwa inabidi ifanyike kwa lengo la kuifahamu nchi kijolojia na hivyo kuweza kufahamu takwimu sahihi za rasilimali zilizopo, ikizingatiwa kuwa yapo maeneo mengi ambayo bado hayajafanyiwa utafiti. Katika kutekeleza azma hiyo, Kamati imebaini kuwa Wakala unakabiliwa na tatizo la upungufu wa vifaa vyta kisayansi pamoja na programu za komputa za

kisasa kwa ajili ya kuchambulia takwimu. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa pamoja na kuiruhusu kuwa na kubaza kiasi cha mapato, Wakala uongezewe fedha ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, imebainika kuwa, hivi sasa Kampuni nyingi za utafutaji na uchimbaji wa madini haziwasilishi Serikalini taarifa za Kisayansi na takwimu zinazotokana na shughuli zao kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Madini ya mwaka 1998. Hali hii inasababisha kasi ya ukusanyaji, uchambuzi na uhifadhi wa takwimu na taarifa za kijiosayansi hapa nchini kuwa ndogo. Kwa hiyo, Kamati inaishauri Serikali kuitia Wizara ya Nishati na Madini kufuatilia kwa karibu takwimu hizo ili Mashirika na Kampuni zitekeleze matakwa ya sheria. Endapo utatokea ukiukwaji wa sheria na taratibu hizo, hatua kali na za haraka zichukuliwe dhidi ya wahusika.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa marekebisho ya Sheria ya Madini ya Mwaka 1998 yazingatie pia kufanya marekebisho Kifungu Namba 18 cha Sheria hiyo ili kuweza kubainisha majukumu ya Wakala wa Jiolojia Tanzania hasa kwenye nyanja za utengenezaji ramani, utoaji huduma za kimaabara na upatikanaji wa taarifa za kijiosayansi. Hali hii inasababisha wadau kutokujua wapi wanatakiwa kwenda kwa ajili ya kupata huduma hizo.

Mheshimiwa Spika, mgodi wa makaa ya mawe – Kiwira mwezi Januari, 2009, Kamati yangu ilipata fursa ya kutembelea Mgodi wa Makaa ya Mawe - Kiwira na kujionea hali halisi ya uwekezaji iliyopo katika Mgodi huo. Kwa ujumla Kamati ilishangazwa na hali iliyopo hususan ugumu wa maisha ulioonekana kwa familia za wafanyakazi na familia zao waishio mgodini hapo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kamati imetoe Taarifa Maalum kuhusu Mgodi wa Mawe – Kiwira basi mjadala zaidi uwe wakati wa kujadili taarifa hiyo ambayo imeonyeshwa kwenye Shughuli za Bunge za Mkutano huu wa Kumi na Sita.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni, Kamati yangu ikishirikiana na Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ilifanya ziara katika Mgodi wa Dhahabu wa North Mara ambapo tatizo la uchafuzi wa mazingira uliosababisha madhara kwa wananchi, mifugo na mazingira katika maeneo hayo na ripoti imewasilishwa kwa Mheshimiwa Spika. Nimatumaini yetu kuwa mapendekezo yaliyotolewa, yatazingatiwa na Serikali, kwa hiyo, suala hili hatuliendeze zaidi katika Taarifa hii. Isipokuwa tunapenda kudokeza hapa kuwa kuna uleguvu mkubwa katika kusimamia utekelezaji wa Mikataba ya Madini na Kanuni za uchimbaji Madini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua mchango wa sekta ya madini katika maendeleo ya Taifa. Hata hivyo, mchango wa sekta hiyo sio wa kuridhisha kutokana na upungufu mbalimbali yaliyojitokeza katika Sheria ya Madini ya mwaka 1998. Sambamba na ushauri uliotolewa na Tume ya Rais iliongozwa na Jaji Mark Boman kuhusu Sekta ya Madini, Kamati inaiomba Serikali kukamilisha haraka mchakato wa marekebisho ya Sheria ya Madini ya mwaka 1998. Marekebisho hayo ya Sheria yaletwe Bungeni kwenye Mkutano wa Bunge wa Kumi na Saba.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa uamuzi wake wa kuondoa msamaha wa ushuru kwa bidhaa za mafuta ya petroli kwa Kampuni za Madini. Serikali imekuwa ikipoteza kiasi kikubwa cha mapato ya kodi kutokana na misamaha hiyo na hivyo, kupunguza uwezo wake wa kutoa huduma kwa Wananchi.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji katika mafuta na gesi, Kamati imefarijika sana na juhudi kubwa zinazoendelea katika utafutaji wa gesi hapa nchini. Jumla ya visima 40 vya gesi vimechimbwa katika maeneo ya Songosongo, Mnazi Bay na Mkuranga.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa inakamilisha haraka miundombinu ya kusafirisha gesi hiyo kutoka maeneo ya uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inashauri utekelezaji wa haraka wa Mradi wa Upanuzi wa njia ya Kusafirishia Gesi kutoka Songosongo hadi Dar- es- Salaam kwa kuwa mahitaji ya gesi hivi sasa yanaongezeka.

Mheshimiwa Spika, vile vile, Kamati inashauri kuwa ni vema iwapo Mwekezaji atajenga miundombinu basi Serikali inunue hisa kutoka kwa Mwekezaji huyo ili kujiepusha na grarama za malipo (*tariffs*) ambayo yatatakiwa kulipwa kwa Mwekezaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwekezaji unaofanywa na Kampuni ya Artumas ambayo imewekeza kiasi cha Dola za Kimarekani milioni mbili tangu mwaka 2004, ambayo ina mpango wa kusambaza umeme wa gharama nafuu katika Mikoa ya Lindi na Mtwara, Kamati inapongeza uwekezaji huu.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua iliyochukua katika kukabiliana na athari za msukosuko wa kiuchumi kwa kuridhia kuikopesha fedha Kampuni ya Artumas ili iweze kuendelea kutekeleza mradi wa kuzalisha na kusambaza umeme katika Mikoa ya Lindi na Mtwara. Hatua hii itaongeza uhakika wa upatikanaji wa nishati ya umeme katika Mikoa hiyo.

Mheshimiwa Spika, Mgodi wa *TANZANITE ONE MINING LIMITED* – MERERANI, Bunge lako Tukufu linafahamu kuwa mgodi huu unamilikiwa na wawekezaji binafsi. Kumekuwepo na malalamiko mengi kutoka kwa wafanyakazi wa Kitanzania wanaofanya kazi katika Mgodi huo. Malalamiko hayo ni pamoja na yafuatayo:-

(i) Kampuni kujiongezea mipaka ya eneo ambalo lilitolewa hapo awali kwa kuchimba Tanzanite nje ya eneo ambalo waliidhinishwa na hivyo kuingilia maeneo ya wachimbaji wengine. Hali hii haionekani kuwa kubwa sana juu ya aridhi bali huko chini inakochimbwa Tanzanite. Hali hii kwa lugha ya Wachimbaji wa Tanzanite inaitwa KUTOBOZANA; na

(ii) Wafanyakazi kufanyiwa upekuzi kwa kutumia mionzi (*X-ray*) kila siku kinyume na taratibu zilizoidhinishwa na Tume ya Mionzi Tanzania - (*Tanzania Atomic Energy Commission*) na hivyo kuwasababishia Wafanyakazi madhara makubwa kiafya. Madhara hayo ni pamoja na wafanyakazi wa kiume kupungukiwa na nguvu za kujamiihana na wake zao.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa imeteuliwa Kamati Maalum ya Kuchunguza malalamiko haya inayojumuisha Wabunge, Watalaan wa Serikali wa Wizara, Tume ya Mionzi na Kamishna wa Madini, mjadala wa suala hili ungojee kuwasilishwa kwa Taarifa ya Kamati hiyo ambayo itakamilika hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA) kwa kudhibiti suala la upandaji holela wa bei za mafuta kwa kupanga bei elekezi kwa wauzaji wa mafuta nchini kama ilivvojitokeza mwanzoni mwa mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, pamoja na udhibiti wa bei za mafuta nchini, Kamati inaendelea kuishauri Mamlaka hii kuendelea kudhibiti biashara haramu ya uchakachauji wa mafuta ambayo imekuwa kero kwa wananchi kutokana na uharibifu mkubwa kwenye magari na mitambo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa, majukumu iliyopewa Mamlaka hii ya kudhibiti Nishati na Maji yapo katika Wizara mbili tofauti yaani Wizara ya Nishati na Madini na Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Pamoja na mgawanyo wa majukumu hayo, EWURA imewekwa chini ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Kwa kuwa kazi nyingi zinazosimamiwa na EWURA ni za Nishati yaani Petroli, umeme na Gesi, Kamati inashauri kuwa, kutokana na umuhimu wa shughuli zake Mamlaka hii sasa ihamishwe na iwe inawajibika moja kwa moja Wizara ya Nishati na Madini na sio kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, biashara ya mafuta imekuwa ikiendeshwa kwa kuhusisha sekta binafsi katika uagizaji wa mafuta nchini, lakini EWURA imepewa jukumu la kudhibiti shughuli za biashara ya mafuta na taratibu za uagizaji wa mafuta kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa mwezi Februari 2008, Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria ya Mafuta ya mwaka 2008 (*The Petroleum Act, 2008*) ambayo katika Kifungu Na. 33 (1) cha Sheria hiyo kinalekeza kuwa mafuta yatakayoagizwa nchini lazima yawe yamenunuliwa kwa mfumo wenye ufanisi zaidi (*efficient procurement*) na kwa kigezo cha unafuu mkubwa wa gharama (*at least cost*). Wakati huo huo Kifungu 33(2) cha Sheria hiyo pia kinalekeza kuwa ufanisi wa uagizaji utafanywa kwa njia kuu nne ambazo ni, “*Joint Procurement*”, “*Competitive procurement*”, “*Bulk Procurement*” na “*By taking advantages of economies of Scale*”. Pia mfumo wowote wa uagizaji utaweza kubadilishwa pindi itakapobainika kuwa inafaa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Vifungu hivyo vya Sheria kuelekeza hivyo, Vifungu Na. 5(1) na (20 (c)-(d) vimeipa EWURA jukumu la kusimamia shughuli zote za biashara ya mafuta hapa nchini na inapobidi itafanya utafiti katika mfumo mzima wa biashara hii na kutoa maelekezo kwa wafanyabiashara waliopewa leseni na EWURA.

Mheshimiwa Spika, Serikali katika kufanya utafiti imekuwa na mapendekezo ya kubadili mfumo wa uagizaji wa mafuta kuwa itumie mfumo wa uagizaji wa pamoja (*bulk procurement*). Chini ya utaratibu huu, kampuni mbalimbali za mafuta zitawasilisha mahitaji yao na zitashindanishwa kwa mfumo wa tenda chini ya usimamizi wa Mratibu “*Petroleum Importation Coordinator*” (PIC) ambaye atakuwa akikusanya taarifa za mahitaji ya mafuta kutoka kampuni mbalimbali. Aidha, Mratibu huyo atatakiwa kusajiliwa na BRELA kama Kampuni binafsi isiyo na faida na inayomilikiwa na wafanyabiashara wa mafuta watakaouna Bodi ya Wakurugenzi wa Kampuni hiyo. Baada ya mafuta kuwasili nchini, kila Kampuni itagawana mahitaji kulingana na kiwango ambacho kila Kampuni iliagiza.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu, kuwa kumefanyika uwekezaji mkubwa kwenye miundombinu ya Mafuta unaofikia zaidi ya kiasi cha Tsh. Bilioni 70 vilivyo maeneo ya kurasini, Miundombinu hii ya kuhifadhiwa mafuta ina uwezo mkubwa-ni mfumo wenye manufaa zaidi, unaweza kuanzishwa kwa kuzingatia yafuatayo:-

(a) Kwa kuwa Sheria ya Mafuta imekwisha pitishwa na ili itekelezwe kwa ufanisi, hapana budi kuandaliwa Mpango rasmi wa utekelezaji (*Implementation Plan*) ambao utaweka muda wa mpito (*transision period*) wakati utaratibu wa utekelezaji wa mfumo uliotamkwa katika

Sheria unaandaliwa kwa maana ya kubainisha majukumu ya kila mshiriki na Ushiriki utakavyokuwa;

- (b) Sekta hii ya mafuta mchango wake wa pato la Taifa ni mkubwa sana. Takribani asilimia 40 ya mapato yote ya ndani yanatokana na mafuta. Hivyo ni eneo nyeti linalohitaji kushughulikiwa kwa umakini mkubwa;
- (c) Kujengwa kwa miundombinu maalumu ya *Single Bouy Mooring-(SPM)* itakayowezesha meli kubwa za ujazo wa “*Metric Tonnes*” (MT) 80,000-100,000 kuweza kushusha shehena kwa ufanisi;
- (d) Miundobinu ya sasa ya “*Kurasini Oil Jetty*”-(KOJ) iimarishwe kwani inafanya kazi chini ya uwezo wake;
- (e) Ichukuliwe taadhari kubwa katika kutekeleza mfumo mpya ili usije ukaathiri biasara na nchi jirani (*Trans Trade*) na kusababisha biasara hii kuchukuliwa na nchi nyingine zenye Bandari kama vile Beira-Msumbiji, Mombasa- Kenya na Cape Town - Afrika Kusini;
- (f) Serikali ichukue tahadhari kubwa ili mfumo unaopendekezwa usijenge taswira kama ilivyojitekeza kwenye mikataba yenye utata ya makampuni ya *RICHMOND, DOWANS, KIWIRA COAL MINE, TICTS, SASKATEL, IPTL* na mengine mengi ambayo inaendelea kuiletea Serikali na nchi kwa ujumla aibu kubwa; na
- (g) Kamati inasisitiza kuwa Serikali katika muda wa mpito ichukue fursa ya kuona mfumo tunao uanza umekuwa na mafanikio kiasi gani na matatizo gani yaliyojitekeza katika nchi nyingine ili uzoefu huo utumike katika kutekeleza azma hii vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mipango ambayo Wizara ya Nishati na Madini imelenga kuitekeleza katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Kamati inaiomba Serikali kuhakikisha kuwa inatenga fedha za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa mambo yafuatayo ambayo Kamati imeyapa msisitizo mkubwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati na Madini imewekwa katika utaratibu wa kuwasilisha maombi yao ya fedha HAZINA kila mwezi na mara nyingine imekuwa ikichelewa kupokea fedha kutoka HAZINA hali inayosababisha ucheleweshaji na kutofanyika kwa shughuli nyingi za Maendeleo. Kwa hiyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba inaiweka Wizara hii katika utaratibu wa kupokea fedha kutoka HAZINA kila robo mwaka (*Quarterly*) kama inavyofanyika kwa Wizara nyingine. Tunasisitiza utaratibu huo uanze mapema katika kipindi cha mwaka huu wa fedha wa 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, Serikali kulipatia mapema Shirika Umeme (*TANESCO*) kiasi cha Shilingi Bilioni 312 kwa ajili ya kuiwezesha kukamilisha utekelezaji wa miradi yake maalumu kama ilivyoolezwa hapo awali.

Mheshimiwa Spika, Serikali kuliwezesha Shirika la Maendeleo ya Petroli (*TPDC*) kupata *kubakiza (retention)* asilimia 50 (50%) ya mapato yake yatokananyo na gesi ili kuliwezesha Shirika hili kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Kuliwezesha Shirika la Madini la Taifa—(STAMICO) katika kutekeleza majukumu yake baada ya kuhuishwa. Uwezeshaji huu uanze katika Kipindi cha Mwaka wa Fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, kukamilisha miradi ya upelekaji umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya zilizobaki kulingana na maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005, pamoja na kukamilisha miradi yote iliyoachwa bila kukamilishwa.

Mheshimiwa Spika, kuboresha na kukarabati njia za umeme na vituo vya kupokea umeme katika Gridi ya Taifa pamoja na kuimarisha udhibiti wa wizi wa Mafuta ya Transfoma.

Mheshimiwa Spika, Serikali iendelee kukishirikisha kikamilifu Chama cha Makampuni ya Wauzaji Mafuta (*TAOMAC*) katika mchakato wa mfumo “*Bulk Procurement System*” ili ueleweke vizuri na uweze kuwa na ufanisi na tija kubwa kwa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza Mpango na Bajeti ya Mwaka 2009/2010, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 226,926,047,000 zinazoombwa kwa ajili ya matumizi ya FUNGU 58 ya Wizara ya Nishati na Madini. Kati ya fedha hizo; Shilingi 55,279,578,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida Shilingi 6,257,173,000 ni kwa ajili ya Mishahara ya Wizara na Mashirika yaliyo chini yake. Shilingi 49,022,405,000 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC). Aidha, Shilingi 171,646,469,000 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na kati ya fedha hizo Shilingi 96,598,691,000 ni Fedha za Ndani na Shilingi 75,047,778,000 ni Fedha za Nje.

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru tena kwa kunipatia nafasi hii muhimu kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Makadirio na Mpango na Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka 2009/2010. Pia nimshukuru Mheshimiwa William M. Ngeleja, Mb, Waziri wa Nishati na Madini na Naibu wake Mheshimiwa Adam K. Malima, Mb, kwa ushirikiano wa dhati walioutoa wakati wa kujadili Bajeti hii. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini Ndugu Arthur Mwakapugi, Wakurugenzi na Wakuu wa Taasisi/Mashirika yote yaliyo chini ya Wizara hii pamoja na Wataalamu wote chini yao kwa ushirikiano wao mkubwa walioutoa wakati wa kujadili Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao waliounyesha wakati wa kuchambua Bajeti hii na kuiridhia sasa iwasilishwe mbele ya Bunge lako Tukufu. Naomba niwatambue kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mwenyekiti na Mheshimiwa Dkt. Harrison G. Mwakyembe, Makamu Mwenyekiti.

Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Faida M. Bakar, Mheshimiwa Asha M. Jecha, Mheshimiwa Yahya K. Issa, Mheshimiwa Daniel N. Nsanzugwanko, Mheshimiwa Halima M. Mamuya, Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya, Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa, Mheshimiwa Rita Louis Mlaki, Mheshimiwa Mohammed H.J. Mnyaa, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mheshimiwa Dkt. James A. Msekela, Mheshimiwa Omar Shekha Mussa, Mheshimiwa Fred T. Mpandazoe, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mheshimiwa Charles N. Mwera, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, Mheshimiwa Christopher O. Ole-Sendeka, Mheshimiwa Mohammed S. Sinani na Mheshimiwa Lolesia J.M. Bukwimba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile kwa niaba ya Wajumbe wenzangu, tunamshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas D. Kashillilah na Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuwezesha Kamati yetu kufanya kazi bila matatizo yoyote.

Mheshimiwa Spika, mwisho, lakini siyo kwa umuhimu, naomba niwashukuru Makatibu wa Kamati, Ndugu Lina Kitosi na Ndugu Stella Bwimbo, kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuihudumia Kamati hii kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa Bunge lako Tukufu lijadili na kupidisha Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini, naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. (*Makofit*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini. Sasa ni zamu ya Kambi ya Upinzani na ninamwita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, kutoka kule Mkanyageni, Pemba.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA (MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA NISHATI NA MADINI):** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumshukuru Mola, kwa kunijaalia uzima na kuniwezesha kusimama hapa leo hii kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, ili kutoa maoni na ushauri kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 99(7), Toleo la 2007 kuhusu mapato na matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nimewasilisha Mezani, ninaomba inukuliwe kama ilivyo katika *Hansard*.

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako, napenda kutumia fursa hii, kuwapongeza viongozi wangu kutoka Jimbo la Mkanyageni waliofika hapa Bungeni leo kuniunga mkono pamoja na wale wote ambao hawakufika. Pia napenda kukipongeza Chama changu cha C.U.F (Chama cha Wananchi), kwa kuniwezesha kuwepo hapa Bungeni. Naahidi kukitumikia pamoja na kuwatumikia wananchi kadri Mwenyezi Mungu atakavyonijaalia kwa kuwa bila ya kura zao, nisingekuwepo hapa leo hii. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza viongozi wangu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid na Naibu wake, Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa na wale wote walionipa moyo katika maandalizi ya hotuba hii. Mwisho lakini si kwa umuhimu, nampongeza Msaidizi wangu wa Wizara hii, Mheshimiwa Sevelina Mwijage, kwa mchango wake wa kina na kukamilisha hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka uliopita, Bunge lako liliidhinisha matumizi ya shilingi 362.922.265.600 na baadaye kiwango hicho kikaongezeka hadi shilingi 368.800.298.884 baada ya kufanyika uhamisho (*reallocation*) kati ya fedha hizo, shilingi 48.732.913.284 kwa matumizi ya kawaida na zile za maendeleo zilikuwa ni shilingi 320.067.385.600.

**SPIKA:** Mheshimiwa umemsahau Mkeo. (*Kicheko*)

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA (MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA NISHATI NA MADINI):** Mheshimiwa Spika, kwa kulinganisha na kiwango kinachoombwa mwaka huu kwa matumizi ya kawaida kuna ziada ya

(55.279.578.000, 48.732.913.284) shilingi 6.546.664.716 au ziada ya asilimia 13.4. Lakini bajeti ya maendeleo kuna upungufu wa (171.646.469.000, 320.067.385.600,) shilingi 148.420.920.000 sawa na asilimia 46.4(ya upungufu).

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa bajeti tegemezi ya maendeleo yaani fedha kutoka nje mwaka jana Wizara ilitegemea Shilingi 223.468.694.600, ambapo mwaka huu Wizara inategemea Shilingi 75.047.778.000,- ikiwa ni punguzo la bajeti tegemezi kwa asilimia 66.4 na kwa fedha za ndani za maendeleo takriban ni sawa na mwaka jana maana kilichopungua ni Shilingi 7000 tu .

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa bajeti ya Serikali (uk. 41 na 42 Hotuba ya Waziri wa Fedha na Uchumi), kiasi kilichotengwa kwa Wizara ya Nishati na Madini ni Bilioni 285.5 lakini Wizara yenyewe leo inaomba shilingi 226.926.047.000. Kuanzia hapa tayari tunapata maswali mengi ya kujiuliza na Bunge lako Tukufu, naomba lizingatie kwa makini maswali haya yote.

(1) Kwa nini Wizara inaomba kiwango cha chini kuliko kile kilichopangwa na Serikali katika Bajeti Kuu?

(2) Kwa nini hii tofauti ya bajeti ya Serikali na Wizara (Tzs.285.500.000.000/- 226.926.047.000/-) ya shilingi 58.573.953.000/- isiende kwenye bajiti ya maendeleo ambayo ni pungufu kwa asilimia 46.4 kwa kulinganisha na ile ya mwaka uliopita?

(3) Kwa nini matumizi ya kawaida yamezidi kwa asilimia 13.4 kulinganisha na mwaka uliopita wakati tumeelezwa kuna mtikisiko wa kiuchumi duniani ambao pia umetuathiri Tanzania?

(4) Kwa nini Wizara izidishe matumizi ya kawaida na ipunguze ya maendeleo?

Mheshimiwa Spika, katika matumizi ya kawaida ya bajeti ya mwaka huu, Wizara imetenga shilingi 6.257.173.000/- kwa ajili ya mishahara ya Wizara na mashirika yake, ukilinganisha na mwaka uliopita zilitegwa shilingi 3.305.639.000/- hivyo ziada ya Shilingi 2.951.534.000/- inabainika. Lakini ukiangalia mgawanyo halisi wa bajeti yote ya mishahara ya Wizara ni shs 3.840.057.000/= tujiulize ziada ya shilling bilioni 2.95 ni kwa ajili ya mini mbona matumizi yake hayaonekeani au zinaenda sehemu nyingine na ni wapi? Namuomba Mheshimiwa Waziri alifafanulie Bunge lako kwa uwazi.

Mheshimiwa Spika, nasema haya kwa sababu zifuatazo:-

Katika ufanuzi wa muhtasari wa fedha za matumizi ya kawaida kwa mwaka jana na mwaka huu ni kama inavyoonyesha katika kijedwali kidogo hapa chini na kwa uchambuzi zaidi angalia Kiambatisho A. Kwa namna fulani Wizara imefumba bila ya ufanuzi wa kutosha katika bajeti ya mwaka huu.

	Mwaka 2008/2009	Mwaka 2009/2010
<i>IPTL capacity charge</i>	18.000.000.000/-	18.000.000.000/-
Matumizi mengino ya Wizara	39.549.241.000/-	49.022.405.000/-
Mishahara ya Wizara	3.305.639.000/-	3.840.057.000/-

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa bajeti ya maendeleo, kuna upungufu wa asilimia 4

Mheshimiwa Spika, sababu zilizotolewa na Serikali ni kumalizika kwa mikataba ya makampuni ya kuzalisha umeme nchini ya *Dowans, Aggreko* na *Alston Power Rental* na sio mtikisiko wa kiuchumi duniani uliotuathiri pia hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inasikitishwa na sababu hizi zilizotolewa na Serikali na kubaini kwamba kumbe shilingi bilioni 320 zilizotengewa Wizara hii mwaka uliopita ni kutokana na mikataba ya kuifilisi nchi zaidi kuliko shughuli za maendeleo. Wakati huo fedha ilipatikana lakini mikataba haipo na fedha haziwezi kupatikana kwa bajeti ya maendeleo. Kambi ya Upinzani inahitaji ufanuzi wa kina katika jambo hili.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa miradi iliyopewa kipaumbele katika mpango wa bajeti 2009/2010 Katika miradi 13 ya kusambaza umeme vijijini (kasma 3001-3112) kwa mwaka 2008/2009 ambayo yote ilitumia fedha za ndani shilingi 1,378,533,000/- ni miradi mitatu tu iliyokamilika sawa na asilimia 23. Utendaji wa aina hii ni wa kutilwa mashaka na tusipo kuwa makini tutajikuta miradi hii kukamilika kwake ni 2015. Miradi iliyoripotiwa kukamilika ni kupeleka umeme katika makao makuu za Wilaya za Mbinga, Simanjiro/Ukerewe na Ludewa kwa maana hiyo miradi 10 iliyobakia imo katika bajeti ya mwaka huu 2009/2010 na imetengewa fedha za ndani shilingi 45,524,153,300/-.

Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu nilikumbushe Bunge lako Tukufu kuwa katika hotuba yangu ya bajeti mwaka jana nilisema miaka miwili iliyopita Bunge lako lilishaidhinisha bajeti ya Tsh 26,025,000,000/- na ukijumlisha na tulizopitisha mwaka jana sasa hivi itakuwa ni jumla ya Tsh.27,403,533,000/-.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa iliyotolewa na *TANESCO* kwenye Kamati ya Nishati na Madini mwezi wa Mei 2008 tulielezwa kwamba gharama halisi ya kukamilisha miradi hii ni shilingi bilioni 22.087. Kwa sababu hiyo, katika bajeti ya mwaka jana nikamuomba Mheshimiwa Waziri kutupatia jedwali linaloonyesha idadi ya fedha iliyopatikana na kutumika katika kila mradi (kasma 3001-3112) kwa mwaka 2005/2006, 2006/2007, 2007/2008 lakini Waziri hajafanikisha hadi hivi leo na leo hii tena Waziri analiomba Bunge lako liidhinishe jumla ya shilingi bilioni 45.524 kwa miradi hiyo ya usambazaji umeme vijijini (kasma 3001 – 3112). Ni dhahiri kwamba gharama hizo zimeongezeka takriban mara mbili kwa sababu ya ucheleweshaji ndio maana wenzetu wanasema “*Time is Money*”.

Mheshimiwa Spika, sote humu ndani tutakuwa mashahidi mwakani Mungu akitujaalia, je,hizo bilioni 45.524 (tena sio fedha ya wafadhili) zitakamilisha miradi hii au bado itakuwa hadithi (“*story*”) ile ile?

Mheshimiwa Spika, tunaelewa kwamba miradi hii baadhi yake imetengewa fedha tangia bajeti ya mwaka 2005/2006 na inaendelea kutokana na ukubwa wa masafa ya mradi wenyewe au kukosekana fedha ya kutosha. Kambi ya Upinzani, inamwomba Waziri kwa mara nyingine tena atoe orodha (*list*) na alieleze Bunge lako ukubwa wa kila mradi kimasafa (km), muda halisi wa kukamilika, makisio ya gharama za mradi husika, fedha zilizopatikana na fedha iliyotumika ili Waheshimiwa Wabunge hasa wanaotoka maeneo hayo waweze kutathmini utendaji halisi na kasoro zake ili kuepusha mradi fulani kuendelea bila kikomo maalum cha kukamilika kwake na pia kuliwezesha Bunge lako Tukufu kutimiza majukumu yake ya Kikatiba ya kuisimamia Serikali na Taasisi zake zote.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine katika bajeti ya mwaka huu wa 2009/2010, kumeongezeka miradi mipya sita (kasma 3001) ambayo ni:-

- *Emergency Power Plants (3001-3147)*
- *Support Project for the stable Power supply system (3001-3111)*
- *Hydro Power Studies (3001-3145)*
- *Energy and Climate Research (3001-3109)*
- *Capacity Development REA (3002- 3146)*
- *Energy Facility (3001-3148).*

Mheshimiwa Spika, miradi hii yote isipokuwa wa *Emergency Power Plants* inatarajiwa kutumia fedha za nje. Miradi hii ambayo yote ni kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa mafundi na Wahandisi wa *TANESCO*, utafiti wa uzalishaji umeme katika bonde la Ruhudji, mradi wa kuwajengea uwezo waendelezaji wa nishati bora vijiji (*REA capacity Development*) na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inatambua jitihada za Wizara kwa kushirikiana na SIDA, JICA na Jumuiya ya Umoja wa Ulaya, kwa kutayarisha miradi hii ambayo ni muhimu sana kwa kuongeza ujuzi na maendeleo ya mafundi na Wahandisi wetu mbalimbali wa umeme.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, napenda kutoa tahadhari moja muhimu sana, kwamba Tanzania yapo mashirika mawili ya serikali ambayo yana wajibu wa kuzalisha na kusambaza umeme nchini (*TANESCO* na *ZECO*) na yote yanahitaji kuwa na wataalam waliobobe kwa kupata mafunzo. Wizara ya Mambo ya nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa Tanzania, ni moja na ni ya Muungano, Shirika la umeme la Zanzibar (*ZECO*), limekosa nafasi hizi kwa muda mrefu hivyo, namtaka Waziri wa Nishati na Madini atufafanulie katika mafunzo hayo Zanzibar imeshirikishwa vipi na nafasi ngapi zitatolewa kwa Zanzibar ukiacha zile za *hydropower* ambazo si muafaka kwa Zanzibar kwa sababu nako kunahitajika kuwaendeleza wataalamu na kupata vifaa vyta kisasa sio kila siku kutegemea *TANESCO* kwa matatizo ya kiufundi yanapotokea.

Mheshimiwa Spika, maeneo 16 yamepewa kipaumbele katika bajeti ya mwaka huu kama yalivyoainishwa katika kiambatisho B kwa lengo la kuweka kumbukumbu nzuri na kufanya rejea miaka ijayo. Ni dhahiri hatuwezi kumudu kuyatekeleza yote kwa pamoja hasa kutokana na upungufu wa fedha, urasimu, na tabia ya serikali yetu kupanga na kusema zaidi kuliko utekelezaji wa vitendo. Hali hii inadhihirika pale tunapoona baadhi ya maeneo haya kupewa kipaumbele tokea mwaka 2007/2008 lakini hadi hivi leo bado hayaja tekelezeka mfano:-

- Shughuli za kuongeza thamani madini kwa lengo la kuongeza pato la Taifa; na
- *TPDC* kushiriki kwa kuwekeza katika miradi ya Songo songo na Mnazibay.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inashauri ni bora kuwa na vipaumbele vichache vinavyoweza kutekelezeka kuliko kuwa na vipaumbele lukuki ambavyo mwisho wa mwaka hakuna ufanisi wowote.

Mheshimiwa Spika, kuimarisha uzalishaji kwa kupanua mitambo ya kuzalisha umeme na njia kuu za usafirishaji. Serikali hatimaye imekamilisha '*Power System Master Plan*' (*PSMP*) mnamo mwezi Septemba 2008 ambayo imebainisha miradi ya muda mfupi (miaka 5), muda wa kati (miaka 6 - 15) na muda mrefu (miaka 16 na zaidi).

Mheshimiwa Spika, mbali na mpangilio wa matukio ya baadaye yanayotabirika au kubuniwa (*scenario*) katika *PSMP* hiyo, miradi iliyoonyeshwa hapa chini imepangwa kutekelezwa na kukamilika katika muda uliotajwa na kwamba ifikapo mwaka 2031 mahitajio ya umeme Tanzania itakuwa ni 4787 MW (wastani wa 4.8 GW).

Mheshimiwa Spika, katika *PSMP* hiyo imeelezwa kuzingatia ukuwaji wa sekta ya kilimo kwa takwimu za mwaka 1985 – 2006 ya asilimia 3.9, sekta ya ukuwaji wa uchumi ya huduma ya asilimia 3.8. pia imezingatia ile waliyoita sekta ndogo ya viwanda (*agro-processing products*) na migodi kwa ukuwaji wa asilimia 5.2 pamoja na ongezeko la watu kwa asilimia 2.9.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutumia takwimu hizo za zamani za uchumi na dira ya Taifa ya 2025 ya ukuaji wa miradi ya maendeleo kwa asilimia 8 kwa mwaka, *PSMP* hiyo haikuzingatia hali ya kisiasa (sio ilani ya CUF wala CCM) kama mtakavyo jionea wenyewe kwenye ratiba ya kuendeleza miradi hiyo (angalia Ilani ya Uchaguzi ya CCM uk.49 na 50).

Mheshimiwa Spika, *PSPM* inapendekeza kununua umeme kutoka Ethiopia kama mbadala wa *ZTK* (*Zambia-Tanzania-Kenya Interconnector*) wa 200MW ifikapo mwaka 2014. Angalizo kubwa hapa ni kuona kwamba mipango iliyoko ya *SAPP* (*Southern African Power Pool*) ni kuendeleza Shirika la umeme la Zambia (*ZESCO*)-Congo ‘*Interconnector*’ kutoka mradi mkubwa *Hydro Power* wa 2000MW huko Caborra Bassa Zambia ambao pia utapeleka umeme Afrika ya Kusini kupitia Shirika la Umeme lao la *ESKOM* ambao ndio wahusika wakubwa kujenga njia kuu ya kusafirisha umeme.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba Serikali ya Ethiopia imechukua hatua za haraka ya kuanzisha Sera ya Kuuza umeme kwa Sudan, Djibuti, Egypt na Kenya kwa upande wa Kaskazini na sisi Tanzania tutachukua kutoka Kenya kupitia hiyo ZTK. Hivi sasa tunapo zungumza mradi wa kuzalisha umeme wa 1100MW unaendelea kujengwa huko Ethiopia na baadaye kujenga miradi ya Tekese 300MW, Gilgel 2 420MW, *Anabeles* 460MW na *Gilgel 3* 1870MW yote kutumia maporomoko ya maji.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka huu hadi 2031, *PSPM* yetu haikuzingatia uzalishaji wa umeme kutokana na rasilimali yetu aliyotubariki Mwenyezi mungu ya ‘Uranium’ kwa sababu zisizokubalika nazo ni:-

- Kiwango cha juu kinacho kubalika kwa kinu kimoja cha ‘*nuclear*’ kisizidi kikomo cha mahitaji ya uhakika ambacho inakisiwa ni 150MW kwa kinu kimoja katika mwaka 2015 na kuongezeka hadi 300MW ifikapo mwaka 2024. (inakisiwa kuwa nuclear reactor ndogo zitakuwa kwenye soko ifikapo mwaka 2015-2020);
- Suala la usalama na uwezo kuendesha kinu cha ‘*nuclear*’;
- Serikali ya Tanzania kukamilisha sera zake kuhusiana na ‘uranium na uzalishaji wa umeme kutumia nishati hiyo; na
- kubainishwa kwa gharama.

Mheshimiwa Spika, hata kama bado hatujakuwa tayari hivi sasa kwa nishati hiyo yenye vikwazo duniani lakini inasikitisha kuona kwamba ikiwa kuanzia mwaka 2015 kutakuweko mitambo ya kuzalisha umeme wa 300MW kwa nini tusiingize kwenye mpango tukawa na

uhakika wa kuzalisha umeme wa biashara na kuitumia vyema hiyo ZTK? Ingefaa mipango iwepo kwa ajili ya mahitaji/maombi ya kifedha ya SAPP.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, haikubaliani na sababu hizo kwani hata baadhi ya nchi zilizoendelea zinatekeleza baadhi ya miradi kwa kutumia njia ya kandarasi ya menejimenti na baada ya muda wa makubaliano kukabidhi mradhi huo kwa nchi husika.

Mheshimiwa Spika, miradi iliyokusudiwa kutekelezwa kwa lengo la kuzalisha umeme wa kutosha nchini kwa kutumia rasilimali tulizonazo na ongezeko la matumizi ya umeme kwa miaka ijayo ni kama ilivyooonyeshwa katika jedwali no. 2.

Mwaka	Jina la Mradi	Uzali shaji (MW )	Fuel	Angalizo
2009	Tegeta(GT)	45	Gas	
2009	Kinyerezi 1	100	Gas	
2010	Kinyerezi 2	100	gas	
2010	Kiwira 1	200	coal	
2012	Kiwira 2	200	coal	
2013	Tegeta2(IPTL)	100	gas	conversion
2014	Ruhudji	358	hydro	
2014	ZTK interconnector	200	-	Importatio n from Ethiopia
2015	Wind(IPP-Singida)	50	wind	
2015	Rusumo	20.5	hydro	Rwanda/B urundi/Tz ( 61.5 MW)
2016	Kakano	53	hydro	
2017	Mpanga	144	hydro	
2018	Mchuchuma 1	200	coal	
2018	Wind	50	wind	
2019	Rumakali	222	hydro	
2020	Masigira	118	hydro	
2021	Mnazibay 1	150	gas	
2022	Mnazibay 2	150	gas	
2023	Mchuchuma 2	200	coal	
2024	Mchuchuma 3	200	coal	
2025	Stiegler's Gorge 1	300	hydro	

2026	Local gas	150	gas	
2027	Coastal CNG(GT)	300	gas	
2027	Stieglers Gorge 2	600	hydro	
2028	Coastal CC LNG 1	174	gas	
2028	Coastal CC LNG 2	174	gas	
2029	Stiegler's Gorge 3	300		
2029	Coastal CC LNG 3	174	gas	
2030	Local coal	200	coal	
2030	Coastal CC LNG 4	174	gas	
2031	Coastal CC LNG 5	174	gas	
2031	Coastal CC LNG 6	174	gas	

Mheshimiwa Spika, mpango wa utanuzi wa njia za kusafirishia umeme; kutokana na kuzidiwa uwezo wa njia za kusafirishia umeme, *PSMP* hiyo imeshauri suluhisho la muda mfupi ni kuzalisha umeme huko Mwanza angalau kuweza kuhimili migodi miwili inayohitaji kiasi cha 55MW. Baada ya hatua hiyo, ni kuongeza uwezo wa njia za kusafirishia umeme kutoka Iringa kwenda Shinyanga mwaka 2031.

Mheshimiwa Spika, pamoja na suluhisho hilo, ikumbukwe kwamba moja katika njia zinazotumiwa na nchi nyingi duniani wakiwemo majirani zetu (Kenya na Uganda) ni kutumia taa maalum (*energy saving bulbs*) ambazo hupunguza gharama za uzalishaji na usafirishaji kwa wastani hadi 30MW kama nilivyoshauri katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka jana na maelezo kama hayo kurudiwa tena mwaka huu wa fedha katika hotuba ya Kiongozi wa Upinzani katika bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, tukifanya hivyo katika miji ya Dar es Salaam, Arusha, Moshi na Mwanza mzigo mkubwa utapungua katika njia za kusafirishia umeme. Lakini kutokana na taarifa ya *TANESCO* katika semina ni kwamba ndio kwanza tunataka kufanya utafiti wa suala hili. Katika *PSMP* kunahitajika njia 32 za kusafirishia umeme ziwe katika msongo wa 400 kV na jumla ya urefu wa 4913km na njia 6 katika msongo wa 220kV zenye urefu wa jumla ya 846km. Kati ya mwaka jana 2008 hadi 2013, njia 13 zenye msongo wa 400 kV na moja yenye msongo wa 220 kV zinahitajika kujengwa kwa gharama inayokisiwa kufikia shilingi bilioni 651.2 (\$500.9 milioni); Kati ya mwaka 2014 hadi 2019, jumla ya njia 20 zinahitajika kujengwa kwa gharama ya shilingi bilioni 769.6 (\$ 592milioni); Kati ya mwaka 2020 hadi 2031 njia 14 za kusafirishia umeme zenye msongo wa 400 kV na njia 5 zenye msongo wa 220 kV zinahitajika kujengwa kwa gharama inayokisiwa shilingi bilioni 883.4 (\$ 679.5 milioni).

Mheshimiwa Spika, baadhi ya njia za kusafirishia umeme zinazopendekezwa, zitalazimika kuwa na ‘circuit 3’ nyingine ‘circuit 2’ na ile ya kawaida ya ‘circuit 1’ kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali no.3

Kutoka Kwenda	Kwenda	KV	Urefu (Km)	Mwaka 2008- 2013	Mwaka 2014- 2019	Mwaka 2020- 2031	Circuits
Mwanza	Shinyanga	400	140	32.8	17.6	-	2
Shinyanga	Singida	400	200	46.8	25.2	-	2
Shinyanga	Bulyanhulu	400	130	30.4	16.4	-	2
Singida	Babati	400	150	35.1	18.9	-	2
Dodoma	Mtera	400	130	29.3	14.6	14.6	3
Mtera	Iringa	400	107	24.1	12	12	3
Iringa	Mufindi	400	130	30.4	16.4	-	2
Singida	Dodoma	400	210	47.3	23.6	23.6	3
Iringa	Kidato	400	160	-	44.8	-	1
Iringa Kihansi	400	95	-	26.6	-	1	Mufindi
Mufindi	Makambako	400	73	20,4	-	-	1
Mufindi	Ruhudji	400	100	-	28	-	1
Mufindi	Mchuchuma	400	220	-	61.6	-	1
Mbeya	Makambako	400	147	41.2	-	-	1
Mbeya	Rumakali	400	150	-	-	42	1
Kidato	Morogoro	400	130	-	23.7	12.7	1
Kidato	Kihansi	400	180	-	50.4	-	1
Kidato	Stieglers	40	100	-	-	28	1
Morogoro	Ubungo	400	179	-	32.6	17.5	1
Morogoro	Tanga	400	200	-	46.8	25.2	2
Ubungo	Stieglers	400	200	-	-	56	1
Ubungo	Dar 2	400	50	-	-	14	1
Makambako	Rumakali	400	200	-	-	56	1
Makambako	Mchuchuma	400	200	-	56	-	1
Kihansi	Ruhudji	400	150	-	42	-	1
Kihansi	Mpanga	400	40	-	14.4	-	2
Babati	Arusha	400	162	37.9	20.4	-	2
Bulyanhulu	Geita	400	150	-	-	42	1
Stieglers	Dar 2	400	160	-	-	44.8	1
Stieglers	Mtware	400	400	-	-	144	2
*Zambia	*Mbeya	400	120	43.2	-	-	2
*Arusha	*Kenya	400	150	54	-	-	2
Kiwira	Mbeya	220	120	28,1	-	-	2
Masigera	Makambako	220	180	-	-	42.1	2
Geita	Nyakanzi	220	133	-	-	25.5	1
Nyakanzi	Ruzumo	220	95	-	-	18.8	1
Rusumo	Kakono	220	150	-	-	28.8	1
Rusumo	Kyaka	220	164	-	-	32.3	1
	JUMLA						

Mheshimiwa Spika, tofauti ziliopo baina ya mpango wa ufufuaji wa *TANESCO (FRP)*, *PSMP* ya Serikali na wazalishaji binafsi (*IPP*), Mpango wa *FRP* wa *TANESCO* umetengenezwa kwa dhana ifuatayo:-

- Usambazaji umeme vijiji kuunganisha wateja wapatao laki moja kwa mwaka;
- Makampuni ya madini kukubali kutumia umeme wa gridi;
- Serikali itatoa fedha kugharamia mitambo ya kuzalisha 60MW Mwanza na kuanza kufanya kazi 2009;
- Serikali itatoa fedha kujenga mtambo mwengine wa 100MW na kuanza kufanya kazi mwaka 2010;
- Kiwira iwe tayari kuzalisha 200MW mwaka 2011 (*PSMP-KIWIRA* 2010);
- Mnazi Bay iwe tayari kuzalisha 300MW mwaka 2013 (*PSMP-MNAZI BAY*2021);
- ZTK *Interconnector* iwe tayari mwaka 2014; na
- Mradi nwa kuzalisha gesi wa Songosongo uweze kuzalisha 1000bcf na ipatikane Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mawazo hayo mazuri yaliyopangwa na *TANESCO* kutekelezwa kwa muda mfupi bado inadhihirika kuwepo na tofauti nyingi kubwa baina ya hawa *IPP*, *FRP* ya *TANESCO* na *PSMP* naomba kuzitaja baadhi yake kama ifuatavyo:-

- *FRP* inazungumzia kuzalisha umeme Kinyerezi 1 kwa kutumia HFO wa 150MW mwaka 2010 na Kinyerezi 2 kutumia gesi wa 100MW mwaka 2013 ambapo *PSMP* imepangwa Kinyerezi 1 kutumia gesi na kuzalisha 100MW na kuwa tayri mwishoni mwa 2009 na Kinyerezi 2 kutumia gesi na kuwa tayari January 2010;
- *PSMP* inazungumzia 200MW ziwe tayari kuzalishwa Kiwira 1 kwa mkaa wa mawe mapema mwaka 2010 kwa mkataba wa kibashara uliopo na Kiwira 2 200MW nyengine 2012 lakini bado hakuna mkataba wa kibashara kwa awamu hiyo ambapo *FRP* ya *Tanesco* inazungumzia Kiwira 1 kuzalisha 200MW na kukamilika mwaka 2011;
- *FRP* ya *TANESCO* inazungumzia umeme wa Mnazi Bay wa gesi 300MW mwaka 2013 ambapo *PSMP* imepanga kutekelezwa mradi wa Mnazi Bay awamu ya kwanza mwaka 2021 kuzalisha 150MW na awamu ya pili mwaka 2022 wa 300MW; na
- *PSMP* inazungumzia umeme wa upopo wa 50MW mwaka 2015 huko Singida ambapo *IPP(Singida Wind Power Ltd)* inakusudia kuzalisha 15MW na kuingiza katika gridi ya Taifa mwezi Agosti mwaka 2010 kwa majoribio na 210MW mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, '*Power System Master Plan*', ni dira kubwa kwa Taifa inayoonesha hali ya sasa katika uzalishaji umeme na mahitajio ya baadaye imetengenezwa kwa gharama kubwa sana ya \$ 2milioni na imechukua muda miaka miwili na nusu kukamilika kwake. Kwa vyovypote vile, hii ndio dira ya kuifuata na kuazimia kikweli kuitekeleza kwa faida ya Taifa hili ikiwa imekubalika kweli. Vinginevyo ni kupoteza fedha za walipa kodi. Pia inahuzunisha kuona kwamba hata mwaka mmoja haujamalizika na bado hakuna hata mradi mmoja

uliotekelawa na kukamilika kwa kutumia *PSMP* hiyo tayari kunafanya mapitio (*Revised 2009*) tena na kampuni ya *SNC LAVALIN* ambayo ni kampuni hiyo iliyo teneza *PSMP* ikishirikiana na Wizara na *TANESCO* kama tulivyo elezwa katika semina ya *TANESCO* na *EWURA* ya tarehe 12/7/2009. Kambi ya Upinzani inauliza, je, hizi sio njia za kutengeneza mlo? Kwa kitu kipywa ambacho hakijaanza kutumika kikawa tayari kina kasoro na kulazimika kurekebishiwa upya? Basi Waziri atufanulie gharama za mapitio haya ni kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, haya yote ninayoyasema kama mapungufu ya *PSMP* wataalamwa *TANESCO*, ninaowaheshimu sana wanayajua na kwa makusudi wamekaa kimya na kwa nini hawajajiuzulu kama ushauri wao haukubaliwi na Wizara? Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri arekebishe kasoro hizi na alifahamishe Bunge lako marekebiso yote yaliyoleta tofauti hizi pamoja na maelezo kamili ya kukubali mpango wa ufufuaji wa *TANESCO* ambaa baadhi ya sehemu unaonesha tofaouti na *PSMP*.

Mheshimiwa Spika, katika miradi yote ya kuzalisha umeme ya muda mfupi iliyo pangwa na *TANESCO* na kukamilika mwaka 2009/2010 na mwaka 2011 sijaona kasma yoyote iliyo tengewa fedha katika bajeti hii. Je, miujiza gani itafanyika ikiwa miradi hiyo haijatengewa fedha kuanzia sasa? Kambi ya Upinzani inaomba ufanuzi wa hilo.

Mheshimiwa Spika, Kiwira; baada ya kauli ya Waziri wa Nishati na Madini hapa Bungeni kuhusu Mgodi wa Kiwira *Coal Mine (KCM)* ulianzishwa kwa msaada wa fedha na ufundi kutoka Jamhuri ya Watu wa China na kuanza uzalishaji wa umeme wa 6MW mwaka 1988 na kuingizwa katika gridi ya Taifa. Mchakato wa kubinafsishwa ulianza mwaka 2004 chini ya *PSRC* na hatimaye mwaka 2005 kampuni ya *TanPower Resources Ltd* ambayo sasa inaitwa *Kiwira Coal and Power Ltd* ikafanikiwa kuutwaa mgodi huo.

Mheshimiwa Spika, ubinafsishwaji huo wenye utata na mizengwe umesababisha matatizo mengi kwa wananchi, wafanyakazi wa *KCM Ltd*, *TANESCO* na Taifa kwa jumla. Naomba niyataje baadhi tu ya matatizo hayo:-

- Wafanyakazi 1632 kulipwa fedha pungufu fedha zilizotoka *PSRC*;
- Kupotea kwa shilingi 50,000,000/- na wahusika hadi hivi leo hawajafikishwa kwenye vyombo vya Sheria;
- Tathmini ya mgodi huo ya mwaka 1988 ni shilingi bilioni 4.2 lakini tathmini ya mwaka 1991 iliyo fanywa na Taasisi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ni shilingi bilioni saba lakini tathmini hizo zikatupiliwa mbali na Serikali ikaamua kuuza hisa asilimia 70 kwa thamani ya shilingi milioni 700 tu;
- Wawekezaji wanadai wamenunua hisa asilimia 70, Serikali asilimia 12 na zilizobaki asilimia 18 hazijanunuliwa lakini Wafanyakazi wanadai Wawekezaji wana asilimia 85 na Serikali asilimia 15;
- Serikali yenye hisa ndogo ilitenga shilingi bilioni 17 kwa ajili ya ukarabati wa mitambo lakini mwekezaji mwenye hisa nyingi hajatoa chochote hata hivyo hakuna ukarabati wowote wa maana uliofanywa na hata zile MW 6 zilizokuwa zinazalishwa sasa hivi ni MW 0; na
- Mwekezaji ameng'oa baadhi ya mitambo na kuuza kama chuma chakavu kama vile '*Crasher*' lakini huko ilikouzwa inazalisha, je, huu si uhujumu uchumi Waziri atueleze hatua zitakazochukuliwa kwa wawekezaji hawa kutokana na hasara hiyo waliofita Taifa.

Mheshimiwa Spika, hiyo ndiyo sura ya mgodi wa Kiwira *Coal and Power Ltd* unaomilikiwa na Serikali (hisa asilimia 15) na kampuni ya *TanPower Resources* ambayo ndani yake ziko kampuni nne (*Fosnick Ltd, Choice Industries, Devoconsult Ltd* na *Universal Technologies Ltd*).

Mheshimiwa Spika, huo ndio mgodi ambao *PSMP* imepanga uzalishe umeme wa 200MW mwaka 2010 na 200MW nyingine mwaka 2012 wakati Waziri wa Nishati na Madini yeye ameiambia Kamati husika mwezi wa Juni 2009 huko Dar es Salaam kwamba Serikali inafanya juhudini kukwamua mradi huo wa Kiwira wa MW200 ili uweze kujengwa na kukamilishwa mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, huu ni usanii na kulidhifikasi Bunge kwa gharama za walipakodi. Huo mradi wa kumalizika 2011 bila ya kutengewa fedha katika bajeti hii unawezekanaje? Kama Bunge haliwezi kuunda Kamati kuchunguza kadha hii, ni sawa na kukwepa wajibu wetu. Namwomba Mheshimiwa Waziri atoe maelezo ya kina bila woga wala ujanja ujanja, namna gani atatatura matatizo ya Wafanyakazi wa Kiwira, shilingi bilioni 17 zimekwenda wapi, shilingi milioni 50 zimepoteaje, kwa nini kama si ufisadi hicho kilichokuwa kinazalishwa sasa hakipatikani na miujiza gani ya kuzalisha umeme Kiwira 2011?

Mheshimiwa Spika, mradi wa Songosongo, Songas. Nchi yetu imebarikiwa kuwa na Gesi asilia katika maeneo mbalimbali. Gesi hii ikitumika vizuri ni mkombozi mkubwa kwa uchumi wa Taifa letu. Hata hivyo, Taarifa zilizoko kwenye *invoices*, taarifa mbalimbali za *TANESCO* zinaonyesha kuwa wawekezaji wamewekeza tu asilimia 15 na Serikali ya Tanzania au kwa fedha zake, mikopo iliyoidhamini imewekeza karibu asilimia 85 kwenye mradi huu, lakini Serikali ya Tanzania siyo mmiliki na haina nafasi ya maana kwenye vyombo vya maamuzi vya Kampuni hii.

Mheshimiwa Spika, kwa mahesabu ya haraka haraka, kwa malipo ya *Capacity Charge* tu, kwa muda wa miaka 20 ya mkataba, gharama zote zilizowekezwa na wawekezaji zitakuwa zimelipwa na Serikali ya Tanzania kupitia kodi ya Watanzania. Katika hali ya kawaada, katika hatua hiyo, Songas ingelikuwa imetumia kikamilifu mali ya Serikali ya Tanzania kwa niaba ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa Taarifa rasmi kuhusiana na hali hii inayoleta utata. Rasilimali za Taifa letu zisiposimamiwa vizuri na kwa sera na sheria zilizowazi tutaendelea miaka nenda rudi kuwa na gharama za juu za umeme (hasa kutohana na *capacity charge*) na umiliki wenye utata wakati tunatumia fedha nyingi za walipa kodi wetu na au kupitia dhamana zinazotolewa na Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, mradi mwengine uliopewa kipaumbele uliopangwa kutekelezwa kwa muda mfupi ni huu wa Kinyerezi ambao kwa mujibu wa taarifa ya Wizara iliyotolewa June 2009 umepangwa kukamilika mwaka 2011, leo Waziri anasema utakamilika mwaka 2013. Kwa kulikumbusha Bunge lako mradi huu ulikuwemo katika bajeti ya mwaka 2006/2007 na kutengewa fedha, utekelezaji wake ulikuwa ni miaka mitatu. Mwaka 2007/2008 na 2008/2009 haukupangiwa fedha.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Wizara ya kukamilika mradi huu mwaka 2011 bila ya kupangiwa fedha katika bajeti hii inashangaza, ni vyema Waziri atueleze kulikoni? Kwa nini Waziri anatoa matamshi hayo kwa Kamati ya Bunge wakati anajua kabisa kuwa haitekelezeki?

Mheshimiwa Spika, Shirika la Maendeleo ya Petroli – *TPDC*, napenda kulisongeza shirika la *TPDC* kwa juhudi na ufanisi mzuri wanaoendelea kufanya ili kufanikisha majukumu waliyopangiwa. Majukumu yaliyopewa kipaumbele kwa hivi sasa ni pamoja na :-

- Utafutaji na uzalishaji wa mafuta na gesi;
- Mradi wa wa usambazaji wa gesi asilia;
- Hifadhi ya Taifa ya mafuta na uratibu wa ununuzi wa pamoja wa mafuta;
- Uwekezaji katika miradi ya gesi asilia ya Mnazi Bay na Songosongo; na
- Uongezaji wa eneo la bahari kuu ziada ya *neutical miles* 200 linalotegemea Sheria ya Bahari ya UN.

Mheshimiwa Spika, pia naipongeza Serikali angalau kwa kuongeza kidogo fedha iliyotengewa *TPDC* kwa mara mbili zaidi kuliko kilichotengwa katika bajeti iliyopita. Hata hivyo mahitajio ya mambo muhimu kwa faida ya Taifa hili kama yalivyo ratibiwa na *TPDC* bado hayaja karibia hata asilimia 40 ya mahitaji halisi ya shirika hili.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa mifano michache ya mahitajio ya shirika hili.

(1) Hifadhi ya takwimu za mitetemo (*seismic data*), bado kuna kiasi cha asilimia 10 cha ‘*raw seismic data* na asilimia 90 ya takwimu zilizotayarishwa tayari katika mfumo wa ‘*Digital Media*’ ambazo zimehifadhiwa huko Norway, Canada na Uingereza kwa ajili ya kukosa eneo maalum la kuhifadhi hapa Tanzania. Pia takwimu nyengine za miamba na visima ambazo zimekosa sehemu ya kuhifadhi.

(2) Uwekezaji katika miradi ya uzalishaji wa gesi ya Songosongo na Mnazi Bay. Pamoja na Serikali kuridhia *TPDC* iwekeze katika miradi ya *PSAs* katika kikao cha Baraza la Mawaziri Na 3/2008 na kukubali ‘*retention*’ ya asilimia 50 kuanzia mwaka huu wa fedha, bado kiwango kinachokisiwa kupatikana ni kidogo sana kulingana na mahitajio halisi.

Mheshimiwa Spika, utafutaji mafuta na usambazaji wa gesi asilia Dar es Salaam kwa kipindi cha miaka mitatu ijayo(2009/2010 - 2011/2012, yamekadiriwa shilingi bilioni 46.28 (USD 35.6 milioni) ambazo ni wastani wa shilling bilioni 15.43 kw mwaka wakati ‘*retention*’ ya asilimia 50 inakadiriwa kuwa wastani wa shilingi bilioni 7.2 kiwango ambacho ni chini ya nusu ya kiwango kinacho hitajika.

(3) Uwezo wa kuhifadhi mafuta ya akiba katika hifadhi ya *TIPER* ambayo Serikali inamili ki asilimia 50 kama ilivyoamuliwa kutumika kama ‘*Bonded Ware House*’(kikao cha Baraza la Mawaziri cha 9 Februari 2009) bado uwezo wake ni mdogo sana wa kuhifadhi tani 120,000 tu. Uwezo unaohitajika ni tani 300,000 kwa matumizi angalau ya miezi miwili bado haupo kwa hivi sasa. Matanki ya tani 150,000 yanahitaji ukarabati.

Mheshimiwa Spika, matatizo ya kuajiri wataalam wapya wa fani mbalimbali kuziba pengo ambalo litakuwepo mwaka huu wa fedha kwa wafanyakazi waliotimiza umri wa kustaafu, ni vielelezo vyta Serikali kutafuta fedha na kulikwamua shirika hilo. Kutokana na hoja hizo za msingi, Kambi ya Upinzani inaisihi Serikali kutafuta njia zingine za dharura kulikwamua shirika hilo mbali na hiyo *retention* iliyokubalika.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa uagiziaji mafuta kwa ufanisi. Katika marekebisho ya Sheria ya Petrol (*Petroleum Supply Act 2008*) kifungu cha 33(1), kinatamka kuwa uagiziaji wa

bidhaa za petroli lazima ufanyike kwa ufanisi na kwa kigezo cha unaifuu mkubwa wa gharama na kufafanuliwa zaidi na kifungu cha 33(2) ambacho kinaleza ufanisi wenyewe ikiwa ni pamoja na :-

- (a) Uagiziaji wa pamoja wa kushirikiana (*Joint Procurement*);
- (b) Uagiziaji wa ushindani (*Compitative Procurement*);
- (c) Uagiziaji wa shehena kubwa (*Bulk Procurement*); na
- (d) Kwa kutumia fursa ya viwango vya kiuchumi (*Taking advantage of economic Scale*).

Mheshimiwa Spika, pia Sheria imetoa fursa ya kubadili kwenye aina nyingine za uagiziaji utakaoonekana unatija zaidi.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (*EWURA*), Sura ya 414 pamoja na *Petroleum Conservation Act (Cap 392)* imeongezewa majukumu ya kudhibiti na kuratibu uagiziaji mafuta kutoka nje. Pia mfumo wa ununuzi na usafirishaji wa mafuta kwa pamoja umependekeza kuwa na mratibu (*Petroleum Importation Co-ordinator - PIC*) wa kukusanya taarifa za mahitaji na kutayarisha zabuni.

Mheshimiwa Spika, suala hili limeleta mtafaruku mkubwa hivi sasa na kusababisha Umoja wa Makampuni yanayoagiza na kusafirisha mafuta nchini (*TAOMAC*)kukutana na Kamati ya Nishati na Madini zaidi ya mara tatu na kuonesha hisia na maoni tofauti.

Mheshimiwa Spika, Maoni ya Wadau –*TAOMAC*. Katika kikao cha pamoja kilichoitishwa na Kamati ya Nishati na Madini na kuhudhuriwa na *MEN*, *EWURA*, *TPDC* na *TAOMAC* cha tarehe 10 Julai 2009 walikubaliana mambo manane na kutokukubaliana mambo matatu ambayo (wasiyokubaliana):-

- Kabla ya mfumo kuanza *TAOMAC* wanataka kufanyike upembuzi yakinifu wa masuala ya kiuchumi na kiufundi(*viability study*);
- *TAOMAC* inaamini kwamba licha ya kuwepo kwa uwazi bado mianya ya rushwa uwezekano upo katika mfumo huo; na
- *TAOMAC* inaamini kuwa gharama za ucheleweshaji wa meli bandarini zitakwisha pindi gati ya kupakulia mafuta (SBM) itakapokamilika.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hoja za pande zote mbili (Serikali na *TAOMAC*), uzito na unyeti wa sekta hii ya mafuta na uwekezaji mkubwa uliofanywa na sekta hii binafsi na maana halisi ya *PPP* na kwa kuwa Serikali imeshafanya uamuza, hivyo basi utekelezaji wake sio busara kuwa wa haraka bila ya kukubaliana na wadau hawa. Athari za kutekelezwa bila makubaliano kamili, au kutekeleza nusu nusu kwa uchumi wetu, shughuli za kijamii na za kisiasa kutokana na kukosekana mafuta zinajulikana kwetu sote. Kambi ya Upinzani, inamtaka Waziri alieleze Bunge lako Tukufu mkakati mahususi wa kututoa katika uwezekano wa janga hilo.

Mheshimiwa Spika, sekta ya madini. Baada ya kuwasilishwa ripoti ya Mheshimiwa Jaji Bomani kwa Rais na baada ya kuwasilishwa hapa Bungeni na Kamati husika ikapata nafasi ya

kufafanua na na kutoa vipaumbele kwa mambo yanayofaa utekelezaji wake uwe wa haraka pamoja na kutilia mkazo baadhi ya mambo bila ya kuathiri mapendekezo ya Jaji Bomani, ni vigumu kuja na jipyu ambalo halikuwemo katika ripoti ya Bomani.

Mheshimiwa Spika, lingine linaloshangaza na kushtusha, ni pale tunapoona mapendekezo ya Kamati ya Bomani yanapuuzwa na Serikali kwa kiwango kinachotia walakini. Mfano mmoja wa hayo ni pale Kamati ya Bomani iliposema tangazo la Serikali Na 99 la tarehe 15 Oktoba 2005 lilisababisha Serikali kupoteza kodi hadi mwaka 2008 jumla ya Tsh.96.6bilioni.

Mheshimiwa Spika, katika mapendekezo ya Tume ya Jaji Bomani ambayo pia yaliridhiwa na Bunge lako Tukufu na kuitishwa kama Azimio la Bunge ni pamoja na kufutwa misamaha ya kodi.

Mheshimiwa Spika, kwa badiliko alilotoa Waziri wa Fedha la kufuta utekelezaji wa GN 99 kuanzia Julai 2009 kwa makampuni yatakayo sajiliwa sasa, marekebisho haya yanahusu kampuni za madini zitakazoingia mkataba na Serikali kuanzia July 2009. Kwa nini ufutaji wa misamaha hii usiyaguse makampuni yaliyopo hivi sasa? Kambi ya Upinzani, inasikitishwa na tabia hii ya kulinda mikataba ya kifisadi na kupuuza mapendekezo ya Kamati ya Bomani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Bunge hili liliridhia taarifa nzima ya Kamati ya Jaji Bomani na hivyo mapendekezo hayo ya Kamati ya Madini iliyoundwa na Mheshimiwa Rais kuwa ni Maazimio ya Bunge. Kambi ya Upinzani inachoweza kusema ni kumuuliza Waziri ni kwa nini anashindwa kutekeleza Maazimio ya Bunge?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inasisitiza kuwa haikubaliani na hatua hii ya Serikali ya kuendelea kuyasamehe makampuni ya madini ambayo yanaendelea kusamehewa ushuru wa mafuta, hasa ukizingatia kuwa makampuni ya nje yananufaika zaidi kuliko ya ndani (ya nje yanalipa US\$ 200,000 kwa mwaka yale ya ndani yanalipa kwa lita, hivyo kulipa mara tatu ya haya ya nje).

Mheshimiwa Spika, kuna matatizo mengi ya wachimbaji wadogo wadogo katika maeneo ya Kalalani Tanga, Mgusu, Nyarugusu, Mtakuja Geita, Winza Mtakanini Mpwapwa, Simangulu Chamwino, North Mara, Rwamgasa, Kasema, Kilindi Nyamongo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, tarehe 3/4/2009 Mheshimiwa Waziri Mkuu aliufunga Mgodi wa Mgusu kwa matatizo ya ajali iliyoua watu saba. Wakazi wa Mgusu wenye maduara katika mgodi huo ni 971 hivi sasa wanahangaika na siku 90 alizosema Mheshimiwa Waziri Mkuu zimeshapita, hawana mahali pengine pa kuchimba madini na maisha yao yamekuwa magumu.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wadogo wadogo katika eneo la Lusu Wilaya ya Nzega ambao tokea mwaka 1987 walikuwa wamiliki halali wa eneo hilo mionganoni mwao walikuwa wafugaji na wakulima. Wahanga hao hadi sasa wanaishi maeneo ya vijiji vya Mkwajuni, Isanga, Insunga, Ngwanda na Mwaluzilo Nzega Mjini na wengine maeneo jirani na Mgodi baada ya eneo lao kumilikishwa kampuni ya *Golden Pride Mine*.

Mheshimiwa Spika, madai ya wachimbaji wadogo wadogo, hao ni mengi yanatokana na fidia kunyanganywa maeneo yao na wachimbaji wakubwa na mengineo. Kambi ya Upinzani inaona muda umekuwa mrefu sana na kuna haja sasa ya Serikali kuunda Kamati Maalum ya kuchunguza kadhia hizo kwa undani na kutoa suluhu ili Watanzania hawa wapate faraja na kuona Serikali yao inawajali.

Mheshimiwa Spika, haiwezekani Serikali iliyo makini ikawafanya wananchi wake kuwa wakimbizi ndani ya nchi yao wenyewe. Wananchi hao wamefuata njia zote za kawaida na inaelekea njia za kiutawala zimeshindikana. Kambi ya Upinzani, inamtaka Mheshimiwa Waziri kulitolea ufanuzi wa kina hatima ya Wananchi hawa, ama ni lini ataunda Kamati Maalum kuchunguza kadhia hiyo kwa lengo la kuhitimisha mateso haya kwa wananchi wasio na hatia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuupongeza uongozi wa *STAMICO* kwa kuwa na juhudu endelevu za kuliokoa Shirika hilo na kufanikiwa kulifufua. Hali hii inathibitika pale *STAMICO* walipoweza kukusanya mapato zaidi katika mwaka 2008 ukilinganisha na mwaka 2007, walipoweza kufufua mitambo miwili ya kuchoronga, kutengeneza *air-Compressor* moja na pale ilipofanikiwa kupata mitambo miwili ya kuchoronga (*Atlas Copco CS 14*) waliyokodishwa kutoka *EFFCO*.

Mheshimiwa Spika, baada ya *STAMICO* kuwa *De-specified* rasmi kuitia *De-specification Order* ya tarehe 14/3/2009, kwa tangazo la Serikali (*Government Notice No. 88*) inabidi sasa lirekebishe Mtaji (*Capital Structure*), lirekebishwe Sheria na majukumu, lirekebishe muundo na Uimarishaji rasilimali watu, kurejeshewa mali zisizohamishika (majengo) ili kuimarisha mizania yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya upinzani inaitaka Serikali iondoe urasimu na ilete Sheria mpya ya *STAMICO* kwa kasi inayostahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuzungumza pia kwamba katika taarifa aliyoitoa Mheshimiwa Nswanzugwanko kwamba *TPDC* kupendekeza kuwa ya Muungano, suala hilo hatujalizungumza katika Kamati ya Nishati na Madini na mimi sina taarifa hiyo na kama alizungumza labda mimi na baadhi ya wenzangu hatukuwepo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Habib Mnyaa, kwa maoni hayo ya Kambi ya Upinzani.

Waheshimiwa Wabunge, orodha ya wachangiaji niliyonayo ni 62, ambao hawajachangia kabisa ni wanne tu. Waliochangia mara moja ni 28 na nadhani tutamalizia hapo tu sidhani kama zaidi ya hapo itawezekana. Wapo waliochangia mara mbili ambao ni 27 na waliochangia mara tatu ambao haiwezekani kabisa hata kuwafikia, wapo watano.

Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na wale ambao hawajachangia kama Kanuni zinavyohitaji, nao ni Mheshimiwa Riziki Said Lulida, Mheshimiwa Hasnain Dewji, Mheshimiwa Ahmed Shabiby na Mheshimiwa Nazir Karamagi. Kwa mpangilio huo, sasa nitaanza na Mheshimiwa Riziki Lulida atafuatiwa na Mheshimiwa Hasnain Dewji wakati huo Mheshimiwa Ahmed Shabiby ajiandaye.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwa mchangiaji wa kwanza kuchangia hoja hii iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijalia afya njema leo kuweza kuchangia katika hotuba hii ambayo ipo mbele yetu. Napenda kutoa shukrani na

pongezi za dhati kwa Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Ngeleja na Naibu Waziri, Mheshimiwa Adam Malima pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini na watalaamu wake wote.

Mheshimiwa Spika, napenda kufuta usemi wa kusema Mkoa wa Lindi tumeshindwa kupata Manispaa kwa muda mrefu kwa vile huu Mkoa ni Maskini, mapato yao ni madogo. Hili neno kwa kweli kila nikilisikia kwa kweli linanikatisha tamaa na linanidhalilisha sana na hata wananchi wa Mkoa wa Lindi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, mapato yanayopatikana katika mapori ya *Selou* hela zote zinakwenda katika Mfuko wa Serikali na Mkoa wa Lindi haunufaiki na mapato hayo yanayotokana na mapori yetu. Pili Mkoa wa Lindi sasa hivi Mwenyezi Mungu ametujalia, tuna rasilimali zote ambazo zingeweza kuwekwa vizuri na Mkoa wa Lindi ukawa katika Mikoa ambayo ina uwezo mkubwa wa kuweza kuijidesha na kuweza kupata heshima zote kama Mikoa mingine.

Mheshimiwa Spika, nitaanza na mradi wa gesi asilia ya Songosongo Wilayani Kilwa, nataka ninukuu hotuba ya Waziri ya mwaka 2007/2008. Utekelezaji wa miradi chini ya mradi mkubwa wa gesi asilia ya Songosongo unaendelea, ujenzi wa kituo cha megawati 6 kinachojengwa katika eneo la Somanga-Funga umekamilika kwa asilimia 90. Umeme utakaozalishwa na kituo hiki utasambazwa katika miji ya Kilwa Kivinje, Singino, Nangurukuru, Utete, Ikwiriri na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, napenda kukufahamisha kwamba kitabu hiki cha leo kime-copy na ku-paste yale yale ambayo yaliandikwa mwaka 2007/2008, page 26 waliyoyaandika hapa wameyarudia. Inahuzunisha kuona mpaka leo Kilwa iko gizani. Kauli za namna hii, zinaleta maswali mengi kulikoni Kilwa, umeme unapatikana Dar es Salaam lakini Kilwa kwa miaka yote imeendelea kukaa gizani bila kupata umeme, ni nini sababu za msingi?

Mheshimiwa Spika, sitaki kushika mshahara wa Waziri wala kukamata fungu lolote, naomba Waziri awaelimishe vya kutosha wananchi wa Kilwa na Mkoa wa Lindi kwa ujumla ili tuone ni kwa nini na ufumbuzi upatikane. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, leo katika uwekezaji wa Songosongo, Kilwa hatupati *royalty* hata kidogo, lakini Mikoa mingine katika Halmashauri zao wanapata dola laki mbili, je, Halmashauri ya Kilwa itajidesha vipi kama pesa za uwindaji na zingine hatupati? *Service levy* hatupati, *land lavy* hatupati, uwekezaji wa namna gani unawekezwa katika Halmashauri ya Kilwa? (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, uwekezaji huu haumnufaishi mwananchi na wala hautatuondolea umaskini katika Halmashauri zetu. Hivyo Kilwa si maskini, Kilwa ina uwezo wa kutosha isipokuwa mazingira yamekuwa mabovu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, niliuliza swalı ndani ya Bunge lako Tukufu, je, Mkoa wa Lindi kuna nini kuhusu madini? Nikajibiwa kuna *gypsum*, kuna dhahabu, kuna *limestone*, kuna *uranium*, *bluesaphier* na *green tomarine*. Je, hawa wachimbaji wadogo wadogo mmewawekea mazingira gani ili baadaye tusingoje migogoro, kuunda Tume ndiyo tukaanza kukimbizana kwenda Kilwa?

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hivi ninavyozungumza, hakuna kilichotekelawa, Nditi kuna uchimbaji wa ovyo ovyo tu wa dhahabu na wababaishaji wanaokwenda kuchukua dhahabu kwa bei ya kutupa kabisa, leo tunangojea mpaka watu waanze kupigana, waanze kuchinjana, ndio tuanze kupeleka Tume huko. Nafikiri ni wakati muafaka sasa hivi haya maneno ya kuzungumza ambayo hayana uhakika yarekebishwe na angalau sasa hivi wachimbaji wadogo wadogo na wao wakatengewa maeneo yao isije baadaye wakaja kunyang'anywa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nililiza tena swalı lingine kuhusu *gypsum* ambayo inavunwa Kilwa eneo la Mandawa, Kilanjelanje na Mkoa mzima wa Lindi una *gypsum*. Lakini cha kushangaza viwanda vyetu vinaagiza *gypsum* Oman, je, tunaendeleza MKUKUTA katika Mkoa wa Lindi au tunataka kuleta MFUKUTO? (*Makofi/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama tunataka kuaagiza *gypsum* kutoka Oman maana yake tumeamua kuwapa mazingira mazuri watu wa Oman siyo kuwawekea mazingira mazuri Watanzania au watu wa Mkoa wa Lindi.

Ninapenda Waziri vile vile anipe ufanuzi kwa vile sasa hivi tumejaribu kwenda mpaka kiwandani kufuatilia, hawa wafanyabiashara wanajaribu kuwakandamiza kuwaambia basi mkitaka kuleta *gypsum* yenu tutachukua kwa shilingi elfu thelathini kwa tani moja, hivi ni kweli utoe *gypsum* Kilwa, uchukue usafiri mpaka ufile pale bei hiyo ndogo, maana yake nini? Ni kumkatisha mfanyabiashara wa *gypsum* wasiweze kuwapelekea pale na kuhakikisha kwamba yale waliyoyakusudia ya kupeleka ajira sehemu zingine unaendelea, hii haikubaliki kabisa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Waziri aliangalie suala hili kwa jicho la huruma ili na sisi tuondokane na adha hii ya kuwa na *gypsum* lakini hatuna sehemu ya kupeleka. Chukua mazingira ya kutoa *gypsum* Asia mpaka Uarabuni mpaka kufika hapa nchini inachukua mwezi mzima na wanakodi meli na wanawenza kuiuza pale viwandani kutoka Kilwa mpaka kuja Dar es Salaam katika viwanda vyetu vya simenti ni masaa matatu tu, kulikoni wakashindwa kuchukua *gypsum* Kilwa wakachukua mbali ambapo ni gharama kubwa?

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo linanisikitisha zaidi ni kwamba, sasa hivi kuna minong'ono kuwa kandokando za bahari katika fukwe za Lindi kuna mafuta, wananchi wana mashamba yao, wana majumba yao hata kama ni ya kizamani lakini ndipo mahali walipozaliwa, hawaambiwi lolote wanangojea saa ya mwisho kuambiwa ninyi ondokeni, tutakata kuweka uwekezaji na uwekezaji kama huu unamfanya mtu asijue anapelekwa wapi. Ninaomba Waziri atamke kama kweli mafuta yapo kando kando ya pwani ya Mkoa wa Lindi na kama yapo aseme ni wapi ili wananchi wawekewe mazingira mazuri na walipwe fidia zao nzuri na wao wajione wako katika nchi yao ambayo wanahitaji kusaidiwa na kufanikiwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sina mengine, naunga mkono hoja asilimia mia moja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Lulida. Anayefuata sasa ni Mheshimiwa Hasnain Dewji baada yake tunayo dharura ya Mheshimiwa Mohamed Sinani ambaye kwa orodha yangu angekuwa mchangiaji wa saba, ningombia hapo katikati basi nimweke Mheshimiwa Mohamed Sinani. Kama mnavyofahamu, mke wake alipata ajali na leo inambidi aondoke kwenda kuchukua hatua nyingine za muhimu kuhusu matibabu. Kwa hiyo, baada ya Mheshimiwa Hasnain Dewji nitamwita Mheshimiwa Sinani atafuatia Ahmed Shabiby na Mheshimiwa Nazir Karamagi.

**MHE. HASNAIN G. DEWJI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuongea katika hoja hii iliyopo mbele yetu, hoja ambayo inalihusu sana Jimbo langu na wananchi wangu wa Kilwa. Vile vile namshukuru sana Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalamu wote katika Wizara hii. Nawashukuru wananchi wa Kilwa kunisimamisha hapa kuwawakilisha, nawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, *natural gas* ama gesi asilia ambayo imepatikana katika kijiji cha Songsongo ambacho ni kisiwa mwaka 1974, baada ya *AGIP* kusema kwamba pale hakuna gesi, wakati huo Tanzania inapigwa vita sana na nchi za jirani hasa Makaburu wa South Afrika, walificha utafiti ule wakasema hapa Songsongo kuna gesi kidogo mno, hailip. Mkombozi wetu katika gesi ya Kilwa ni Kampuni ya India ikasema kuna gesi ya kutosha, leo wananchi wa Kilwa tunashukuru kuwa na hiyo gesi lakini gesi yenye ni maneno matupu.

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema hivyo, leo Kilwa hali yake ni duni sana ukilinganisha na gesi hiyo ambayo inasaidia gridi ya Taifa kwa asilimia 42 kupata umeme, asilimia 42 inawanufaisha watu wengine sehemu zingine za nchi yetu lakini mwana wa Kilwa hana gesi, hana umeme, hali ni taabani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunapata upinzani wa kijingajinga kwa ajili ya mambo haya, samahani sana kusema hivyo, kwa sababu maendeleo ni ya kila mtu na mimi na ndugu zangu pale tunaishi vizuri tu, upande wa kushoto, upande wa kulia wote tupo sawa, lakini baadhi ya matatizo yanachangia kupata matatizo pale Kilwa.

Mheshimiwa Spika, mradi wa kuzalisha umeme wa Somanga- Fungu, dada yangu amesema na mimi ninasema. Tunamwaibisha Rais, mwaka jana Mheshimiwa Rais ilikuwa aje Kilwa kuzindua mradi ule, leo naambiwa mradi bado ni kitendawili. Tumekula ng'ombe mzima amebaki mkia, nauliza huu mkia hauliwi, nyama yake ni ngumu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana hatuna umeme, leo nimeongea na Kilwa siku saba hatuna umeme. Masomo wameniambia hatuwezi kukuangalia Mheshimiwa Mbunge kwenye TV hatuna umeme. Tunashindwa kuwakilisha, tunashindwa kupata maendeleo kwa sababu hatuna umeme. Kuna kila sababu ya kupata umeme sisi kwanza kuliko sehemu zingine za nchi hii. Naambiwa leo Mheshimiwa Waziri, Jumatatu unajumuisha, utawajibu watu wa Kilwa wewe mwenyewe. Maana mimi naonekana mwongo, naaibika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, siku moja alikuja ndugu yangu, Mheshimiwa Adam Malima, Naibu Waziri, tumeshuka na ndege Kilwa, rafiki yangu akatamani samaki, akasema twende sokoni Mheshimiwa Mbunge, nikamwambia tusiende sokoni, utapigwa mawe, wakishakujua wewe ni Waziri wa Nishati na Madini, utapigwa mawe. Samaki wanaharibika, hatuna maendeleo tusiende, basi hatukununua samaki. Huwezi kuzalisha samaki au huwezi kukamata samaki kwa wingi wakati huna barafu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile nataka njue azma ya gesi asili tuliyokuwa nayo Kilwa kwa nini tusipewe mrahaba. Sikubali, Jumatatu vifungu nitavishika. Hali yetu ni taabani Halmashauri haina hela 200,000 tunazihitaji. Kwenye hiyo sheria mpya inayokuja, naomba tupate mrahaba kwenye gesi asili. Kama sikupata mimi, Mheshimiwa Adam Malima naye baada ya miwili, akianza kuitumia ile gesi yake na yeche atakosa na mama Ghasia atakosa. Kwa hiyo, hiyo sheria yenu mpya mnayosema hapa, umeitaja Mheshimiwa Waziri, nataka unieleze katika kujumuisha kama tutapata mrahaba kutokana na gesi asilia iliyokuwa kwetu Kilwa. Kwa sasa hatupati mrahaba, hatupati fedha yoyote ya maendeleo kutokana na gesi ile.

Hatupati kodi ya kiwanja, hatupati kodi aina yoyote kutoptana na gesi yetu. Sitakubali jambo hili, tukishindana hapa, nakwenda kwa Mheshimiwa Rais, kumuuliza wana wa Kilwa tumekosa nini? Hiyo gesi inayopatikana chini ya ardhi na hizo dhahabu zinazopatikana vyote ni neema ya Mwenyezi Mungu. Kama gesi inapatikana huko chini dhahabu iko huko huko chini tunakosa mrahaba, sikubaliani kabisa. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Sawa sawa.

**MHE. HASNAIN D. DEWJI:** Tunazidi kuchimba visima Songsongo. Tulikuwa na visima vitano sasa tunaambiwa kuna visima saba, tulishaongeza lakini mwana wa Kilwa bado hajaongezeka. Gesi inatakiwa, ina mahitaji makubwa sasa hivi lakini hatuoni maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nikitoka kwenye umeme, nataka niongelee kuhusu utafiti unaofanyika katika mwambao wa Kilwa. Wakati utafiti unapofanyika wa mafuta na gesi, hawatushirikishi sisi Wabunge, tunashtukia tu kampuni fulani inafanya utafiti wa gesi, wanachukua maeneo ya wananchi sisi hatuambiwi, Mwakilishi hana habari labda ambaye ana habari ni *DC* na *Mkurugenzi* tu. Wakati tatizo linapotokea, sasa hivi tuna tatizo Kisongo, Tarafa ya Pande, wananchi wanadai fidia, maeneo yamechukuliwa kwa ajili ya utafiti, ndiyo wanakuja kwa Mbunge, Mbunge tuna tatizo, wakati tatizo lipo ndiyo anatakiwa Mbunge, wakati mnapopeleka mradi kwa nini hamtuambii? Wizara haituandikii kwamba kuna mradi fulani.

Mheshimiwa Spika, leo mimi nina matatizo Kilwa, wananchi wa Kisongo wameshachukuliwa maeneo makubwa, mengine ni mashamba ya korosho. Wanakuja wazee kwangu, Mheshimiwa Mbunge sisi hatujalipwa sina habari. Ninakuwa sina habari ya huo utafiti. Nimeambiwa wameshachukua maeneo kwa ajili ya utafiti na kuweka kambi yao lakini mpaka leo wananchi wa Kisongo hawajalipwa fidia yao. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri mambo mengine mkituficha sisi Wawakilishi mnaficha madonda kwa sababu ugonjwa ule ule unarudia kwa Mbunge, wanakuja jamani kuna hili. Nakuomba ndugu yangu wakati kama mradi kama huu unakuja inabidi tufahamishane. Tatizo likitonea wanamfuata Mbunge. Lakini mimi nilikuwa sina habari ya utafiti wa kule baadaye nikajua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu mrahaba huo wa kupata Halmashauri yangu na kuhusu kituo cha Umeme cha Songomnara, naomba Mheshimiwa Waziri, wakati unajumuisha, tafadhali wajibu wananchi wangu kuhusu azma ya umeme waliyokuwa nayo, tafadhali utujibu tunaomba 200,000 zituendeleze Kilwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, nashukuru kwa kunipa nafasi, nasema siungi mkono hoja mpaka nipata majibu mazuri kutoka kwa Waziri. (*Makofi*)

**MHE. MOHAMED S. SINANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunikubalia ombi langu la kuchangia mapema ili niwahi Dar es Salaam, kuwahi chachu ya maisha yangu kama alivyosema Mheshimiwa Ngeleja. Kwa hiyo, nakushukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa kijiji kile ambacho kulitonea ajali, Kijiji cha Chamangwana kati ya Mlandizi na Chalinze. Mwenyekiti wa kijiji kile na wananchi wa pale walitoa msaada mkubwa sana kwa familia yangu. Mfano ule ni wa kuigwa katika maeneo mengine. Kwa hiyo, nawashukuru sana, ninachukua fursa hii kuitia katika Bunge lako Tukufu, kuwashukuru kwa msaada wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile nitoe shukurani kwa Serikali yetu kwa jinsi ilivyotusaidia katika suala la umeme katika Mkoa wa Mtwara. Katika bajeti hii, imeonyesha kwamba fedha zimetolewa na sasa hivi msongo/gridi ya umeme kupitia katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Mtwara na Lindi sasa utakamilika. Tunashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa shukrani hizo, ninaomba nami nichangie na nitoe mawazo yangu juu ya masuala ya gesi na chumvi. Kwanza nianze na gesi asilia au utafiti wa mafuta. Sasa hivi maeneo ya Mtwara, kuna kampuni ambayo inafanya utafiti na itachimba visima vitatu vya awali baadaye visima viwili na kuna kisima kimoja ambacho nacho kitachimbwa katika Manispaa ya Mtwara. Lakini la kushangaza ni kwamba wawekezaji hawa wakija wanakuja na watu wao, madereva wao, maofisi *boy* wao, wafagizi wao na kupelekea wananchi wa maeneo yale kukosa ajira.

Mheshimiwa Spika, nchi hii Mwenyezi Mungu ametujalia neema katika maeneo mbalimbali. Kuna wengine wamepewa milima inawasaidia, wengine wamepewa Tanzanite inawasaidia na sisi tumepewa gesi, basi na hii gesi itusaidie. Wanapokuja, wanakuja na wafanyakazi wao wananchi wa Mtwara wanauliza hivi huku hakuna mtu wa kufagia ofisi, hakuna dereva, hakuna msaidizi wa ofisi? Tunaomba Wizara iwape miongozo hawa wawekezaji ambao wanakuja kufanya utafiti wa mafuta kwamba wawaajiri watu wa maeneo yale ili kukuza mahusiano mazuri. Huagiza vitu vingine hata nchi jirani. Kwa mfano Mnazi Bay, wapishi wengine walitoka Msumbiji kukaanga tu samaki au kusonga ugali mtu kutoka nchi za jirani! Ina maana hapa kwetu hakuna wapishi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kampuni za *catering* nazo ni za kigeni. Tunaomba hawa wawekezaji wanapokuja, waajiri watu ambao wako katika maeneo yale na wao wafaidi matunda ya rehema ambayo wamepewa na Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, wananchi wanalalamika sana na hii inaweza ikapelekea katika matatizo mengine makubwa zaidi. Hata tulipokwenda North Mara, tulisomewa pale risala, Mheshimiwa Waziri akiwepo kwamba watu wanaagiza hata *stationary* na vitu vingine hata vyakula ambavyo vinaweza vikapatikana katika Wilaya ya Mara vinatoka katika Mikoa mingine au nchi jirani ya Kenya. Kwa hiyo, inaonyesha kwamba hawa wawekezaji wanapokwenda katika maeneo haya wanafanya vile wanavyotaka wao. Kwa hiyo, naomba Wizara inayohusika ijjtahidi kuwaambia hawa watu waajiri watu kutoka katika maeneo yale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, samahani, naomba kurekebisha kidogo, kile Kijiji kulipotokea ajali ya mama watoto, kinaitwa Makweza siyo Chamangwana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya na Mheshimiwa Hasnain Dewji naye amepiga kelele sana juu ya gesi inatoka Songsongo inakuja kuwasha umeme Dar es Salaam wale kule wako gizani. Juzi kuna mtambo umefunguliwa Dar es Salaam ni ile *project* ya kutumia gesi katika magari, nayo huko maeneo ya kwetu sijui tutanufaika vipi. Sasa imeondoka, inawasha umeme katika magari na sisi huku tutanufaika namna gani? Watueleze basi, watafungua walau mitambo midogo na sisi tufaidike au ni Dar es Salaam kila kitu?

Mheshimiwa Spika, nilichangia katika hoja ya Waziri Mkuu kwamba Dar es Salaam sasa itakuwa haitoshi maana kila kitu ni Dar es Salaam na tutajenga *Machinga Complexes* kwa utaratibu huu, hata lukuki na hazitatosha kwa sababu huko tunakotoka nako kunahitajika

maendeleo. Sasa gari zinawekwa gesi, zinabadilishwa na kupewa gesi asilia basi watuambiena Mtware na Lindi, inakotoka gesi na sisi tutafaidika vipi? (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba sasa nichangie katika chumvi. Nakumbuka tulizungumza na Mheshimiwa Waziri katika Kamati juu ya suala la chumvi. Hakuna mtu ambaye hana chumvi katika jiko lake. Majiko yote yawe ya tajiri, yawe ya maskini, kuna chumvi. Hakuna nyumba ambayo haina chumvi. Lakini zaidi ya yote hayo, chumvi ni dawa au kipelekeo cha dawa ya *iodine* lakini naona Wizara ya Nishati na Madini haitilii maanani juu ya suala la chumvi, halizungumzwi kabisa, suala la wachimbaji wadogo wadogo wa chumvi halizungumzwi kuna madini mengine tu.

Mheshimiwa Spika, hata wakati mmoja nilimuuliza Mheshimiwa Waziri kwamba kuna Chuo cha Madini, Chuo cha Madini labda nchi kavu, haya yanayotoka baharini huku hayatakiwi, maana hawapewi elimu, hawapewi mikopo midogo midogo kwa sababu sioni kama kuna mpango wa kuwapa mikopo midogo midogo kama wachimbaji wengine. Sioni wakipewa elimu kwa sababu katika chumvi nako kuna elimu, njia ya kisayansi ya kuandaa *salt pan*, njia ya kisayansi ya kutengeza *free flowing table salt*, chumvi ambavyo tunaitia mezani, inatoka bila matatizo, kuna elimu yake lakini sioni kwamba inazungumziwa.

Mheshimiwa Spika, katika miaka ya 1980 kulifanyika utafiti kwa wananchi amba wanaishi katika maeneo ya miinuko, ikagundulika kwamba asilimia ya 40 wananchi wanaoishi katika maeneo ya miinuko wanakosa madini joto. *Percent 40* ya wananchi wale walikuwa wanaonekana kukosa madini joto. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikafanya utafiti mwaka 1980 na kwanza waliamua kwamba wananchi wapewe vidonge, ikaonekana ni gharama kubwa, ikaja sasa ikaamuliwa kwamba madini joto itiwe katika chumvi, kwa hiyo, zikaanzishwa sheria kwamba lazima chumvi iwekwe madini joto. Kwa hiyo, wananchi wengi walipata madini joto kupitia katika chumvi. Baada ya miaka kadhaa, utafiti ulipofanyika, ikaonekana sasa ile idadi ya watu amba wameathirika kwa kutokuwa na madini joto imeshuka mpaka 8%. Kwa hiyo, chumvi ni kipelekeo kikubwa kabisa cha madini joto na athari zake ni kwamba mama mjamzito anaweza akaharibu mimba kwa kukosa madini joto. Watoto wakizaliwa wanaweza kuwa walemau kwa kukosa madini joto, wanaweza kuwa na matatizo ya akili kwa kukosa madini joto lakini sasa chumvi haitiliwi maanani pamoja na umuhimu wote huu, haiguswi kabisa. Toka mimi nimeingia katika Bunge hili hapajaguswa juu ya madini ya chumvi.

Mheshimiwa Spika, mimi ningeomba Serikali sasa itilie maanani suala la chumvi. *Demand* ya chumvi katika nchi yetu ni tani 125,000 chumvi inayolazimishwa hapa nchini ni tani 15,000 nyingine huagizwa kutoka nje. Lakini tungeweza kuzalisha zaidi kama ungepatikana msaada mdogo wa Serikali kwa kuwajali hawa wazalishaji wadogo wadogo, tukapata na chumvi ya ziada kusafirisha nje. Sasa kwa kukosa chumvi matatizo yake na madhara yake ni kama nilivyoyaeleza.

Mheshimiwa Spika, matatizo mengine ni kwamba wazalishaji chumvi hulipa kodi kwa mali asili ya kukata mikoko. Mikoko hukatwa michache wakati tunapoanza kutayarisha shamba la chumvi kwa kiwango kidogo sana. Inakuwaje walipe miaka yote, yule anayekata miti akajenga nyumba, kwa nini halipi miaka yote miti ile aliyokata pale? Au akakata miti akatengeneza shamba, kwa nini halipi miaka yote? Lakini huyu anayezalisha chumvi anatakiwa kulipia mikoko ambayo amekata mara moja tu alipokuwa anaanzisha shamba la chumvi. Wazalishaji wa chumvi mikoko kwao inawasaidia kwa sababu inapunguza kasi ya mawimbi ya bahari wakati wa *high* na *low tide* au mmomonyoko wa ardhi kwa hiyo, wao hawana bugudha na mikoko. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nashauri Mheshimiwa Waziri ashauri Wizara ya Fedha ufaneti mfano wa Mheshimiwa Magufi ambaye anasema atawaomba Wizara ya Fedha isamehe kodi ya maziwa. Sasa tunakuomba Mheshimiwa Waziri ikiwezekana ushauriane na Mawaziri wenzio wa maliasili waondoe kodi hii. Iondolewe VAT na *import duty* ya *iodine* ambayo inaingizwa hapa nchini kwa sababu ile ni dawa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, hili ni tatizo kubwa na sijui ni kwa nini Mheshimiwa Waziri anasahau maana kila siku yeche anakula chumvi, hata Kamishna wa Madini naye anakula chumvi. Inakuwaje wanashahau madini haya? (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, tija nyingine ambayo inapatikana katika chumvi, inatoa ajira kwa wananchi waishio waishio kandokando ya bahari ya Hindi hususan vijijini. Akina mama hupata ajira kubwa sana katika maeneo haya na kupunguza kasi ya umaskini. Kwa hiyo, zaidi ya kuwa ni dawa chumvi inaleta ajira na pia inatumika na wafugaji kwa kuwapa mifugo yao na pia wanatumia katika kukausha ngozi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofî*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mohamed Sinani, nakutakia safari njema na shughuli za matibabu za mkeo ziende vema. (*Makofî*)

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya mimi kuwa mmoja wa wachangiaji katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini. Vile vile napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri mwenyewe pamoja na Naibu wake na wote ambao wako katika Wizara hii ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, mimi nataka kuanza kuchangia upande wa upatikanaji umeme katika Jimbo langu la Gairo. Ukiangalia katika utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Ibara ya 43 (c), kama inavyoijeleza katika ukurasa wa 13 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, nina wasiwasi kabisa kwamba Ilani itaweza kutekelezeka kwa ufasaha zaidi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2006 nikiwa mmoja wa wachangiaji Julai, 18, nilizungumzia kuhusu upatikanaji wa umeme katika Kata ya Chakwale, Kata ya Kibeja na Kata ya Lubeho na ukiangalia sehemu zote hizi nilizozitaja ni kilomita tisa tu kutoka katika sehemu ambako umeme umeishia katika Mji Midogo wa Gairo. Aliyekuwa Waziri kipindi hicho, Mheshimiwa Msabaha, alieleza kwamba umeme ule ulikuwa bado una nguvu ndogo, ulikuwa wa kilowati 11 kwa hiyo utakapobadilika kuwa kilowati 33, miji Midogo ya Chakwale na Lubeho itapatiwa umeme. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lakini cha ajabu sasa sielewi kila Waziri akibadilika na mipango nayo inabadilika! Kwa sababu ukiangalia katika hotuba ya Waziri ya mwaka 2007 na ya mwaka huu, hakuna sehemu yoyote iliyotajwa kama ilivyoahidiwa mwaka 2006, haipo Chakwale wala haipo Kibeja wala Lubeho wala Msingisi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni, tarehe 27/06/2009, alipokuja Mheshimiwa Rais Chakwale na katika Kijiji cha Ukwamani alipomuita mtalaam wa umeme kueleza ni kwa nini maeneo yale hayana umeme, kilichojibiwa pale ni kwamba katika kijiji cha Ukwamani kumetengwa fedha kwa ajili ya bajeti ya mwaka huu za kupeleka pale umeme. Lakini

ukiangalia katika ukurasa wa 103 ambao unataja sehemu ambazo zitapatiwa umeme sehemu hizi zote hazipo. Sasa sielewi tatizo liko wapi.

Mheshimiwa Spika, sisi Jimbo la Gairo, liko katika Mkoa wa Morogoro lakini kiumeme tunawajibika katika Mkoa wa Dodoma. Sasa hapa inaleta mashaka kwa sababu ukiangalia katika ukurasa wa 103 utakuta kwamba kuna baadhi ya vijiji vingi tu katika Mkoa wa Dodoma lakini katika laini hiyo hiyo ya kwenda Gairo vimepatiwa umeme na viko umbali zaidi ya kilomita 40 na vile vijiji havizidi nyumba tisa au nyumba nane lakini ukiangalia kama Chakwale ambapo kuna wakazi 20,000 wanaoishi kwenye ule mji mdogo. Sasa sielewi hawa watalaam wanafuata vigezo gani kwa urafiki au wanafuata vigezo wanavyotaka wao au kwa vile Gairo iko Mkoa wa Morogoro basi haitakiwa kupata umeme? (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kutoka Dodoma mpaka Gairo, vijiji vyote vimeshushiwa *transformer* na vina umeme. Lakini kijiji cha Ukwamani ambacho kipo Gairo ambapo umeme umepita, haujashushwa pale. Sasa hii hata haifahamika.

Mheshimiwa Spika, kwa vile Mheshimiwa Waziri, kwa mazungumzo yake na yeze alifika Chakwale na aliona na alisema kwamba atajaribu kutenga fedha kwa ajili ya kuangalia upatikanaji wa umeme kwa leo sina haja ya kushika shilingi yake lakini Bunge lijalo kwa kweli sitaiachia hiyo shilingi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia upande mwingine wa mafuta. Mimi ni mfanyabiashara wa mafuta. Naanza na bei ya mafuta Dar es Salaam. Ukiangalia katika Miji ya Tanzania, utashangaa kuona kwamba Mji wa Dar es Salaam bei zake za mafuta kwenye vituo vya mafuta ni kubwa kuliko sehemu nydingine yoyote. Cha ajabu bei ya mafuta katika vituo vya *BP* kwa mfano kama Dar es Salaam kwa petroli ni shilingi 1,540 na ukija kwa hapa Dodoma utakuta *BP* hiyo hiyo inakuwa 1,400 na kidogo. Ukienda vituo vya *GAPCO* au vituo vyote vya mafuta Dar es Salaam vinakuwa na bei kubwa, lakini Mikoani kunakuwa na bei ndogo. Sasa sielewi hawa *EWURA* hii bei elekezi wanaelekeza Dar es Salaam iwe na bei kubwa au wanaelekeza vipi? (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia Miji ya Bandari, uchukue Mji wenye Bandari au shusha mafuta *port* kama Mombasa, Mombasa bei ya *diesel* kwenye bei ya vituo vya mafuta ni shilingi 1,185 mpaka 1,225 Tshs. Lakini kwa bei ya Dar es Salaam hiyo ni bei ya kununulia kwenye *depot* za mafuta. Sasa haieleweki hapa ni nini kwa sababu ushuru tunafanana na vitu vingi sana tunafanana. Hapa inavyoonyesha hamna ushirikiano kati ya *EWURA* na *TRA* kwa sababu hakuna mtu yeyote mwenye kituo cha mafuta anayeonyesha faida zaidi ya shilingi 50 mpaka 80 kwa lita moja ya mafuta. Sasa inakuwaje kwa bei za Dar es Salaam za *depot* kuwa 1,200 mpaka 1,280 lakini bei ya kituoni ikawa ni kuanzia shilingi 1,500 yaani mtu anachukua faida ya zaidi ya shilingi 300. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sijaelewa hapa hii bei elekezi ni bei elekezi ya staili gani au inafuata *population* ya watu kwamba magari yakiwa mengi na bei nayo inakuwa kubwa. Kwa sababu hata sasa hivi ukifanya *research* ukichukua Mkoa wa Dodoma, Arusha, Morogoro, Iringa ukifananisha na Dar es Salaam utakuta bado bei ya mafuta Dar es Salaam ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, halafu bado kuna tatizo, wakati wa hotuba ya Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa alichangia kuhusu uchanganyaji wa mafuta (kuchakachua) wa *diesel* na mafuta ya taa, katika eneo la kuanzia Mdaula mpaka Kibaha kwa Ma-*transport* ambao wanapeleka Mikoani.

Mheshimiwa Spika, lakini cha ajabu katika *seminar* za *EWURA*, mimi bahati mbaya sikuwepo, utakuta wao wanakueleza habari wamekamata vituo vingapi vya mafuta ambavyo vimechanganya mafuta ya taa lakini pale ambapo Wabunge siku zote wanalamika kwamba ndio huwa kuna matatizo ya uchanganyaji wa mafuta wao hawapashughulikii. Tanzania nzima mafuta yanachanganya kuanzia Mdaula, Kibaha na Chalinze na kila siku kuna utiriri wa vituo vya mafuta sio nchini ya mitaa 50 unakuta kuna kituo. Lakini cha ajabu wao anaenda kule anaenda Arusha au Tanga au Mwanza au kokote au Urambo anaenda kupima kwenye *petrol station*, sasa wewe kama *source* iko pale, unaenda kupima kwenye *petrol station* ambayo yule mtu mwenye *petrol station* hana kipimo cha kugundua haya yakoje, weka rangi basi ajue kwamba yakiwa ya *blue* sio ya wake, yakiwa ya kijani ndiyo yake. Lakini huwezi wewe ukaenda ukapima mafuta wakati pale kwenye *source* unajua kama hawapajui, waje mimi nitawaelekeza sehemu moja moja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ukiwaliza, wanakuambia tumejunja ma-*godown* 11 sijui tumewatoza watu wenyenye magala 18 kama alivyojibu Mheshimiwa Malima tarehe 16, walikuta mafuta hayana ubora magala 18 lakini hawaelezi kama hayo magala 18 walimwaga? Kwa hiyo, hayo magala 18 ina maana walisambaza tena kwenye vituo vya mafuta.

Mheshimiwa Spika, sasa hapo udhibiti huu ni udhibiti wa aina gani kama sio udhibiti wa uonevu. Huwezi kwenda kwa mtu mwenye *petrol station* kwa sababu yeye mwenye *petrol station* ananunua *depot*; kutoka *depot* kuna mtu anaitwa *transporter* anasafirisha mpaka yanapofika pale, yanapofika pale mwenye *petrol station* hana kipimo cha kuonesha haya mafuta yamechanganya au hayajachanganya, anashusha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katikati pana *transporter* na siku zote Wabunge wanalamika kwamba wanao changanya ni ma-*transporter*, iko wazi, watu wanachanganya pale mafuta wazi kabisa, sasa hatuelewi hapa kuna nini kati ya *EWURA* na hawa watu wa pale Mdaula mpaka Kibaha au ndiyo mahali wao wanajipatia kidogo ulaji au vipi? Halafu wakija kwenye *seminar* za Wabunge, tunasikia tumezungu vituo fulani, tumepega faini vituo fulani na Wabunge nao kwa sababu hatuelewi tunasema ongeza hiyo faini. Lakini hatuangalii *source* iko wapi. Kwa hiyo, mimi kwa ushauri wangu, kabla hawaajaanza hivi, *otherwise* wakitaka kupata ukweli ni lazima waweke vituo vya kupimia mafuta kila Mkoa au kama hawawezi basi kila makutano ya barabara. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, huwezi ukatoka hapa ukaenda Nzega ukamkamata, ukamwambia umechanganya mafuta wakati yeye hana kipimo cha kujua mafuta yamechanganya vipi na aliyeleta ni mtu mwengine. Hapa ndugu zangu *EWURA*, kwa kweli huwa tunawasifia lakini huwa tunawasifia bila kuelewa tu na wao wana sehemu zao ambazo wanafanya mambo yao halafu huku wanajificha.

Mheshimiwa Spika, hii kama ni kweli kabisa mtu anaenda Mahakamani, anashinda. Hakuna hata kesi moja *EWURA* atakayoshinda pamoja na kuwa na vizibiti vingi. Anayeulta mwengine, anayesafirisha mwengine, anayepokea mwengine, sasa hapo katikati mchezo wote huo unaweza kufanyika, halafu wa mwisho kuuza ndiyo alaumiwe, haiwezekani! Mimi sijawahi kufungiwa kituo lakini kwa namna ninavyoona, huu ni uonevu.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia masuala ya mpango wa *BARRICK*. Kweli mpango wa *BARRICK* unataka muda, lakini na hawa nao watu wenyenye makampuni ya mafuta wa nje nao wababaishaji. Mimi mnunuzi wa mafuta, kwa wiki moja unaweza ukakuta mtu kama *GAPCO* ana-change bei mara nne kwa wiki moja na ushahidi ninao. Kwa wiki moja ana-change bei mara nne...

*(Hapa kengele ililia kuashiria  
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofî*)

**SPIKA:** Nakushukuru Mheshimiwa Shabiby na hasa kwa kuwa unaielewa vizuri sekta hii ya mafuta kutokana na shughuli zako, nadhani wahusika wamesikia.

Mheshimiwa Spika, namwita sasa Mheshimiwa Nazir Karamagi, atafuatiwa na Mheshimiwa Ernest Mabina, wakati huo Mheshimiwa Anna Kilango Malecela ajiandae.

**MHE. NAZIR M. KARAMAGI:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukurani zangu kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hoja ambayo iko hapa mbele yetu.

Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu Mwakapugi, Makamishna, Ndugu Mlindoko na Dkt. Kafumu na kwa watendaji wote ambao wapo katika Wizara hii, kwa kazi nzito wanazozifanya. Kweli Wizara hii ina changamoto na ina umuhimu mkubwa sana katika maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu, kwa sababu sekta hii ni kubwa na nafasi ambayo tunayo ni ndogo, utajikita kwenye upande wa nishati na hususani umeme.

Mheshimiwa Spika, nitaanza kwa kutoa mkakati alioufanya mwanafalsafa mmoja, Lenin, alikuwa mwanamapinduzi Urusi, alipoingia madarakani, Urusi, ilikuwa nyuma kiviwanda, mpango wake mkubwa alioufanya ulikuwa ni kusambaza umeme nchi nzima, *electrification of the whole country*. Kama sisi tulivoamua Kilimo Kwanza, mwenyewe aliamua Umeme Kwanza.

Mheshimiwa Spika, katika mpango huo na Urusi wakati ule walipofanya mapinduzi ilikuwa kama kwetu tu wakulima walikuwa maskini na nini, lakini walibadilika haraka kwa sababu ya mchango wa umeme. Kwa hiyo, umeme unaweza kuwa chachu sana katika kuharakisha sekta zote ambazo tunazzungumzia katika kubadilisha nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imetangaza mikakati mbalimbali ikiwemo ile *Mini Tiger Plan* ya kuwa na viwanda vya kati ifikapo mwaka 2020 au 2025. Suala hili ili lifanikiwe lazima tuwe na mpango madhubuti wa kuweza kusambaza umeme katika maeneo kimkakati, *strategic areas*.

Mheshimiwa Spika, nimesikitika sana niliposikiliza hotuba ya Waziri, amasema kwamba kwa sasa hivi, kati ya uzalishaji na mahitaji kuna upungufu. Mfano amesema mwaka 2007 uzalishaji ukilinganisha na 2008 umepungua kwa asilimia 11; wakati ule ule akasema kwamba mahitaji ya nchi yanaongezeka kwa asilimia 12 kila mwaka, kama hali hii haitarekebishwa haraka, itakuwa hatari sana katika kufanikisha malengo yetu katika dira tulizojojivekea.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa mpango kabambe ambao wametuletea *Power System Master Plan*. Mipango hii ni mizuri ambapo umelenga katika kupunguza haya mliyoyaeleza, lakini tatizo sijaelewa kama pamepangwa rasilimali ya kutosha ili kuweza kutekeleza mpango huo? Kama rasilimali ya kutosha haitawekwa ili kutekeleza mpango huu, basi mpango huu utabaki kwenye makabrasha tu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, unajua tumeshaona kuna hasi kati ya uzalishaji na mahitaji. Hivyo Wizara inabidi kufanya haraka ili kupunguza hasi hii kwa sababu inaonekana mahitaji yanakuwa haraka zaidi ya uzalishaji ulivyo na uzalishaji wa umeme sio kitu ambacho kinachukua muda mfupi, ni kitu cha muda mrefu. Mfano tunajua kwamba uzalishaji kwa kutumia maji ndiyo rahisi, lakini ili kuweza kujenga uzalishaji wa maji lazima utumie miaka mingi, ukianza mpango sasa hivi utafika mwaka 2013-2014. Tunajua kwamba mpango wa haraka haraka ni kwa kutumia gesi maana ule kwa mwaka mmoja tu unaweza kuzalisha umeme kwa kutumia gesi.

Mheshimiwa Spika, sasa ninachomuomba Mheshimiwa Waziri na nimesikia mipango yake aliiweka kwa vinu mbalimbali vilivyozunguka Dar- es Salaam ni kuangalia je, gesi ambayo sasa ndiyo tunaitegemea sana kutoka Songosongo, kuna miundombinu ya kutosha ya kuweza kuleta gesi ya kuweza kuingiza vitu hivi kama alivyozungumza? Kwa sababu, usipofanya hivyo, utakuwa na mitambo ambayo umeishaiweka lakini baadaye ukajikuta gesi huna.

Mheshimiwa Spika, wamewahi kuligusia hivi maana unasikiliza hii sijui *megawatt* 200 ambazo wanataka kujenga 45 halafu kuna ile kugeuza mtambo wa *IPTL* lakini sasa ukija kuangalia, je, gesi inatosha? Kama haitoshi, je, maandalizi ya kuandaa miundombinu mipy ya kuleta gesi kutoka Songosongo ipo? Kama haipo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri awe makini baadaye isije ikatokea kwamba tumefanya hayo yote lakini hatujafanikiwa.

Mheshimiwa Spika, haraka haraka nizungumzie ile ya *EWURA* kuweka *standard aggements*. Mimi nampongeza Waziri kwa kubuni hilo ili kuweka mikataba ambayo ni *standard aggements* ambayo inaweza ikuatuondolea utata ambao umeanza kujitokeza kwa wanasiwa na wananchi wengine ambapo kila mwekezaji anaonekana ni fisadi, ni mbaya. Tukiwa na hii *standard aggements* labda zitaeleweka kwa urahisi ili na sisi Wabunge tuziunge mkono ili kusudi tusije kuwafukuza wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, hii miundombinu ya umeme ni ya gharama bila kuwapa *confidence* wawekezaji, hawatakuja na wasipokuja, sisi ndiyo tutaumia maana kwa kiwango kikubwa uzalishaji utahitaji *private sector*, usambazaji, nakubali lazima Serikali yenyewe lakini uzalishaji kwa kiwango kikubwa utahiatji *private sector*. Kwa hiyo, lazima tuweke mazingira ya kutowakatisha tamaa haswa wale ambao wana nia njema na nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, umeme vijijini. Niipongeze Serikali kwa muda mrefu imetambua kwamba wananchi walio wengi ambao ukiwageuza kidogo tu hata kwa asilimia moja tu katika uchumi wao unaweza kupata *GDP* ya haraka na kubwa; wanaishi vijijini. Pia tumejua kwamba kila wakati kutegemea wahisani kutoka nje inaturudisha nyuma kwa sababu *mnawork* katikati humo anabadilisha mawazo, Mheshimiwa Waziri umekwishesemba inakuwa tabu sana lakini mimi nafurahi kuona kwamba *Rural Energy Agency*, sasa mmeiwekea karibu shilingi bilioni 85, lakini cha kufurahisha kabisa asilimia 90 ya fedha hizo ni pesa za ndani ni asilimia tisa tu ndio za nje. Kwa hiyo, inaonesha kwamba sasa mtakwenda, mtafanikiwa katika lengo hilo kwa sababu lengo lilokwamisha kwa muda mrefu ilikuwa ni utegemezi kwa nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Waziri ulisimamie hilo na pale ambapo miradi imepangwa, uhakikishe kwamba imekamilika pasije pakawa na viporo maana Wabunge wengi tunalamika, wengine wana nguzo zimesimama, wengine wana ahadi

zilizotolewa muda mrefu hazijatekelezwa lakini sasa naona umepata silaha na nina hakika utafanikiwa.

Mheshimiwa Spika, sasa waajiri wangu hawawezi kunisikia vizuri kama nitamaliza bila kuzungumza juu ya matatizo yao ya umeme vijijini, Jimbo la Bukoba vijijini. Nampongeza Waziri kupitia *REA*, angalau wameweza kwa kuanza kutoa matumaini kwa eneo la Bukoba Vijijini, ahadi ambayo ilianzia kwa Rais Mkapa akairithi hiyo ahadi Rais wa Awamu ya Nne. Vile vile akaitoa Rais, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na Mawaziri mbalimbali humo katikati humo wamepita wakitoa ahadi hiyo hiyo bila kufanikiwa. Lakini naona sasa kwa Mheshimiwa Ngeleja, imetua, naona itakamilika.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza kwamba nimeangalia kwenye mpango wenu wa mwaka jana, mmepanga hela za angalau umeme utoke Kanazi upitie Igwela mpaka Kafunjo, baadaye uende Izimbia na mwingine uende Katoro. Mmeanza pesa kidogo mmeweka shilingi milioni 800, nafikiri kwa sababu ule mradi ni mkubwa, kila tutakapo kwenda hamtausahau, mtaendelea kuwa mnaongeza mpaka mradi ukamilike.

Mheshimiwa Spika, kwa hali hiyo, nisisahau, mimi ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Kagera, vile vile niwapongeze kwa kumkumbuka mwenzangu Mheshimiwa Blandes, kwa kukumbuka vijiji vyake vya Nyaishozi, Ihembe, Rugu, Kiruma, Chakaiga Kitundu na Illogwa. Mheshimiwa Blandes amesema hapa sana na kila wakati huwa ananisemea, kwa hiyo, niseme kwa nini namsemea; ni Mkoa wa Kagera, mimi ni Mjumbe wa Halmashauri ya Mkoa wa Kagera. Lakini tunapongeza Mheshimiwa Waziri kwa kufanya hilo. Tutakachokuomba ni kwamba kama ulivyoanza, uende taratibu, tunajua kwamba sungura ni mdogo lakini usisimame kabisa, mradi uende taratibu mpaka ikamilike kabisa jinsi ya uwezo wenu utakavyoweza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa na hayo, lakini kwa sababu nina muda kidogo nizungumzie juu ya utumiaji wa nishati ya gesi ambayo tunayo. Tutambue kwamba gesi ni rasilimali ambayo inamalizika, ni kama madini inamalizika ili tunufaize, inabidi kuiwekeza hiyo nishati katika vitu ambavyo baadaye hata ikiisha vyenyewe vitajiendeze. Ingekuwa katika ile Tume ya Mipango, labda hata hii pesa inayotokana na michango ya gesi iende katika uwekezaji labda wa *uranium* ama iwe mchangano katika *petroleum* kusudi baadaye hata hiyo nishati ikiisha, tutakuwa na uwekezaji tayari katika eneo lingine ambao utakuwa ni endelevu vinginevyo tukitumia tu hivi hivi bila kufanya hivyo, baada ya nishati hii kumalizika, tutajikuta hatuna kitu kingine cha kuweza kuzalisha umeme na tukiangalia kwamba umeme mwingi unazalishwa katika mashariki ya nchi yetu ya Tanzania, lakini watumiaji wakubwa sasa hivi inavyoonekana kwa sababu ya migodi, wako magaribi ya nchi; kwa hiyo kuna usafiri mkubwa kutoka mashariki kwenda magaribi.

Mheshimiwa Spika, vile vile Mheshimiwa Waziri pamoja na kwamba umeanza kufungua kituo cha *megawatt* 60 Mwanza, kuna haja ya kuangalia vyanzo ambavyo vinawewe vikaibuliwa upande wa magaribi kama wenzetu wa Uganda, wanaweza kutumia maji ya Nile kuzalisha umeme, kwa nini sisi tusitumie maji ya Kagera kabla hayajaingia Ziwa Victoria na yenewe yakazalisha umeme mkubwa kusudi kuweza *ku-balance grid* yetu ambayo inayumba kwa sababu ya usafirishaji mrefu kusudi tuwe na uzalishaji mkubwa huku wa magaribi ambao na wenywewe utasaidia wa mashariki kusudi grid ambayo sasa hivi inasumbua mpaka kuwe na kituo cha mafuta Mwanza ambacho najua kitakuwa cha ghali sana kwa sababu kuendesha vituo hivi kwa mafuta ni ghali, vitasaidia *ku-balance hii grid* yetu ya Taifa ambayo itakuwa ni mwelekeo wa mbele kabisa kama ambavyo sijui kama umeufikiria katika

hiyo *Power Master Plan*, kama hamkuifkiria ninaomba na lenyewe kama suluhisho, mliangalie kuliweka katika *Power Master Plan*.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Nakushukuru Mheshimiwa Nazir Karamagi kwa mchango wako.

Namwita sasa Mheshimiwa Ernest Mabina na atafuatiwa na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela wakati huo Mheshimiwa James Musalika ajiandae.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii kuweza kuzungumzia katika Wizara hii ya Nishati na Madini. Niwashukuru Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, ndugu yangu, Mheshimiwa William Ngeleja, Naibu wake, Mheshimiwa Adam Malima, Katibu Mkuu wa Wizara hii, Makamishna wote hasa Kamishna Kafumu wa Nishati na Madini ambaye ananihusu sana mimi.

Mheshimiwa Spika, nitoe angalizo tu kwamba Wabunge wote ambao tunatoka katika migodi au sehemu wanamochimba madini, kwa kweli tuna kazi. Kwa sababu Wabunge ambao tunatoka sehemu hizo, wananchi karibu wote wa Tanzania wanakuwa katika maeneo hayo, kwa hiyo, kunakuwa na mawazo tofauti. Kwa hiyo, inabidi mwakilishi katika maeneo yale, uwe mahiri kabisa kwa kuweza kukabiliana na matatizo ambayo yanajitokeza katika maeneo yale.

Mheshimiwa Spika, sisi tunaotoka kwenye migodi, kitu kikubwa hasa ambacho kinatuhusu ni matatizo ambayo yanajitokeza katika maeneo yale. La kwanza, nipende kutoa pole kwa wananchi wa Mgusu walipata matatizo ya kuangukiwa na udongo na wakafariki tarehe 29 mwezi wa tatu, naomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili lilikuwa kubwa na linatokana na wananchi kukosa maeneo maalum au kutengewa sehemu maalum ya kuweza kuchimba, kwa hiyo, watu au wananchi wanalahazimika kuingia katika migodi ambayo ya zamani, kwa hiyo wanachokonoachokonoa katika maeneo yale kiasi ambacho wanaweza kupata matatizo kama yaliyowapata wananchi wangu kule Mgusu tarehe 29. Lakini pia niishukuru Serikali, Serikali ilifanya jitihada kubwa sana ya kuja kuokoa maisha ya watu wale, uongozi wa Mkoa ulikuwepo, uongozi wa Taifa ulikuwepo lakini jitihada zile zilishindikana. Lakini kwa busara ya Wizara na Waziri na Kamishna wa Madini walilazimika kuufunga ule mgodi kwa muda na ninawashukuru sana wananchi wa Mgusu na Geita kwa ujumla wamekuwa watulivu sana kwa wakati wote ule mpaka sasa hivi hamjasikia lolote, wanasubiri kauli ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namkumbusha Waziri, tarehe 6, alituambia kwamba tumeshafunga mgodi kwa muda wa siku 90 mwezi wa 4, siku 90 zimekwisha tarehe 9 mwezi wa saba. Sasa naiuliza Serikali hawa wananchi watakuwa na hatima gani? Kwa sababu mpaka sasa hivi hawajui waende wapi na Serikali inasema kwamba kunakuwa na mgawanyo wa kazi. Wananchi wa Mgusu kazi yao kubwa ni uchimbaji wa madini ya dhahabu, hawana kazi nyingine, sasa mmeshawafungia mgodi wao, mpaka sasa hivi hamjawafungulia, hamjawaonesha sehemu ya kuchimba, naiuliza Serikali itawapa maeneo gani wananchi wa Mgusu ili waweze kuendeleza shghuli zao za kila siku za kuweza kunusuru maisha yao? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hilo lilikuwa ni swali ambalo nilitaka kabisa Mheshimwa Waziri kama kuna uwezekano basi wananchi wa Mgusu waendelee na shughuli zao, hawana shughuli nydingine zaidi ya kuchimba, kazi yao ni kuchimba tu. Naomba sana Mheshimwa Waziri wa Nishati na Madini kwa busara yako na Wizara yako, najua mtafanya lolote la kuweza kuleta tija ya wananchi hawa wa Mgusu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili. Mtakumbuka kabisa kwamba kulikuwa na mgogoro wa wananchi 47 wa mgodi mpya ambao mpaka sasa hivi wako pale mjini wanakaa kwenye Mahakama na wamejengewa mahema, mahema yale mpaka sasa hivi yameshaanza kuisha na wananchi hawajui hatima yao. Lakini, kauli ya Serikali wanasema kwamba kesi yao bado ipo Mahakamani na uwezekanao wa kushinda kesi hiyo, ni mgumu sana kutokana na jinsi hali yao ilivyo na jinsi tunavyojifahamu, lakini uwezekano wa kushinda kesi ile utakuwa ni mgumu sana. Sasa nawauliza kiubinadamu kama watashindwa kesi ile, mnawaandalia nini na wataenda wapi? Hilo ni swali ambalo nataka kuwaauliza tu. Lakini mlikuwa mmetuambia kwamba Serikali au Halmashauri ya Wilaya itafute maeneo ya kuweza kuwapa viwanja wananchi hawa, nataka kuiambia Serikali kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Geita imepata viwanja 56 maeneo ya Mpomvu ambapo kulikuwa na *Nyanza road*; wameshapewa sasa tunaomba Wizara kama alivyoainisha Naibu Waziri alipokuja pale na akazungumza na wale wananchi, aliwaambia kwamba atafanya jitihada za hali na mali ili iweze kupatikana hela angalau wajengewe nyumba za gharama nafuu, je, huu utaratibu uko wapi na utatekelezwa lini? Hilo nilitaka kulijua wakati wa majumuisho angalau wananchi wangu wa pale mjini ambao mpaka sasa hivi hawajui sehemu ya kwenda, basi wapate jibu la kuweza kuwafurahisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la tatu ambalo nataka kumuuliza Waziri wa Nishati na Madini, kuna wananchi 72 wa sehemu ya Nyamatatakata. Wao waliambiwa na *GGM* waondoke katika maeneo yao, walikuwa 111, 39 wakafidiwa, wakabaki 72, hatima yao iko wapi? Tunaomba watu wale wapewe fidia na wao waweze kujikimu katika maeneo yao kwa sababu wenzao sasa hivi wameshaondoka na eneo lile sasa hivi limekaliwa na *GGM*, lakini wananchi hawa sasa mpaka dakika hii bado wanaangaika, hawajapata fidia, Serikali inasemaje kuhusu wananchi wa maeneo hayo? Hilo lilikuwa ni eneo la tatu.

Mheshimiwa Spika, lakini eneo la nne, nilitaka kuzungumzia wananchi wa Nyakabale. Wananchi wa Nyakabale wamekaa pale kwa muda mrwefu, eneo lile lote liko ndani ya mgodi na wananchi wanapata matatizo makubwa hasa wanapolipua mgodi wao, kwa sababu mgodi wa Geita ni *open cast* ina maana wanapolipua vumbi lote linajaa katika nyumba za watu. Sasa kijiji cha Nyakabale kimeathirika kwa matatizo haya, naiomba Serikali iwaangalie wananchi hawa kwa makini kabisa. Kama kuna uwezekano basi watafutiwe ufumbuzi wa kuweza kunusru maisha yao, hali ya wananchi wa pale Nyakabale ni mbaya mno. Ninaionomba Serikali kama kuna uwezekano, Mheshimiwa Spika, utakapofika Geita basi nikupeleke sehemu za Nyakabale hata wewe utawahurumia wale wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, uliingia pale mjini ukaona mambo ni safi, lakini kuna wananchi ambao wanaishi kando kando ya ule mgodi, maisha yao sio mazuri kutokana na harakati ambazo zinafanyika za ulipuaji na vumbi ambao linawapata wananchi wa Nyakabale.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naingia sekta ya umeme. Geita mpaka sasa hivi umeme wake una nguvu ndogo sana. Naishukuru Serikali, mmesema kwamba mtajenga grid ya Taifa katika maeneo yale, kama utatekelezeka mradi huo, basi itakuwa ni bora. Lakini kuna miradi ya *MCC*, mradi wa *MCC* unakuta kwamba umeweza kubainisha katika Majimbo mawili tu ya Wilaya ya Geita, Geita ina Majimbo matatu, Jimbo la Nyang'hwale, Jimbo la

Busanda na Jimbo la Geita. Mradi wa *MCC* ambao ulikuwa unatoka Geita kuitia kijiji cha Bugurura kwenda Igate, Nzela, Nyamboge, Katoma mpaka Nkome wameufuta ule mradi, namuuliza Waziri, je, hawa wananchi ambao tayari mlikuwa mmewaaahidi kwamba watapatiwa umeme, huu umeme utatoka wapi tena na kwa nini wameufuta huu mradi? Ni vigezo gani vimetumika kuufuta mradi huu wa kupeleka umeme kutoka Geita kwenda Nkome? Hilo nilitaka nipaye majibu ya hakika ili ninapoondoka hapa nikawaambie wananchi wangu sehemu za Nzela na Nkome kama umeme hapa umefutwa lakini mbadala wake ni huu hapa.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kazi inayofanyika katika Wizara hii, hasa katika upande wa *TANESCO*. Nilikuwa na matatizo katika kijiji changu cha Kasamwa lakini waliweza kuweka *transforma* mbili. Lakini mwaka huu mwanzoni mwezi wa kwanza niliwauliza swali na nikainisha maeneo mengi ambayo yalihitaji yapelekewe umeme, katika Kituo cha Afya cha Kasamwa, shule ya sekondari ya Kasamwa, Makanisa mbalimbali, taasisi mbalimbali za Makanisa na wakaniambia kwamba wametenga shilingi milioni 72 kwa ajili ya kupeleka umeme katika maeneo yale, lakini hadi leo hii mradi huu haujatekelezeka, je, wanasemaj? Niliuliza kwamba mnanipa majibu ya haraka haraka kweli huu mradi utatekelezeka? Mpaka sasa hivi, mwaka wa fedha umeshakwisha na haujatekelezwa kweli! Kweli niliyofikiria kwamba hautatekelezeka imekwishajitokeza, nawauliza huu mradi utatekelezeka lini?

Mheshimiwa Spika, lakini cha ajabu kinachowenza kujitokeza hata Wabunge wenzangu mnawenza mkaninga mkono ni pale unapoomba umeme kupeleka *TANESCO* mradi mkubwa kama huu wanakuambia hatuna vifaa, hatuna uwezo. Lakini mfanyakazi akipelekewa mmoja mmoja, hawa wanaofungafunga nguzo za umeme, akipewa nje ya Ofisi, unakuta wanafunga umeme haraka sana kiasi ambacho huwezi ukategemea. Tumekuwa na matatizo kwa sababu tumeenda katika sehemu kama ya Kasamwa, tumeshaambiwa kwamba tutafungiwa umeme, lakini mtu binafsi anapoenda nje ya utaratibu, anafungiwa umeme, je, hivi vifaa vinatoka wapi? Tuulize vifaa hivi vinatoka wapi au viko nje ya vifaa vingine? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba katika sekta hii ya umeme au kwa mafundi hawa ama Mameneja wa Wilaya basi waache mtindo huu mara moja kwa sababu siyo Geita tu, hii nimeisikia Geita, Sengerema nimeisikia, hata Kahama nimeisikia, yote kunakuwa na matatizo ya watu kufungiwa umeme kinyemela nje ya taratibu ambazo zinahitajika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, unaweza ukaambiwa kwamba tutakufungia umeme labda nguzo moja shilingi milioni moja na laki nne. Lakini ukienda nje ukiwapa hata laki sita wanakufungia na kukuwekea nguzo ile ile kwa gharama za nje ya milioni moja na laki nne. Huo utaratibu unatoka wapi na kwa nini tuwape watu faida badala ya kulipa faida Shirika hili? Hili nilitaka kubainisha kabisa kwamba kuna mchezo ambao unafanyika ambao unaliweka Shirika la *TANESCO* katika gharama kubwa wakati watu binafsi wanawenza kufaidi pesa za Shirika lenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya haya machache, nisisahau naunga mkono hoja ya Wizara ya Nishati na Madini kwa asilimia mia moja, ahsanteni sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mabina. Namwita Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, atafuatiwa na Mheshimiwa James Musalika na ajiandae Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia hoja ya Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ambayo ni muhimu sana sana sana katika nchi yetu. Lakini kabla sijasahau niseme naunga mkono kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tukiri kabisa kwamba Wizara ya Nishati ya Madini, ni Wizara ambayo ina ugumu wa peke yake. Lakini naomba kabisa, kwa moyo wangu wote, niwapongeze vijana wangu wawili, Waziri pamoja na Naibu Waziri. Mnajitadi sana na kikubwa ni kwamba mnakuwa wasikivu. Mkiendelea hivyo, tutakuwa tunawasaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hata kama nawasifu lakini sasa nianze kwa kufanya kazi. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwanza nianzie Jimboni kwangu. Mimi nimejaliwa na Mwenyezi Mungu watoto watano lakini mtoto wangu wa sita ni Jimbo langu la Same Mashariki na nimewaadi wananchi wangu kwamba nitawatumikia kwa nguvu zangu zote na vile vijigazeti vinavyosema Jimbo hili liko wazi si kweli. Ni vigazeti uchwara, Jimbo lile lina Mbunge tena Mbunge wa nguvu na wala mwaka 2010 mtu asihangaike kuja huku. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuzungumzia umeme katika Jimbo la Same Mashiriki na hapa naomba Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri mnisikilize vizuri, mimi wala sitaki mishahara yenu. Nimekuwa na tatizo kubwa la viporo kwenye Jimbo langu. Hivi viporo vimeduwa vyta muda mrefu. Sehemu zingine kuna njia kubwa, lakini umeme umeishia hapo kwenye njia kubwa. Sehemu zingine nguzo tu hakuna umeme. Mfano, kuna Kijiji cha Kizerui, ni kiporo cha siku nyingi hicho, muende huko. Kuna Kadando, kuna Mtii, kuna Kizangaze kuna Mroyo, hivi vijiji vyangu vyote ni viporo vyta muda mrefu sana. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, lakini naomba kwa wale ambao hawafahamu, mimi nina Kata 14, Kata nne ndizo za tambarare tu, Kata 10 wananchi wangu wanaishi milimani na huko milimani ndugu zangu kuna miti, kuna mazao, kuna giza. Wananchi wangu hawana umeme, wanalazimika ikifika saa 11 walale, kwa sababu tayari ni giza zito. Hakuna binadamu ambaye angependa kulala saa 11. Kwa hiyo, nawasihi sana Serikali mjue kwamba wananchi wangu wa milimani nao wangependa *ku-socialize* kwamba jioni waweze kwenda kwenye vilabu, lakini kuwe na umeme, wamekuwa ndiyo wateja wakubwa wa tochi. Kila mwananchi ana tochi si chini ya tano. Nina Tarafa mbili za milimani Mambavunta na Tarafa ya Gonja. Umeme umefika sehemu ndogo ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, nimekwenda kuchukua hii karatasi kutoka kwenye Ofisi ya Wilaya ya Same. Kwa hiyo, ni *document* ambayo nikimaliza nitakukabidhi.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nije kazini. Utandawazi ni mzuri sana, una faida nyingi mno lakini utandawazi una hasara nyingi sana tusipokuwa makini na tunapokuja kwenye nishati na madini asilimia kubwa utandawazi unaingia hapo. Kwa sababu sehemu nyingi mambo mengi hatuwezi kuyafanya wenywewe. Inabidi tuwakaribishe na wenzetu wenye uwezo mkubwa, utandawazi hapo, sasa inabidi tuwe makini na mikataba.

Mheshimiwa Spika, nimefanya utafiti wangu mwenywewe kusoma soma vitabu, hii mikataba ambayo tunaingia kwa sababu ya utandawazi, wakati mwingine wenzetu wanaopaswa kuingia mikataba hii hawaingii kwa makusudi. Wakati mwingine, anafanya

makusudi, anajua anachofanya, anafanya makusudi anapindisha, mwingine anafanya kwa kutokujua.

Mheshimiwa Spika, inapokuja haswa *issue* ya madini, wenzetu wa nchi za nje hawa *investors* unamkuta mtu amesomea kuingia mikataba ya madini tu. Amesoma Sheria amekwenda mpaka kwenye *Masters* amekwenda mpaka kwenye *PhD*, yeye ame-concentrate na jinsi ya kuingia mikataba ya madini, jinsi ya kuingia mikataba ya wanyamapor, jinsi ya kuingia mikataba ya utalii. Sisi kwetu wanapokutana na hawa watu ambao wao sasa wanajua jinsi ya kuingia mikataba hii, wanakutana na Mwanasheria tu. Hapa mahali hapa, ni kama ukienda kwenye watu wanapopigana hawa mabondia wanapimwa uzito ili walingane isije ikawa mwingine ni mzito sana na mwingine ni mwepesi sana halafu huyu mzito akamuua mwenzie. Sisi katika uzito wetu kwenye kuingia mikataba na wenzetu hawa sisi tumezidi kuwa wepesi mno.

Mheshimiwa Spika, ninaisihi Serikali ijue kwamba hakuna njia nyingine lazima tuishi na huu utandawazi. Hatuna njia, ni lazima tuishi na utandawazi, muwe na mkakati ambao ni wa dharura tena uanze sasa baada ya mimi kumaliza kusema wa kuwaelimisha watu wanaoingia hii mikataba, wasome ipasavyo jinsi ya kuingia mikataba, kila sekta iwe na watu ambao wame-specialize kwenye kuingia hii mikataba ili tusiwe tunabanwa na wenzetu. Mtu hasomi mkataba vizuri anatia mkono kwa sababu haelewi. Anakutana na mtu mwenye uwezo mkubwa, utandawazi tusipokuwa makini utamaliza Taifa letu. Mheshimiwa Waziri, nafikiri amenielewa, Serikali imenielewa. Ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, sasa nakuja kwenye agenda yangu ambayo ndiyo agenda kubwa. Mimi tatizo langu, huu ni mwaka wa tano nalizungumza kuhusu uchimbaji wa madini ya vito, *Tanzanite*. Naomba Serikali inisikilize vizuri kwa sababu *this time* nimeingia vizuri kwenye *internet*, nimekuja na mifano hai. Hakuna nchi yenyе madini ya vito ambayo inaleta *investors*, madini ya vito, ni madini ambayo hayahitaji *heavy machinery*, hapana. Yako juu juu, yanahitaji *machinery* za kawaida, bado Taifa lina uwezo wa kuwawezesha wachimbaji wadogo wadogo na tukaachana na hawa wanaokuja kutoka nje. Tunapoteza *Tanzanite* yetu sana kwa kumweka mwekezaji kutuchimbia madini ambayo siyo lazima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kutoa mifano, mfano wa kwanza, nchi ya Syrilanka ina madini ya vito na wenzetu madini yao ni gauda safaya, lakini wameweka ndani ya sheria za nchi hakuna *investor* kuchimba madini yale ni wachimbaji wadogo wadogo. Maana yake wana uwezo, nchi ina uwezo wa kuwawezesha wachimbaji wadogo wadogo kuchimba madini hayo. Wachimbaji wadogo wazawa wa Tanzania, wa ndani na wengine wana uwezo wao, wawezeshwe ili wachimbe wenyewe, hiyo ni Syrilanka. Ingieni kwenye *internet*, mtaona. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nenda Madagascar. Wao ni matajiri sana sasa hivi. Tena wamekuwa kama sisi, wao ndiyo nchi peke yake duniani inayotoa madini ya vito yanayoitwa *Pezotite*. Kisheria ile nchi imekataa *investors*. Hakuna mwekezaji anayechimba yale madini, wanaringia madini yao kwamba ni wao wenyewe duniani wanayachimba. Kwa hiyo, wao walichofanya ni kuchimba yale madini wenyewe na kuhakikisha wanakataa wageni, wanaauza wenyewe, ulimwengu mzima unajua ni Madagascar tu. Madagascar wametajirika na madini haya ya vito. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, twende Thailand, Thailand wana *pink ruby*, thubutu hawakubali, wamekatakata kumwita *investor*, wameweka kisheria. Madini ya vito ni yao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, mimi nitamwomba Waziri katika hili, hapa kidogo shilingi nitaishika. Hapa hatutaelewana, ni vema utueleze, kuna ugumu gani wa sisi sasa leo, utujibu vizuri, ni mwaka wa tano huu naongea jambo hili, sasa leo nimechoka, utueleze vizuri leo, mikakati yako ikoje, mpaka lini huyu *investor* ambaye si muhimu kuwepo ataendelea kuwepo? Wazawa tuna uwezo, wachimbaji wadogo wadogo wana uwezo, mbona Syrilanka wameweza, mbona Madagascar wameweza, sisi kwa nini tusiweze? Tukitaka tutaweza, kila jambo jamani linawezekana tukitaka. Tufike mwisho na *Tanzanite one*.

Mheshimiwa Spika, mimi huwa naweka *cuttings*, mwaka 2005 nilisema, mwaka 2006, nikafanya *cutting* ya gazeti moja, naomba Mheshimiwa Spika, uniruhusu ninukuu hili gazeti ni la *Business Times*, likikuwa ni la siku ya Ijumaa, Decemba 2 mpaka 8 mwaka 2005, tena aliyeandika anaitwa Eric Toroka aliandikia akiwa Johannesburg, akilalamika jinsi ambavyo hawa wenzetu South Afrika wanapotosha ulimwengu kuhusu *Tanzanite* nina *exhibit* hapa, wao wana vijarida vyao kwenye ndege zao vinavyotangaza *Tanzanite* lakini hawasemi inatoka Tanzania. Vjarida vyao vinasema *Tanzanite* inatoka Afrika. Kwa nini wasiseme moja kwa moja kwamba *Tanzanite* ni ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ndiyo sababu nasema kuna umuhimu Mheshimiwa Spika wa sisi kuhodhi uchimbaji wa hivi vito, tutokane na mambo kama haya. Huu ni upotoshaji, huu ni udhalilishaji, sisi tuna uwezo wa kuchimba yale madini. Sisemi kwamba tufanye mara moja lakini Serikali hebu nendeni awamu kwa awamu, msichukue muda mrefu sana, muda mfupi tu, tuenze kuwafanya wazawa wenye wachimbe madini ya vito ili jamani tujkwamue kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, tunacheckwa sasa, mimi nimeingia *South African Airways*, unasoma mtu anatangaza *Tanzanite* hasemi inatoka Tanzania anasema inatoka Afrika, kwa nini asitaje Tanzania? Kwa hiyo, Watanzania sisi hatujui kuringa. Turinge, hakuna nchi yenye *Tanzanite* huku duniani, ni sisi tu, lakini tusipokuwa makini hili ni angalizo, itafikia mwisho, *Tanzanite* Tanzania itakwisha kuna mtu ambaye atajitangaza kwamba yeche ndiye mwenye *Tanzanite* huku duniani. Kabla hatujafika huko, hebu tujirekebishe.

Mheshimiwa Spika, sina nia ya kuchukua shilingi ya Mheshimiwa Waziri lakini katika hili atoe maelezo mazuri na Watanzania ambao ndiyo wenye *Tanzanite* waone kwamba sasa na sisi tuko imara kupambana na utandawazi. Utandawazi unaua, utandawazi unaponya. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hali yangu ya mafua na hali ya baridi humu ndani haviendi vizuri, kwa hiyo, naomba kidogo nikapumzike. Namwomba Mwenyekiti, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, aje aendeleze shughuli hadi hapo baadaye.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Zubeir Ali Maulid Alikalia Kiti)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Sasa namwita Mheshimiwa James Musalika, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi na Mheshimiwa Profesa Feetham Banyikwa ajiandae.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikushukuru kwa kwanza, kwa kunipa nafasi nichangie hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini. Lakini ningependa kwanza niwapongeze sana Waheshimiwa Mawaziri, Mheshimiwa Ngeleja, Mheshimiwa Malima, kwa ushirikiano wao ambao wanatuonyesha Wabunge tunaofuatilia masuala ya umeme na masuala ya Wizara yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niwapongeze Watendaji wote wa Wizara kuanzia Katibu Mkuu na hata wale ambao wapo kwenye hizi *programs* za MCC, REA wana ushirikiano sana na baada ya kuwapongeza, sasa nao nitaomba wanisikilize shida zangu, naanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuanzia na umeme kwenye Jimbo la Nyang'hwale. Kwa muda mrefu sana, nimekuwa nikipigia kelele umeme na kwa sababu wananchi wangu wamekuwa wakinituma hilo hususan wananchi wa Kijiji cha Karumwa ambao kwa miaka mingi sana wamepitwa na nyaya za umeme unaotoka Shinyanga kwenda kwenye mgodi wa Bulyanhulu na ule umeme unaotoka Bulyanhulu kwenda kwenye chanzo cha maji ya kwenda Shinyanga. Lakini baadaye nimefurahi sana kwa hotuba ya Mheshimiwa Waziri na hotuba cha bajeti nimesoma kwamba sasa Jimbo la Nyang'hwale litapata umeme chini ya mradi huu wa MCC.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niishukuru sana Wizara kwa kukubali maombi ya wananchi hasa wa Karumwa ambao waliomba umeme huo badala ya kutoka Kasamwa ambako ni mbali kidogo utoke pale kwenye *sub-station* ya Bulyanhulu na wataalam wa mradi huu pale Ubungo wameniambia utakuwa na kilomita 70 na umeme utatoka kituo cha kupozea umeme yaani *sub-station* pale Bulyanhulu kwenda kijiji cha Karumwa na baadaye utakwenda Ilkangara, Kijiji cha Kitongo, Nyarubere, Nyijundu, Nyaruguguna na hatimaye Nyang'hwale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pale Nyarubere, ni sehemu kubwa kidogo kwa sababu pale kuna Kanisa kubwa sana na jirani sana kuna shule ya sekondari Kakola. Kwa hiyo, nadhani sasa nitaomba hapa ndugu zangu TANESCO wakishapitisha umeme wa MCC wateremshe sasa umeme kwa wananchi katika vijiji ambavyo nimeshavisema hapa kwamba baada ya *line* kupita mara moja TANESCO nao wafunge waya katika nyumba za wananchi isije ikawa tena kama kilichotokea Karumwa kwamba umeme umeshapita Karumwa, umeme umepita juu ya watu lakini pale chini kwa wananchi hawana umeme. hili ninapenda sana lifanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na kutekeleza huo mradi maana nimeambiwa sasa upimaji wa njia za umeme tayari umeshafanyika, kinachofanyika sasa hivi ni uthamini wa mali na mazao ya wananchi. Kwa hiyo, hili nalo ninapenda lifanyike, naomba sana kabla ya mradi kutekelezwa, uthamini huu uambatane na ulipaji wa fidia. Tumeshaona miradi mingi ikifanyika kabla ya ulipaji wa fidia, baadaye sasa mradi unakuwa kero kwa wananchi na ni kero zaidi kwa Mbunge kwa sababu itabidi sasa turudi Bungeni hapa kupigia kelele suala la ulipaji fidia za wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme huu ukishafika pale Nyang'hwale, utakuwa umeishia kilomita 70. Lakini sasa pale Nyang'hwale kijijini, pale kwenye *centre* utakuwa umeacha Kituo cha Afya cha Nyang'hwale na Shule ya Nyang'hwale kwa upande mmoja na iko kilomita kama nne hivi. Halafu kwa upande mwininge kutokea pale Nyang'hwale kama kilomita tano, kuna kijiji cha Busolwa, pale kuna *centre* kubwa, Busolwa ina wafanyabiashara wengi tu na wana nyumba za kisasa, matofali ya kuchoma, pia na kuna sekondari na mgodi mdogo wa dhahabu. Wako katika hatua ya kuanza kutekeleza, yuko mwekezaji mmoja anaitwa Alhaj Kilahama ana mgodi wake pale na yuko katika hatua ya kuanza kutekeleza mradi wake kwa kuanza kuchimba, sasa watahitaji umeme sana. Kwa TANESCO pale watauzi vizuri sana umeme na wananchi wako wengi nimesema, kuna wafanyabiashara na nyumba nyingi tu nzuri za kuweza kufungwa umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitoka pale, kuna kijiji cha Ngoma, lakini labda ni-*declare interest* hapa kwamba Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, ni jirani yangu kwamba Kijiji cha Busolwa kwenye Jimbo langu kinapakana na kijiji cha Ngoma na kwa hiyo wananchi wake nawajua na wa kwangu anawafahamu pia na mazao yanafanana. Sasa pale Ngoma ni *centre* kubwa sana lakini pia na penyewe kuna mgodi, wanafanya utafiti *Barrick* na nadhani wakati wowote nao watafungua mgodi. Kwa hiyo, mahitaji ya umeme katika hivi vijiji viwili ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna maombi ya wananchi wa Busolwa, Nyang'hwale na wale wa Ngoma kwa Mheshimiwa Waziri mwenyewe kwamba wameshamwambia na mimi wameniambia wameshamwambia, namkumbusha hapa, walishamwomba umeme wananchi wa Ngoma na wananchi wa Busolwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri ana dhamana na Wizara hii lakini kuna siku moja, nimkumbushe kuna Waziri mmoja hapa ndani tulimwuliza kwenye Kamati, wewe mbona unapeleka miradi ya barabara kwako? Akasema, mpishi naye huonja! Sasa na wewe nakukumbusha tena usisahau kuonja pale Ngoma ukiwanyima umeme wale na wale wa Busolwa ukiwanyima umeme, adhabu yako na mimi wanayo mwaka kesho. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna huu mradi wa *REA*, mradi wa usambazaji umeme vijijini, kwa kuwa *MCC* inaishia pale Nyang'hwale, ninaomba sasa *REA* ianzie Nyang'hwale kule kwenye Kituo cha Afya iingie Nyang'hwale *Centre* kama kilomita nne, tano kwenda Busolwa na kilomita kama saba hivi kwenda pale Ngoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika kitabu chako cha bajeti, nimeona kuna umeme nadhani unatoka Busisi kwenda Buyagu pale kuna *ginnery* na leo asubuhi hongera sana umesema umepata mwekezaji Shirika la Kidini wanajenga Chuo Kikuu pale Isore, moja kwa moja watahitaji umeme utakuwa umesogea ukitoka Buyagu kuja Isore umesogea karibu na Ngoma. Sioni sababu ya Mheshimiwa Waziri kushindwa au Wizara kushindwa kuunganisha umeme kutoka Buyagu - Isore - Ngoma - Busolwa - Nyang'hwale. Usipofanya hivyo, Mheshimiwa Waziri, majibu hayo sijui kama utakuwa nayo mwaka kesho, sijui, sina hakika. Wananchi wanazalisha sana mahindi, pamba, mpunga, wana mifugo bila shaka tukipata umeme watu sasa wataanza kujenga viwanda ili wananchi wa maeneo yale wapate ajira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nije sasa kwenye tatizo la uchanganyaji wa mafuta. Watu wenye magari wanalamika sana kwamba baadhi ya vituo vya mafuta vingi sana wanachakachua mafuta ya dizeli na mafuta haya baada ya kuyachakachua yanaharibu mitambo, pampu na injini za magari yao. Hili *EWURA* wanalfahamu na hawa wafanyabiashara wa mafuta hawajali, kwa sababu Sheria iliyopo ni nyepesi sana, kwamba akikamatwa analipa faini ya shilingi milioni tatu lakini kinachoendelea ni kwamba katika *process* ya kuchakachua wanafanya *ratial* ya asilimia 30 kwa 70 kwamba katika lita laki moja, 30,000 anaweka mafuta ya taa, lita 70,000 ni dizeli, jumla hapo ni laki moja. Faida inayopatikana pale ni haramu, ni shilingi milioni 18. Kwa hiyo, akikamatwa na hawa watu wa *EWURA* analipa hizo milioni tatu atakuwa bado ana faida haramu shilingi milioni 15. Kwa hiyo, anaweza akafanya makosa mara sita bado hajaingia kwenye hasara kwa sababu atakuwa anacheza kwenye faida haramu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watu wana mtandao wao hata *EWURA* wanafanya kazi katika mazingira mazito, wengine wanatishia. Nadhani hapa tungerekebisha Sheria kwamba mtu anayekamatwa anachakachua mafuta adhabu yake ya kwanza kabisa ni kumfungia na kumfilisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, afungwe na afilisiwe. Sasa hivi kila mtu anafanya biashara ya mafuta, ukitoka pale Mlandizi kwenda Ubungo yaani Vituo vya mafuta ni vingi kuliko ile miti ya mikorosho iliyoko pale njiani. Kwa hiyo, kuna faida haramu kubwa sana na Sheria haitoshi, haina meno ya *EWURA* kuweza kuwazuia. Hili nilikuwa nakuomba sana uliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la mwisho, niseme haraka haraka, ni usalama wa raia kwenye vituo vya mafuta. Huko nyuma maelekezo yalikwishatoka, sina uhakika kama ni sheria kwamba *bus* linapoingia kwenye kituo cha mafuta abiria wanatakiwa wateremke ili kuepuka ajali ya moto ambayo inaweza ikatokea lakini hili halifanyiki. Lakini mbaya zaidi, nadhani inagusa hata Wizara ya TAMISEMI, inagusa pengine *EWURA* na Wizara yenyewe kwamba kuna *time bomb* wanaita, tunasubiri kupata matatizo makubwa sana watu wengi kuangamia, kuna baadhi ya vituo vya mafuta vya petroli viko kwenye makazi ya watu na Wizara husika inatoa leseni na mifano mingine iko wazi wazi kabisa. Pale Dar es Salaam pale Buguruni kuna hoteli moja inaitwa *Three Way* lakini pale pale kuna kituo cha mafuta kikubwa sana. Kwa hiyo, wale watu ambaa wanakaa kwenye ile hoteli maana yake wana *risk* ya moto wakati wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Singida, kuna kituo cha mafuta, magari yote ya kwenda huko Mwanza, Shinyanga, Kagera, Bara huko, yanapita pale kunywa mafuta lakini pale kuna Mgahawa wanakula, kwa hiyo, wakati wote pale kuna watu ambaa wana-*risk*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo Gairo hapo, kwa Mheshimiwa Shabiby, ana mabasi yake pale, mabasi yake yanakunywa mafuta pale Gairo. Mabasi yote ya Shabiby, ya kutoka Dar-es-Salaam, yanapita pale yanakunywa mafuta pale na abiria wakiwa kwenye basi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo Dodoma, kuna *Shabiby Petrol Station*, pale chini kuna Mgahawa, halafu kwa juu kidogo kuna *Super Market*, halafu kwa usiku kuna ukumbi wa diskon; kwa hiyo, pale masaa 24 watu wanasubiri moto siku moja. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Wizara husika au mamlaka husika wanaangalia tu, baadaye yakinoteka, Waziri Mkuu aunde Tume ya kuchunguza na kuja kulishauri Bunge namna ya kufanya. Sina hakika kwamba hii inahitaji Tume, ni busara za kuamua sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kenya imetokea na hapa Mbeya imewahi kutokea, gari la mafuta linaanguka, wananchi kwa sababu ya ukiasi wao wanaenda kuchukua mafuta, wenzetu wanaanza kuchukua tahadhari; sasa sisi tumeshachukua tahadhari gani? Nadhani mnaotoa leseni za mafuta ya petroli kwenye makazi ya watu, hatutahitaji kuwaundia Kamati, tutawataka muwajibike siku hiyo hiyo, moto ukitoka muwajibike na Serikali kwa ujumla pale itabidi iwajibike kwa sababu suala hili linafahamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sipendi kupigiwa kengele, nasema naunga mkono moja, ila nawakumbusha tena watendaji wa Wizara, umeme wa Nyang'hwale, naomba sana, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja hii ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siko tofauti na wale wachangiaji wawili waliotoka Mkoa wa Lindi, Mheshimiwa Riziki Lulida pamoja na Mheshimiwa Hasnain Gulamabbas Dewji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa uchungu mkubwa, nitazungumzia kuhusu gesi ya Songosongo peke yake kama nitapata nafasi ya kuendelea nitazungumza mengine zaidi, lakini nitazungumzia kuhusu gesi ya Songosongo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu, tumekuwa tukilia kilio kuhusu gesi hii. Takribani tangu mwaka 1974, gesi hii ilipogunduliwa, wananchi wa Mikoa ya Kusini, waliunda Umoja wao wa Maendeleo wa Mikoa ya Kusini. Wananchi hao walikuwa kama 15 katika umoja huo. Wananchi hao waliliona jambo hili kwamba itakuwa ni kitendawili kwa wananchi wa Wilaya ya Kilwa, Mkoa wa Lindi na Kusini kwa ujumla, kufaidika na mradi huu wa gesi ya Songosongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nitatoa historia ndogo, kwanza nitaeleza kwamba katika kila mahali kuna *National interest* na vile vile kuna *interest* ya mahali ambako mtu anaishi. Imekuwa ni tatizo kubwa kwamba mradi huu umekuwa ni kwa *National interest* tu na sio wananchi wa Mikoa ya Kusini, kwa kweli hili ni jambo la kusikitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Mikoa ya Kusini walipogundua jambo hili, waliunda Kamati ambayo inafuatilia masuala haya. Kulikuwa na barua ya kwanza ya Wakili, ambayo ilipelekwa kwa Mheshimiwa Lamwai, ambaye alizungumzia suala hili, kwa kuona kwamba mradi wa gesi ya Songosongo, wananchi wa Kilwa, wananchi wa Mkoa wa Lindi, hawanufaiki. Kwanza *pipe* yenyewe imetolewa Songosongo ikaletwa Somanga, ambako ilitakiwa waweke *T*, ambapo *T* hiyo, sehemu moja itaelekea Dar-es-Salaam, sehemu moja ilekee Mikoa ya Kusini, lakini hilo halikufanyika. Kwa hiyo, kutoka hapo kukawa na mgogoro amba wananchi wa Kilwa, hawakutaka kuendelea na mradi huu kwa sababu ni wa manufaa ya Taifa tu na wakati wenyewe hawapati kitu chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo kulikuwa na mkutano amba ulifanyika tarehe 27/08/1995 na Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Pili, lakini na hapo haikufua dafu. Kulifunguliwa na kesi, nayo haikufanikiwa. Mkutano wa Madiwani na Mawaziri, ulifanyika kwa ajili ya kudai haki hizo kwa wananchi wa Mikoa wa Lindi na Kusini, amba ulifanyika tarehe 27/05/1997, pia hatukufua dafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hayo, hapa nina muhtasari wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Oktoba, mwaka 2005. Hii Ilani inaeleza kuhusu sehemu ya nishati, ukurasa wa 24, nitasoma yale yanayohusu upande wa Kusini, sisomi yote. Sehemu moja imeeleza kwamba:-

*“Kufikisha umeme katika Miji Mikuu ya Wilaya.”*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mpaka sasa hivi, Miji Mikuu ya Wilaya, haijafikiwa na umeme. Pamoja na hayo, Wilaya ya Kilwa ambako ndiko Songosongo ilipo, hakuna umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na lingine limesema kwamba:-

*“Kuhakikisha gesi ya Songosongo, inafika majumbani ili kupunguzia matumizi ya kuni na mkaa.”*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya, kama Wilayani umeme haujafika, je, hawa wananchi wa vijijini wanaotumia kuni wataupata lini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili linahitaji lifanyiwe kazi na wakati Mheshimiwa Waziri, anafanya majumuisho atueleze. Najua wao wamelikuta, lakini kwa sababu wao ndio wenye dhamana kwa sasa hivi, nina hakika watalifanyia kazi. Kama hawakulifanyia kazi wanangojea mwaka 2010 walioutamka hapa, kwa ajili ya uchaguzi, waandike wameumia katika Wilaya na Mkoa wa Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa katika meza, hii nina gazeti la Uhuru, la tarehe 01/02/1997, naomba kunukuu. Gazeti hili liliandika kwamba:-

*“Pingamizi la wananchi lasimamisha ujenzi wa njia ya gesi Songosongo.”*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni moja ya malalmiko ya wananchi wa Mikoa hii ambayo walikuwa wanalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gazeti lingine la Taifa, la tarehe 08–14 Septemba, 1996, liliandika habari ifuatayo:-

*“Sakata la gesi ya Songosongo, Mbilinyi, Dokta Harid, Magani, waukana Umoja wa Kusini.”* (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kwamba hawa waliukana umoja huu baada ya kupata nafasi kubwa kubwa, kama za Uwaziri. Wakati huo kabla hawajapata hizi nafasi, walikuwa pamoja na wananchi wa Mikoa ya Kusini katika sakata hilo lakini baada ya kupata nafasi hiyo, wakaona kwamba haina maana kuendelea kwa sababu na wao ni mionganoni mwa wale ambaa wanahujumu maisha na hali halisi ya wananchi wa Kusini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi inaniuma sana. Inaniuma kwa sababu sisi tumekuwa tukiitwa wananchi wa pembezoni, tumekuwa tukipewa jina la umaskini, lakini ukiangalia rasilimali tulizonazo katika maeneo ya Kusini haifanani kabisa na sisi kuitwa watu wa pembezoni, jina ambalo linaashiria sisi tupewe misaada tu wakati rasilimali zetu tunazo. Kuitwa “*Wamachinga*”, hayo yote ni majina tunapewa sisi, lakini sisi katika Mikoa ya Kusini tuna rasilimali zinazotuwezesha kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukosekana kwa gesi ya Songosongo, kwenye Kitabu hapa cha mambo ya Mradi wa Songosongo, wamesema kwamba:-

*“It will provide power, gas and associate economy benefit to Songosongo Island and the community along the pipeline route.”*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi katika Mkoa wa Lindi, achana na Mikoa ya Kusini, Mkoa wa Lindi tuna Wilaya sita na kama wata-*provide* umeme huu, hii *pipeline* ndio watapewa umeme, je, Wilaya nyingine kama Liwale, Ruangwa, Nachingwea, Masasi na zile nyingine umeme wataupata wapi kama gesi hii itakuwa inaenda Dar-es-Salaam na watu watakaopewa *benefit* za huu mradi ni watu waliokuwa kwenye *pipeline* tu? Ninasema kwamba hii si haki. Ninapenda kusema kwamba kama Ilani inavyosema, itekelezwe na sio

mnanipamba hapa kwa kura nyingi, kwa mambo mengi wakati wa kuitisha kura lakini mambo haya huyatekelezi, napenda Ilani itekelezwe. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote nimeyazungumza kukumbushia kwamba sisi wananchi wa Mikoa ya...

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kuhusu Utaratibu, endelea!

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 73(3) inasema:-

*“Endapo Mbunge ye yote atatakiwa kuthibitisha ukweli wa maneno aliyoyasema...”*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilitaka tu atuthibitishie ukweli, kwa sababu Mheshimiwa Marehemu Harid wala Mheshimiwa Magani, hawakuwahi hata siku moja kuwa Mawaziri katika Serikali. Kwa hiyo, amesema maneno ambayo sio ya kweli. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, kaa kwanza. Labda nimpe nafasi tu ili aweze sio kufuta, lakini aseme tu, alionekana kama alikuwa anasoma sehemu, ili atuthibitishie ni kitu gani.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 63(4) inasema kwamba:-

*“Yule ambaye anaona ya kwamba mimi ninazungumza uwongo, athibitishe kwanza yeye ndipo na mimi nthibitishe.”*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mimi ninaongea uwongo, ninafikiria Mheshimiwa atanimbia, kwa sababu hawa niliowataja ndio wengine walikuwa kwenye hiyo Kamati ya Umoja wa Maendeleo ya Mikoa ya Kusini. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Samahani, ulichokisema ni kwamba wamo kwenye Kamati kama Mawaziri au vipi maana sikuelewa kidogo hapo.

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MWENYEKITI:** Naomba ukae Mheshimiwa, mimi niko na huyu ambaye umemtolea Utaratibu.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sikutaja Mawaziri, nimesema kwamba...

**MWENYEKITI:** Aaah, hakutaja!

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Sikusema Mawaziri, nimesema viongozi...

**MWENYEKITI:** Ongea na mimi tu, usiongee na Bunge, ongea na mimi.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema viongozi ambao walikuwa katika umoja huo, katika mkutano, ndio nilipotaja Mawaziri. Mkutano ambao ulifanyika...

(*Hapa kulikuwa na minong'ono*)

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Subiri!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, nakuomba uendelee kuchangia. Malizia mchango wako halafu baadaye tutaangalia kwenye *Hansard*, ili kujuu uhalisia ukoje na baadaye tutarekebisha baada ya hapo. Naomba uendelee tu na mchango. (*Makofi*)

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nimeeleza historia hiyo ili kuonesha kwamba sisi wananchi wa Kusini, tumerudishwa nyuma. Kulikuwa na kiwanda, *KILAMCO*, ambacho kilitakiwa kujengwa Kilwa Masoko wakati wa mradi huo, lakini kiwanda hicho hadi leo hakijajengwa, wananchi walitoa maeneo yao, lakini hakijajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungepata viwanda vingi haswa kwa wakati huu ambapo tuna *gypsum*, tuna utalii uliokubuhu katika maeneo yetu, lakini watu hawa wanashindwa kukaa katika maeneo yetu kwa sababu hakuna umeme. Walimu tunawapata, lakini vilevile kama alivyosema msemaji aliyetangulia, Walimu hawa ni vijana, wameishi kwenye mazingira ya umeme, wameishi kwenye kutumia vitu vya umeme, wakija Kilwa, wakija Mikoa ya Lindi, MtWARA, wanashindwa kufanya kazi kwa sababu vitu hivyo havipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyozungumza, ni wiki karibu na nusu sasa, Kilwa Masoko Wilayani, umeme hakuna. Hili ni jambo la kawaida katika maeneo yetu. Kutokana hayo na ndio maana nimesema kwamba zinapozungumzwa Ilani za Uchaguzi zitekelezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu fikirieni, kuanzia mwaka 1974, kipindi ambacho gesi ya Songsongo imepatikana, gesi hiyo imeelekezwa Dar-es-Salaam, lakini Mikoa ya Kusini hakuna; hizi Ilani zinatekelezewa wapi? Nitazungumza na nitazungumza, labda mnangojea mwaka 2010 ndio mtuletee umeme katika maeneo yetu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sheria ya Umeme inayopitishwa, ninaitaka Serikali kwanza iweke sheria ambayo itafuta ile mikataba feki iliyopitishwa katika mlolongo mzima wa gesi ya Songsongo.

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji*)

**MWENYEKITI:** Naomba uunge mkono hoja, ili tuendelee.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu, unajua nimekatishwa?

**MWENYEKITI:** Aaaah!

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MHE. PROF. FEETHAM F. BANYIKWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa fursa niweze kuchangia kwenye hoja hii ya Waziri wa Nishati na Madini. Awali ya yote, nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Waziri William Ngelleja, Naibu Waziri, Mheshimiwa Adam Malima, Katibu Mkuu, Ndugu Mwakapugi na Wakurugenzi wote waliomsaidia Waziri, kutekeleza majukumu yake ya kuandika hotuba nzuri. Nianze kwa kusema ninaiunga mkono hoja hii. Ninaiunga mkono hoja kwa sababu nimesoma na baada ya ile semina ya *TANESCO*, kwa kweli nimejiridhisha kwamba Wizara imejipanga vizuri kuleta maendeleo katika sekta ya umeme na madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nizungumzie umeme wa Ngara – Kabanga. Katika miaka ya karibuni na kwenye Ilani ya Uchaguzi, tuliahidiwa ya kwamba kila Makao Makuu ya Wilaya, watapata umeme na Makao Makuu ya Wilaya ya Ngara, ni mojawapo ambayo imepewa umeme, kwa hilo tunaishukuru Serikali. Kwa sasa hivi, Ngara Mjini kuna umeme na vijiji vinavyozunguka Ngara Mjini, kuna umeme. Kwa hapa nizungumzie kijiji cha Murugwanza, ambacho kina umeme na kina Hospitali, hata usiku kuna taa zinaonesha kwamba umefika Murugwanza. Ukienda vijiji ambavyo vinazunguka hospitali ya Murugwanza, kijiji kama Mukanywampezi, umeme unaenda mpaka kwenye migomba na watu wana umeme. Kijiji kama Mumiterama, ambayo iko jirani sana na Ngara Mjini, na wenyewe wana umeme. Kijiji kama Mukididili ambacho kiko karibu sana na Ngara Mjini, kuna umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba kwa sababu umeme umefika Kabanga *Border*, naomba Vijiji ambavyo viko njiani kati ya Ngara Mjini na Kabanga *Border* na vyenyewe vipate umeme. Vijiji vyenyewe, tunaanza na kijiji cha Mheshimiwa Mbunge, kinaitwa Murugarama. Tunaomba umeme katika kijiji cha Murugarama ili na sisi tupate kufaidi matunda ya uhuru. Tunaomba umeme katika Kijiji cha Mabawe, ambacho kina hospitali ya Kata, ili na wenyewe wajisikie kwamba wako kwenye maendeleo. Tunaomba umeme kwa kijiji cha Ntungamo, ambapo kuna Kanisa kubwa la Katoliki na wenyewe wajione kwamba wanapata maendeleo. Hapo katikati kabla hatujafika Kabanga *Border*, kuna vijiji vya Mugoma, Kanazi, Kabalenzi, Kirusha, Kasange, Lemera na Shanga, ambavyo na vyenyewe vinahitaji umeme. Kwa sababu umeme unapita kufuata barabara ya lami inayoenda Burundi, basi kuwepo na *transformer* pale Kanazi, ili umeme uweze kwenda Mugoma, uweze kwenda Shanga na uweze kwenda mpaka Kirusha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupeleka umeme mpaka vijiji vya Nyamiaga na Mumiterama, sasa naomba umeme upelekwe mpaka Rusumo *Border*, pale kuna kivuko na kuna *Customs Check*. Tukipata umeme unafika Rusumo *Border*, tutakuwa tunaweza kuweka utaratibu wa ulinzi ulio imara kwenye mpaka. Tukishapeleka umeme Rusumo *Border*, basi tupeleke huo umeme Benako, ambako kuna Jeshi la Wananchi wa Tanzania, K9 na kuna shule ya Sekondari ya Baramba na shule ya sekondari ya Rukole, ambayo ina *Form V* na *Form VI*. Hapo tutakuwa tumeboresha umeme katika Wilaya ya Ngara, hasa Tarafa za Nyamiyaga na Tarafa za Kanazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, ninachokiomba ni umeme wa kutoka Ngara kwenda Rulenge, hili ni tatizo la siku nyingi. Hii ni *phase II*, *phase I* ilikuwa ni kupeleka umeme kutoka Ngara Mjini mpaka Kabanga *Border* na vijiji vya jirani. *Phase II*, tuliahidiwa ya kwamba tutapeleka umeme kutoka Ngara Mjini kwenda Mji mdogo wa Rulenge. Naomba umeme usambazwe katika mjini wa Rulenge na vijiji vinavyozunguka Mji wa Rulenge. Vijiji vyenyewe ni kama vile Mbubha, Keza, Kanyinya, Nyakisasa, Bukirilo na Bugarama. Kwa sababu hii ni ahadi ya Rais Mkapa alipokuwa madarakani, nina matumaini kwamba Serikali imesikia na itajitahidi kuweka umeme huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo, ninaomba nizungumzie umeme wa *Rusumo Falls*. Tulipokuwa kwenye semina ya *TANESCO*, hili lilizungumzwa, kuna uwezekano wa kupata umeme wa *Megawatts 60* katika *Rusumo Falls*, kwa mgawo unaofanana. Burundi watapata *Megawatts 20*, Rwanda watapata *Megawatts 20* na Tanzania tutapata *Megawatts 20*, hizi ni *Megawatts 60*. Kwa mawazo yangu na baada ya kufanya utafiti, nimegundua kwamba Burundi hawahitaji *Megawatts 20*, ingawaje huu mradi ni *joint*; ni nchi tatu ambazo zitahusika katika kuujenga mradi huu, Rwanda vile vile hawahitaji *Megawatts 20*, sasa tukiweza kupata *Megawatts 20* za kwetu, tukapata au tukanunua *Megawatts 10* kutoka mgawo wa Burundi na tukapata *Megawatts 10* kutoka kwenye mgawo wa Rwanda, tutakuwa tumepata *Megawatts 40*. Hizi *Megawatts* tukizipeleka kwenye mgodi wa *Kabanga Nikel*, tutakuwa tumetimiza mahitaji ya mgodi wa *Kabanga Nikel*. Ninaomba Serikali ijielekeze katika uwezekano wa kuujenga mradi wa *Rusumo Falls*, ili tuweze kupata hizo *megawatts 60* na tunaweza kabisa kupata *megawatts 40* tukinunua 10 kutoka Rwanda na 10 kutoka Burundi, ili mradi tupate *megawatts 40* tunazozihitaji kwa ajili ya ku-*develop* mradi au mgodi wa *Kabanga Nikel*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho ninapenda kuzungumzia ni maporomoko madogo yaliyoko kwenye mto Ruvuvu, sisi kwetu Ngara tunaita Ruvubu. Pale ukitoka kwenye daraja kama unatoka Rulenge kwenda Ngara Mjini, kwenye daraja chini kidogo upande wa Kusini, kuna maporomoko madogo karibu na Kijiji cha Kanyinya. Haya Maporomoko yameshafanyiwa tathmini, tathmini imeonesha kwamba unawenza kupata *Megawatts* mpaka sita. Ninachoiomba Serikali, ichukue huu mradi iufanyie tathmini upya, maana yake ulifanyiwa tathmini na Kanisa la Katoliki la Rulenge, kama miaka 15 iliyopita. Wana *documents* zote, wanachohitaji ni mwekezaji anayeweza kuu-*develop* mradi huu ili uweze kuzalisha umeme. Tukipata *megawatts* sita kutoka kwenye *falls* hizi za Ruvubu, tutaweza kupata umeme wa kutosha Ngara nzima na hata kuuza kwa jirani zetu wa Karagwe na itakuwa imetuletea maendeleo makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia umeme, sasa nizungumzie madini, Wilaya ya Ngara, ina madini mengi sana. Ukiangalia ramani ambazo watu wanazo, kuna kijana mmoja anaitwa Peter Rusibamahira, ana *GIS* ya ramani ya Ngara na madini yaliyopo. Kuna *deposits* za *lid* karibu Wilaya nzima. Kuna *gold deposits* karibu Wilaya nzima. Kuna dhahabu karibu kila mahali na kuna...

#### **MBUNGE FULANI:** Dhahabu ndio *gold*. (*Kicheko*)

**MHE. PROF. FEETHAM P. BANYIKWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dhahabu ndio *gold*, kuna almasi vile vile. Sasa ninachoomba ni kwamba haya madini yaliyopo, Serikali ifanye utaratibu wa kufanya tathmini ili tuenze kuyachimba. Nina uhakika ya kwamba *Barrick* wana vitalu, wame-*claim* areas ambapo mpaka nyumbani kwangu kuna madini, kijiji cha Murugalama, kuna madini ya *lead* mengi sana na hiyo *deposit* inaenda karibu kilometra 40 kutoka kijiji cha Murugalama, kijiji cha Kabanga, kijiji cha Nzaza, mpaka Burundi, ni *deposits* kubwa sana ya *lead*. Sasa hiyo tukiifanyia utafiti na tukaanza kuchimba, tunaweza kuboresha maisha ya wananchi wa Ngara na maisha ya Watanzania. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hilo, nizungumzie Kabanga *Nikel*. Kuna tatizo na Kabanga *Nikel*, mtikisiko wa uchumi Duniani, ume-*affect* Kabanga *Nikel*. *Kabanga Nikel*, ilikuwa ianze kuchimbwa mwaka huu 2009 na kwenye *Data sheet* waliyokuwa wameonesha wangelianza kuchimba haya madini ya Kabanga *Nikel*, kwa kuujenga kwanza mgodi na kuanza kuchimba mwaka kesho na *full scale production* ianze mwaka 2011 – 2012. Mtikisiko wa

uchumi umetuzubaisha kidogo kwa sababu *main investor*, *Barrick*, amesema asimame kwanza ili afanye tathmini ya ununuzi wa madini yenyewe. Lakini huu mgodi ndio utakuwa mgodi mkubwa wa *Nikel* katika Afrika na *deposit* ni kubwa sana, imekuwa *estimated* ya kwamba itachukua miaka 50 kabla ya mgodi wenyewe kuisha. Ninachoiomba Serikali, iendelee kuzungumza na wawekezaji hasa *Barrick*, ili waweze kufanya tathmini ya mradi wenyewe na wapate *investor* ambaye anaweza kutusaidia kuwekeza katika huu mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachohitaji kwa sasa hivi kama kuuvuta mradi wenyewe, ni barabara ya kubeba madini kutoka *Kabanga Nickel*, kwenda Mizani. Kwa sababu kuna barabara ya lami inayoenda Rwanda, na Burundi pale mizani...

*(Hapa Kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. PROF. FEETHAM P. BANYIKWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji barabara hiyo ili tuweze ku-exploit haya madini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, ni kengele ya pili.

**MHE. PROF. FEETHAM P. BANYIKWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Profesa kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, kama tulivyoolezwa awali kwamba tutarudi tena hapa saa 9.00 ili kuendeleza michango hii, kwa sababu wachangiaji waliopo ni wengi. Kwa hiyo, nachukua nafasi hii niwatamke wachangiaji wanne wa mwanzo ili waweze kujitayarisha na kuweza kufika mapema. Tutakapoingia tutaanza na Mheshimiwa Esther Kabadi Nyawazwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Brigedia Jenerali Mstaafu Hassan Ngwilizi, atafuatiwa na Mheshimiwa Bujiku Sakila na Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, ajiandae. Hao ni watu wanne.

Kabla sijasitisha shughuli za Bunge, labda nisome matangazo machache niliyonayo. Kwanza, kulikuwa na tangazo la mgeni wa Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, anaitwa ndugu Richard Kasesera, anayemwakilisha Mwenyekiti wa Kamati ya Ushauri ya Madini kwa Wizara ya Nishati na Madini. Bwana Richard kasesera, kama yupo? Inaonekana ametoka, anamsubiri Mheshimiwa nje. (*Makofi*)

Mgeni mwingine tuliyenaye, ni mgeni wa Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii, naye ni Mheshimiwa Mzee Stephen Kahumbi, ambaye alikuwa ni Mbunge wa zamani wa Bukene. Mzee Kahumbi? Naye atakuwa ametoka. (*Makofi*)

Matangazo mengine, taarifa ya Kikao, Katibu wa *TWPG*, Mheshimiwa Elietta Switi, anaomba kuwatangazia Wabunge wanawake wote na wanachama wa *TWPG* kuwa kesho siku ya Jumapili baada ya kuisha kwa semina ya *TICRA*, kutakuwa na Kikao katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Kwa hiyo, mnaombwa mhudhurie, baada ya semina.

Mheshimiwa George Simbachawene, Mwenyekiti wa Kamati Ndogo ya Bunge ya Sheria, anaomba kuwatangazia Wabunge wa Kamati yake, kwamba kutakuwa na Kikao cha

Kamati hiyo, leo tarehe 25/07/2009 saa 7.00 mchana, Ukumbi namba 133, ghorofa ya kwanza, jengo la Utawala.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba kuwatangazia kwamba kutakuwa na burudani za Wabunge, zilizoandaliwa kwa ushirikiano wa Ofisi ya Bunge na *Cargo Stars*, kama ifuatavyo:-

Tarehe 25/07/2009, saa 2.00 usiku, kutakuwa na tafrija kwenye viwanja vya Bunge. Bendi itakayotoa burudani ni Sikinde. Tarehe 26/07/2009, kuanzia saa 12.00 asubuhi, kutakuwa na mashindano ya mbio za *VIP*. Mbio hizo zitaanza uwanja wa Jamhuri na kumalizikia katika Viwanja vya Ofisi ya Bunge. Washiriki wote munaombwa mfike uwanjani kuanzia saa 11.45 alfajiri na Mgeni Rasmi katika hafla zote mbili, atakuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Tangazo letu la mwisho ni tangazo la Semina. Naomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa, kutakuwa na semina kesho Jumapili, tarehe 26/07/2009 kuanzia saa 5.00 asubuhi, katika Ukumbi wa Pius Msekwa, mara baada ya *VIP Race*. Semina hiyo inaandaliwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania na itahusu mpango wa utekelezaji wa miradi ya *Post Code* na Utangazaji kutoka *Analog* kwenda *Digital*.

Waheshimiwa Wabunge, naomba kusitisha shughuli za Bunge, mpaka saa 9.00 barabara, mchana wa leo.

(*Saa 7.02 Mchana, Bunge lilisitishwa mpaka saa 9.00 alasiri*)

(*Saa 9.00 alasiri Bunge lilirudia*)

**MWENYEKITI:** Kabla sijasitisha shughuli za Bunge pale saa saba, nilitangaza kwamba tutaendelea na majina manne niliyotangaza, nilianza na jina la Mheshimiwa Nyawazwa nikasema atafuatiwa na Mheshimiwa Brg. Gen. Ngwilizi, Mheshimiwa Bujiku Sakila na Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, kwa hiyo, naomba sasa kumwita Mheshimiwa Esther Nyawazwa ili aweza kuanza.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 64(2) kanuni iliyokiukwa ni Kanuni ya 64(1)(a).

Asubuhi wakati Mheshimiwa Mnyaa, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, anawasilisha taarifa ya Kambi ya Upinzani, alitoa kauli ambayo sikubaliani nayo na amevunja Kanuni ya 64(1)(a), alisema kwamba alikuwa anasoma taarifa ya Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, alimwita Mhehimiwa Nsanzugwanko kwamba amesema kitu ambacho hakiko, ambacho sio cha Kamati na hii si kweli kwa sababu alilosema Mheshimiwa Nsanzugwanko liko katika taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini ambayo mimi ni Mwenyekiti, iko ukurasa wa 15, Ibara ya 5.4.6 na napenda niinukuu kama ifuatavyo:-

*“Kamati inaishauri Serikali kuwa TPDS liwe shirika la Muungano. Hii ni kwa sababu shughuli za utafutaji mafuta zinajumuisha maeneo yote ya Tanzania yaani Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Kulifanya shirika hili kuwa la Muungano, ni sawa kama ilivyofanyika kwa taasisi ya Mamlaka ya Mawasiliano ya Anga (TCAA), narudia hapo, Kamati inaishauri Serikali kufanya kazi suala hili ili sheria ilioanzisha TPDS ihuishwe na kuwezesha kukabili changomoto zinazojitokeza kwa sasa.*

Labda tulitaka kumrudisha kwenye taarifa za nyuma za Kamati kwamba sio mara ya kwanza kwa Kamati kupendekeza kwamba sheria ile ihuishwe kwa sababu ni ya mwaka 1969 na kuzingatia hali halisi ya sasa tukizingatia kwamba majukumu yake yanahusu mambo ambayo yameorodheshwa katika mambo 22 katika nyongeza ya kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Kwa hiyo, sheria ile iko nyuma ya wakati. Nimefanya mawasiliano na *TPDS* kwenye Shirika hilo Bodi yake ina Mjumbe mmoja anayewakilisha Zanzibar, Katibu wa Wizara inayohusika na Mambo ya Nishani. Kwa hiyo, Kamati inazidi kusisitiza kwamba hilo ni pendekezo la Kamati na angesahihisha wala sio la Mheshimiwa Nsanzugwanko. Mheshimiwa Nsanzugwanko ni Msemaji wa Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shellukindo, nashukuru lakini labda nikwambie hivi sasa tutaendelea lakini hilo tunalichukua na baadaye utapata uamuzi kutoka kwa Spika kuhusiana na hilo na maamuzi yake. Mheshimiwa Esther, endelea!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa husikiki labda ungebadirisha *microphone*.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii, kukushuru sana ili na mimi niweze kutoa mawazo yangu katika Wizara hii ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na taasisi zote zilizoko chini ya Wizara hii kwa kazi nzuri ambayo Watanzania sasa tumeanza kuiona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii, kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, kweli nimeamini wewe ni Mwanasheria, ulivyotüonyesha Watanzania kuvunja mkataba wa *IPTL* mikononi mwako, naomba nichukue nafasi hii, kukupongeza sana kwa ujasiri huo wa kuonyesha Watanzania kwamba sasa tuna wazalendo ndani ya Serikali yetu hasa Wizara hii ya Nishati na Madini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru tena Naibu Waziri baada ya kufika pale katika kijiji cha Malya kuangalia mradi wa umeme kutoka Ngudu mpaka Malya, navyozungumza hapa sasa hivi mafundi wako kwenye kazi, wameshaweka nyaya kutoka Lyoma wanaelekea Kimiza nasema ahsante sana. Naomba sasa nichukue nafasi hii kuwashukuru sana ndugu zetu wa Wizara ya Nishati na Madini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kama Mtanzania niongelee kuhusu suala la madini. Tanzania yetu tumekuwa na bahati nzuri sana kuwa na madini ya aina mbalimbali, mimi kwa kweli sisemi kwamba nawachukia wawekezaji, nimefurahi sana walianza kuja lakini imefika mahali sasa kama Mtanzania niyazungumze kama nilivyoyaona. Kabla sijafika kwa hao wawekezaji naomba sasa nitumie nafasi hii kuiomba Serikali sasa tuimarishe taasisi zetu zilizoko chini ya Wizara hii ambayo ni *GST*, (*Geological Survey of Tanzania*), *STAMICO* na Chuo cha Madini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalizungumza hili kwa sababu tukiwa na Watanzania wazalendo, Chuo cha Madini kikiimarishwa, kikiwezesha kikafundisha watalaam wetu ambao watahakikisha kwamba madini yetu wanayalinda na kuyasimamia, tutafika mbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba nisisitize alipochangia Mheshimiwa Mama Malecela kuhusu madini ya vito, ifike sasa wakati madini ya vito, Watanzania wenyewe tuyasimamie kwa sababu nimeomba kwamba Asasi zetu hizi za *STAMICO* na Chuo cha Madini ziwezeshwe na madini kama tulivyozungumza haya ya vito yanapatikana kwa urahisi basi Watanzania tusimamie wenyewe ili tuweze kuendeleza madini hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumze juu ya wawekezaji, nilipokuwa niko nje ya Kamati ya Nishati na Madini, kila wakizungumza masuala ya madini nilikuwa sielewi, nilikuwa naona kama wawekezaji ndio wa maana kuliko sisi Watanzania. Lakini tangu nimeeingia kwenye Kamati ya Nishati na Madini kwanza naomba nimpongeze sana Mwenyekiti wa Nishati na Madini na niunge mkono kwamba hiyo ni taarifa ya Kamati sio taarifa ya Nsanzungako, nakiri kabisa tulijadili na maamuzi ndiyo tuliyoyatoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili la madini, kwanza imeonekana kabisa mahusiano ya wananchi na wawekezaji katika maeneo haya ya madini sio mazuri, wananchi wamekuwa wakilalamika, Serikali inalalamika, sisi Wabunge tunalamika lakini sasa nitaomba kwa sababu Mheshimiwa Ngeleja uko hapa na ni Mwanasheria na jinsi ulivyoanza kwa gia nzuri kabisa kuhakikisha kwamba unasimamia maslahi ya Watanzania, sasa naomba tuhakikishe kwamba wananchi nao walioko katika maeneo hayo hawanyanyasiki, wanapata haki zao, wanafaidi madini ambayo walijatunza miaka ya nyuma hadi sasa wanayo katika maeneo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba nizungumzie malalamiko yaliyoko katika maeneo ya madini. Kwanza matatizo ya fidia. Kumekuwa na matatizo makubwa sana hasa katika eneo letu la Wilaya ya Geita, pale Nyakabale, kuna watu ambao walitolewa katika eneo lile kama Mheshimiwa Mabina alivyosema watu wale 72, ninaomba Mheshimiwa Waziri, huruma yako, Utanzania wako ulionao hebu ulimalize tatizo hili kwa kuwapa fidia zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo la Kiwira, naipongeza Serikali yangu ya Chama changu cha Mapinduzi, maamuzi yaliyochukuliwa juzi kusema kwamba mgodi huu urudi Serikalini, nasema ahsanteni sana. Sasa linalofuatia ni kuwalipa watumishi wa mgodi huo, wameteseka kwa miezi kumi na mbili, hawapati mshahara na wameendelea kutunza mali zote zilizoko pale, lakini niwaombe na wao wafanyakazi wa Kiwira, sasa kumeanza kujitokeza baada ya kusikia kwamba Serikali inachukua mgodi huu wanaanza kuchukua mali zilizoko pale. Naomba nitumie Bunge hili Tukufu kuwaomba sana wafanyakazi wa Kiwira kama waliweza kuwa wavumiliu kutokulipwa mishahara miezi kumi na mbili, kwa nini sasa wasiendelee kuvumilia Serikali yao inajiandaa vizuri kuwalipa fedha zao na mishahara, walinde mali ambazo ziko pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena niipongeze tena Serikali kwa kuhakikisha kwamba inatenga maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo wadogo. Lakini pamoja na kutenga hayo maeneo ya wachimbaji wadogo wadogo, je, katika mgao huo wa maeneo sijui Serikali imejipanga vipi kwa kufuata jinsia zote mbili? Nazungumzia jinsia zote mbili nikiwa na maana kwamba kuna jinsia moja ambayo na yenewe inafanya kazi hiyo, jinsia ya kike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Chama cha Wanawake Wachimbaji Madini wadogo wadogo wanaitwa TAWOMA, bahati nzuri sana na Mwenyekiti wa chama hiki anaitwa Eunice Nengele. Nitaomba sana Serikali inapoamua kuweka maeneo kwa ajili ya wawekezaji, naomba sasa tuzingatie kuona *association* kama hizi ambazo zimejitokeza kuhakikisha na

wenyewe wanapewa maeneo. Kwa hiyo, nawaombea ndugu wa TAWOMA na wenyewe katika kugawa maeneo hayo muwakabidhi na wenyewe ili waweze kupata madini hayo, kwa sababu uwezo wanao, wanachimba, wanaauza na wanatafiti. Kwa hiyo, naomba nichukue nafasi hii ndugu zangu wa TAWOMA, niendelee kuwaombea kwa kazi hii ngumu ambayo si ngumu sana katika kuiona lakini kama wanawake mnaweza basi na Serikali yenu waweze kuwasaidia kwa kuwapa maeneo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijaribu kumuuliza Mheshimiwa Waziri, pale Mwabuki, kumetokea madini ya vito, ya Almasi, sasa naomba Waziri anisaidie tu kuwaelewesha hawa wananchi walioko maeneo hayo au na mimi Mbunge wanitoe wasiwas, je, maeneo haya yameshapimwa? Je, Serikali inajua kuna watu wanachimba pale? Kama watu wanachimba basi naomba mazingira mazuri wawekewe wachimbaji walioko sehemu ya Mwabuki ili waweze basi na wenyewe kama ule mfuko wa kukopesha wachimbaji wadogo wadogo basi waanzie maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo yenyenye matatizo, ninaomba nizungumzie kijiji cha Buhunda, kata ya Irujamate, Wilaya ya Misungwi. Eneo hilo ni la *East Africa Mine* na halitumiki, kwa nini sasa Serikali isilichukue likawagawia wachimbaji wadogo ili na wenyewe waendeleze maeneo hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa nizungumzie katika eneo la Mererani. Tarehe 21, Kamati yetu tulitumwa na Mwenyekiti wetu baadhi ya wajumbe kwenda kutembelea mgodi wa *Tanzanite One*. Mimi inapofikia mahali kunakuwa na ukiukwaji wa haki za binadamu, mimi kwa kweli simtetei mwekezaji hata siku moja. Katika mgodi huo wa *Tanzanite*, kuna kitendo ambacho kinatendwa ambacho hata Naibu Waziri amesikia kwa masikio yake, vijana wafanyakazi wa eneo la *Tanzanite One* wakilalamika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale kumeletwa *scanning machine*, navyofahamu *scanning machine* wakati mtu amehisiwa kuna kitu amekifanya, lakini wanapoamua kumpitisha binadamu katika mashine hiyo, nina uhakika Polisi awepo wa kuthibitisha kwamba kweli hii mashine itatoa matokeo mazuri. Mbaya zaidi haya yote hayajafuatwa katika *Tanzanite One*. Kuna *scanning machine* pale imefungwa inatoa mionzi ambayo hata yule *operator* wa mionzi hiyo hana utaalami huo. Mbaya zaidi, nina picha hapa ambayo watumishi wa pale *Tanzanite One*, nitawapa vijana waione, ni jinsia ya wanaume ipo hapa, imetolewa mtu akifanyiwa *scanning*, nitaomba wale vijana waje waichukue na wewe Mwenyekiti uione. Kwanza inawadhalilisha wanaume, pili inamdhililisha Mtanzania na tatu inadhalilisha jinsia ya kiume. Namshukuru Mwenyezi Mungu, *scanning* hii tumeletewa sisi ni jinsia ya kiume lakini yule anayetoa mionzi pale kwenye ile ni mwanaume na wa jinsia ya kike huwa wanafanyiwa vitendo kama hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashine hii imegundulika na vijana wamelalamika kwamba kila siku wanapotoka kazini kwenye mgodi lazima wapimwe, lakini kinachonisikitisha sana wanaopimwa ni Waswahili tu, Watanzania kama Mama Nyawazwa hapa, inakuwaje Wazungu hawapiti kwenye hiyo mashine? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ninasikitika sana ndiyo ninalizungumzia kwa uchungu sana kwa nini tunafikia hapo? Kwa mfano, kama *Tanzanite* kila mtu anaingia mle, ile *Tanzanite*, ni ya Watanzania kama Mzungu anataka kuiba, ni vito ya Watanzania na huyu ndugu yangu Mmasai kama khabila gani, naye ni Mtanzania kama ni kupimwa basi tupime wote kwenye hiyo mashine, kama kuathirika tuathirike wote Wazungu na Waswahili. Lakini inasikitisha sana ukiona kwamba mashine ile wale wenzenetu wa kutoka nje wanapita kabla,

wakati wa kutoka wale kila siku wanasema kuna mikutano, lakini inakuwaje iwe kwenye mikutano kabla ya saa za kazi tu, wamegundua kwamba wanapoondoka kabla ya watumishi wengine kupita wenyewe wana mlango wao wa kuitia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakuomba Mheshimiwa Waziri, hii ni kuvunja haki ya binadamu, hii ni kuwadhalilisha Watanzania. Mbaya zaidi, vijana walitulalamikia sana naomba wanaume mnisamehe, wanasema na nguvu za kiume zimeanza kupungua na ndoa zao sasa ziko mashakani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachukue dhahabu zetu, wachukue *Tanzanite* zetu na wachukue afya zetu, hili sitakubali, hili naliaacha ndani ya Wizara lifanyiwe kazi na ninaomba Waziri Jumatatu anapo-*windup* awe na majibu ama sivyo mimi kwa kweli siko tayari kuhakikisha kwamba ndugu zetu wa Mererani wanaumia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe sasa nizungumze masuala mawili kabla ya kengele kugongwa. Ninaomba tu Wizara ya Fedha na Uchumi, ikiwezeshe chuo hiki kiweze kutoa wataalam ambao wanaweza kuja kutusaidia kuhakikisha kwamba madini yetu sasa hayachukuliwi nje tukabaki tunalalamika tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono naomba hilo la Mererani, hatua zichukuliwe. (*Makofi*)

**MHE. BRIG. GEN. HASSAN A. NGWILIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na awali, nichukue nafasi hii, nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri, makadirio aliyowasilisha, nimeyaelewa na mimi sina matatizo nayo hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nadhani sio vibaya kusema kwamba leo hii ni siku ya maadhimisho ya Siku ya Mashujaa Tanzania, wapo ndugu zetu ambao walijitolea mhanga katika kuleta ukombozi wa nchi hii, tumwombe Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi, Amen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi niseme kwa ujumla kwamba jukumu la Wizara hii, ni nyeti, ni muhimu na kwa kweli ni sehemu ya usalama wa Taifa, kwa sababu umeme kwa ujumla ni kitu ambacho binadamu anakitumia, binadamu anakitegemea sana na binadamu huyu mara nydingi tunachukulia tu kwa ujumla kwamba labda watu wa vijijini hawana haja ya umeme lakini mahitaji ya umeme katika dunia ya sasa sio anasa, mahitaji ya umeme, ni haki ya kila mkazi wa nchi hii kama ambavyo ni haki kwa wakazi wa nchi nydingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kuona kwamba mpaka sasa hivi ni asilimia 10 ya Watanzania ndiyo ambao wanafaidika na nguvu hii ya umeme, zaidi ya miaka 40 sasa toka tumepata uhuru, nilidhani kwamba iko haja ya kufanya juhudhi ya makusudi. Najua kwamba *TANESCO* wana hiyo *master plan*, lakini *master plan* hii ilitakiwa kwa kweli iwe katika miaka ya 70 na 80, hivi sasa tumechelewa kwa sababu kwa utaratibu huu tunaokwenda nao hivi sasa, nadhani itatuchukua miaka mingi sana mpaka kuweza kuja kufikisha umeme katika kila kona ya Tanzania. Tusinghau kwamba nguvu ya nishati ni muhimu kwa ajili ya kuendeshea mitambo, ni muhimu katika majumba yetu lakini vile vile ni muhimu kwa ajili ya kuendeshea reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kila mara tunazungumzia jinsi gani tutaboresha reli zetu lakini hatuzungumzii tutatumiaje umeme katika reli zetu badala ya kutumia mafuta? Hata mabasi yaliyoko mijini, umeme ni muhimu katika kuendesha na kwa ajili ya mapishi katika nyumba zetu. Kwa hiyo, ni kitu ambacho ni lazima tuweze kufikiria kukifikisha kwa wananchi haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunazungumzia suala la mazingira, mazingira bila umeme kwa kweli ni jambo ambalo haliwezekani, kwa sababu lazima mwananchi apike, mwananchi lazima atahitaji, kutumia nguvu ya umeme, sasa kama haipati, basi miti lazima iendelee kukatwa na unapokata miti ndiyo unaendelea kuua mazingira. Kwa hiyo, mimi nasema kwamba Wizara hii ni nyeti, Wizara hii isijione kwamba ni Wizara ya kawaida kwa sababu ni sehemu ya usalama wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *of course* tunazungumzia suala la vyanzo vya nishati, hiyo mimi naamini kwamba pamoja na kwamba tuna mkaa wa kutosha, tunayo gesi asilia sasa hivi na Mungu akijalia tutapata mafuta, lakini mimi nadhani tungewekea mkazo katika hizi wanazosema *renewable resources*, umeme unaotokana na nguvu za maji, upepo, juu na hata maji moto yaliyoko chini ya ardhi, hivi ni vitu ambavyo tunauhakika navyo, mkaa wa mawe na petrol hayo yanakwisha haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ipo kazi mbele yetu, ipo kazi na itabidi kwa kweli Tume yetu ile ya Mipango itakapoanza kufanya kazi. Ione ni jinsi gani itaoanisha sio tu mbali ya mahitaji mengine lakini vilevile na nguvu zetu za umeme tunafanya namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala ambalo sikumsikia Mheshimiwa Waziri akilitaja, nalo ni kuwasha umeme kwenye miji yetu, *street lighting*. Katika eneo hili la dunia na hata katika Afrika hii, kwa kweli Tanzania ndiyo miji yake ina giza, tunajitahidi kuwasha taa za barabarani lakini katika barabara kuu tu, barabara zile ambazo zinaishi watu wa kipato cha chini ni giza, maeneo ya Buguruni, Keko Machungwa huko, Manzese, yote yale unakuta ni giza usiku. Lakini ukivuka tu mipaka nenda Msumbiji utakuta kwamba miji ya wenzetu taa zinawaka, Kenya, Uganda na hata Rwanda, lakini sisi miji yetu inagiza. Kwa hiyo, lazima tuwe na programu ya kuwasha umeme katika miji yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mkoloni yuko hapa, miji yetu ilikuwa bado ina taa, walifanyaje wao? Tunajua kwamba katika kila mtumiaji wa umeme anapopelekewa *bill* kulikuwa kuna *percentage* inakatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya 1990 nilikuwa Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, tulijaribu kufuatilia suala hilo lakini tukaambiya hilo sasa tuliache kwa sababu fedha hizo tukianza kuzidai itakuwa labda ni kujaribu kulifilisi shirika la *TANESCO*. Lakini hata kama hatudaiani lakini sasa hivi ipo haja ya kuja na mkakati wa jinsi gani tutawasha umeme katika miji yetu na kazi hiyo ni budi ipewe shirika la *TANESCO* kwa sababu ndiyo wenye umeme, ni suala la kuangalia jinsi gani watakubaliana na Halmashauri na halafu waweze kupewa jukumu la kuwasha umeme katika miji yetu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo, sasa nirudi katika Jimbo langu la Mlalo. Jimbo la Mlalo liko katika Wilaya ya Lushoto. Jimbo la Mlalo na Wilaya Lushoto tumekuwa na umeme pale miaka mingi sana nadhani ni mojawapo ya Wilaya za mwanzo kupewa umeme kwenye mwaka 1936, 1937 ndiyo tumekuwa na umeme pale Lushoto. Lakini umeme ule uliishia pale pale Lushoto tu haukwenda vijijini waliko wananchi na ndiyo

tumekaa mpaka kwenye miaka ya 1980 na 1990 ndiyo sasa tumeanza kupeleka umeme kwenye kata na kwenye vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie hasa mradi wa Mlalo ambao nimekuwa nikijaribu kumbugudhi Mheshimiwa Waziri pale na ninaamini kwamba akija kujumuisha atawaeleza wananchi wa Jimbo la Mlalo hatma ya mradi ule imefikia wapi kwa sababu umeme umefika Mlalo lakini umeme ule vile vile ultakiwa ufile Mtæ. Lakini ulipofika Mlalo ukaachwa mpaka sasa hivi imekuwa ni kitendawili, wananchi kule walikuwa wamehamasishwa, wamefanya *wiring* katika nyumba zao sasa hivi ni zaidi ya miaka 10 wamekaa na *wiring* katika nyumba zile hawajui watapata lini umeme. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nitaomba utueleze na uwaeleze wananchi wa Mlalo hatma ya umeme kufika Mtæ kutoka Malindi upite Makose, Rangwi, Nkelei, Mambo, Sunga mpaka Mtæ. Vile vile kwenye kata ya Shume uende Manolo utokee Kibaoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilianza kusema kwamba, suala la umeme siyo suala la anasa tena ni hitaji la muhimu na mpaka hapo tutakopofikia mahali pa kusema kwamba kila Mtanzania anao uwezo wa ku-access umeme basi tutasema kwamba na sisi tuko tayari kupiga hatua ya maendeleo sawa na nchi nyingine, lakini ili umuendeleze binadamu basi hitaji lake la umeme liko palepale sawa na ambavyo ni lazima tumpatие dawa na ni sawa na ambavyo binadamu apate chakula. Umeme ni lazima upatikane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini nimezungumza vyta kutosha na baada ya kuzungumza hayo, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. BUJIBU P. SAKILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuongea katika bajeti ya hotuba ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sijapata hoja nyingine katika Wizara hii, hoja yangu ni ileile ya kila mwaka, tangu mwaka 1996 naomba umeme kwa ajili ya vijiji vyta Jimbo la Kwimba. Nimeomba umeme kwa ajili ya kijiji cha Hungumalwa, Ilula, Buyongo, Kawekamo, Mwamashimba, Mande, Kikubiji pamoja na Shilima, tangu mwaka 1996 na mpaka sasa hivi sina mpango hata wa kubadilisha hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa umeme kwa maendeleo ya wananchi unajulikana, sidhani kama ni lazima sana nianze kuelezea kwamba ni kwa nini naomba umeme, lakini ikibidi mwishoni nitaeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuendelea, kwanza labda nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri sana, naamini kwamba Mheshimiwa Waziri ameshirikiana na Naibu Waziri katika kuandaa hotuba hii, nawapongeza sana. Lakini peke yao wawili ingekuwa ni vigumu sana kuleta hotuba nzuri kama hii, kwa hiyo, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Watendaji wote katika Wizara hii, nawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa pongozi hizo kwa Mheshimiwa Waziri na watu wake, naomba sasa nitoe shukurani kwa Mwenyezi Mungu kwanza kwa kunifikisha hapa leo. Nilichaguliwa mwaka 1995 na ndiyo maana nikaanza kuomba umeme, katikati nikapata matatizo, ile kasi ya kuomba umeme ikawa imepungua. Nimerudi na sasa nimeendelea kuomba umeme. Mwaka 2000, wapiga kura wangu wa Jimbo la Kwimba wakanichagua, nawashukuru sana. Nawashukuru sana kwa sababu tangu mwaka 2005 wameshirikiana na mimi kwa karibu sana. Nimefanya miradi mingi sana ambayo sina sababu

yoyote ya kupoteza muda kuorodhesha mambo ambayo yamefanyika katika Jimbo la Kwimba, nawashukuru sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapiga kura wangu wa Jimbo la Kwimba, nawapenda sana na ninawaheshimu sana, hawa ni wazazi wangu. Kazi yangu kama Mbunge ni kutumwa na wapiga kura wangu kuleta hoja zao hapa Bungeni. Kuhusu umeme nimeshaleta na kazi yangu nyingine ni kurudisha majibu ya Serikali kwa wapiga kura wangu hao, kazi hiyo nimeduwa nikiifanya. Lakini kinachonisumbua ni kwamba naleta hoja, napata majibu halafu nawapelekea wapiga kura watu ambao nawapenda na kuwaheshimu, halafu baadaye nakuja kuonekana kwamba ile taarifa niliyoipelea haitekelezwi, inaumiza sana. Ndiyo maana katika swali langu namba 54 nilouliza katika Mkutano huu, nilimwomba Waziri au Naibu Waziri twende naye mpaka kwenye Jimbo langu akawaeleeze mwenyewe maana mwisho wake wapiga kura wangu wataona kama mimi nasema uongo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, alikubali kuja katika Jimbo la Kwimba lakini bado nasubiri aniambie ni tarehe ngapi atakuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini naomba umeme? Nafahamu masikio ya wengine yatakuwa yameshachoka kusikia, lakini naomba nirudie tena. Nina *ginnery* mbili za pamba zinahitaji umeme, pia nina shule zaidi ya 10 ambazo kama *ginnery* hizo zikipelekewa umeme shule hizo zitapata umeme. Kwa hiyo, naomba umeme kwa ajili ya Shule ya Imalilo, Nera, Mwamala, Mwamashimba, Fukalo, Bupamwa, Mhande na shule za Kata ya Kikubiji ambazo kuna shule mbili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika zote hizo baada ya kupata maelezo ya bajeti ya mwaka jana, nilipita katika maeneo hayo nikaongea na wananchi pamoja na wanafunzi katika shule hizo kuwaambia kwamba tumeahidiwa umeme tutapata mwaka huu, wanasubiri umeme. Mwaka umepita lakini umeme bado haujapatikana. Natarajia kwenda kufanya ziara sasa hivi, nitakwenda kuwaeleza nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu namba 54 katika Mkutano huu, napenda nitumie nafasi hii kuishukuru *TANESCO* kwa kukubali kutenga shilingi bilioni tatu kwa ajili ya mradi huu kwa ajili ya kujenga kituo cha kutunzia umeme Mabuki, ili kutoka hapo umeme ndio usambazwe kwenda katika maeneo niliyoyataja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana hatua hiyo ya *TANESCO*, lakini bado umeme haujawafikia walengwa wangu. Nimeambiwa kwamba umeme kufika kule, tutahitaji msaada wa *ADB* yaani *African Development Bank*, lakini bado hatujaambiwa ni kiasi gani kilichotengwa kwa ajili ya kazi hiyo. Nimeambiwa kwamba mradi huo uko ndani ya *Electricity Five*, mimi sielewi *Electricity Five* ni kitu gani, naomba niambiwe ni kitu gani hicho?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kikubwa ili kunihakikishia kwamba kweli kuna umeme unakuja na utafika katika maeneo hayo naomba kitu kimoja tu, niambiwe kwani nimeona kwenye kitabu kuna shilingi bilioni 8.5 kwa ajili ya *Electricity Five*. Naomba kufahamu katika hizo ni kiasi gani kimetengwa kwa ajili ya mradi huu ili angalau nipate picha kama kweli umeme unakuja, kwa sababu kuandikwa hilo ni jambo moja lakini fedha kupatikana ni jambo lingine. Lakini angalau basi kama kweli mradi huu unajulikana hata kile kiasi kinachotakiwa kitakuwa kinajulikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Mheshimiwa Waziri wakati atakapokuwa anahitimisha bajeti yake atueleze ni kiasi gani kimetengwa kwa ajili ya mradi wa kupeleka umeme kutoka Mabuki mpaka Shilima ili wananchi waweze kufahamu kama hiyo pesa imepatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda vilevile nitumie nafasi hii kumpongeza Meneja au Mkurugenzi wa Nishati Mbadala wa Wizara hii kwa kunisaidia na kunielekeza kwenye Mradi wa *Solar* ambao kwa kiasi kikubwa nimeutumia vizuri sana angalau shule zangu nne zimeshapata umeme wa *solar*. Namshukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile nawashukuru sana Watendaji wa mradi huo ambao wako Mwanza, nawashukuru sana kwa sababu wametoa ushirikiano mkubwa sana kwani bila wao isingekuwa rahisi. Kwa sababu mradi huo ni wa kuchangia basi na wananchi wamechangia. Kwa hiyo, napenda vilevile niwashukuru wananchi wa vijiji vyta Mwakilyambiti, Bupamwa na Mande ambao wameshiriki katika kuchangia mradi huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, narudia kitu kimoja tu, kama nilivyosema kwa wapiga kura wangu, mimi nawapenda na ninawaheshimu sana, naomba sana tena sana taarifa tunazopewa hapa ziwe za kweli. Inasikitisha sana kwa sababu mwaka jana katika bajeti, ukurasa wa 81 wa kitabu cha hotuba ya Bajeti ya mwaka jana ya Mheshimiwa Waziri, nilikuwa nasoma jedwali namba 12 ambalo lilitaja vijiji kwa makosa, nikasahihisha, lakini mwaka huu limetoka jedwali hilohilo na kwa makosa hayohayo, sasa hapa nakuwa na wasiwasi kwamba mchango wangu wa mwaka jana, je, ulisomwa au ilikuwaje? Ulipotelea wapi? Kwa nini haya makosa hayakusahihisha? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana ahadi zilizotolewa leo niambiwe ukweli kama umeme utafika au hautafika katika maeneo niliyoyataja. Nasema hivyo kwa sababu wananchi wanansikiliza na wanamsikiliza Mheshimiwa Waziri. Kwa hiyo, naomba sana tusije tukawafanya wananchi kama ni watu ambao hawasikilizwi kama walevi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa mfano wa mlevi kwa sababu moja, mwaka 1967 nilipokuwa Mazengo kwenda Mwanza nilikuwa natumia usafiri wa treni. Siku moja akaingia jamaa mmoja pamoja na bosi wake baadaye mlevi mmoja akaingia akakaa katikati ya huyo mtu pamoja na bosi wake basi huyu jamaa akawa ameudhika sana. Baadaye huyu mlevi akaanza kusinzia, alipokuwa anasinzia *boss* akasema huyu mtu ni Punda, yaani anamsema yule mlevi. Kwa hiyo, kwa kutaka kumfurahisha *boss* wake yule jamaa akasema bila shaka huyu ni mbwa. Huyu mlevi akaamka kwani aliwasikia walivyokuwa wanasesma akasema mimi niko katikati ya hawa mliowasema. (*Kicheko*)

Kwa hiyo, watu wetu wanatusikiliza, wanatusikia tusije tukafikiri kwamba hawatusikii. Naomba sana tuwapatie heshima yao na tuwaambie ukweli, mahali pa hapana tuseme hapana na mahali pa ndiyo tuseme ndiyo na inapokuwa ndiyo basi itekelezwe. Naomba kufahamishwa, je, umeme utakuja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, sina mpango wa kuchangia upande wa madini kwani mwaka juzi nilichangia, sasa hivi naomba tu nikumbushie. Nchi yetu ilikuwa haijawa tayari kuchimba madini yake, ilikuwa bado. Tilitakiwa sisi wenyewe tujiandae, tumeanza mapema mno hatukuwa na maandalizi. Mama Malecela asubuhi amesema vizuri sana, angalau basi kwa yale madini ambayo ni ya hapa hapa nchi, pekee tusiwapatie watu wengine

chonde chonde, tuangalie mikataba kama tunaweza kurudi nyuma tuireseshe katika mikono ya Watanzania basi irudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mambo mengi sana ila naunga mkono hoja na ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na kunilinda hatimaye nimefikia siku hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nitumie nafasi hii, kuwashukuru wananchi wa Bukombe walionichagua kwani wananiemini, wanaendelea kunitia moyo, kwa ushauri ambao wanaendelea kunipa bila kumsahau mke wangu Martha ambaye ni mshauri mkuu katika masuala yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Makamishna na Watendaji wote wa Wizara kwa pamoja kwa kazi nzuri wanazofanya katika Wizara na hasa walivyoweza kuandaa hotuba hii na kuwaikilisha katika Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini Waziri na Naibu wake ni vijana wasikivu sana, wanatusikiliza na kwa kweli haijawahi kutokea ukaenda ofisini kwao wasikupokee kwa heshima zote na kufanya kila *entertainments* zinazowezekana. Mungu awabariki muendelee kuwa na moyo huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kuwaomba wananchi wa Wilaya ya Bukombe, najua sasa hivi ni msimu wa pamba wanauzwa lakini ni msimu wa kurina asali, watakapopata pesa zile waweke akiba ya chakula ili tusije tukakumbwa na tatizo la njaa. Pia tunamshukuru Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kwa sababu wametuweka katika mfumo wa ruzuku ya mbegu na mbolea, tutumie vizuri Wataalamu wetu wasaidie kushauri ili mbolea hii isije ikaleta kero katika Wilaya yetu. Baada ya maneno hayo, niende kwenye hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilio cha wengi, kila mmoja anayesimama kwa asilimia kubwa tunalilia umeme, tofauti ninayoiona ni kwamba wengine wanalilia umeme wa vijijini na wengine wanalilia umeme wa Makao Makuu. Bukombe tuna tatizo la umeme katika Makao Makuu ya Wilaya yake. Katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi, kwa ridhaa yako ninaomba nisome Ibara ya 43(b) inasema:-

*“Kufikisha umeme katika miji ya Wilaya ya Bukombe na Wilaya nyingine mpya”*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina uhakika kama matakwa ya Chama cha Mapinduzi tunayatakeleza, haikusema kufanya utaratibu wa kupeleka umeme Bukombe. Sidhani kama watu wa Wizara hii wanaisoma Ilani ya Chama cha Mapinduzi ipasavyo na anayesimamia Ilani hii ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, anajua ni kufikisha umeme na siyo kuandaa utaratibu wa kupeleka umeme Bukombe kwa maana maandalizi hayo yalishafanywa miaka mingi iliyopita kabla ya Ilani. Cha ajabu leo ni mwaka wa nne umeme haujafika wala haujapelekwa mahali popote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swalii ambalo niliuliza yaani swalii namba 107 tarehe 7/2/2008 lilijibiwa na Naibu Waziri wa wakati huo ambaye sasa hivi ni Waziri wa Nishati na Madini naomba ninukuu:-

*“Mheshimiwa Spika, mpango wa kupeleka Umeme Wilayani Bukombe, uko katika hatua za mwisho za ukamilishaji na Benki ya Maendeleo ya Afrika imekubali kufadhili mradi huu na unajulikana kama Electricity Five kwa sasa Serikali inakamilisha taratibu za kusaini mkataba.”*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ulikuwa ni mwaka 2008 mwezi wa pili Serikali ilisema inakamilisha mchakato wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye bajeti ya mwaka jana 2008/2009, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, katika ukurasa wa 45 naomba ninukuu:-

*“Kwa sasa mchakato unaendelea wa kumpata mtaalamu mshauri na matarajio ni kuwa atakuwa ameanza kazi ya kuandaa kabrasha ya zabuni na kushauri uteuzi wa Mkandarasi mwishoni mwa mwezi Julai 2008”.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya mwaka huu, katika ukurasa wa 99, naomba ninukuu:-

*“Zoezi la kumpata Mshauri Mwelekezi wa mradi linaendelea na litakamilika August, 2009”*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno haya hayakubaliani kabisa na sentensi zinazotolewa labda ninachotaka nijue na Serikali waniambie wanawaaminisha nini wananchi wa Bukombe katika swali langu la 107 la Julai, 2008 kwa sababu inaonekana kila kitu bado kinaendelea kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaumiza, unaposimama katika Bunge Tukufu unaendelea kuongelea kitu kilekile. Lakini naomba tena uniruhusu ninukuu maneno ya Mtumishi Mika, anasema:-

*“Mungu anachukia udanganyifu, hila, kudhulumu wengine, jeuri, uongo kwa ajili ya mambo hayo huja ghadhabu ya Mungu”*

Maneno hayo ni kutoka Mika 6:9-16, siyo maneno yangu ni maneno ya Mwenyezi Mungu kama amekosea kakosea yeze siyo mimi na Mwenyezi Mungu hakosei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema toka mwaka 2006, nimeingia Bungeni hapa sijarejea katika bajeti ya 2006/2007, maneno yaleyale lakini anasema hebu tujipime katika mizani ya Mwenyezi Mungu tunafaa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana Serikali ituhakikishie, wananchi wa Bukombe wamekuwa wakisikiliza mara zote, bahati mbaya kwa sababu hawana umeme basi hawawezi hata wakaangalia kwenye TV, leo wangemuona Mbunge wao anazungumza lakini hawana bahati hiyo. Najua wanasikiliza kwenye vyombo vy ya habari, je, tunakubaliana hatuogopi maneno yaliyoandikwa na Mika 6:9-16? Kwamba Mungu hapendezwi na dhuluma zile? Tunapeleka umeme Bukombe? Naomba muwaambie wananchi wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku moja nilichangia kwa Waziri Mkuu na nikamuomba kwa heshima zote Mheshimiwa Waziri Mkuu aende Bukombe akawajibu, hakufanya hivyo, hata katika kuhitimisha hotuba yake hakusema kitu. Sasa Mheshimiwa Waziri sijui

tunasemaje? Au nimuombe Mheshimiwa Rais ambaye alifika pale mwaka 2008 akasema kwamba umeme utawaka pale na Ilani hii ambayo Mheshimiwa Rais ndiye anaisimamia, labda arudi kule tena akawaambie watu wa Bukombe kwamba umeme haupo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaongea kwa uchungu na ninapata masikitiko, Mawaziri wetu tusaidieni. Naomba Jumatatu muwajibu wananchi wa Bukombe kwamba umeme uko katika hatua gani? Najua mmeeleza hapa Mshauri Mwelekezi anategemewa kuteuliwa mwishoni mwa mwezi *August 2009*, lakini mwaka jana mlisema angeteuliwa mwishoni mwa mwezi Julai, sasa kwa sababu kila mwaka hotuba inaelekeza mwezi unaofuata ninapata shida kidogo, ninaomba sana mtusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niongelee suala la wachimbaji wadogo wadogo wa madini, ninawashukuru sana Wizara mmetusaidia na hapa mngewaahidi wachimbaji wa kule Katente na wengine, lakini pia hata upatikanaji wa leseni. Kwa kweli nimpongeze sana Kamishna, Waziri na Naibu Waziri kwani mmetusaidia wananchi wetu sasa wanapata leseni lakini tunataka uwezeshaji. Kuna kampuni ya *Africa Precious Metal* wakati wanakuja, *objectives* zao moja ilikuwa ni kusaidia wachimbaji wadogo wadogo. Nitaomba mniambie ni wangapi wamesaidiwa au ni wangapi wamehudumiwa katika huduma za jamii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo sitaki sana kuingiza kwenye madini, niongelee suala la mafuta ambalo ni suala la Kitaifa. Wazungumzaji wengi wameongea suala la mafuta, tulipitisha Sheria hapa ya *TPDC* kuagiza mafuta wanasma *bulk procurement*. Mimi nashangaa Serikali inakuwa na kigugumizi gani kuchukua utaratibu huu, kwa nini hatuagizi mafuta kwa pamoa? Pengine hatujui faida zilizopo, kwa sababu tunapoacha ndiyo uchekechuaji wa mafuta unaendelea. Ndiyo maana tunashindwa kudhibiti bei na Taifa halipati mapato yake, msongamano katika meli unakuwa mkubwa. Mheshimiwa Waziri utuambie hii Sheria tuliyopitisha *TPDC* wafanye kazi hii, mmeamua kuiweka kapuni? Au mnaendelea kuifanyia kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, naomba tena na narudie kwenye msingi wa hoja yangu, umeme Bukombe. Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, sina haja ya kushika mishahara yenu, shemeji zangu watakula nini hawa akina Blandina? Ninataka muwaeleze wananchi wa Bukombe, umeme unakwenda lini? Muwaambie kama umeme umeshindikana kufika Bukombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja ili wapate fedha waende kutekeleza mradi wa Bukombe. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofî*)

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia mchana wa leo hoja ya bajeti ya Wizara inayoongozwa na vijana wenzangu, Mheshimiwa Waziri William Ngeleja na Naibu Waziri Mheshimiwa Adam Malima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumueleza Mheshimiwa Waziri kwamba ninatambua mambo makubwa matatu mazuri sana ambayo Wizara yake imeyafanya kwa Wilaya ya Simanjiro na kwa maana hiyo nisipoyatambua, wapiga kura wangu wataniona mtu wa ajabu na kuniona kama mwizi wa fadhila. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmewezesha Serikali ya Awamu ya Nne kupeleka umeme Makao Makuu ya Wilaya ya Simanjiro Orkesmet, mmetatua tatizo la Ngage B ila bado Ngage A. Lakini mmetuahidi pia kushughulikia suala la umeme katika Tarafa ya Msitu wa Tembo pale ambapo tunapakana na *TPC* kwa maana ya Msitu wa Tembo, Kirwani, Magadini na Ngorika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nitambue mchango wa kipekee wa Mheshimiwa Naibu Waziri Adam K. A. Malima ambaye mwaka jana tulikesha naye na kushinda naye wakati wa dhahama ya mvua iliyopoteza maisha ya ndugu zetu karibu 80 au zaidi katika Migodi ya Tanzanite Mererani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia la pili ninalompongeza ni jinsi ambavyo ameshirikiana na sisi juzi kwenye Kamati ndogo ya Nishati na Madini tulipokwenda kuona matatizo kwa wafanyakazi wa kampuni ya *Tanzanite One* ambayo walikuwa na malalamiko mazito sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote hayo mazuri na mengine mengi ambayo wadogo zangu hawa wamekuwa wakiyafanya kwa dhamana walizopewa, ninaomba kueleza kwa masikitiko makubwa wala sio kwa chuki dhidi yao ila kwa hoja na kwa nguvu ya hoja nitakayoieleza. Nianze bila kusahau kwa kutamka kwamba sikusudii kuunga mkono hoja hii mpaka hapo nitakapopata maelezo sahihi katika maeneo nitakayoyazungumzia sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ni Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tukiwa tunawakilisha muhimili mmoja wa dola baada ya mihimili mingine miwili *Executive* na Mahakama. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inabainisha wazi kwamba mamlaka tuliyopewa, ni Watanzania ambao ni wananchi. Lakini ukienda katika kipengele (b) cha Ibara ya 8 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tunaelezwa kwamba lengo la Serikali ni ustawi wa wananchi na sio ustawi wa wawekezaji. Ni ustawi wa wananchi ambao kwa lugha rahisi ni ustawi wa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo linalotupata sasa, hapa nina ripoti ya Kamati ya Rais ya kuishauri Serikali kuhusu usimamizi wa sekta ya madini, ripoti ya Jaji Mark Bomani. Kwenye ripoti hiyo, kuna mambo mengi mazuri sana yaliyopendekezwa katika sekta ya madini. Ukienda nyuma, kuna ripoti ya Jenerali Mstaafu Mboma, rudi nyuma utakuta ripoti ya Mang'anya, utakuta ya Kipokola na ya juzi tena ya Masha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mapendekezo ya msingi ambayo tungakuwa tumeyafanya kazi sasa, kilio cha Watanzania kingakuwa kimepungua kama sio kuisha kwa asilimia mia moja (100%) lakini tatizo letu liko hapa. Mtaalamu mmoja wa Fizikia na Hisabati mwishoni wa karne ya 18 na mwanzoni mwa karne ya 19, aitwae Albert Einstein na ninaomba ninukuu kwa ruhusa yako, aliwahi kusema:-

*“Dunia ni mahali hatari pa kuishi sio kwa sababu ya kuwepo watu wengi waovu, bali kwa sababu ya kuwepo watu ambao hawachukui hatua zozote dhidi ya uovu huo”*. Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtaalamu huyu anaona kwamba tatizo ni kuwepo kwa watu wengi ambao hawachukui hatua dhidi ya maovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ripoti hizi zote zinaleza upungufu mkubwa sana ambao umejitokeza katika sekta ya madini na tulitarajia dawa yake ni kuchukua hatua ili uovu huo na

uzo huo uweze kuisha. Kinachonitatiza ni pale ambapo kasi ya Serikali inakuwa ni ndogo katika kuchukua hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika ripoti ya Jaji Mark Bomani, yapo mambo ya msingi ambayo yamebainishwa kwa faida ya Taifa letu. Moja, ambalo wenzangu walitangulia kulisema leo na mimi ninalirudia tena ni kuhakikisha kwamba, uchimbaji wa madini ya vito unafanywa na Watanzania wenye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu huhitaji zana za kisasa, kubwa ili kuchimba madini ya *Tanzanite*, unahitaji wachimbaji wadogo ambao ni Watanzania na niseme unaweza ukacheza na madini mengine ya vito ukasema waingie kwa asilimia hamsini (50%) kwa asilimia ishirini (20%) lakini nataka kusema kwamba, kwa madini ya *Tanzanite* ambayo yamebeba jina na heshima ya nchi yetu, ni vizuri yakachimbwa na Watanzania kwa asilimia mia moja (100%).

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikuhakikishie kwamba, tatizo letu lingine ni kwamba tuliwahi kufanya maamuzi na Ndugu Yona wakati huo akiwa Waziri wa Nishati na Madini, alieleza dunia na kulieleza Bunge hili katika bajeti ya mwaka 2003/2004 kwamba, kufikia mwaka 2005, tutakuwa hatusafirishi tena vito ghafi nje ya nchi. Hiyo ni mwaka 2005, leo ni mwaka 2009 hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa kuhakikisha kwamba, madini ya vito yanasanifiwa hapa nchini ili kuongeza thamani na ajira kwa Watanzania. Bado tunapeleka ajira nje, lakini bado pia tunapoteza fedha nyingi kwa Serikali yetu kutokana na ukweli kwamba wataalamu wetu mpaka sasa hawajui thamani halisi ya madini haya ya vito, ambayo hayasanifiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo hiki sio cha kuvumiliwa, ni kitendo ambacho kinastahili Serikali isukumwe, ishauriwe, ifanye maamuzi kwa maslahi ya Taifa letu. Lakini yako mengine ambayo leo Mheshimiwa Nyawazwa ameyazungumza hapa, nayo ni tabia ya wawekezaji kuwadhalilisha Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale *Tanzanite One*, juzi, Kamati ya Nishati na Madini, tulikwenda, ukielezwa mambo yanayotokea pale utasikitika sana, utasikitika Watanzania wanapitishwa katika *Scanner* na leo nitawapeni nakala kila Mbunge, ninazo hapa za picha wanazopigwa Watanzania pale katika mgodi huo lakini watu wengine, Wazungu na watu wa Nepal na wengine walioko pale hawapitii katika mashine ile kama ambavyo watu wetu wanafanyiwa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, fikiria mwenzako anavuliwa nguo hata kama mko wanaume watupu, mko watu 30, unatoa nguo mpaka ya mwisho, unapewa kibukta ukivae halafu unapelekwa kwenye *Scanner* ambayo inaendeshwa na mtu ambaye hana taaluma ya mionzi, huu ni udhalilishaji, ni ukiukaji wa haki za binadamu, Bunge hili linalotokana na Watanzania halina ruksa ya kutokutoa tamko leo baada ya bajeti hii. Waziri wa Nishati na Madini hana ruhusa ya kuhitimisha bajeti yake na kuitishwa vifungu vyake iwapo Bunge hili limetokana na Watanzania wakati vitendo hivi vinafanyika na vinafanywa na kampuni ya *Tanzanite One* kwa Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa nini mnakuwa wasahafulifu? Hivi mnasahau kwamba katika ripoti ya Jenerali Mboma wenzetu wachimbaji wadogo walieleza jinsi ambavyo wanapigwa risasi na wawekezaji hawa wakubwa? Nimenyamaza kwa miaka minne nikieleza kwa lugha ya chini, leo ni lazima niseme kwa sauti ya wazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazo ripoti za kutosha za wachimbaji wadogo na nitaziwasilisha kwako, zinazobainisha wazi Watanzania waliopigwa risasi na kampuni ya *Tanzanite One*, waliong'atishwa mbwa na kampuni ya *Tanzanite One*, kampuni inayodaiwa inaongozwa na aliyekuwa Balozi wa Tanzania nchini Afrika Kusini ambaye mara baada ya Ubalozi wake amejitwalia sifa ya kuwa Mtanzania wa kwanza aliyekuwa mtumishi wa Umma kuwa na hisa katika makampuni mengi ya Afrika Kusini yaliyowekeza Tanzania, Balozi Ami Mpungwe. Ana *share*, ni Mkurugenzi, ni Mwenyekiti katika makampuni yasiyopungua 10 ambayo mkitaka majina yake nitawakabidhi hapa na ni makampuni yanayotoka huko alikokuwa anatuwakilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya makampuni hiyo ni *Tanzanite One*, aliingia pale kama Mwenyekiti. Nimemuuliza Ami, kaka yangu, wewe unadai ulikuwa mtetezi wa ukombozi, wewe unadai ulikuwa unachukia *apartheid*, hapa katika kijiji cha Mererani na Mesinya mnakofanya kazi, kuna wajibu wa *Tanzanite One* katika *corporate social responsibility*, Balozi Ami ananijibu wakati jirani zake hawana maji ya kunywa, watoto 72 wamepelekwa katika Hospitali ya Seriani kutokana na tatizo la kupinda miguu kutokana na maji ambayo hayafai kwa matumizi ya binadamu, saidieni haya, saidieni shule, saidieni barabara, anasema mbele ya Kamati ya Nishati na Madini kuwa:-

“*Siwezi kufanya haya kwa sababu nitakuwa nakufanya wewe kampeni ya kisiasa*”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema dhambi hii haiwezi kuvumiliwa na ninataka niiambie Serikali, tumevulimia kiasi cha kutosha, tumewaacha waendelee kubaki pale, *we are fedup. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikuhakikishie kwamba, wale watu ni wavumilivu. Watanzania ni wavumilivu kwa kiwango ambacho mimi kama mwakilishi wao lazima niwaeleze kwamba leo, *Tanzanite One* wako pale kwa sababu tumenyamaza. Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa Jumatatu iko pale kwa sababu kuna Mzungu mmoja amekwaruzwa tu na wachimbaji wadogo. Wakati Watanzania wanapigwa risasi hakuna Kamati ya Ulinzi na Usalama iliyohamia pale, wakati tunang'atishwa mbwa hakuna Kamati ya Ulinzi na Usalama iliyohamia pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema Serikali hii, ni Serikali ya Watanzania, tuna jukumu la ustawi wa Watanzania sio ustawi wa Makaburu, siyo ustawi wa mtu mwingine wa nchi nydingine. Uvumilivu una ukomo na ninataka niwaambieni, mtakapoonja adha ya watu ambao wameshindwa kuvumilia, nawaambieni hamjawahi kuiona, lakini siku moja mtaiona sijui ni miaka mingapi 10 ijayo au ni lini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema tatizo letu ni kuchukua hatua katika mambo ya msingi, katika mambo tuliyolahidi, kuna kitu kinaitwa *Tucson Protocol*, Waziri wa Nishati na Madini, Edigar Maokolo Majogo alikwenda Arizona ambako alikaa na wenzetu wa Marekani wakaja na kitu kinaitwa *Tanzanite Tuscon Protocol* ambayo katika ahadi aliyoitota alisema hivi, naomba kunukuu:

“*Finally and perhaps most critically we are now in a final stage of establishing a Charter and Constitution for Tanzanite Board which will be moulded along similar lines to other mineral boards in developed mining countries. The board will comprise Government and non government stakeholders in the industry and its mandate will include oversight of the mining trade, export of Tanzanite, the promotion of value adding industry within Tanzania and the deploying of Tanzanite certification system similar to the Kimberley Process*”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bodi hii ya Tanzanite haijaanzishwa mpaka leo na hili ni tamko la tarehe 8 Februari 2002. Serikali yetu imeahidi dunia itafanya hivyo ili kuunda bodi itakayosimamia uchimbaji, biashara, usafirishaji, usanifu na uwekaji wa alama katika mambo haya ya madini ya vito, hatujafanya na leo bado mnataka hoja hii iungwe mkono!

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mambo ya msingi ambayo ni muhimu sana kulikumbusha Bunge lako na kujikumbusha katika kipindi hiki ambacho tunaelelekea kuwaomba tukatae kupitisha hoja hii mpaka tupate maelezo. Moja ni hili ambalo nimesema, udhalilishaji wa faragha wanaofanyiwa wachimbaji wadogo na mashine zinazoendeshwa na watu wasiokuwa na taaluma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni ajira. Pale *Tanzanite One* ukiishakuwa mwana Simanjiro ni *disqualification* ya kuajiriwa katika *Tanzanite One* na nikuhakikishie tu kwamba, Wanepali wako pale wengi wanashughulika na masuala ya ulinzi, yaani ajira ya ulinzi unachukua watu kutoka Nepal! Kazi ambazo tunaweza kuzifanya Watanzania, unachukua wageni ambao ni Wazungu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa hatuko *serious* katika kuwawezesha Watanzania.

*(Hapa kengele ililia kuashiria  
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Hiyo ni kengele ya pili?

**MWENYEKITI:** Ndiyo ya pili.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Siungi mkono hoja mpaka nitakapopata maelezo. (*Makofi*)

**MHE. ARCHT. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii jioni ya leo katika kuchangia Wizara yetu muhimu kabisa ya Nishati na Madini.

Awali ya yote, niwape pongezi Vijana wenzetu kwa jinsi wanavyojitahidi kuiongoza Wizara hii pamoja na ukubwa na ugumu wake, lakini ni ukweli kwamba wanajitahidi pamoja na mikingamo yote wanayokumbana nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mwenyezi Mungu pia kwa kutujalia amani tuliyonayo ndani ya Taifa letu mpaka hivi leo tunavyozungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwamba hakuna asiyefahamu umuhimu wa nishati. Tumekuwa tukizungumzia kufundisha masomo ya sayansi katika shule zetu, haya masomo ya sayansi itakuwa ni vigumu sana kuyafundisha pasipokuwepo na nishati ya aina yoyote katika mashule yetu, tunahitaji nishati katika zahanati zetu, hata swalilangu la wiki mbili zilizopita hapa lilikuwa ni mbadala wa nishati ya umeme tulionao wa kawaida kwa maana ya *solar* au umeme wa upepo na Mheshimiwa Naibu Waziri alijitahidi kujibu vizuri nami nilikubaliana naye lakini nikaomba kwamba tuongeze jitihada zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianzia kule Jimboni kwangu kwa wananchi wetu wa Hai, maombi yangu ni kama ambavyo nitakuwa nimeshanong'onezana na Mheshimiwa

Waziri na Naibu wake kwamba, tunavyo vijiji ambako umeme unapita lakini haujashushwa kwa maana ya kupoozwa, kuwekewa *transformer* ili viweze kupata umeme kama maeneo mengine yanavyoweza kupata umeme. Maeneo hayo ni kwa mfano kule kijiji cha Longoi, Ngosero, Shirimgungani, Kwatito, katika kijiji cha Chemka kuna Mradi wa PADEP ambako tulimpeleka hata Mheshimiwa Makamu wa Rais, akajione kazi kubwa iliyofanywa na wale wananchi pamoja na shule ya ufundi iliyoko katika kijiji cha Chemka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna maeneo mengine katika kijiji cha Mungushi, umeme mkubwa kabisa umepita pale kuelekea Wilaya yetu mpya ya Siha ambako niliishaomba na nikaahidiwa kwamba vifaa vile viliishapatikana ili umeme uweze kusambazwa kwa wale wananchi wa kijiji cha Mungushi, maeneo ya Sawe, Mboreni, Uscaa katika kitongoji cha Mbweera na vitongoji vya Gezaulole pale Bomang'ombe mjini, Kanda C, Kengereka na hapohapo Bomang'ome mjini kwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikumbushe tu kwamba katika ukurasa wa 97 katika miradi ya usambazaji wa umeme vijiji iliyopitishwa na Bodi ya Wakala wa Nishati Vijini kwa mwaka wa 2008/2009, nadhani ni kwa sababu tu ya kujisauh kidogo. Ukurasa 97, namba 17 vile vijiji viliviyotajwa pale mwanzoni siyo vya Wilaya ya Hai, siku hizi tunayo Wilaya ya Siha, hivyo vile vijiji ni vya Wilaya ya Siha pengine ni katika uchapishaji labda nadhani na kwa sababu Wilaya ya Siha ni mpya, kwa hiyo, ni suala la marekebisho tu kwamba vile ni vijiji vya Wilaya ya Siha na si vijiji vya Wilaya ya Hai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hivi vijiji vya Wilaya ya Hai nilivyovitaja niwakumbushe tu watendaji kwamba na wale wananchi wa vijiji vile wangependa kupata umeme na kadri wanavyosambaza umeme ndivyo ninavyoamini kwamba mapato yataongezeka kwa TANESCO na hivyo kuwapatia uwezo zaidi wa kuweza kusambaza umeme katika maeneo mbalimbali ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha anieleweshe mimi pamoja na wale wananchi wa Hai na Watanzania kwa ujumla nini kinachoendelea katika eneo la Kikuletwa? Kikuletwa ni eneo ambako umeme ulikuwa unazalishwa miaka mingi sana kabla ya uhuru bahati mbaya mashine zile zilikufa kwa njia ambazo hazifahamiki vizuri lakini kuna wakati tulikuwa tumeshasema kwamba, tutafufua kile kituo ili tuweze kuzalisha umeme na wataalamu kutoka Japan walisema tungeweza kupata zaidi ya *Megawatt* 20 kama wangezalisha kwenye kitu wanachoita *turbines series*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha anieleweshe kwamba nini kinachoendelea katika eneo la Kikuletwa ambako pia kwa upande wa Wilaya ya Hai tungepata mapato. Kwa hiyo, nitaomba Mheshimiwa Waziri, akija kuhitimisha atuelezee nini kinachoendelea katika kituo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nizungumzie kuhusu madini ya vito lakini aliyetoka kuzungumza, Mheshimiwa Ole -Sendeka yeze ndiye yuko jikoni zaidi. Madini ya vito nikimaanisha Tanzanite, Rubi na mengineyo ambayo tuliishayazungumzia sana kwamba haya madini ni kwa ajili ya wachimbaji wadogo wadogo, wa kizalendo, wa Kitanzania na sioni kuna dhambi gani Watanzania wakichimba haya madini, tutapata hasara gani? Kwa sababu watachimba hata kwa teknolojia yao ambayo ni ndogo, watachimbachimba kama vile kuku wa kienyeji anavyofukuafukua kinachobakia watakuja Watanzania wa kizazi kinginge na kizazi kingine na hiyo ndiyo jinsi ya kumkomboa huyu Mtanzania na kumuondoa katika hali ya umaskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo miji mingi sana hapa Tanzania ambayo iliendelezwa kutokana na uchumi uliokuwa unapatikana Mererani. Maeneo ya mji wa Arusha wenyewe, mji wangu wa Bomang'ombe, Moshi mjini yenyewe, maeneo ya Singida kule kuna wachimbaji wengi kutoka huko na karibu kila kona ya nchi hii wako pale Mererani. Lakini hali siku hizi ni ngumu sana, wale vijana wanataabika na wanapata mateso makubwa sana. Je, Serikali inasema nini kuhusu madini ya vito? Tutaendelea kulizungumzia hili suala mpaka miaka mingapi? Mimi ningeomba tuwe na uzalendo wa kutosha, tuamue hata kama kuna mahali tuliteleza basi tuwaambie wawekezaji samahanini lakini sasa hivi msimamo wetu uko namna hii na huo si mwagine isipokuwa ni kwamba madini ya vito yachimbwe na Watanzania peke yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki iliyopita nilipata fursa na nikaweza kufika katika Jimbo la Kibakwe la Mheshimiwa Simbachawene. Kule nako nimekuta kuna matatizo, kuna malalamiko, vijana wanalamika, hawa ni wale waliowahi kushika vitalu au kwenda mapema katika baadhi ya maeneo kuna tetesi huenda wakahamishwa kwa sababu utaratibu unaotumika kuwarasimisha katika vile vitalu sio sahihi, kuna baadhi ya wakubwa amba wanataka kuchukua vile vitalu ambavyo vinaonekana kuwa huenda vikawa na madini. Huu ni unyanyasaji na sio kitu kizuri, mimi ninaomba sana tuogope dhuluma kwa sababu ninavyofahamu hakuna mtu anayeweza akaendesa magari mawili ndani ya barabara moja. Utaweza kuendesa gari moja kwa wakati mmoja, utaweza kula kasahani kamoja tu ka chakula, hata ukijenga nyumba yenye ghorofa ya vyumba vingapi utalala kwenye kitanda kimoja tena sehemu ndogo sana kama futi tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokimaanisha hapa ni kwamba, sisi binadamu tusijenge sana tamaa, tuwe na kiasi halafu, tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kile anachotujalia kwa sababu kinachoonekana ni baadhi ya watu kutumia nafasi zao, kutumia hila kuwapokonya wale wadogo. Hii ni dhuluma na hakuna kitu kibaya kama dhuluma, dini zote zinakataza dhuluma, niombe sana tumwogope Mwenyezi Mungu na tukumbuke kuwatendea Watanzania wenzetu haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nihitimishe kwa kusema tu kwamba, madini ya vito ni ya Watanzania peke yao, nchi nydingine zote duniani madini ya vito hayaguswi na mtu wa nje, wala hasogelei jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeambiwa hapa kutokana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri, mchakato unaoendelea kuhusu madini ya *Uranium*. Madini ya *Uranium* tunayafahamu, kwanza ni hatari sana kutokana na kwamba haya ni *radioactive*, lakini yakiishaanza kurutubishwa ni hatari zaidi, lakini pia ni madini ambayo yana thamani kubwa sana duniani na yanatafutwa na mataifa yote. Mimi niombe tu kwamba, mchakato wake uende haraka, vizuri na kwa uangalifu mkubwa. Ile mikataba sasa, mwaka 2006 mojawapo katika maswali yangu lilikuwa kwamba, ni lini tutakuwa na kitu wanachoita *blue print* ya mikataba? Tutayarische sampuli za mikataba yetu ili ye yeyote anayetaka kuwekeza katika Taifa letu la Tanzania afahamu anakuja kuwekeza katika *conditions zipi*? Katika mazingira yapi? Sijui kama hicho kitu kimeishafanyika au bado?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaomba sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wako nyie ni vijana kwa lugha nydingine tunasema *digital* muende kiusasa, zitayarishwe sampuli za mikataba ambapo wawekezaji watakapokuja ndani ya Taifa letu wawe wakijua kwamba, wanakuja kuwekeza katika mikataba ya aina gani! Ikiwa na maana ni kulinda uzalendo wetu na Taifa letu liweze kuneemeka zaidi na vile ambavyo Mwenyezi Mungu ametujalia kuwa navyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali kwa ilichokisema kuhusu *STAMICO* lakini mimi niseme tu kwamba, muda umeishapita sana tulitakiwa tuipe *STAMICO* nafasi muda mwangi uliopita, *STAMICO* ni shirika letu ambalo litawenza kutusaidia, hasa kwa wale wachimbaji wadogo wadogo. Kwa hiyo, mimi niombe tu kuwa, hizo hatua wanazokusudia kuhusu *STAMICO* zifanyike kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda unakimbia lakini kuna suala nyeti linalogusa kila Mtanzania, suala la mafuta '*petroleum products*'. Hakuna ambaye haguswi na hili suala la mafuta, awe tajiri, awe maskini na bahati mbaya zaidi maskini au mtu mwenye kipato cha chini ndiye anayeumia zaidi kwa sababu siku zote mfanyakiareshara yeye gharama atakazoziingia atazitafsiri kwenda kwa yule mlaji wa mwisho ambaye ndiye mwananchi wa chini kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge, labda tutafakari tena upya kuhusu suala tuliloliweka kwamba tukaweka ushuru mdogo kwenye mafuta ya taa huenda ndilo linalosababisha shida kubwa katika hii biashara. Tofauti kubwa iliyopo ya shilingi 400 kwa lita, je, ni kweli kwamba tunataka kumsaidia huyu Mtanzania wa kima cha chini, au tunaboresha hali nzuri ya kikundi kidogo sana cha watu wachache? Ninaomba tutafakari upya na ikibidi tuwaeleze wananchi wenzetu kwamba, ni kwa nini labda tunazungumzia sasa ushuru wa mafuta ya taa uje ukaribiane na ushuru wa petroli au dizeli ili kuondoa hasara inayopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokimaanisha hapa ni kwamba, tofauti kubwa iliyopo ya shilingi 400 kwa lita katika mafuta ya petroli na mafuta ya taa ni kuwepo kwa tatizo la kuchakachua mafuta. Magari yanaharibika sana, pampu za magari zimekufa sana lakini ile hasara inatafsiriwa kwenda kwa yule mlaji wa mwisho. Kwa hiyo, ninaomba sana tuangalie upande wa kodi katika upande wa mafuta ya taa na petroli, tukiweza kuipunguza ile tofauti, huenda ikasaidia kuondoa tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia katika hii biashara ya mafuta kuna kitu tunachoelezwa siku nyingi kidogo kinachoitwa *bulk procurement*. Pamoja na mazungumzo yaliyopo, malalamiko yaliyopo lakini ni kwamba mimi ninachoamini *bulk procurement* itatuokoa na madhara mengi sana ambayo tunayapata hivi leo. Ninaomba uzalendo uzingatiwe, uzalendo uchukue mkondo wake, tufanye haraka zaidi Shirika letu la *TPDC* tunaliamini lina uzoefu tuliwezeshe. Kuna asilimia ambayo tulikuwa tunesema kwamba *TPDC* wawe wanapewa, kwenye masuala ya gesi, *retention* ile tunaambiwa kwamba huenda wakaanza kupata lakini ni siku nyingi, muda umekwenda, tuliwezeshe hili shirika ili liweze kujitegemea, liweze kuingia katika hizi biashara za ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakuja kuwapa watu wa nje faida. Kwa mfano, biashara ya gesi, usambazaji wa gesi tuanaozungumzia sasa hivi majumbani au kwenye magari tukimuachia mtu wa nje, mfanyakiareshara binafsi, yeye atataka afanye kwa kipindi kifupi aweze kurudisha pesa yake ili apate faida, lakini shirika letu kama *TPDC* litafanya kwa taratibu, halina haraka ya kupata faida tafsiri yake ni gharama ndogo ya gesi kwa mwananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe kabisa kwamba tuliwezeshe Shirika la *TPDC* pasipo kigugumizi cha aina yoyote. Shirika hili limenyanyaswa miaka mingi, niombe sasa vijana wenzangu msikubali hiyo hali iliyotokea miaka ya nyuma, fanyeni kila linalowezekana kama ni ku-restructure Shirika hili lifanyiwe huo ukarabati, tulitengeneze

vizuri, tulipe uwezo kile kiasi cha pesa ambacho linatakiwa lipate basi liweze kupata. *TPDC* walianzisha na kampuni inaitwa *GASCO* ambayo ilikuwa ni kampuni ya ku-deal na mambo ya gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu jiulize endapo usambazaji wa gesi majumbani utafanywa na kampuni binafsi ni sawasawa na tungenesema usambazaji wa maji safi na salama uwe unafanyika na mtu binafsi. Mtu huyo atataka kukusanya pesa kwa haraka sana, lakini ndio maana ni vyombo vyya Serikali ndivyo vinavyofanya hivyo, havina haraka ya kupata faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme naunga mkono hoja kidogo kidogo nitaunga vizuri zaidi Mheshimiwa Waziri atakapomalizia. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, kwa hotuba ambayo kwa kweli ni nzuri sana, kadri miaka inavyokwenda, hotuba ya Mheshimiwa Waziri inazidi kupendeza sana, hivyo ninampongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue fursa hii kumpongeza Katibu Mkuu wake, ndugu Arthur Mwakapugi, Wakurugenzi wake Mrindoko, pamoja na Dkt. Kafumu kwa kazi nzuri wanazozifanya, tunapokwenda kwenye ofisi zao kwa kweli tunajisikia ni ofisi za Umma, hawana maringo wanatusikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee, nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Adam Kigoma Malima. Nampongeza kwa sababu amekuwa ni mahiri sana na amekuwa na kasi ya ajabu katika kujibu maswali vizuri hapa Bungeni, namtakia afya njema na Mwenyezi Mungu amsaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea, nitumie nafasi hii kuwapa pole wananchi wa kijiji cha Kaundwe katika Kata ya Ihanda, Jimbo la Karagwe kwa msukosuko ambao unajitokeza kati ya wafugaji na wakulima. Ninawaomba watulie, ninaamini Serikali itajitahidi kusawazisha hali hiyo na pia niwatake wakulima na wafugaji waendelee kukaa pamoja na mimi baada ya kuchangia hapa kwenye hotuba hii nategemea kuelekea huko kuhakikisha kwamba tatizo hili tunalitatua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Ngeleja, kwanza kwa mzigo mkubwa sana ambao anaubeba wa Wizara hii ambayo ni nyeti. Wengi wanasema mzigo mkubwa mpe Mnyamwezi, sasa huyu bwana sijui kama ni Mnyamwezi, lakini ninaamini ni Msukuma. Kusema kweli anajitahidi sana, nimejaribu kupitia hotuba yake, kuna mambo mazuri amenifurahisha na mengine ambayo ameyafanya huko nyuma na mojawapo ambalo limetupa heshima kubwa kwa nchi yetu hasa ni lile ambalo aliweza kufuta Mkataba wa Dowans kwa ujasiri mkubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ule Mkataba umeweza kutuondolea kitu kinaitwa *capacity charge*, ni Mawaziri wachache sana wenye ujasiri wa kufanya jambo kama hili bila kusita, nakupongeza sana Mheshimiwa Ngeleja na siyo hilo tu, naambiwa ni pamoja na *IPTL* ameifanya kazi, ninakupongeza sana na wakati unatokea huku *bench* unakwenda kuwa Naibu Waziri, nilikuwa na wasiwasi kwamba unaingia kwenye Wizara ngumu lakini hapo hapo ukafanya kazi, ukapanda kuwa Waziri kwa hiyo nakutakia kila la kheri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Ngeleja kwa kazi ambazo amezifanya mojawapo ikiwa ni kutembelea Wilaya ya Karagwe na hasa alipofika mpakani mwa Karagwe na Uganda, kule Mrongo wananchi wa Karagwe walifurahi sana na walipomuona walijua kwamba umeme utawaka mara moja lakini kwa masikitiko makubwa tangu atoke huko hakuna dalili hata ya nguzo moja ambayo imefika pale na leo wamenituma kwa niaba ya wananchi wa Karagwe, likiwemo Jimbo la Karagwe, Jimbo Kyerwa kwa Mheshimiwa Katagira, wanasema wale wenzetu wa Uganda tayari nguzo zimeishafika mpakani na muda wowote umeme utawaka lakini kule kwetu hata mafundi kupitapita hawaonekani. Sasa ninakuomba sana Mheshimiwa Ngeleja atupe majibu wakati anahitimisha hotuba yake. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa sisimami kumpamba mtu, ninasimama kuzungumzia kazi nzuri zinazofanyika. Ninafahamu kwamba Wizara hii ni ngumu sana na hata hivyo yanayofanyika, hawa ndugu zetu wanajitahidi mno lakini nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitalishukuru Shirika la *TANESCO* kwa kazi hii wanayotufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ni wepesi sana wa kulaumu lakini kama sio *TANESCO* hata hii *microphone* leo isingekuwa inafanya kazi humu ndani. Kwa hiyo, nimshukuru sana Dkt. Rashid pamoja na Bodi ya Wakurugenzi, kwa kweli wanafanya kazi nzuri mno. Umeme unawaka mijini, unawaka Wilayani na vijiji unakwenda, matatizo yaliyopo ni ya kawaida naamini watayafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nimetembelea Wilaya ya Biharamulo nilifanikiwa kupita pamoja na maeneo ya Kigoma, nilisikitika sana wakati niko pale Biharamulo kuona hali ya umeme jinsi ilivyo, utadhani kwamba ile nchi labda iko kwenye karne ya mawe, hakuna umeme, hakuna chochote yaani ni giza tupu. Sasa nimwombe Mheshimiwa Ngeleja na Naibu wake wajitahidi kuangalia lile Jimbo la Biharamulo kwa kweli linatia aibu sana. Kamati yetu ilikwenda kutembelea Kigoma Mjini, tulikuwa pale Waheshimiwa Wabunge wengi wa Kamati ya Miundombinu, kusema kweli tulisikitishwa na hali ya Kigoma Mjini. Ule Mkoa wa Kigoma kama utaweza kupewa umeme wa uhakika, ninaamini utakuwa ni Mkoa ambaa utakuwa ni wa Kimataifa na mzuri sana kama ilivyo miji ya Arusha na miji mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio Wilaya ya Kigoma peke yake, nilibahatika kidogo kwenda Wilaya ya Kibondo kwa Mheshimiwa Kijiko. Nilipofika pale, nilikuta wale wananchi, Waha wamekata tamaa sana, nikawauliza nyinyi mna makosa gani kwa Serikali hii ya Tanzania, kwa nini mko gizani miaka hii ya uhuru? Wakasema Mheshimiwa, Mbunge wetu tumeshamwambia na anasema kila siku labda na wewe ukienda huko ukatusemee. Nichukue nafasi hii kuisemea Wilaya ya Kibondo lakini wao wanasema kwamba tayari jenereta za umeme zilishaagizwa, mpango upo, sasa sijui zimefika wapi, Mheshimiwa Ngeleja nitapenda unifahamishe. Lingine wanasema kuna fedha zimelala pale Kibondo kwa ajili ya kutengeneza miundombinu ya umeme. Lakini hizo fedha mpaka sasa hivi hazitumiki, kwa nini mnazikalia, nilitaka nifahamu hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti yote hii ya Wizara ya Nishati na Madini, mara nyingi tumekuwa tukizungumzia habari ya nguzo za umeme kutoka nchi jirani. Niliangalia katika bajeti ya Mheshimiwa Waziri, sikuona jibu sahihi, lakini leo nilitaka nimpe ufumbuzi na nimwombe sana akienda katika Mkoa wa Kagera na hasa katika Wilaya ya Karagwe, sisi ni wakulima wazuri sana wa miti ambayo ni maarufu, inaitwa mikaratusi. Ile miti ikishakua kabisa haina faida tena inatakiwa ivunwe wakati ikiwa katika *stage* ya uchanga kidogo. Miti

ile inafaa sana kwa nguzo za umeme huna haja ya kwenda Malawi au Zambia. Sasa nitapenda Mheshimiwa Waziri anieleze ni kwa nini haji Karagwe kuchukua nguzo za umeme kwa wananchi wa Karagwe? Namwomba Mheshimiwa Waziri ajitahidi sana kufika Karagwe na kuwasaidia wananchi ambao wamejitahidi kulima sana na wanaendelea na kaulimbiu ya Kilimo Kwanza, kwa hiyo, wameanza na miti lakini wanahitaji soko la miti yao itengeneze nguzo za umeme Karagwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi huwa najiuliza, hivi Mheshimiwa Rais anapofanya ziara Mikoani na akaongozana na timu ya wataalam na wale wataalam huwa ni mahiri wa kurekodi, wengine wana *tape recorder*, wengine utakuta wanaandika yale ambayo Mheshimiwa Rais anayasema na kuahidi kwa wananchi. Sasa huwa nashangaa pale huwa wanafanya usanii au wanaandika taarifa ya ukweli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hivyo kwa sababu nimekuwa nikisikitishwa sana tangu Mheshimiwa Rais alipokuja Karagwe wakati anagombea, akiomba nafasi, ahadi ya kwanza aliyoitoa ni umeme kwenda vijijini na wale watu wakaandika sana na mimi nikafurahi sana. Nilipokuja hapa Bungeni nilikuwa wa kwanza kuuliza swali kuhusu umeme vijijini. Alinijibu Mheshimiwa Lawrence Masha ambaye sasa hivi ni Waziri wa Mambo ya Ndani, kwa ufasaha mzuri mno mpaka nikapiga na makofi humu ndani. Akasema umeme vijijini unakuja, ilikuwa ni mwaka 2006. Nikamshukuru, nikampongeza na jioni tulivyotoka, nikampa kikombe cha chai kidogo kumpongeza. Sasa mwaka 2007 akarudia jibu hilo hilo, siku hiyo nikampa angalau chupa moja ya soda. (*Makofi/Kicheko*)

### **WABUNGE FULANI:** Rushwa hiyo!!!!

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Sio rushwa ni rafiki yangu. Mwaka 2008 akajibu hivyo hivyo. Sasa nikamnyima hata kikombe cha chai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imefika leo mwaka 2009 kwa masikitiko makubwa sana sioni hata dalili hata kidogo ya umeme kwa wananchi wangu kule Karagwe Vijijini. Kwenye kitabu hiki nimekisoma kwa makini kuanzia mwanzo mpaka mwisho. Kwenye ukurasa 96 wameonyesha kwamba watapeleka umeme vijiji vya Bisheshe, Nyaishozi, Ihembe, hivi vijiji vitatu navifahamu na wametenga shilingi 200,000,000/= kati ya shilingi 740,000,000=/. Halafu wakasema watumiaji watakuwa 350, kwanza hizi taarifa zenyewe sio sahihi, ukanda huo una watumiaji wa umeme zaidi ya 3,000 na fedha ambazo zinatakiwa sio shilingi 200,000,000/= kama tunataka kupeleka umeme, hizi shilingi 200,000,000/= labda kusimika nguzo tu na sisi tunataka umeme uwake. Kwa hiyo, nataka niseme hizo shilingi 740,000,000/= Mheshimiwa Ngeleja, azitafute sana na kupeleka umeme Nyaishozi, Ihembe, Nyakasimbi, Bisheshe, Rugu na sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Jimbo la Karagwe limegawanyika katika pande tatu, pande ya kwanza ndiyo hii ambayo naisemea. Nashukuru si haba hizi shilingi 200,000,000/= kwa kuanzia lakini kuna upande ambao uko mpakani mwa Tanzania na Rwanda na upande huu unahuisha vijiji vya Ihanda, Lukole, Rwabere, Kiruruma, Nyakagoyagoye, Nyabionza pamoja na Nyakaiga. Sijaona hata shilingi moja hapa na hii ni ahadi ya Mheshimiwa Rais. Ni ahadi ambayo imekuwa ikitolewa hapa Bungeni na Mawaziri mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia hapa nitoe shukrani kwamba kuna ukanda mwingine wa kuanzia Kayanga kwenda Ndama, Kakiro, Runyaga, Kituntu hadi Igurwa, nguzo naona zinakwenda. Lakini sikuomba nguzo, mimi nimeomba umeme. Mheshimiwa

Ngeleja katika kipindi chako chote kusema kweli pamoja na sifa zote nilizokupa yaani hujanipatia angalau hata balbu moja ya umeme inayoweza kuwaka? Sasa mimi napata shida kule Karagwe, naonekana kama msanii mkubwa sana. Wananchi wa Karagwe, kila nikitoka hapa nawaambia Wizara imepitisha na umeme unakuja. Sasa leo umetoa kwenye kitabu hiki, sio nyaya za umeme zinazokwenda Karagwe na pengine umezitoa hapa ili mimi niunge mkono hoja yako hii, napenda kusema kwa uchungu mkubwa sana, Mheshimiwa Ngeleja namheshimu, ni rafiki yangu lakini nikiunga mkono kama huu umeme usipokwenda kule, lile jinamizi alilolisema Mheshimiwa Mpresa, naona linaanza kuninyemelea na kwa masikitiko makubwa hoja hii sitaiunga mkono mpaka nipate uhakika kwamba umeme sehemu hizo unakwenda ndani ya mwaka huu wa fedha na wala sio mwaka kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Blandes, sasa namwita mchangiaji wetu wa mwisho Mheshimiwa Estherina Julio Kilasi.

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niwe mmojawapo wa wachangiaji wa hoja hii iliyopo mbele yetu. Sitofautiani na wenzangu, napenda niwapongeze sana vijana wetu, Mheshimiwa William Ngeleja na Adam Kighoma Malima, kwa kazi nzuri ambazo wanazozifanya. Kwa kweli, walipokuwa wanapewa Wizara hii kubwa, mimi nilikuwa nawaangalia na kuwaonea huruma kwamba wataweza kweli kuruka vihunzi hivi, lakini wameviweza nawapongeza sana. Lakini niwapongeze Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa kazi nzuri ambazo wamekuwa wakizifanya na zenyé malalamiko makubwa na kwa sababu ya ukata na fedha chache za kuweza kutekeleza ahadi zote lakini wamekuwa wakisema ndio bila ya kutekeleza, kwa hiyo nao nawapongeza kwa sababu wamejithidi sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze Serikali hasa kwa kuchukua ushauri wa Kamati ya Mashirika ya Umma na Kamati ya Mheshimiwa Bomani aliyoindua Mheshimiwa Rais, *STAMICO* kuiondoa kwenye orodha ya Mashirika ambayo yanabinafsishwa. Kwa hiyo, naomba nipongeze kwamba Serikali imekuwa siku sana kwa hili. Lakini kama Makamu Mwenyekiti wa Kamati, ninachoomba tu ili hii hoja isiendoolee kuwepo na zile mali zote za *STAMICO* ambazo zilikuwa zimechukuliwa wakitegemea kwamba zinauzwa zirudishwe mara moja ili *STAMICO* iweze kufanya kazi yake kwa haraka na hasa majengo ambayo *TBA*, *TBA* ni warasimu, naomba wawarudishie, Serikali iweke mkono wake tukikutana tena tusipate tena hii hoja tujue kwamba majengo yote ambayo yalikuwa chini ya *STAMICO* yaweze kurudi haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu kuhusu madini. Mwanzoni nilikuwa namsikiliza Mheshimiwa Ole-Sendeka, nikafikiri hii hoja yake sio nzito, lakini naomba niseme malalamiko ya wawekezaji wa madini ukisikia kwenye Serikali wanasema hakuna matatizo, ukisikia wawakilishi Wabunge wenzetu wanasema kuna matatizo, sasa jambo likisemwa lazima lipo. Kwa hiyo ninaomba niungane na wenzangu, hatuna tatizo kubwa la kupata wawekezaji wa sehemu hii, hatuwezi kupata mwekezaji ambaye ana ubinadamu na utu na kujali watu kusudi wananchi wetu wafurahie ule uwekezaji na maendeleo? Kwa hiyo, hili kama linawezekana basi lifanyiwe kazi haraka iwezekanavyo, mbona hatusikii nchi zingine kuna malalamiko, sisi kulikoni? Tanzania tunakuwa tunaonewa kwa kiasi hicho na hawa wawekezaji, ni umaskini, mipango yetu mibovu, ni kitu gani, naomba lifanyiwe kazi kwa kweli haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakumbuka kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama chetu mwaka 2000, Serikali iliahidi kwamba kulikuwa kumebakia Wilaya 17 tu ambazo hazina umeme na Ilani ya sasa kwamba Wilaya zote tuhakikishe kwamba zimewekewa umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya ifikapo mwaka 2010. Sasa mpaka leo wote tunapoongea hapa, tunapodai umeme wa Kata tuwe sawa, tunasema umeme uje kijijini tuwe sawa, kusiwe na mmojawetu ndani ya uwakilishi hapa anayetaka kusema kwamba mbona Wilayani kwangu hamna umeme. Nimuulize Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii kwamba, je, bado kuna Wilaya ambazo hazijawekewa umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya zao na kama zipo sababu ni zippi zinazopelekeea kwamba wasiweke umeme na kutotimiza ahadi hii? Tuna miezi nane tu kufikisha mwaka 2010 ili tukawaambie Watanzania tulichowaahidi kweli kimetekelezwa. Tujue sababu ni nini. Kwa hiyo, naomba hili Mheshimiwa Waziri atujibu hapa na atupe sababu ni kwa nini hizo Wilaya ambazo zimebaki kwa sababu tuliahidiwa mwaka 2010 tutakuwa tumehakikisha kwamba Makao Makuu yote na Wilaya zote Tanzania nzima itakuwa na umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nipongeze kwa semina ile ambayo tulifanyiwa juzi na wenzetu wa *TANESCO*. Kwa mkakati ambao walikuwa wameuweka kuhakikisha kwamba baada ya adha ya miaka 10, tutakuwa tumehakikisha fursa zote tulizonazo zikifanyiwa kazi, tutakuwa tumepata umeme kwa Tanzania nzima. Kwa sababu sasa inasikitisha, asilimia 12 tu kwa wale watumiaji wa umeme ndio wamefikiwa. Mwaka 2004 tulikuwa na semina, wenzetu wa *SUNNY* walitufanya semina, wamefanya *analysis* sisi tulikuwa hatujui wakasema hivi mnafahamu Tanzania kuna asilimia nane tu ya umeme uliosambazwa, watumiaji asilimia nane huwezi kuelewa sababu yake. Lakini juzi kwa sababu *TANESCO* wenywewe wamekiri hawajafikia hata asilimia 20, lakini wameonyesha fursa ambazo zipo, zikitekelezwa zote baada ya miaka 10 au 20 Tanzania nzima kwa wale ambao wanaweza kutumia umeme utakuwa umetekelozwa. Lakini swali langu linakuja kwa Mheshimiwa Waziri na Serikali wameonyesha fursa, ni mkakati gani basi wa Serikali ambao umewekwa kuweza kuiwezesha *TANESCO* kwa vipaumbele walivyoweka ili waweze kukamilisha na kuweza kufikia lengo ambalo wamelipanga? Basi Waziri atuambie hilo kwamba ni mkakati gani ambao umewekwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine niseme tu sasa hivi umeme sio anasa tena, sio *luxury*, ni kitu cha muhimu sana kwa kila mtumiaji wa umeme. Lakini vile vile inatusaidia sana tusiweze kuharibu mazingira. Unapopita kila mahali unapokuta Mtanzania anasema umeme lini, umeme lini maana yake wananchi wameshajua umuhimu wa matumizi ya umeme. Lakini sasa kwa wale ambao wamebahatika kupata umeme kwenye Wilaya zao kule vijijini gharama ya uingizaji umeme imekuwa ni kubwa mno kati ya shilingi 500,000/= mpaka shilingi 1,000,000/= kwa Mtanzania wa sasa wa kijijini, ni tatizo kwa kweli. Ninachokiomba hapa kwa *TANESCO* wajaribu basi kuititia kwa kadri wanavyoweza pamoja na kwamba wamegawanywa kwa awamu ya ulipaji, lakini hata ukisema ni shilingi 800,000/= kuingiza umeme ugawanye hata kwa awamu nne kwa mwananchi wa kawaida akalipa shilingi laki mbili, mbili ambazo hajawahi kuzishika kwa mwaka mzima inampa shida sana. Kwa hiyo, waangalie ni kiasi gani wanaweza wakarekebisha kumwezesha huyu mwananchi wa kijijini ambaye ana hamu na ana uwezo wa kuweza kutumia umeme aweze kupata hivyo wakiweza hata wakamwekea kwenye bili akawa analipa kidogo kidogo lakini wamuingizie umeme. Kama haiwezekani basi Serikali iangalie ni jinsi gani kwa sababu haya ni matumizi ya lazima, Serikali inaweza ikatoa ruzuku kwa wananchi hawa kijijini ili wasaidiwe kuingiza umeme kwenye nyumba zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa na Mheshimiwa Ngeleja anafahamu, nimekuwa nikimwandikia vi-note vingi sana mradi wa umeme Wilaya ya Mbarali. Mwaka

2002 mradi umeingia kwa ajili ya kuingiza umeme Wilaya ya Mbarali na nashukuru sana kwa pale Makao Makuu ya Wilaya ya Mbarali uliwekwa ule umeme kwa maana ya *transformer*, kazi ikabakia kusambaza umeme kwenye nyumba mbalimbali. Mheshimiwa Msabaha nimshukuru sana kwa wakati huo aliweza kuharakisha kuweza kupata umeme kwa Makao Makuu pale. Mheshimiwa Makamu wa Rais alikuja kuzindua umeme pale, alipozindua baada ya kuona mwamko wa wananchi pale na mabango mengi kwamba tunahitaji umeme na hali ya Mbarali ilivyobadilika akasema Mbarali ninayoifahamu sasa ya miaka mitano iliyopita sio hii kwa changamoto naomba ninukuu na akasema:-

*“Kwa mwamko huu wa wananchi wa Mbarali na mahitaji yao, naomba niseme umeme usambazwe sasa kwenye Kata zote na vijiji vyote ambavyo vitahitaji umeme viwekewe”.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikasema kwa kauli ile sasa mambo yatakuwa murua. Lakini kilichofanyika pale ni kuweka umeme Rujewa na Kata inayofuata, Kata zingine kimya mpaka leo na nimekuwa nikifuatilia sana. Kwa wakati huo, nimefuatilia kwa Mheshimiwa Waziri aliyekuwepo pale Mheshimiwa Msabaha kweli aliniitia wataalam wa *TANESCO* tukakaa pamoja na Meneja wangu wa Wilaya alikuwa ameniainishia vifaa gani vinatakiwa kutumika pale na uzuri naongea hili na nitataja vijiji kwa sababu Ndugu Mhando alikuwa ni Meneja wa Mkoa wetu wa Mbeya, kwa hiyo nikisema anafahamu ni kitu gani ambacho nakisema na tukaainisha pale, akasema baada ya mwezi mmoja tutaweza kujitahidi tukaleta hivyo vifaa. Toka wakati ule tulipozungumza mwaka 2002 mpaka sasa usambazaji wa umeme Mbarali haujakamilika, kulikoni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri anieleze hili, Wilaya ya Mbarali iko barabarani kwa wale wenyeji amba mnatoka Makambako kwenda mpaka Mbeya, Kata zangu nyingi zinaambaaambaa kwenye barabara. Nikianzia Kata ya Mahongole, Ilongo, nguzo ziko pale wananchi walishajiorodhesha kila kijiji ambacho nakisema wamejiorodhesha ili wagawane gharama ya nguzo kwenda kwenye nyumba zao, lakini inatia aibu zaidi viongozi wanapokuja pale wananchi wameshika mabango tunataka umeme. Mara ya kwanza alikuja Waziri Mkuu aliyekuwepo zamani, Mheshimiwa Lowassa wakashika mabango alikuwa anakagua mradi mmoja wa Uturo pale, sasa bahati wakasema ficheni hayo mabango, lakini nashukuru kwa sababu viongozi wote ni Wabunge wanajua kuangalia macho pembeni wakasema kulikoni hamna umeme? Wakajibu hamna umeme, kwa sababu gani, sababu hazikutolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi amekuja Mheshimiwa Rais pamoja na yote na kufunga ule mradi, kijiji hicho hicho wananchi bado wakawa na mabango, DC akasema kwamba ficheni hayo mabango haraka. Lakini Mheshimiwa Rais, namshukuru sana akaangalia akasema niambieni tatizo ni nini, kwani umeme haupo kwenye sehemu hii, majibu wakasema tunayafanyia kazi Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, nataka njue sasa Kata ya Mapogolo, Kata ya Mahongole, Kata ya Riwa, Kata ya Utengule Usangu, Makao Makuu tu hayo ambayo yako barabarani wala sio hatua kubwa na nguzo zinapita hapo na kukamilisha Makao Makuu ya Wilaya, ni lini hiyo kazi itafanyika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, bahati nzuri alikuja akafikia Kata ya Madibira ambapo kawaida yake anaitwa Mwanakijiji au Mwenyekiti wa Kijiji. Ebu nielezeni kero, ni faraja yangu, kwa kweli kero yetu hapa ni umeme. Tuna kinu cha kukobolea mpunga ambacho kimejengwa kuanzia mwaka 2002 chenye gharama zaidi ya shilingi bilioni 20, kinashindwa kufanya kazi kwa sababu hakiwezi kufanya kazi kwa kutumia dizeli ni gharama sana. Tungepata umeme tungeweza kusaidia

kukoboa mpunga mwangi sana huu wote wanaolima Wilaya ya Mbarali. Akamuuliza Meneja wa *TANESCO* wa Wilaya ya Mbarali kama ana jibu, akasema kwa kweli hana jibu. Akasema basi nakuagiza wewe ukawaambie wakubwa wako, ongea na Wizara uhakikishe kwamba Madibira sasa hiki kinu kinafanya kazi na umeme unakuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba walikuja wataalam kutembelea pale na kuangalia hali halisi ikoje, lakini kuanzia siku hiyo mpaka leo ni kimya. Ninachokuomba Mheshimiwa Waziri, jibu nilipate leo kwanza usambazaji wa umeme Wilaya ya Mbarali kama Makao Makuu, lakini la pili ahadi ya Mheshimiwa Rais imefikia wapi na kama wataalam wameleta majibu kwako, una mkakati gani kuhakikisha kwamba ile ahadi ya Rais, ambayo wananchi waliipokea kwa furaha zote kwamba sasa Makao Makuu yangu na Kata zote ambazo zinazunguka Makao Makuu zinapata umeme? Kwa sababu muda umeshafika, ni kesho kutwa tu tunaanza tena kupita, tunakwenda kuwaambia nini? Hivi ni nini ambacho kimesababisha tusipate hata lile jibu na mimi nashindwa hata kurudi sasa kwa sababu hii ni bajeti ya mwisho tuseme ijayo itakuwa haina utekelezaji watu watakuwa tumeshakwenda kwenye Majimbo kuhangaika na wapiga kura. Kwa hiyo, ninachokuomba Mheshimiwa Waziri, nipate jibu wataalam walivyopita kwenye ile ahadi ya Rais kwa ajili ya kufanya kile kinu kiendeshwe, walileta jibu gani kwako na wewe umewajibu nini na kuna mpango gani wa kufanya hiyo kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hizi Kata nyininge tano ambazo zimebaki, ninazitaja Kata ya Ruhiwa, Mahongole, Utengule Usangu, Ubaruku na Mapogoro, mtaalam wako, Bwana Mhando, anajua nafikiri viji vyote anavijua na wananchi walishalipa fedha, wengine walishajiandikisha na orodha wakaifikisha kwenye Makao Makuu ya *TANESCO* ya Wilaya ya Mbarali. Kwa hiyo, naomba majibu haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasita mpaka nipate majibu, kwanza ni rafiki wa Wabunge wote hapa, umekuwa ukitujibu maswali mazuri sana na unafanya kazi nzuri sana, lakini naomba nipate majibu, nikipata majibu nitaunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda uliobaki ni dakika 10 ambazo wachangiaji wanaofuata wote haziwatoshi.

Sasa naomba nitoe tangazo, naomba kumtangaza mgeni wa Mheshimiwa Waziri Ngeleja, anaitwa Ndugu Mbaraka Igangula Mwenyekiti wa TAMICO, Ndugu Igangula popote ulipo naomba usimame, hajafika Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma, Mheshimiwa Estherina Julio Kilasi anaomba kuwatangazia Wajumbe wa Kamati yake kwamba kesho tarehe 26 Julai, 2009 kutakuwa na Kikao cha Kamati katika ukumbi Na. 227, saa 3.00 asubuhi, anawaomba usimame, hajafika Mheshimiwa Waziri.

Waheshimiwa Wabunge, naomba nisitaje orodha ya wale ambao wataanza kuchangia siku ya Jumatatu. Lakini walioomba wako wengi na Jumatatu tutaendelea lakini nitamwachia Mheshimiwa Spika au yejote atakayekuwa kwenye Kiti ili aweze kuweka utaratibu mzuri zaidi wa wale ambao watakuwa wanaochangia kwa sababu wengi walikuwa wameomba kuahirishiwa michango mpaka hiyo siku ya Jumatatu. Kwa hiyo, naomba nisiwataje, lakini michango inaendelea siku ya Jumatatu.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nachukua nafasi hii kuwatangazieni kuwa naahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya Jumatatu saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 10.50 jioni Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Jumatatu Saa 3.00 asubuhi)*